**9 MEI, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### Kikao cha Ishirini na Moja – Tarehe 9 Mei, 2023

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe David M. Kihenzile) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tukae. Mkutano wa Kumi na Moja, Kikao cha Ishirini na Moja.

Katibu.

**NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:** Hati za kuwasilisha Mezani.

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI - K.n.y. WAZIRI WA MAJI):**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu kwa niaba ya Waziri wa Maji.

Katibu.

**NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:** Maswali.

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Tunaanza na maswali, Ofisi ya Waziri Mkuu. Namuita Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini, aweze kuuliza swali lake.

Na. 264

### Kushughulikia malalamiko kuhusu kikokotoo

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU** aliuliza:-

Je, Serikali imejipanga vipi kushughulikia malalamiko kuhusu kikototoo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilitangaza matumizi ya kanuni mpya ya mafao ya kikokotoo ya pensheni kuanzia tarehe 1 Julai, 2022 kupitia Gazeti la Serikali Na. 357 Toleo la Tarehe 20 Mei, 2022. Kanuni hiyo iliandaliwa kwa kuzingatia haja ya kuboresha, kuwianisha mafao ya wanachama na kuifanya Mifuko ya Pensheni kuwa endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua wajibu wa kuwaelimisha wananchi hususan waajiri na wanachama wa Mifuko ya Pensheni kuhusu Kanuni mpya ya Mafao ya Pensheni, elimu imeendelea kutolewa na Mifuko ya Pensheni kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi *(TUCTA)*. Hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2022, Mifuko iliweza kutoa elimu kwa jumla ya waajiri 2,927 *(PSSSF),* waajiriwa 318 na *NSSF* waajiriwa 2,609 ambapo wanachama 71,836 wa *PSSSF* wakiwa 19,656 na *NSSF* 52,180 walifikiwa na mafunzo hayo. Mifuko inaendelea kutoa elimu kama sehemu ya majukumu yao ya kila siku, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kikokotoo, *issue* siyo elimu, *issue* ni ile *percent* inayotolewa. Watu wanalalamikia *percent* inayotolewa kwamba hawajakubaliana nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; tuna malalamiko kutoka kwa kundi muhimu la wafanyakazi ambao wote tunajua historia ya wafanyakazi ndiyo hasa kundi kubwa lililokuwa likifanya mapinduzi mbalimbali, sehemu mbalimbali duniani. Sasa ni lini Serikali pamoja na majibu iliyoyatoa, itafanya ile ujumuishi? Kwa sababu wafanyakazi waliostaafu pia wanasumbuka sana. Wapo ambao walikuwa *NSSF* wakahamishiwa *PSSSF,* wanapokwenda kudai mafao yao wanalipwa kidogo na *PSSSF* na wanatakiwa tena kuanza kufuatilia *NSSF;* imeleta usumbufu mkubwa. Ninyi kama Serikali mmejipangaje kuwasaidia ili walipwe kwa pamoja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Askari wetu au Jeshi la Polisi, wao ni kama majeshi, lakini kikokotoo hiki kinaoneka kwamba hakiwahusu majeshi mengine, isipokuwa askari wameingizwa kwenye kikokotoo hiki, nao

hawakubaliani na hiyo. Wanasema kwa nini wao wasiwe *regarded* kama majeshi mengine yalivyokuwa *regarded?* Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Msambatavangu alivyoeleza, ni kwa sababu tu ya pengine taarifa kuwafikia watu vizuri na ndiyo maana wakati wote kumekuwa na mkakati wa kutoa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali watumishi waliokuwa wakichangia kwa asilimia 25, kama alikuwa anapata shilingi milioni 46, kwa sasa malipo ya mkupuo analipwa shilingi milioni…; wakati huo alikuwa analipwa shilingi milioni 44 na katika pensheni ya kila mwezi alikuwa analipwa shilingi 800,000. Kwa mabadiliko haya ya sasa ambayo yalikubaliwa na wadau wote pia wakiwemo vyama vya wafanyakazi, katika asilimia 33, ukiangalia mkupuo umeongezeka. Ukiangalia mchango wake ule wa milioni 46 sasa hivi analipwa milioni 58. Pia ongezeko lingine kwenye pensheni ya kila mwezi, analipwa zaidi ya shilingi 700,000. Kwa hiyo, unaweza ukaona utofauti ambao umekuwepo hapo katika hiyo. Umekuwa na faida. Zaidi ya asilimia 81 kwa sasa wananufaika na mpango huu. Lilifanywa hili baada ya kushirikisha wadau, kwa sababu asilimia 31 ndio wamekuwa wanufaika wa kikokotoo hiki kipya. Kumbuka tulikuwa asilimia 25, tumekuja asilimia 33.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna faida nyingine ya kutengeneza uendelevu wa mifuko. Hii mifuko utakumbuka, awali kulikuwa kuna mifuko mingi; *LAPF*, tulikuwa tuna *PSSF*,

na mifuko mingine mingi. Wajibu wa Serikali na agizo lililotolewa ilikuwa ni kuangalia ile faida kwamba hii mifuko itakuwa inaendeshwa lakini mwisho wa siku wanachama wake wapya hawawezi kunufaika nayo kwa sababu ya kutokuwa na ustahimilivu au *stability* ya mifuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kilichofanyika ni kuunganisha mifuko ili kutengeneza utaratibu ambao utawasaidia zaidi wanachama kuweza kunufaika na ndiyo maana tukawa na skimu hizo mbili. Moja ya upande wa wafanyakazi wa Serikali ambapo ni *PSSSF* na pili *NSSF* inashughulika na wale ambao ni watumishi katika kada za kawaida. Kwa hiyo, faida ni nyingi kuliko hasara kwa kipindi hiki. Walioongezeka hapo ni asilimia 81 ambao wanapata faida zaidi hasa kwenye mkupuo ule wa mwisho, imekuwa fedha wanayolipwa kwenye mkupuo ni kubwa zaidi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Paschal Patrobass Katambi. Tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, namwita Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa, Mbunge wa Handeni Mjini aulize swali lake.

Na. 265

**Ukarabati wa Hospitali ya Halmashauri ya Mji Handeni**

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA K.n.y. MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati Hospitali ya Halmashauri ya Mji Handeni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, Mheshimiwa Deo Ndejembi majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Reuben Kwagilwa, Mbunge wa Jimbo la Handeni Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ukarabati wa hospitali kongwe nchini. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetenga fedha shilingi bilioni 17.1 kwa ajili ya ukarabati wa Hospitali 19. Aidha, hadi kufikia mwezi Februari, 2023 kiasi cha shilingi bilioni 12.95 zimeshatolewa kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya hospitali kongwe 14 ikiwemo Hospitali ya Mji wa Handeni iliyotengewa shilingi milioni 900.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali itatenga shilingi bilioni 27.9 kwa ajili ya ukarabati wa hospitali kongwe 31 zilizosalia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Timotheo Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Pamoja na kutengewa fedha, shilingi milioni 900 hali ya hospitali ile ni mbaya na fedha hiyo ni ndogo. Serikali iko tayari kuwaahidi wananchi wa Handeni Mjini kwamba itaendelea na utaratibu wa kupoteza fedha hizi kila mwaka ili hospitali hii ifanyiwe ukarabati yote? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Wananchi wa Handeni Mjini, kama walivyo wananchi wa Korogwe Vijijini, wamejenga sana zahanati, maboma yamesimama na hayajakamilika; Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha

kwamba inayamalizia na kuyakamilisha maboma yote ya zahanati nchini ambayo wananchi wameyajenga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu maswali mawili ya nyongeza, la kwanza kwamba fedha ni ndogo; fedha hii inatengwa na Serikali kuhakikisha wanafanya ukarabati wa yale majengo ambayo yalikuwepo toka zamani. Kwa mfano, nikisema kwenye Hospitali hii ya Handeni Mjini, wao walitaka kujenga hospitali mpya kabisa ya wilaya, lakini fedha iliyotengwa ilikuwa ni kwa ajili ya ukarabati wa majengo yaliyopo. Tutaendelea kutafuta fedha na kuhakikisha kwamba tunaendelea kupeleka fedha kwenye Halmashauri hizi kwa ajili ya ukarabati zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye swali lake la pili la kumalizia zahanati, nyote ni mashahidi humu ndani, katika majimbo yetu na Halmashauri zetu, Serikali hii ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imekuwa ikileta fedha shilingi milioni 50 za kumalizia zahanati na tutaendelea kutafuta fedha, na kadri ya upatikanaji wa fedha hizo basi tutaendelea kuleta katika majimbo hayo kuweza kumalizia zahanati ambazo zimejengwa kwa nguvu ya wananchi.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea. Namwita Mheshimiwa Venant Daud Protas, Mbunge wa Igalula aweze kuuliza swali lake.

Na. 266

**Hitaji la vifaa tiba na majengo ya *OPD* – Vituo vya Afya Igalula**

**MHE. VENANT D. PROTAS** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itamalizia Vituo vya Afya Kizengi, Tura, Lutende na Goweko kwa kujenga *OPD* na kupeleka vifaa tiba?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Venant Daud Protas, Mbunge wa Jimbo la Igalula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa Vituo vya Afya katika kata za kimkakati ili kusogeza huduma za afya karibu na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Serikali ilitenga shilingi milioni 200 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Lutende katika Halmashauri ya Wilaya ya Uyui. Aidha, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali ilitenga shilingi milioni 300 kwa ajili ya ukamilishaji wa Kituo cha Afya Lutende.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa vituo vya afya vya kimkakati kote nchini ikiwemo ukamilishaji wa Kituo cha Afya

Lutende, na Tura, pamoja na ujenzi wa vituo vya afya katika Kata ya Goweke na Kizengi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Venant, swali la nyongeza.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, Kata ya Lutende ambayo unasema mmetenga shilingi milioni 300 ambayo itaenda kumalizia kituo cha afya, fedha hiyo haijaenda mpaka siku ya leo; je, ni lini fedha hiyo itakwenda kumalizia Kituo cha Afya cha Kata ya Lutende?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Wananchi wa Kata ya Igalula wamejenga boma la wodi ya kulazia wagonjwa na Serikali imeleta fedha nyingi na tumenunua vitanda, hakuna sehemu ya kuvipeleka; je, Serikali haioni haja ya kupeleka fedha kumalizia wodi hiyo kwa sababu *operation* mpaka sasa hivi ni 27 hakuna sehemu ya kuwalaza? Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Venant, la kwanza fedha hii shilingi milioni 300 katika Kituo cha Afya Lutende, kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi kwamba ilikuwa ni kwenye mwaka wa fedha ambao umepita, sasa nitakaa na Mheshimiwa Mbunge tuweze kuona nini kilitokea hata fedha hii mpaka sasa haijafika, na kama kuna mkwamo wowote, basi tutashirikiana kwa pamoja kuhakikisha kwamba fedha hii inafika katika Kituo cha Afya cha Lutende.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye swali lake la pili la Igalula, fedha ya kukamilisha wodi. Serikali itaendelea kutoa fedha kadiri ya upatikanaji ili kukamilisha majengo

mbalimbali kwenye vituo vya afya, zahanati na hospitali za wilaya kote nchini. Kwa hiyo, fedha itakapopatikana, basi tutahakikisha Kituo cha Afya Igalula nacho kinapata fedha.

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri *especially* kwa kusema kwamba Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa vituo vya afya vya kimkakati kote nchini.

Nimeona kuna waheshimiwa wamesimama, lakini hata hivyo tunaendelea, namwita Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma, Mbunge wa Hanang aulize swali lake.

Na. 267

**Ujenzi wa barabara ya Mureru hadi Waama - Hanang**

**MHE.SAMWELI X. HHAYUMA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga barabara ya Mureru – Diloda – Gorimba – Masusu hadi Waama ili ipitike wakati wote?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Samweli Hhayuma, Mbunge wa Hanang, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Mureru – Diloda – Gorimba – Masusu hadi Waama imegawanyika katika vipande viwili vya Mureru – Waama chenye urefu wa kilometa 34 na Diloda – Gisambalang’ chenye urefu wa kilometa 25.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2022/2023, *TARURA* imefungua kipande cha barabara ya Mureru - Waama kwa kiwango cha tabaka la udongo yenye urefu wa kilomita 34 na ujenzi wa *(culvert)* yaani vivuko 11 vya maji kwa gharama ya shilingi milioni 284.99. Awali kipande hiki kilikuwa ni njia ya ng'ombe (Pario). Aidha, katika mwaka wa fedha 2023/2024, shilingi milioni 80 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa *culvert,* yaani vivuko 16 vya maji katika barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufunguzi wa kipande cha barabara ya Diloda – Gisambalang' chenye urefu wa kilometa 25.1 utafanyika kadiri ya upatikanaji wa fedha ambapo kwa sasa kinatumika kama njia ya ng'ombe (pario).

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Samweli Hhayuma, swali la nyongeza.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, hii barabara ili ilete tija inayokusudiwa, ni muhimu kufungua barabara ya Mashaw - Waranga, barabara ya Masusu – Gisambalang – Mhanda; je, Serikali iko tayari kutenga fedha haraka ili barabara ziweze kufunguliwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Wilaya ya Hanang' ina maeneo mengi ambapo mvua ikinyesha yanakuwa kama kisiwa. Mfano Mara, Uteshi, Merekwa, Gaulol, Ghetaghul na Gijetamogh; je, Serikali haioni ni wakati muafaka sasa kuingozea *TARURA* Wilaya ya Hanang' bajeti?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu maswali mawili ya nyongeza; la kwanza, hii barabara ambayo ameitaja ya Marang,

Masusu, Gisambalang na maeneo ya kule Hanang' Serikali itaendelea kutenga fedha kadiri ya upatikanaji wa fedha hizi. Vile vile kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi, barabara hii ilikuwa ni ya kupita mifugo (Pario). Kwa jitihada kubwa za Serikali hii ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na *TARURA* kuongezewa fedha, imeanza kufunguliwa na sasa zaidi ya kilometa 30 tayari zimetengenezwa na kadiri miaka inavyokwenda tutazidi kuhakikisha barabara hii inafunguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye swali lake la pili la barabara hii za Katesh, Berekwa na maeneo yale ya kule Hanang ambayo ameyataja Mheshimiwa Hhayuma, *TARURA* kwa mwaka wa fedha huu unaomalizika ilitengewa shilingi bilioni 2.33 kwa Wilaya ya Hanang peke yake. Hii ni zaidi ya mara tatu ya bajeti ambayo ilikuwa 2020/2021 ya barabara katika Wilaya ya Hanang'. Hivyo Mheshimiwa Mbunge awe tu imani kwamba katika bajeti inayofuata hii, vilevile *TARURA* wametengewa bajeti hiyo hiyo ya shilingi bilioni 2.33 kule Wilaya ya Hanang na barabara nyingi zitafunguliwa kuhakikisha kwamba wananchi wake kule wanapita bila matatizo yoyote.

**MWENYEKITI:** Ahsante tunaendelea. Namwita Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris Mbunge wa Morogoro Kusini aweze kuuliza swali lake.

Na. 268

**Ujenzi ya shule ya msingi ya watoto wenye mahitaji maalum – Morogoro**

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga shule ya msingi ya watoto wenye mahitaji maalum katika Halmashauri ya Morogoro?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba uwashe *mic*, hatujakusikia. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mbunge wa Jimbo la Morogoro Kusini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Halmashauri ya Morogoro ina watoto wenye mahitaji maalum. Hadi sasa halmashauri imeanza kujenga bweni kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalum katika shule ya msingi Mvuha. Shule hii ina jumla ya wanafunzi 24, Serikali tayari imekwishapeleka kiasi cha shilingi milioni 100 katika shule hii katika mwaka wa fedha 2022/2023 kwa ajili ya ujenzi wa bweni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga na kupeleka fedha katika Halmashauri ya Morogoro kwa kadiri ya upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kalogeris, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Pamoja na fedha kupelekwa katika halmashauri na ujenzi wa mabweni kuendelea bado kuna uhitaji wa walimu wa fani hiyo…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kalogeris, Mheshimiwa Naibu Waziri hakusikii vizuri atashindwa kukujibu, hebu weka maiki vizuri Mheshimiwa.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali pamoja na kupeleka fedha ile shilingi milioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni na

kazi inaendelea bado kuna uhitaji wa walimu pindi kazi itakapokuwa imekamilika. Vilevile kuna uhitaji wa uzio ili kuweza kuweka usalama kwa watoto hao wenye mahitaji maalum. Je Serikali ina mpango gani wa kupeleka fedha hizo na walimu pindi kazi itakapokamilika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, Mheshimiwa Naibu Waziri uko tayari kufanya ziara katika Jimbo la Morogoro Kusini na kuandamana na mimi ili kwenda kuangalia mahitaji mengine ya elimu na afya katika halmashauri yetu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajibu maswali yake haya mawili kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge Mheshimiwa Kalogeris kwa sababu jambo hili ni wiki iliyopita tu alikuja kulifatilia pale ofisini kuhakikisha kwamba wanapata walimu. Nimuhakikishie mbele ya Bunge lako Tukufu nikijibu swali lake la kwanza kwamba katika ajira hizi ambazo zimetolewa kibali na Mheshimiwa Rais kuweza kuajiri tutahakikisha shule hii kwa sababu ni watoto wenye mahitaji maalum wanapata walimu wa kuweza kuwafundisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye swali lake la pili nipo tayari kuongozana na Mheshimiwa Mbunge mpaka kwenda Jimbo Lake la Morogoro Kusini kwenda kuitembelea shule hii na tuone ni nini kinaweza kikafanyika na Serikali kwa ajili ya kujenga uzio ambao ameuzungumzia Mheshimiwa Mbunge pale.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deo Ndejembi, ahsante sana. Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa majibu yako. Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, namwita Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa Mbunge wa Namtumbo aulize swali lake.

Na. 269

**Kutokamilika kwa Skimu za Umwagiliaji za Liyuni na Limamu – Namtumbo**

**MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza: -

Je, ni kwa nini skimu za umwagiliaji za Liyuni na Limamu – Namtumbo hazijakamiliki ingawa Serikali imetumia fedha nyingi?

**MWENYEKITI:** Aliyeulizwa yuko wapi? Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, skimu ya umwagiliaji ya Mtakuja iliyopo katika Kata ya Limamu yenye ukubwa wa eneo la hekta 350 na Liyuni iliyopo katika Kata ya Mchomoro yenye ukubwa wa hekta 140 ni miongoni mwa skimu zilizopo katika Wilaya ya Namtumbo. Katika mwaka 2006/2007 hadi 2012/2013, Serikali iliwekeza kiasi cha shilingi bilioni 1.260 kwa ajili ya ujenzi wa mfereji mkuu mita 3,950, vivuko viwili, daraja moja, kalvati na barabara yenye urefu wa kilomita 25 katika mradi wa Liyuni na ujenzi wa banio, mfereji mkuu mita 3,000 vivuko katika skimu ya Mtakuja kupitia fedha za *DADPs, DIDF na MIVARF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa usanifu wa skimu hizi ulifanyika muda mrefu, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji katika mwaka wa fedha 2023/2024 imepanga kufanya mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili kubaini gharama halisi za kukamilisha miundombinu ya

umwagiliaji na kuhakikisha skimu hiyo inakamiliaka na kuleta tija ya kilimo cha umwagiliaji katika kata za Limamu na Mchomoro.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kawawa, swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa maeneo haya yana jumla ya hekta zaidi ya 490 na Serikali iliwekeza kama ilivyosema bilioni 1.260 lakini sasa maeneo haya imekuwa wafugaji wanafanya kama maeneo ya malisho na kuharibu mazingira katika maeneo yale. Je, Serikali inaweza kuharakisha kazi iliyokusudia ili kumaliza miundombinu yake na kuweza kufanya kazi ya kilimo cha umwagiliaji kiweze kuendele kwa mwaka mzima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Serikali kuu inaweza kutusaidia kuondoa wafugaji hawa katika maeneo yale ili yabaki kama eneo la kilimo kama lilivyokusudiwa na kwa kuwa Serikali iliwekeza fedha nyingi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa Mbunge wa Namtumbo kama ifuatanvyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la kwanza la kuharakisha nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika miradi ambayo tuliipitia nchi nzima na kuangalia hatua ambayo imefikia na imekwamia wapi ni pamoja na miradi hii ambayo ipo Kata za Liyuni na Limamu nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge, kwamba katika mwaka huu wa fedha tutahakikisha kwamba tunafanya upembuzi yakinifu ili kazi ya ujenzi ianze mara moja na wananchi waanze kufanya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ya kuhusu wanyama, hili liko ndani ya Uongozi wa wilaya husika na sisi tuko tayari kusaidia nao kuhakikisha kwamba eneo hili linalindwa hivyo nitoe rai kwa uongozi wa Wilaya kuhakikisha kwamba maeneo haya yanasimamiwa vizuri na yanalindwa ili yabaki katika matumizi ambayo yamekusudiwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea, namwita Mheshimiwa Daktari Florence George Samizi Mbunge wa Muhambwe aulize swali lake.

Na. 270

**Malipo ya mauzo ya tumbaku**

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI** aliuliza: -

Je, ni lini Wakulima wa Tumbaku watalipwa fedha zao kutoka Kampuni ya *JESPAN* ya msimu wa mauzo 2021 Jimboni Muhambwe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi Mbunge wa Muhambwe kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika msimu wa mwaka 2020/2021, kampuni ya *JESPAN Company Limited* ilinunua jumla ya kilo 512,426 za tumbaku zenye thamani ya Dola za Marekani 662,651. Kampuni hiyo iliweza kulipa wakulima wa Kibondo, Kakonko na Kasulu kiasi cha Dola za Marekani 471,500 na kubaki deni la kiasi cha Dola za Marekani 191,151.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ucheleweshwaji wa malipo, Serikali imeanza kuchukua hatua za kisheria kwa kampuni zilizonunua tumbaku kwa wakulima na kushindwa kufanya malipo. Hivyo basi, malipo ya wakulima yatafanywa kwa mujibu wa maamuzi ya vyombo vya haki ikiwemo Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni hiyo iliyoshindwa kulipa wakulima baada ya soko la kuuza tumbaku iliyonunua kuyumba na kutouza kutokana na athari za UVIKO – 19. Aidha, Wizara kupitia Bodi ya Tumbaku na Chama Kikuu cha Wakulima wa Tumbaku Mkoa wa Kigoma *(KTCU)* na Ofisi ya Mashtaka ya Mkoa wa Kigoma inakamilisha taarifa za kuifungulia kesi ya madai kampuni ya *JESPAN Company Limited* ili kukamilisha malipo ya wakulima.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Daktari Florence Samizi, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naishukuru sana Serikali kwa majibu hayo mazuri pamoja na majibu hayo mazuri bado nina maswali ya nyongeza. Wahanga waliozulumiwa pesa zao katika Jimbo la Muhambwe ni Lugongwe *AMCOS*, Chapakazi *AMCOS*, Amani *AMCOS* na Migwezi *AMCOS* ambao hawa waliingia mikataba na *JESPAN* baada ya kuwa wamejiridhisha kwamba Serikali imewapatia vibali hawa *JESPAN*.

Je, Serikali aioni iko ukunimu wa kulipa hizi pesa kwa sababu wao ndiyo waliyowadhamini hawa wakulima halafu wenyewe Serikali itaendelea na hizo kesi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa makampuni haya ya wazawa yanawazulumu hawa wakulima hii *JESPAN* ni mfano tu. Serikali imejipanga vipi

kuyadhibiti haya makampuni ili wakulima wetu wasiendelee kudhulumiwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli makampuni haya tumeanza kuchukua hatua za kisheria, baadhi ya makampuni yanatoa huduma kwenye sekta ya tumbaku baadhi yao tumeishayakata fedha kupitia *TCJE* kama dola lakini nne ambazo walitoa huduma ili tuweze kuzirudisha kwa wakulima. lakini hatua ya pili ni kwamba Serikali inapompa leseni kwenda kufanya biashara anapokwenda kinyume kuna utaratibu wa kisheria na kwake yeye kupewa leseni ya kwenda kufanya biashara haina maana ile *responsibility* siku ya mwisho itahamia kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tabia ya wakulima kudhulumiwa na wafanyabiashara na hii haipo tu kwenye tumbaku, ipo kwenye pamba, ipo kwenye korosho, ipo kwenye maeneo mengi, na wizi mwingine hushirikisha vyama vya ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano kesi iliyoko Mkoa wa Katavi chama cha ushirika kimeshirikiana na Kampuni ya *NEIL* kuweza kuwaibia wakulima. Kwa hiyo, tunachukua hatua za kisheria niwaombe Waheshimiwa Wabunge wa Sikonge Wilaya ya Sikonge Mkoa wa Katavi, Mkoa wa Tabora na Wilaya ya Chunya wa tumbaku waliyopata madhara mwaka 2019/2020 niwahakikishie kwamba Serikali inachukua hatua na tutamaliza haya matatizo na yamekuwa fundisho kwetu ndiyo maana tumewaondoa wanunuzi wa namna hii na

tunakuja na sheria ya kilimo itakayoweza ku–*criminalize* wizi unaofanyika kwenye sekta ya kilimo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu. Tunaendelea Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi namwita Mheshimiwa Omar Issa Kombo, Mbunge wa Wingwi, aulize swali lake.

Na. 271

**Hitaji la nyumba za Askari Polisi- Wilaya ya Micheweni**

**MHE. OMAR ISSA KOMBO** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga nyumba za Askari Polisi katika Kituo cha Wilaya ya Micheweni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omar Issa Kombo, Mbunge wa Wingwi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua mahitaji ya nyumba za makazi ya kuishi askari Polisi katika Wilaya ya Micheweni. Mpaka sasa ujenzi unaoendelea ni wa hanga la kuishi familia 18 za askari na uko kwenye hatua za umaliziaji. Kiasi cha shilingi milioni 60,000,000 kinahitajika ili kumalizia na fedha hizo zinatarajiwa kuombwa kutoka Mfuko wa Tuzo na Tozo kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Serikali itaendelea kujenga nyumba za maofisa na askari kutegemea upatikanaji wa fedha, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante kwa majibu mafupi. Subiri nikuite Mheshimiwa, Mheshimiwa Omar Issa Kombo swali la nyongeza.

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi. Hadi sasa katika Wilaya ya Micheweni hakuna nyumba za askari ambazo ujenzi unaendelea. Pamoja na hili sasa naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kituo cha polisi Wilaya ya Micheweni ndiyo Makao Makuu ya Polisi Wilaya ya Micheweni. Je, Serikali ina mkakati gani wakujenga nyumba za polisi katika Wilaya ya Micheweni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; katika kituo cha polisi cha Wilaya ya Micheweni kuna hanga la Jeshi la Polisi ambalo lilijengwa kutokana na nguvu za wananchi miaka kumi iliyopita hadi sasa hanga hili kutokana na kwamba halikumaliziwa tayari limeanza kuharibika ikiwemo paa kuvuja na saruji kuharika. Je, Serikali haioni haja kuunga mkono jitihada hizi za wananchi kwa kumalizia jengo hili? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati nimeusema ni kuendelea kutenga fedha kujenga nyumba za askari na maofisa kutegemea upatikanaji wake hata hivyo alichosema kwamba ujenzi umesimama kule Micheweni Mheshimiwa Mbunge ni kweli ndiyo maana kwenye jibu la msingi nimesema zinahitajika milioni 60 ili kumalizia jengo hilo na fedha hizi zinatengwa kwenye bajeti ya mwaka 2023/2024 kutoka Mfuko wa Tuzo na Tozo. Kwa hiyo, Mheshimiwa eneo hilo litakamilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uendelezaji wa ujenzi wa nyumba, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi tutaendelea kujenga nyumba za askari kadri tunavyopata pesa kwenye bajeti yetu au pale tunaposhirikiana na wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, namwita Mheshimiwa Felista Deogratius Njau Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake.

Na. 272

**Msongamano wa wafungwa magerezani**

**MHE. SALOME W. MAKAMBA K.n.y. MHE. FELISTA D. NJAU** aliuliza: -

Je, nini mkakati wa Serikali wa kupunguza msongamano wa wafungwa magerezani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Felista Deogratius Njau, Mbunge wa Viti maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika magereza yetu upo msongamano mkubwa unaosabishwa na idadi kubwa ya mahabusu kuliko wafungwa hususani katika magereza ya mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada zinazochukuliwa na Serikali kupunguza msongamano wa wafungwa magerezani,

ni pamoja na kuhimiza matumizi ya vifungo vya nje kama vile *Parole*, *Extra Mural Labour*, huduma kwa jamii na huduma za uangalizi kwa wafungwa wenye viashiria vya kujirekebisha, msamaha unaotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika maadhimisho ya sherehe za Muungano wa Tanzania na Uhuru wa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkakati wa Serikali ni kuendelea kuelimisha na kuhimiza wananchi waishi kwa maadili bora na waepuke kuvunja sheria ili waepuke kufikishwa mahakamani na kufungwa. Aidha, Serikali itaendeleza mpango wa kujenga magereza mapya na kufanya upanuzi kwa magereza ya zamani ili kuongeza nafasi ya kuwahifadhi wafungwa na mahabusu kulingana na mahitaji na kutegemea upatikanaji wa fedha, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Njau swali la nyongeza. Mheshimiwa Salome Makamba kwa niaba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru pamoja na majibu ya Serikali ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali langu la kwanza juzi wakati Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu swali linalofanana na hili alieleza bayana kwamba mahabusu wengi wanashindwa kutoka, kwa sababu ndugu zao au jamaa hawaendi kuwawekea dhamana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu yapo makosa ambayo mtu anaweza akajidhamini mwenyewe na hili litapunguza msongamano mkubwa kwenye magereza. Nini kauli ya Serikali kwa Jeshi la Polisi na Magereza ambao mpaka sasa hivi wanaweka vikwazo kwa mtu kujidhamini mwenyewe na kuweza kutoka katika vizuizi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; bado katika magereza yetu njia zinazotumika kufanya ukaguzi kwa wafungwa hasa wanawake zinawadhalilisha wanawake na

zinawaondolea utu wao na kuvunja haki zao. Kwa nini Serikali inashindwa kununua vifaa vya kisasa vya kufanya ukaguzi ili kuweza kutunza staha za wafungwa na maabusu hasa wanawake? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba masuala ya dhamana yapo ya namna mbili moja inaweza kutolewa na polisi na nyingine inatolewa na Mahakama. Sasa pale ambapo kuna changamoto za polisi juzi nilieleza kwamba tunawahimiza *RPC'S, OCD'S* na Wakuu wa vituo wazingatie sheria kila inapotokea kosa inastahili dhamana watu waweze kutoa dhamana lakini pale inaposhindikana Mahakama ikitoa amri mtu apewe dhamana *always* tuta–*comply* ili dhamana iweze kutolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upekuzi unaodhalilisha tunatambua hilo na ndiyo maana kwenye bajeti yetu ijayo tumetenga fedha kwa ajili ya kununua vifaa vya kisasa vya kiteknolojia kuepusha ukaguzi unaodhalilisha siyo wanawake tu hata wanaume pia ili mtu akishapita pale anaonekana kama alivyo salama basi itakuwa imekamilika, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi namwita Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo, Mbunge wa Singida Kaskazini aulize swali lake.

Na. 273

**Ujenzi wa barabara ya Singida – Ilongero – Haydom kwa kiwango cha lami**

**MHE. ABEID R. IGHONDO** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara ya Singida – Ilongero hadi Haydom?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, majibu

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo, Mbunge wa Singida Kaskazini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *TANROADS* tayari imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina pamoja na kuandaa nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Singida – Ilongero – Haydom yenye urefu wa kilometa 93. Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kuanza kazi ya ujenzi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ighondo, swali la nyongeza.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana pamoja na majibu hayo mazuri ya Serikali nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; kwa kuwa upembuzi yakinifu sasa umekamilika je, Serikali iko tayari sasa kutenga fedha kwenye bajeti hii tunayoijadili hivi sasa ya 2023/2024 kwa ajili ya kuanza rasmi ujenzi wa barabara hiyo ambayo inakwenda mpaka makao makuu ya halmashauri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili je, Serikali sasa iko tayari kufanya upembuzi yakinifu kwa kipande kinachounganisha barabara hii cha kutoka hapo Ilongero makao makuu ya halmashauri kupitia Ighanoda kwenda

ngamu kilomita 27.1 ambayo inatuunganisha na Wilaya ya Hanang Mkoa wa Manyara? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, kwamba tumeshakamilisha usanifu wa hii barabara na sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha. Na nataka nisiji-*commit* hapa, kwamba kama bajeti tumeshatenga, lakini itategemea na upatikanaji wa fedha, kwa sababu baada ya kukamilisha usanifu kazi inayofata ni kuijenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami; na ndiyo hiyo dhamira ya Serikali kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kuhusu barabara aliyoitaja ambayo inaanzia Ilongelo hadi Ngamo ni barabara fupi kama kilomita zisizozidi 27. Naomba nimuagize Meneja wa Mkoa afanye tathmini ya gharama kwa ajili ya kuanza kufanya usanifu kwa barabara hiyo, halafu aipeleke Makao Makuu kwa ajili ya kufikiria kuiweka kwenye mpango wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa hicho kipande cha barabara cha Ilongelo kwenda Ngamo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, ujenzi na uchukuzi. Tunaendelea na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Namwita Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mbunge wa Viti Maalumu aweze kuuliza swali lake.

Na. 274

**Utafiti wa kurasimisha pombe kali ya Mwiki**

**MHE. AGNES E. HOKORORO** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani kufanya utafiti na kurasimisha pombe ya mwiki inayotokana na mabibo ili kuongeza thamani ya zao la korosho?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara napenda kujibu swali la Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto kadhaa zinazowakabili wazalishaji wa pombe za kienyeji hivyo kushindwa kukidhi matakwa ya viwango na kukosa ithibati ya ubora, Serikali kupitia Shirika la Viwago Tanzania (*TBS*) pamoja na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (*SIDO)* imeweka utaratibu wa kutoa mafunzo kwa wazalishaji wa pombe za kienyeji kuhusu matumizi ya teknolojia bora na matumizi sahihi ya viwango katika kuzalisha pombe za kienyeji ikiwemo pombe aina ya mwiki ili ziweze kukidhi viwango vinavyokubalika na hivyo kuruhusiwa kuingia sokoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Oktoba, 2022, jumla ya leseni 43 za ubora zimetolewa kwa bidhaa mbalimbali za pombe za kienyeji, na maombi mengine mapya 22 yapo kwenye hatua mbalimbali za tathimini kuelekea kwenye kupata ithibati ya ubora. Aidha, Serikali

kupitia Shirika la Viwango Tanzania itaendelea kutengeneza viwango vya pombe za kienyeji kwa kadri mahitaji yatakavyojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnes Hokororo, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru lakini sio mwiki ni mvuke. Maswali mawili ya nyongeza;

a) Je, kwa nini *SIDO* na *TBS* isijielekeze katika kuboresha teknolojia za asili za watengenezaji wa pombe ya mvuke ya mabibo badala ya kuendelea kutoa mafunzo?

b) Je, kwa nini Serikali, isipitie watengenezaji wote wa pombe ya mabibo, badala ya kusubiri waombaji wachache wenye uwezo wa kuagiza mitambo kwa ajili ya kupata hizo ithibati za *TBS* na *SIDO*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni kweli kabisa kwanza nimpongeze Mheshimiwa Agnes Hokororo kwa kuleta tena hili swali ambalo ni hoja muhimu sana kwa Watanzania wengi ambao wengi tumeendesha shughuli zetu za kusoma shule na mambo mengine kupitia pombe hizi za kienyeji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, kweli tunachofanya sasa ni kuboresha teknolojia zilizopo lakini pia kuna wakati mwingine tungependa kupata teknolojia rahisi lakini za kisasa zaidi. Ndiyo maana *SIDO* tunahakikisha tunawatembelea wazalishaji hawa na kuwasaidia. Kama ambavyo nimesema, tayari kuna haya maombi, maana yake

hawa ni wale ambao wana uwezo wa kuomba; lakini ambao sasa hawana uwezo wa kuomba, kama ambavyo nimesema wale wazalishaji wa pombe hii ya mvuke kupitia mabibo, tumeshaamua sasa tutawatembelea wauzaji wote wa pombe za kienyeji ili tuwaelimishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, tutawaelimisha kuhusu mazingira sahihi ya kuzalishia, kwa maana ya kuzalisha pombe, ambapo itakuwa na mazingira sahihi mazuri. Pili tuwasaidie teknolojia rahisi na kuzihuisha zile zilizopo ili ziwe katika mazingira ambayo yatapelekea kupata viwango sahihi vya pombe. Tatu, tuwasaidie kuhakikisha wanapata teknolojia ya kutunza, *packaging* ili zile pombe zisiharibike mapema au zipate shida ambayo itapelekea kuwa sumu kwa walaji katika mazingira mabayo si sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu, tunaendelea na Wizara ya Madini. Namuita Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara, Mbunge wa Tarime Vijijini, aulize swali lake.

Na. 275

### *Madai ya fidia Mgodi wa Barrick North Mara*

**MHE. MWITA M. WAITARA** aliuliza: -

Je, lini Wananchi wa Komarera, Nyamichele na Murwambe katika maeneo ya Mgodi wa Barrick North Mara watalipwa fidia?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI K.n.y. WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Madini naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara Mbunge wa Tarime Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mgodi wa Barrick North Mara ulionesha nia ya kutaka kuchukua baadhi ya maeneo ya Vijiji vya Komarera, Nyamichele na Murwambe ambavyo ni sehemu ya vijiji vinavyozunguka mgodi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baada ya wananchi wa vijiji hivyo kupata taarifa ya maeneo yao kuhitajiwa na mgodi wa Barrick North Mara, walianza kuongeza majengo haraka haraka maarufu kama Tegesha. Hali hiyo ilipelekea mgodi huo kuachana na maeneo hayo kwani hayaathiri uendeshaji wa shughuli zao za kila siku, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisikitike sana na niseme tu kwamba kumbe watu wa Tarime hawajui adui yao mkubwa ni nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarahe 28 mwezi wa tatu, Waziri wa Madini anajumuisha hoja yake hapa alisema kwamba malipo ya fidia Nyamichele na Murwambe hayatafikia mwezi wa sita watakuwa wamelipwa. Lakini vilevile eneo la Nyamichele, Komarera, Nyabichunya na Kiwanja mgodi umeniambia mimi wameenda kuomba maombi maalumu kwenye bodi ili watu walipwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majibu haya, eneo la Nyamichele limekaa tangu mwaka 2012 mpaka leo miaka 11. Serikali inasema eti kwa kuwa mgodi unachimba hauathiriki, wananchi wangu waendelee kuathirika kiuchumi na kisiasa.

Haya majibu ni majibu ya maumivu makubwa kwa watu wa Tarime. Nataka niwatangazie watu wa Tarime wamjue mbaya wao ni nani, pamoja na mengine yote yanayoendelea kule Tarime.

**MWENYEKITI:** Sasa Mheshimiwa Waitara, uliza swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina swali. Hakuna majibu hapa, swali gani? *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Majibu ya uongo kabisa haya.

**MWENYEKITI:** Tunaendela. Namuita Mheshimiwa...

*(Hapa Mhe. Mwita M. Waitara alizungumza bila kutumia kipaza sauti)*

Mheshimiwa naomba uketi.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Sasa mimi nauliza kwa nini...

**MWENYEKITI:** ...ahsante Mheshimiwa utafata utaratibu. Utafata utaratibu wa kama swali lako halikujibiwa vizuri...

**MHE. MWITA M. WAITARA:** ...wanatoa majibu ya uongo tu.

*(Hapa Mhe. Mwita M. Waitara alivua koti na tai na kutoka ndani ya Ukumbi wa Bunge)*

**MWENYEKITI:** Haya tunaendelea namuita Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mbunge wa Liwale aulize swali lake. Mheshimiwa naomba uketi.

Na. 276

**Hitaji la Ofisi ya Madini-Liwale**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA** aliuliza: -

Je ni lini Serikali itafungua Ofisi ya Madini Liwale?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI K.n.y. WAZIRI WA MADINI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mbunge wa Liwale kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishwaji wa ofisi ya madini unazingatia vigezo mbalimbali ikiwemo uwepo wa shughuli kubwa za madini katika eneo husika. Kigezo hiki kinalenga katika kuhakikisha kunakuwa na usimamizi na udhibiti madhubuti wa rasilimali madini inayoanzishwa katika eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mkoa wa Lindi, pamoja na kuwa na Ofisi ya Madini ya Mkoa iliyopo Nachingwea pia Wizara imefungua ofisi ndogo iliyopo Lindi Mjini ili kurahisisha uratibu wa shughulil za madini katika maeneo mengine katika mkoa huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli za uchimbaji katika Wilaya ya Liwale zipo chini ukilinganisha na Wilaya za Ruangwa, Kilwa na Nachingwea. Kwa sasa wachimbaji wa

madini katika Wilaya ya Liwale wanashauriwa kutumia Ofisi ya Afisa Madini Mkazi ya Nachingwea pamoja na ofisi ndogo ya madini iliyopo Lindi Mjini. Hata hivyo, Wizara itaendelea kuboresha huduma kwa wadau wake kwa kadiri itakavyopata fedha za kutekeleza jukumu hilo.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tutulie. Waheshimiwa Wabunge naomba tutulie. Waheshimiwa wabunge wote naomba tutulie; na kiti kikisimama wote mliosimama au mnatembea mnatakiwa mketi, kabla sijawataja kwa majina; Mheshimiwa Pindi Chana. haya swali la nyongeza Mheshimiwa Zuberi Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaja na swali la nyongeza kwanza nisikitike kwa majibu ambayo hayajaridhisha. Hayajaniridhisha mimi wala wananchi wa Liwale. Nina sababu zifuatazo; kwanza Wizara haikuzingatia umbali uliopo kutoka Liwale kwenda Nachingwea lakini vile vile haikuzingatia miundombinu ya usafiri uliopo kutoka Liwale kwenda maeneo iliyotajwa. Hata Mkoa wenyewe wa Lindi ukiuangalia ukubwa wake Wilaya ya Liwale ndiyo yenye eneo kubwa Mkoa wa Lindi. Takriban theluthi moja ya Mkoa wa Lindi iko Liwale. Sasa kuniambia kwamba Wilaya ya Liwale ina shughuli pungufu ya uchimbaji wa madini napata shida kukubaliana na jambo hilo. Hii ni kwa sababu kuna eneo kubwa sana ambalo linazungumzwa Wilayani Nachingwea, eneo la Kitowelo. Eneo hili la Kitowelo liko mpakani na Liwale...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa uliza swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Swali langu,

(a) Je, Wizara hii ya Madini haiko katika mfumo ule wa kusogeza huduma kwa wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana kama ingekuwa kwenye hiyo mpango wa kusogeza huduma kwa wananchi kwa karibu basi na sisi tungepatiwa Ofisi. Ile taasisi ya *GST* ilikuja Liwale ikakaa mwezi mzima ikakaa pale Liwale waliweka kambi Mpigamiti pale, mwezi mzima. Wamefanya utafiti wa madini lakini mpaka leo hatujapata sisi kama Wilaya, kupata hata kile kitabu cha matokeo yale ya uchimbaji wa madini. Matokeo yake sasa watu kutoka Kanda ya Ziwa ndio wanachukua vitalu kule kwa wingi sana kwa sababu matokeo yote yako hapa *GST* Makao Makuu.

(b) Je, Wizara ya madini iko tayari sisi kama Halmashauri kutupatia vile vitabu vya matokeo ya utafiti ule?

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa swali la nyongeza. Mheshimiwa Naibu waziri wa Nishati kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI K.n.y. WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kuchauka, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali la kwanza, Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni Serikali ya wananchi, na nia yake kubwa ni kupeleka huduma kwa wananchi. Kama tulivyosema kwenye jibu la msingi, ni kwamba, ofisi zitafunguliwa kulingana na Wingi na uhitaji wa ofisi hizo kwenye maeneo hayo. Lakini pia nimemalizia kwa kusema Wizara itaendelea kuboresha huduma kwa wadau wake kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimuhalkikishie Mheshimiwa Kuchauka, mpaka sasa Tanzania ina masoko 42

ya kununua na kuuza madini, ina vituo 93. Kadri maeneo yanavyozidi kuongezeka na uhitaji unavyotokea huduma hii inazidi kusogezwa kwa wananchi. Hata katika Jimbo la Liwale watakwenda kutizama na kuona wingi na upana wa mahitaji ya ofisi hizi, na zitapelekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali la pili; nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge; wananchi wa Liwale niliwashauri kutembelea ofisi za madini watapata hizo taarifa za madini yaliyopo kama ambavyo anasema, kwamba waliotoka sehemu za mbali wamepata taarifa hizo. Lakini pia ofisi itahakikisha inatoa taarifa hizo kwa sababu si za siri, kwa wananchi, ili waweze kuzi-*access* na kuweza kuingia kwenye maeneo hayo kuweza kuchimba madini ili kunufaika nayo. Sisi sote tunaohitaji kunufaika nayo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati kwa niaba ya Waziri wa Madini. Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, namwita Mheshimiwa Dkt. Thea Merdad Ntara, Mbunge wa Viti Maalumu aweze kuuliza swali lake.

Na. 277

**Vyuo Vikuu kuwa na hospitali za kufundishia**

**MHE. DKT. THEA M. NTARA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kuwa vyuo vikuu vyenye taaluma ya sayansi na tiba vinakuwa na hospitali za kufundishia?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Elimu Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Omari Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKINOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara Mbunge wa Viti Maalaum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, mitaala ya Mafunzo ya Sayansi ya Utabibu *(Medical and Health Training)* vyuoni hutekelezwa kwa mafunzo ya nadharia na vitendo ambavyo hufanyika katika hospitali zenye wagonjwa halisi. Kwa vyuo ambavyo havina hospitali za mafunzo kwa vitendo, upo utaratibu wa makubaliano kati ya vyuo na hospitali za rufaa, mikoa, wilaya pamoja hospitali za watu binafsi zenye kukidhi vigezo kwa ajili ya kuwawezesha wanafunzi wanaosoma katika vyuo hivyo kufanya mafunzo kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa vyuo vikuu vyenye taaluma ya sayansi na tiba kuwa na hospitali za kufundishia; ambapo kwa sasa inaendelea na ujenzi wa Hosipitali ya Mloganzila kama hospitali ya kufundishia ya Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili. Aidha, Serikali itaendelea kutafuta vyanzo mbalimbali vya fedha kwa ajili ya kujenga hospitali za kufundishia katika vyuo vikuu vingine vyenye taaluma ya sayansi na tiba ambavyo havina hospitali hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri nikupongeze yaani kwa hilo kwa leo nikupongeze, lakini nina swali moja tu la nyongeza. Chuo cha Dodoma ambacho ni kikubwa Afrika Mashariki, na ni kikubwa kweli, kina pia hizo kozi; na kwa hiyo katika kuendelea kufata hizi Sera za Kimataifa, je, Serikali ni lini itaanza kujenga sasa maana yake

mmesema vyuo vingine vitajengwa lakini kwa Chuo hiki cha *UDOM* ni lini chuo hicho mtaanza kujenga *teaching hospital*?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKINOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, Mbunge wa Viti Maalumu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishukuru kwa pongezi alizotoa Mheshimiwa Mbunge na pongezi hizi moja kwa moja ziende kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu yeye ndiye ambaye amewezesha mambo haya yote kuweza kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokwisha eleza kwenye majibu ya msingi, wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wale ambao wanasoma fani au kozi hizi za tiba, wanafanya mafunzo yao kwa vitendo katika hospitali yetu ya Benjamin Mkapa, ambayo iko karibu kabisa na Chuo hiki cha Dodoma. Lakini vilevile wanafanya mafunzo yao katika Hospitali yetu ya Milembe hapa Dodoma. Pia wanafanya mafunzo yao kwa vitendo kwenye hospitali za mikoa ya Dodoma, Singida Pamoja na Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu, na nilithibitishie hapa kwamba Serikali inaendelea na jitihada za kuona vyuo hivi vinakuwa na hospitali zake zenyewe za kufundishia ikiwemo na chuo hiki cha Dodoma. Kwa hiyo tutaendelea kutafuta fedha ili takwa hili la kimafunzo liweze kufikiwa,

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako. Tunaendelea na Wizara ya Maji, namwita

Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Mbinga mjini aulize swali lake.

Na. 278

**Kumaliza tatizo la maji – Mbinga**

**MHE. JONAS W. MBUNDA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakarabati miundombinu chakavu ya maji na kuhakikisha upatikanaji wa maji ya kutosha katika Mji wa Mbinga.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jonas William Mbunda Mbunge wa Jimbo la Mbinga Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza ukarabati wa miundombinu chakavu katika Mji wa Mbinga. Kazi zinazoendelea ni pamoja na ukarabati wa mabomba ya maji umbali wa kilometa 21, ukarabati wa kitekeo cha maji Ndengu na ununuzi wa dira za maji 2,500 kwa ajili ya kuunganisha wateja wapya. Utekelezaji wa kazi hizo unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha wakazi wa Mji wa Mbinga wanapata huduma ya maji safi, salama na yenye kutosheleza, Serikali imekamilisha usanifu wa Mradi wa Maji Mbinga utakaohusisha ujenzi wa vitekeo viwili vya maji, matenki matatu yenye jumla ya ujazo wa lita 450,000 na ulazaji wa mabomba umbali wa Kilometa 83. Utekelezaji wa mradi huo utafanyika katika mwaka wa fedha 2023/2024.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jonas William Mbunda, swali la nyongeza.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafsi ya kuuliza swali la nyongeza. Lakini pia nichukue nafasi hii kuishukuru sana Serikali kwa utekelezaji wa hiyo miradi. Pia nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi zake nzuri. Alifika Mbinga, na wakati huo amekuja kukagua vyanzo vya maji aliona hali halisi ya mahitaji ya maji katika Mji wa Mbinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali moja la nyongeza. Pamoja na Serikali kusema kwamba imeanza kufanya ukarabati kilometa 21 na kununua dira za maji 2,500 kiwango hiki bado ni kidogo. Nilitaka nijue, sasa Serikali ina mpango gani wa kuongeza fedha ili kuhakikisha kwamba ukarabati ule unaendelea katika Mji wa Mbinga? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge wa Mbinga kwa kazi kubwa na namna ambavyo anawapigania wananchi wake. Nataka nimhakikishie na ukisoma maandiko ya dini kwa maana ya Mathayo 7:7 yanasema: "Ombeni nanyi mtapewa, bisheni hodi nanyi mtafunguliwa."

Nataka nimhakikishie tutaiangalia Mbinga kwa namna ya pekee ili kuhakikisha wananchi wake wanapata maji. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Maji. Sasa unaweza kwenda kuketi.

Tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria. Swali la Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, litaulizwa na Mheshimiwa Rashid Shangazi.

Na. 279

**Mchakato wa kupata Katiba Mpya**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI K.n.y. MHE. USSI SALUM PONDEZA** aliuliza:-

Je, lini hatua iliyobakia katika mchakato wa kupata Katiba Mpya itakamilishwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu sasa swali la Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutambua umuhimu wa mchakato wa kupata katiba mpya aliunda kikosi kazi kilichoongozwa na Profesa Mukandara ambacho pamoja na masuala mengine, ilikuwa ni kuhuisha mchakato wa Katiba mpya. Katika hilo, kikosi kazi hicho kimetoa mapendekezo ya hatua sita za kufuatwa katika kukamilisha mchakato wa kupata Katiba Mpya. Hatua hizo ni hizi zifuatazo:

(i) Kuwepo kwa mjadala wa Kitaifa wa kupata muafaka wa masuala ya msingi;

(ii) Kuhuisha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba;

(iii) Kuundwa kwa Jopo la Wataalam wa kuandaa Rasimu ya Katiba;

(iv) Rasimu ya Katiba kupitishwa na Bunge;

(v) Kutoa elimu ya uraia; na

(vi) Rasimu ya Katiba kupigiwa kura na wananchi.

Mheshimiwa Spika, baada mapendekezo ya kikosi kazi, tarehe 6 Mei, 2023, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassani, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alimuagiza Msajili wa Vyama vya Siasa kuitisha Kikao Maalum cha Baraza la Vyama vya Siasa wakiwemo wadau mbalimbali kujadili mapendekezo ya kikosi kazi na kupendekeza taratibu za kuzingatia katika kuanzisha mchakato wa kupata Katiba mpya. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Rashid Shangazi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. pamoja na majibu ya Serikali, lakini nina maswali madogo mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kwenye mapendekezo ambayo ameyataja hapo sikuona suala zima la elimu kwa raia, kwa wananchi, kwa maana Katiba si mali ya wanasiasa pekee ni mali ya wananchi. Je, Serikali imejipangaje kuanzisha elimu japo kwa Katiba hii iliyopo ya mwaka 1977 ambayo wananchi wengi hawaifahamu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; wakati wa rasimu ya Mheshimiwa Warioba, mwaka 2012, mpaka sasa ni takribani miaka kumi na moja, wapo Watanzania ambao wakati ule walikuwa na umri mdogo na sasa wametimiza miaka 18.

Je, Serikali katika mapendekezo hayo itazingatia kwenda upya kutafuta maoni ya wananchi ili kujenga wigo mkubwa wa ukusanyaji wa maoni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Shangazi, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwanza kuhusu elimu kwamba, itolewe ya Katiba iliyopo. Serikali tumejipanga na ndio maana katika bajeti yetu ambayo tuliileta kwenu Waheshimiwa Wabunge tumeweka pia bajeti kwa kazi hiyo. Kwa hiyo Serikali tutatoa elimu ya Katiba iliyopo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, lakini pia Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Katiba hizi zote tutapeleka elimu kwa wananchi ili wazifahamu kabla mchakato huu haujaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, amependa kufahamu pia kama wananchi ambao kipindi kile cha rasimu ya Mheshimiwa Warioba hawakushiriki kutoa maoni yao kwa sababu ya umri, kama kipindi hiki watashirikishwa:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wote wa Tanzania watashirikishwa. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan kuona hili, ndio maana sasa mchakato huu unaanza ili na wale ambao hawakupata nafasi ya kutoa maoni yao basi na wao waweze kutoa maoni yao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la

nyongeza. Suala la Katiba Mpya ni kilio cha muda mrefu sana kwa Watanzania wote, tukiondolewa sisi wanasiasa. Ni lini Serikali italeta Sheria ya Vyama vya Siasa kuhakikisha hii Katiba Mpya tunapokwenda kwenye hilo tamko ambalo Rais ameliridhia, ataenda kulizungumzia na Watanzania wakafahamu, ni lini tunaanza na tutatumia mbinu gani na mipango gani ambayo Serikali imejipanga kuhakikisha Katiba hii inakuwa ya wananchi jumuishi na maoni yanachukuliwa kwa ujumla wake? Tunaomba *commitment* ya Serikali iseme itaanza lini na itatumia mbinu gani kuhakikisha Katiba hii inaenda kusimama upya tena?

**MWENYEKITI:** Nimemwona Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuungana na Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote ambao wamempongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Muungano wa Tanzania kwa kukubali sasa mapendekezo ya kikosi cha Baraza la Vyama vya Siasa na wadau wengine kuhakikisha tunaanza mchakato wa Katiba Mpya, ikiwa ni pamoja na kuhuisha na kutungwa kwa sheria zinazohusu uchaguzi hapa nchini Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba, kwa kuzingatia maelekezo ya Mheshimiwa Rais, tayari Baraza la Vyama vya Siasa linashirikiana na wadau mbalimbali na limeshaweka mpango kazi kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini na ofisi nyingine zinazohusika ili kuhakikisha kabla mwaka huu wa 2023 sheria

zote zinazohusu uchaguzi Bunge lako tukufu lipate nafasi ya kuzipitia, kuzitunga na kuzifanyia marekebisho kama itabidi kufanya hivyo. Kwa hiyo, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, Serikali imezingatia sana maoni hayo na tayari tumeshajipanga kwa utekelezaji wa mabadiliko ya sheria hizo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya swali hilo.

**JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Mwongozo wa Spika, kutoka wapi?

Enhee, Mheshimiwa Jesca Msambatavangu.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapema hii leo niliuliza Swali Namba 264 na nikapata majibu ya Serikali kwa swali la msingi, lakini sijapata majibu ya Serikali kwa swali langu la nyongeza la kwanza na la pili. Naomba Mwongozo wa Kiti chako.

**MWENYEKITI:** Ahsante. nani mwingine Mwongozo wa Spika. Mheshimiwa Chege.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Kanuni ya 76, kwa sababu ya muda tu, naomba niendelee. Wakati wa Kipindi cha Maswali na Majibu, wakati Serikali

ikijibu swali namba 275 la Mheshimiwa Waitara pamoja na majibu ya Serikali, Mbunge alioneshwa kutokuridhishwa na majibu ya Serikali na ikapelekea yale yaliyotokea. Naamini wote Waheshimiwa Wabunge na Kiti chako mmeliona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo tunaweza tusiwe upande wowote kwa sababu yale ni majibu ya Serikali, lakini yule ni Mbunge aliyekuwa anauliza kuhusiana na sintofahamu inayoendelea ndani ya jimbo lake. Mwongozo wangu ningetamani Kiti chako kituelezee kwa yale yaliyotokea kwa Mheshimiwa Mbunge kutokuridhishwa na yaliyotokea ambayo kimsingi sisi kama Wabunge tunadhani imeleta taharuki ndani ya Bunge na haijawahi kutokea tangu tumeanza Bunge hili. Ni mara yangu ya kwanza, lakini kwa mara ya kwanza nimeona taharuki hii iliyokuwa inaendelea ndani ya Bunge kuhusiana na Mbunge kwanza kutokuridhishwa, lakini na yale mengine yaliyoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nipate mwongozo wako kama hili lililotokea kutokana na majibu ya Serikali ni sahihi? Kama sio sahihi nini Mwongozo wako ili kama majibu yale yaliyotolewa na Serikali hayakuwa sawasawa, nini Mwongozo wako upande wa Mbunge na nini ambacho unaweza ukaongoza, Kiti chako kituongoze katika hili lililotokea ndani ya Bunge, ili Mbunge huyu na yeye aweze kupata haki yake, lakini upande wa Serikali nayo kama Serikali yetu ya Chama Cha Mapinduzi nayo tuilinde ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nipate Mwongozo wako, je, hili jambo lililotokea pamoja na kwamba, mimi siye Mbunge niliyekuwa nahusika, lakini kwa sababu limetokea ndani ya Bunge hili ni vyema kiti chako kikatoa maelekezo na maelezo sahihi ili tupate *standard* ambayo iko sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, wamesimama Waheshimiwa Wabunge wawili wawili wakihitaji miongozo, Mheshimiwa Jesca Msambatavangu hoja yake ni kwamba, maswali yake ya nyongeza hayakujibiwa ipasavyo, lakini pia Mheshimiwa Jafari Chege hoja yake ni kwenye Swali Namba 275 ambalo liliulizwa na Mheshimiwa Waitara. Sasa wanataka kufahamu, je, mambo haya yanaruhusiwa ama hayaruhusiwi, kwa mujibu wa Kanuni yetu Namba 76?

Kwanza ukienda kwenye Kanuni namba 53(1), (2), (3) na (4) inaainisha maswali kujibiwa kikamilifu. Sasa tutapata fursa kupitia kama je, jibu la Mheshimiwa Mbunge Jesca Msambatavangu la Nyongeza halikujibiwa kama alivyoeleza halafu Kiti kitatoa Mwongozo.

Pili, tutapata fursa pia ya kupitia hoja ya Mheshimiwa Chege ambayo ndani yake inaonesha Mbunge hakuridhika. Pia kama kilichofanyika baada ya kutokuridhishwa kama kinaruhusiwa au hakiruhusiwi, baada ya hapo Kiti kitatoa Mwongozo.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa Maswali na Majibu na hapa ninayo matangazo kadhaa. Nitaanza na matangazo kutoka Ofisi ya Katibu wa Bunge; la kwanza, Katibu wa Bunge anasema, naomba uwatangazie Wabunge wote kuwa Wizara ya Afya itaendesha semina kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Bohari ya Dawa *(MSD),* Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF),* pamoja na mafunzo kuhusu afya ya akili. Kwa hiyo, tunawaomba Waheshimiwa Wabunge msikose semina hii muhimu kwa sababu, inahusisha pia afya ya akili.

Semina hii itafanyika leo siku ya Jumanne, tarehe 9 Mei, 2023 mara baada ya kusitisha Shughuli za Bunge, saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Waheshimiwa

Wabunge wote mnakaribishwa kuhudhuria semina hii muhimu yenye lengo la kuwajengea uelewa kuhusu utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya taasisi hizi.

Tangazo la pili anasema; naomba uwatangazie Wabunge wote kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, itaendesha semina kuhusu Mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 na Mitaala ya Elimu, ili kuwajengea uelewa kuhusu taarifa ya mapitio, hatua iliyofikiwa, pamoja na kupata maoni na ushauri wao. Semina hii itafanyika siku ya Jumatano, tarehe 10 Mei, 2023, mara baada ya kusitisha Shughuli za Bunge, saa 7.00 mchana katika ukumbi wa Pius Msekwa. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kuhudhuria semina hii muhimu kwa mustakabali wa elimu nchini.

Tangazo la tatu ni Wageni waliopo Bungeni leo:-

Wageni waliopo Bungeni asubuhi ya leo, kundi la kwanza ni wageni walioko Jukwaa la Spika; moja ni wageni wa Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana, Mbunge, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao ni Ndugu Aditia Kurana ambaye ni *Mr. World* na muigizaji kutoka India, karibu sana Ndugu Kurana; na wa pili ni Ndugu Mohamed Latif, mwanzilishi wa *International Iconic Award* kutoka India. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tunao wageni, wageni hawa wamekuja na Tuzo ya Mheshimiwa Rais ya Masuala ya Utalii na Mazingira. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana ni wadau wa filamu ambao ni moja Dkt. Ghyabo Kilonzo, Katibu Mtendaji wa Bodi ya Filamu Tanzania; pili ni Ndugu Vinod Mishra, muandaaji wa Filamu ya *The Green Tanzanite* kutoka India; tatu ni Ndugu Salman Vamla, muigizaji wa Filamu ya *The Green Tanzanite* kutoka India na nne ni Ndugu Ignas Mkindi, muongozaji wa Filamu ya *The*

*Green Tanzanite* Kutoka India. Wamesimama wote kwa pamoja na mwingine ni Mheshimiwa Samwel Malugu, Mkurugenzi wa *Miss Jungle International,* karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni watano wa Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana, ambao ni Wajumbe wa *Miss Jungle International* kutoka Jijini Dar-es-Salaam, wageni watano, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Pia tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambao ni:-

Wageni tisa wa Mheshimiwa Godfrey Kasekenya, ambaye ni Naibu Waziri wa Ujenzi ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, wanatokea Ileje Mkoani Songwe, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Ali Makoa, ambao ni watoto wa rafiki yake *Bishop* Dkt. Mmanga kutoka Kinondoni, Mkoa wa Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Benaya Kapinga, ambao ni wapiga kura wake kutika Jimbo la Mbinga, Mkoa wa Ruvuma, ambao ni Ndugu Angelus Mbilinyi na Ndugu Abel Mbilinyi, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 35 wa Mheshimiwa Luhaga Mpina, ambao ni wafugaji kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Mrida Mshota, karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Michael Mwakamo, ambaye ni mtumishi kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, Mkoani Pwani, Ndugu Shedrack Oswald, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni 28 wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, Mbunge, ambao ni wanakwaya wa *Bible Study* kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 26 wa Mheshimiwa Anna Lupembe, Mbunge, ambao ni Wanamaombi kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 30 wa Mheshimiwa Antipas Mgungusi, ambao ni Mawakala na Wasambazaji wa Pembejeo za Kilimo kutoka mikoa mbalimbali Tanzania, ahsante sana. *(Makofi)*

Pia tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi wanne na walimu wawili kutoka Taasisi ya Uhasibu Tanzania, wakiongozwa na Ndugu Kamili Rutabingwa, karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 100 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM),* karibuni sana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2023/2024**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na majadiliano, Wizara ya Kilimo na tunao wachangiaji hapa. Mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa ni Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, akifuatiwa na Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, ambaye anajiandaa.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi na kuwa mchangiaji wa kwanza siku hii ya leo. Jimbo la Mbinga Vijijini, kama inavyotamkwa vijijini ni wakulima. Kwa niaba ya wakulima wote na mimi mwenyewe ni mkulima wa Mbinga, tunaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita kwa mpango ule wa mbolea za ruzuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbinga bila mbolea hatuvuni. Mwaka uliotangulia kabla ya msimu huu tulipata shida sana kupata mbolea, lakini tunaishukuru Serikali, tunamshukuru Mheshimiwa Waziri, tunamshukuru Naibu Waziri, kwa mpango huu wa ruzuku ya mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu hii kupitia hizi mbolea za ruzuku kila mkulima alipata mbolea na amelima vizuri, shida ndogo tu kwamba mbolea hizi awamu hii kwa sababu ulikuwa ni mpango wa awamu ya kwanza haukufika kwa wakati, kulikuwa na ucheleweshaji wa baadhi ya mbolea. Kwa hiyo, ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri kwamba msimu huu unaokuja, najua mpango huu bado upo, nimepitia kwenye bajeti, lile lililotokea msimu uliopita basi tusilione safari hii.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na shida ya baadhi ya mbolea, mbolea za ya *CAN* na *SA* hazikuwa zinapatikana, kama zinapatikana basi ni kwa shida sana, ninashukuru ulinialika kwenye kikao chako cha maandalizi ya msimu ujao kupitia watu wa *TFS* na wale wengine wanaoagiza hizi mbolea, nimeona maandalizi yanakwenda vizuri. Hivyo, Mheshimiwa Waziri ninakuomba na ninakuamini sana, uko vizuri kwenye kupanga na kusimamia, msimu huu ile mipango niliyoishuhudia kwa watu wa *TFC* basi isimamie vizuri kusiwe tena na wimbi la wananchi kulalamikia baadhi ya mbolea kutopatikana ndani ya nchi yetu. Hili nina uhakika Mheshimiwa Waziri utalitekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la ushirika. Ni ukweli kabisa umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu. Nimesikiliza baadhi ya michango jana, watu wanasema tuachane na ushirika tukaribishe mnunuzi mmoja mmoja. Kwetu Mbinga habari hiyo ya kuachana na ushirika hatuitaki, tunajua wanunuzi hawa wana nia tofauti tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mfanyabiashara mwenye lengo la kumsaidia mkulima, hayupo. Mfanyabiashara yeyote anayefanya biashara nia yake ya kwanza ni kupata faida, kwa hiyo hatakuwa na nia ya kuwasaidia wakulima, lakini wakulima hawa wakiwa pamoja ninajua watajenga nguvu ya pamoja na watauza kwa pamoja, watauza kwa bei nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anaweza akaja mfanyabiashara mmoja akajifanya ananunua vizuri kwa mtu mmoja rafiki yake, akapandisha bei ataenda ku-*substitute* kwa wakulima wengi kwa kununua bei ya chini. Kwa hiyo, najua kuna matatizo kwenye ushirika, lengo hapa liwe kuboresha siyo kwenda kubomoa kabisa na kwamba tuanze upya, hapana. Hata mimi mambo yangu hayajawa vizuri sana kwenye ushirika lakini nashukuru vyama vingi msimu huu uliopita vimelipa vizuri, vichache havijalipa, nami najua kwa nini havijalipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ushirika hapa upo utaratibu wa hizi *AMCOS* kukopa kwenye mabenki. Hapa Mheshimiwa Waziri mimi nikushauri kwamba utaratibu huu ulisumbua sana kwenye korosho, kwamba *AMCOS* inakwenda kukopa halafu inakuja kuwalipa wakulima malipo ya awali, inalipa malipo ya pili na inalipa malipo kule kwenye korosho walikuwa wanaita majaliwa. Ilikuwa ni shida sana kwa wakulima hawa kulipwa malipo ya pili na yale ya majaliwa, lakini malipo ya awali kwa sababu wanakwenda kuchukua benki wanalipa, ikifika yale ya pili ni ngumu sana kulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ninakuomba korosho sasa hivi wanalipa kwa mkupuo, mkulima akipeleka korosho zake kwenye *AMCOS* zikaja zikauzwa analipwa malipo yake yote, sasa hivi hakuna kelele, lakini huu mfumo wa benki kuruhusu *AMCOS* ikakope waje walipe mara ya kwanza, waje walipe mara ya pili, fedha zote zinaishia kulipa kwenye benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitolee mfano Mahenge *AMCOS* ni chama kizuri sana lakini kimeshindwa kulipa malipo ya pili hata mkulima mmoja, milioni zaidi ya 89 wanadaiwa, hawajamlipa hata mkulima mmoja. Siyo kwamba hawana uwezo, walikusanya mazao wakauza kwa milioni 480 lakini huku nyuma kwa sababu walikopa benki milioni 500 ikabidi malipo yale yote yaingie benki na wakulima sasa hawajalipwa, wanabaki wanalalamika mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nikuombe, vyama vile ambavyo vinalipa malipo kwa mkupuo safari hii hawana kelele, lakini vyama vile ambavyo vimeenda kukopa benki halafu wakalipa malipo ya awali halafu wanakuja walipe tena malipo ya pili wengi wamepata matatizo kwa sababu kiasi wanachouza kinakwenda kuishia kulipa benki. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ninakuomba sana toa kauli vyama hivi vilipe kwa mkupuo, hatutakuwa na shida wala malalamiko kama yale waliyosema Songwe, nasi Mbinga tutakuwa na furaha zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, mwaka jana au mwaka juzi tulisherehekea hapa kwa kauli ya Waziri Mkuu ya kupunguza makato kwenye kahawa. Sasa hivi karibuni msimu huu ulioisha Mheshimiwa Waziri mmeweka makato pale ya shilingi 200 kwa kilo bila makubaliano na mkulima, ninakuomba utakapokuja hapa utoe ufafanuzi yale makato kwa nini umeyaweka, yana manufaa gani kwa mkulima na kwa nini akatwe mkulima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kama huku tunapunguza kwa nini huku tena tunaongeza kwa njia nyingine? wakulima wangu wanalalamikia sana hilo. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri utakapokuja hapa utoe majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, hivi kwa nini kwenye vikao hivi vya wadau wa kahawa hamuwaaliki Wabunge…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Benaya Kapinga.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** …ambao ndiyo wanapokea kero zote za wakulima?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, muda wako umekwisha.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja lakini ninaomba Waziri ujibu haya maswali niliyokuuliza hapa mwisho, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ni dakika nane na kwa kuwa wachangiaji ni wengi hatutazidisha hata sekunde moja. Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, nilimuita Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, wakati huo Mheshimiwa Anne Kilango Malecela anajiandaa.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa nafasi hii ambayo umenipa. Kabla sijanza kuchangia nianze kwa kuunga mkono

hoja kwa sababu hii hoja ni hoja kubwa, Wizara ambayo inashika wananchi wote wa kawaida na tumekuwa tukisema kilimo ni uti wa mgongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Bashe, naomba nianze kwa masikitiko kuonesha kwamba mimi msimu wa kilimo uliopita kwenye Wilaya ya Uvinza, Jimbo la Kigoma Kusini sikupata mbolea kabisa. Mheshimiwa Bashe tulikutana pale *airport Dodoma* nikakueleza jambo hili, ulinifahamisha kwamba mbolea ilikwenda pale Nguruka lakini baadae mbolea ile iliondolewa, ni kweli nilifuatilia mbolea ile iliondolewa. Sababu ya kuondolewa mimi sikuwa naijua, kwa hiyo naomba sana Mheshimiwa Bashe kwa kweli msimu huu wa kilimo naomba unikumbuke Wilaya ya Uvinza kwa sababu ni Wilaya ambayo kwa kweli inajishughulisha kwa kilimo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto iliyopo ya mifugo kwa sababu mifugo inapingana na kilimo, wenzetu wale wa mifugo hata mahindi, hata muhogo, chochote kinacholimwa na binadamu wao wanasema ni majani pia, kwa hiyo wanafyeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilete masikitiko yangu kwa mara ya kwanza, nadhani kwenye Wilaya zote msimu uliopita nimepata njaa kwa sababu debe la mahindi lilifika shilingi 30,000. Nilimuona Naibu Waziri kujaribu kuona na mimi nipelekewe mahindi kwenye Wilaya yangu lakini masharti aliyonipa ni kwamba Mkuu wa Wilaya aandike barua. Ni kweli Mkuu wa Wilaya nilimwambia aandike barua lakini sijui kama barua iliandikwa na ikaja. Kwa sababu tatizo ni kwamba Mkoa wa Kigoma ni Mkoa ambao haujawahi kuingia kwenye njaa tangu tumepata uhuru. Sasa nadhani Serikali walipata kigugumizi kuandika barua kwamba Mkoa wa Kigoma una njaa, kwa maana ya Wilaya ya Uvinza, lakini wananchi wangu kwa kweli walipata shida sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu ruzuku ya mbolea ya tumbaku. Wenzangu wamezungumza sana, tumbaku ni kilimo. Kwa nini tumbaku isiwekewe na yenyewe mfumo wa kupata ruzuku ya mbolea, kwa sababu ni kilimo. Naomba sana kwenye jambo hili kwa sababu Wilaya yangu pale Nguruka wanalima sana kilimo cha tumbaku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri lingine ni kwenye eneo la mbegu ya mchikichi. Mheshimiwa Waziri Mkuu amepambana kuhakikisha kwamba Mkoa wa Kigoma unakuwa miongoni mwa mikoa ambayo inazalisha chikichi kwa wingi kwa sababu kwa kweli kimsingi ndiyo Mkoa ambao una historia na chikichi, kwa bahati mbaya sana pamoja na juhudi za Serikali mbegu hizi bado. Kwa sababu mimi mwaka jana niliomba miche 7,500 kwa sababu mimi nina shamba la ekari 200, kwa kuzingatia kwamba ekari moja ni miche 58, niliomba nipatiwe 7,500 sikupata, niliambulia miche 1,000, unaweza kuona kwamba bado.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili Mheshimiwa Bashe lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba chikichi pamoja na alizeti yanakuwa ni mazao ambayo ni mkombozi ili tuweze kupata mafuta sisi wenyewe wananchi kwa maana ya nchi yetu ili tupunguze fedha ambayo inatumika kuagiza mafuta nje, bado Mheshimiwa Bashe wananchi hawa ni kweli wana vishamba vidogovidogo, nakuomba sana. Mpango wa kuhakikisha unapata wawekezaji kwa ajili ya zao hili kama ambavyo Serikali imekuwa ikihakikisha inashawishi wawekezaji kuweza kuchukua maeneo kwa ajili ya kilimo cha miwa ili tuweze kupata sukari na kwenye eneo hili naomba sana Mheshimiwa Bashe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi tukiwategemea sana uwezo wao ni mdogo. Utawapa miche lakini uwezo wa kifedha wa kulima na kupalilia hawana. Kwa hiyo kwenye eneo hili naomba sana Mheshimiwa uone namna ya kuweka wawekezaji waje kuwekeza kwa ajili ya kilimo ili sasa hawa

ambao ni wakulima wadogo waweze kuuza kwa hao wawekezaji ambao nao najua lazima kutakuwa na viwanda vikubwa kwa ajili ya kuchakata hayo mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo jingine ni eneo la kilimo cha umwagiliaji. Mimi nashukuru mwaka 2016 jimbo langu lilipata bilioni mbili kwa ajili ya skimu za umwagiliaji, lakini kwa bahati mbaya sana Mheshimiwa Bashe, skimu hizo zilikwenda kujengwa kwenye mashamba ya watu, hili ni jambo la kusikitisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, skimu ya Kalya…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Bidyanguze kwa mchango wako, na muda wako umekwisha.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimuita Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, wakati huo Mheshimiwa Halima Mdee pamoja na Mheshimiwa Kaboyoka wanajiandaa.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa jinsi ambavyo ametujalia amani kwenye nchi yetu ya Tanzania jamani, kwa sababu tuangalie hali halisi ya ulimwengu lakini Tanzania Mungu ametubariki mpaka leo nchi yetu imekaa vizuri. Pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuzungumza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Bashe na Mheshimiwa Naibu Waziri wake, tunakiri kwamba hawa ni Mawaziri vijana, wanafanya kazi vizuri na kikubwa ni wasikivu, wanapokea simu zetu, wanashirikiana na sisi, naomba niseme nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie dakika zangu nane vizuri. Kwanza naomba niipongeze Serikali ya Awamu ya Sita kwa kujitofautisha. Awamu ya Sita inayoongozwa na Mama Samia Suluhu Hassan imejitofautisha sana kiutendaji upande wa kilimo. Kwa nini nasema hivi? Tanzania nzima tuna Majimbo ya uchaguzi 264, katika Majimbo hayo, Tanzania Bara yako Majimbo 214, Tanzania Zanzibar yako Majimbo 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kidogo niongee upande wa Majimbo 214 ya Tanzania Bara. Haya Majimbo 214, Majimbo 188 ni Majimbo ya Vijijini na Majimbo ya Vijijini ni Majimbo ya wakulima. Kwa nini nilikuwa nasema Awamu ya Sita imejitofautisha. Rais Samia Suluhu Hassan amefanya kitu kikubwa sana kutuletea pesa za kutosha za barabara za *TARURA*. Tulipopata pesa za kutosha kwenye barabara za *TARURA* ina maana vijijini mazao yatatoka kwenda kwenye masoko makubwa kwa urahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme ukweli, mimi mazao yangu mengi yanatoka milimani. Tangawizi inatoka kwenye Tarafa mbili ambazo ni asilimia 70 ya Jimbo langu. Kule kulikuwa hakuna barabara. Walanguzi walikuwa wanafwata tangawizi milimani. Kwa hiyo wao walikuwa wanafaidi sana kilimo cha milimani pamoja na tambarare, lakini baada ya kupata pesa za kutosha za *TARURA* wananchi wangu sasa wanapeleka mazao yao kwenye masoko makubwa. Niipongeze sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Naona niishie hapo kwa hili la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije upande wa umwagiliaji. Mheshimiwa Waziri nakushukuru sana kwa kujali umwagiliaji kwenye Jimbo langu. Nitakushukuru halafu nitakuomba msaada. Mimi nina mazao mawili makubwa, tangawizi na mpunga. Tarafa mbili zinalima tangawizi, zinahitaji umwagiliaji. Nakushukuru sana Mheshimiwa Bashe, umeanza kuboresha umwagiliaji, umeanza na Kata mbili Kata ya Miamba na Kata ya Mpinji. Sasa naomba nikupe siri ambayo hujui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu Tarafa ya Mambavunda inategemea mto mkubwa unaitwa Mto wa Saseni ambako ndiyo mto huu unamwagilia tangawizi yote kule juu, lakini Mheshimiwa Waziri ule mto umeteremka ukaja mpaka Kihurio. Kihurio mto ule unalima mpunga, nikwambie ukweli ule mto sasa hivi umekwisha, umeharibika upande wa huku tambarare. Wananchi wa Kihurio wanalima mpunga, wananchi wa Kalemawe wanalima mpunga, ule Mto wa Saseni umebomoka lakini siyo wa kutengenezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Same. Ninakuomba Mheshimiwa Waziri, kwa sababu umeshakuja Jimboni kwangu usije wewe aje Mheshimiwa Mavunde, auone Mto wa Saseni ili aje akueleze muuboreshe Mto Saseni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme ukweli Kata ya Kihurio ndipo nilipozaliwa mimi. Sisi ni wakulima wa mpunga, tangu nimekuwa mtoto mdogo mpaka sasa bila ya Mto Saseni hakuna Kihurio, hakuna Kalemawe. Naomba Serikali mje muone mto muuboreshe Mto Saseni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia upande wa mbolea ya ruzuku. Nakiri Waheshimiwa mmeliongea hili lakini na mimi niongelee kwa upande wangu. Mheshimiwa nakushukuru sana, mbolea ya ruzuku nilikusumbua kwelikweli na hukuchoka kupokea simu zangu. Ulipokea simu zangu na ulinisaidia, lakini nikwambie ukweli; kwanza naipongeza

Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan kutoa ruzuku asilimia 50 ni mara ya kwanza inatokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatokea mara ya kwanza mfuko unaonunuliwa kwa shilingi 140,000, mwananchi anaununua kwa shilingi 70,000. Tumpongeze Rais, amefanya kitu kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikiri kwamba kuanzia tarehe 21/12/2022 mpaka tarehe 21/1/2023, nikiri nilipokea mbolea ya ruzuku mifuko 4,240 ambazo ni tani 212. Mheshimiwa Waziri nikwambie ambacho wenzangu wamekwambia, hii mbolea yote ilikwenda Kata ya Ndungu. Kata ya Ndungu ni Tarafa ya Ndungu. Kwa hiyo, wananchi wa Tarafa za Milimani zote walikuwa wanakuja Kata ya Ndungu. Nashukuru, nakupongeza, umeanza vizuri, lakini changamoto ya kwamba haikufikia wananchi wengi ni kubwa sana.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, lakini hili mlisahihishe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Nilimwita Mheshimiwa Halima Mdee, wakati huo Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka na Mheshimiwa Jafari Wambura Chege anajianda. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mwaka 2022 tulipokuwa tukijadili Wizara ya Ardhi, moja kati ya mjadala mkubwa ni kwamba nchi yetu mpaka sasa haina mpango wa matumizi bora wa ardhi uliokamilika. Mwaka jana 2022 tulikuwa tunapigana hapa kuomba Tume

ya Taifa ya Mipango ipate Shilingi bilioni 10 tu ili ifanye mipango tujue ardhi ya kilimo na ardhi ya wafugaji, ili tuweze kuepukana na migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu Waziri wa Kilimo ambaye hana dhamana kwenye masuala ya ardhi, ana jukumu la kugawa hekta milioni moja za ardhi ya nchi hii wakati hatuna taarifa za hali ya ardhi ikoje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zote nasema, tuangalie kizazi kinachokuja, tusiangalie sasa. Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yako unasema, 2050 tutakuwa na Watanzania milioni 136 kutoka milioni 61 ya sasa hivi. Tunapozungumza sensa ya makazi, asilimia 44 ni ya watoto chini ya miaka 18; sijazungumza chini ya miaka 21, sijazungumza chini ya miaka 35. *We have a very young generation*. Tunagawiana ardhi. Sipingi vijana kupata ardhi, napinga *concept* ya Wizara kutafuta wakulima kama ambavyo tunatafuta ma-*nurse* na walimu. Ndiyo shida yangu kubwa na ninyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kwa sababu, hata hayo mashamba yenyewe, nilisoma tangazo lenu, hizo *block farms* bila kuwa na mwekezaji mkubwa, hii *program* haiwezi ku-*take off;* kwa mujibu wa tangazo lenu na kwa maelezo yenu. Unahitaji mwekezaji mkubwa ambaye atapewa kuanzia heka 1,000 mpaka 20,000 na vijana wetu ambao watapewa kuanzia hekta moja mpaka hekta 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasikitika kwa sababu, Waziri anasema, katika hizi hekta milioni moja atakazozigawa, wastani wa kusafisha hekta moja ni shilingi 16,800,000; kusafisha, kusawazisha udongo, kuweka miundombinu ya umwagiliaji. Hapa tuna wakulima. Hivi kweli mkulima anaweza kusafisha heka moja, kusawazisha kwa Shilingi milioni 16 na kuweka miundombinu ya umwagiliaji? Mheshimiwa Waziri anasema mpaka 2025 – 2030 wanatarijia

kutumia Shilingi trilioni 16.8. Hiki ni kilimo cha *iPad,* hiki ni kilimo cha mjini. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza kusaidia nchi. Mheshimiwa Mama Kilango anazungumza vizuri hapa. Majimbo 188 ni ya wakulima, tena wakulima wanaolisha nchi hii ni wakulima wadogo wadogo, wanasaidia 26 *percent* ya *GDP* ya nchi hii miaka yote. Hivyo, tujiulize basi, Mheshimiwa Bashe, kama ni wakulima wadogo *given the fact* kwamba Tanzania ni *young generation*, vijana wakulima wako kule; wakike wakiume wako kule. *I can assure you my friend,* najua *you guys are working hard,* lakini lazima tushauriane. Hii Shilingi trilioni 16 mkienda mki i-*pump in* kwa wakulima tuliokuwanao, *I can assure you GDP* ita-*move from 26 to 50 even to 60 percent*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikiliza. *I am very disappointed!* Tusifanye kilimo cha *politics*, tusifanye kilicho cha kusema tunaangalia uchaguzi 2025. Tufanye kilimo kwa kuangalia *the coming generation*. Mheshimiwa Bashe nakuomba, hao watoto wa watu hapa umeshawakusanya, ndiyo hivyo, umeshawapa matumaini, huna namna. Ninachokisema ni hivi, hii tuitumie tu kama *case study,* kuwamba ngoma, ndiyo imeshapanuka hivyo, huwezi kuwakatisha tamaa, lakini kuanzia mwaka ujao wa fedha 2023/2024 tunataka utuambie ni kwa namna gani hayo mafungu mengine yaliyobaki mnaenda ku-*inject* kwa wakulima wadogo tuliokuwanao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni akili ya kawaida! Nasikia Wabunge wenzangu hapa wanashukuru ruzuku, hivi unafikiri wakulima wetu wangekuwa na hela wangekuwa na njaa ya mbolea? *Poor commonsense!* Yaani tuko hapa, kila mtu anashukuru eti ruzuku, sijui kimeenda, kimerudi, ruzuku hiyo ni ya mbolea, *for God's sake, that is poverty! That is poverty!* Kwa hiyo, tunafurahia wakulima wetu waendelee kuwa masikini halafu tunakuja kuwapa mbolea, halafu mbolea

zenyewe za Wazungu tunazoagiza huko kwa *billions of money. We should use our brains.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi, mmeanza hapa, mmeshaita Watoto, mmeshawakusanya huko, sawa hao wapoozeni. Mwaka ujao wa bajeti tunataka tuambiwe mnawasaidiaje wakulima wadogo wa nchi hii? Mheshimiwa Bashe, kingine, hivi mazao ya kimkakati ya nchi hii ya kutuingizia *foreign currency* ni vipi? Huwezi kuridhisha kila mtu *my friend.* Wamezungumza juzi hapa, wamesema ngano kila mwaka *more than five hundred billion* tunatumia; na sita nimesoma ripoti ya *CAG* ya ufanisi kwa miaka minne tumetumia 2.7 *trillion* kuagiza nje. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, parachichi, *OUSB* na *FAO* wanasema, *by twenty thirty* thamani ya soko la parachichi duniani ni *fourteen trillion*. Bashe, nchi hii ina mikoa zaidi ya nane, inalima parachichi tena inayotakiwa Ulaya huko, inayotakiwa Asia huko. *Why aren't you using common sense? This is fourteen trillion,* tungeenda kuwasaidia wakulima wa parachichi, wakulima wa ngano, wakulima sijui kwenye maeneo *strategic,* nchi ingepata fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme tu ndugu yangu, *we should think of the next generation*. Unagawa hekta milioni moja, hivi ninyi mnajua hekta milioni moja! Hivi mnazijua, ama ni kwa sababu huko Wizarani hakuna wakulima! Kenya kwa parachichi pekee, kwa sababu Kenya ndio *a leading country* kwa ku-*export* parachichi kwa Afrika. *eighty five percent* ya *export* za parachichi zinachangiwa na wakulima wadogo wa Kenya. *The remaining fifteen percent* ndio wakulima wakubwa. Kwa hiyo, ni vizuri kuwa na wakulima wakubwa, lakini tusijipe utumwa wa wakulima wakubwa, tusaidie wakulima wetu, nchi itasogea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee, ahsante sana kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka aweze kuchangia. *(Makofi)*

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika bajeti hii ya Wizara ya Kilimo. Baada ya Mheshimiwa Halima kuongea, sauti yangu itaonekana imepwaya sana, lakini mnisikilize tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nami niungane na Wabunge wenzangu kwa kumpongeza Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri ambayo ameifanya ya kuipaisha nchi yetu mpaka sasa hivi hata Kimataifa tunajulikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, maana najua nina muda mfupi sana, nimwambie tu Waziri Bashe, kweli tunapenda mambo ya *block farming,* lakini isiwe *to the expense* ya wakulima wadogo. *That is one. But two,* tujue kwamba *block farming* inahitaji umwagiliaji sana, na umwagiliaji huo uwe wa *drip* au wa *system* gani, ambao hautaleta *siltation*. Tuangalie basi tume yetu ya umwagiliji kama ina *capacity* hiyo ya kuchukua hii *role* ya kufanya hii *block farming* na hii *programme* ya *BBT* kufanikiwa

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia ripoti ya *CAG* ya ukaguzi wa kiufundi, 2018/2019 mpaka Januari 2019/2020 – 2022/2023, inaonesha upungufu mwingi ambao uko kwenye tume yetu hii ya umwagiliaji. Nitasema machache tu ambayo ni *key* kwa ajili ya *argument* yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, tume hii haifanyi upembuzi yakinifu kabla ya kuanza ujenzi wa miradi ya umwagiliaji. Hii tunaweza kusema kwamba tangu mradi

ukianza umeshakufa kabla hata haujasimama. Pili, kuna udhaifu mkubwa kwenye kuzingatia Sheria ya Manunuzi. Maana yake ni nini? Fedha ya umma itatumika vibaya sana kama Sheria ya Manunuzi haifuatwi. Tatu, hii Tume ya Umwagiliaji haifanyi uhakiki wa viwango vya ubora wa miradi, na hivyo miradi mingi imeonekana ina kasoro sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kuna miradi ambayo imekuwa ikichelewa sana kukabidhiwa, na hivyo inaongeza gharama katika kuendelea kutekeleza. Haya yote yanafanya tujiulize, hivi tunapoenda kwenye kufanya *block farming* na kama tume yenyewe ndiyo hii hii, na jinsi inavyo-*operate* ni hivi hivi, kweli tunategemea mafanikio? Kama Mheshimiwa Halima alivyosema, kwamba hizi fedha nyingi ambazo zinaenda kwenye miradi hii ambayo tunaona kuna upungufu sana katika hii tume ambayo ndiyo tunaitegemea, zingekwenda kusaidia wakulima wadogo wenye skimu zao kutengeneza vizuri, nafikiri tungefanya mazuri zaidi, maana naona hatujajipanga vizuri kuhusu *block farming*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, linalonisikitisha kubwa zaidi, tukiangalia pia upungufu huo, kwenye bajeti ya Tume ya Umwagiliaji kwa mwaka wa fedha 2022/2023 iliidhinishwa shilingi bilioni 257.5 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji, lakini hadi kufikia Februari, 2023 ilikuwa imetolewa asilimia 18 tu ya fedha iliyotakiwa, yaani katika miezi minane ni shilingi bilioni 46.68 tu zilizokuwa zimetolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiingii akilini kwamba katika kipindi hiki cha robo mwaka kilichokuwa kimebaki, tume itaweza kutumia shilingi bilioni 210 wakati kwa miezi minane ilitumia tu shilingi bilioni 47. Kama hivyo ndivyo, hata huu mradi wa *block farming* nina mashaka sana kama utafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kwamba kweli wakulima wadogo wanahitaji kusadiwa sana, ukichukulia

mfano kama alivyosema Mbunge wa Same Mashariki. Kule kwetu miradi mingi ya mpunga ambayo ilisaidia sana kulisha Mkoa Tanga, Kilimanjaro na Arusha ilikuwa ni ya kilimo cha umwagiliaji. Ukiangalia kilimo cha umwagiliaji cha skimu ya Ndungu, mfereji wa fidia, Kalinga Maore na hizo za Kihurio zilizosemwa zote zilikuwa zinalisha mikoa hiyo mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu miradi hii imejengwa tangu mwaka 1999 imetelekezwa. Kwa mfano, mradi wa fidia wa Ndungu, sasa hivi mvua ikinyesha kubwa inakuwa ni shida kwa wakulima hao. Mradi uliojengwa kwa msaada wa kutoka Japani ambao hatukuweza hata kuuhudumia, leo mvua ikija ni mafuriko kwa kwenda mbele, mashamba yanaharibika, zile barabara zilizotengenezwa za kuingia mashambani zinaharibika. Matokeo yake, badala ya kuwa baraka, mvua inakuwa laana kwa wakulima wale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameomba wafanyiwe kitu kinaitwa kudebua mifereji ile. Nilishangaa kwamba kweli tume ilipeleka mitambo ile ya kudebua, lakini bila tume kuwasiliana na Halmashauri, ikitegemea Halmashauri itatoa Shilingi milioni 80 ikapeleka mashine ile, *equipments* zile, zikakaa mwezi mmoja na kitu bila kufanya kazi yoyote. Mwisho zikaondolewa. Kwa hiyo, ukiangalia usimamizi wa vyombo vyetu ni hafifu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiingii akilini kwamba unawezaje kutoa mitambo Dodoma uipeleke Ndungu ikae mwezi mzima na zaidi, *machine* iko pale yame ku *tide up,* wafanyakazi wako pale hawalipwi au watalipwa na hela ya Serikali, lakini kazi haifanyiki. Maana Shilingi milioni 80 Halmashauri haijatoa. Sasa hapo tunajiuliza, hivi kweli *are we serious? Are we serious* kwamba tunataka kulima kilimo kikubwa, lakini cha hawa wadogo ambao miaka yote hii ndiyo wametubeba, tumeshindwa kukilima!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia shirika letu la *NFRA* haliweki akiba ya mpunga au maharage au mbegu za alizeti, *at most* inaweka tu mahindi na nafaka nyingine inaitwa mtama. Sasa ukiangalia wananchi wengi wanakula wali, halafu *NFRA* haiweki hiyo kama akiba. Pamoja na upungufu uliyooneshwa jana, juu ya kwamba *NFRA* inakuwa na akiba ya kama siku tatu na nusu, hata huo mpunga haupo kwenye *list*. Sasa unajiuliza, hivi nchi yetu tunakwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kwamba Mheshimiwa Waziri hebu u-*rethink* kwamba hivi hii *BBT* kweli itafanikiwa kwa *approach* hii tunayokwendanayo? Tuko *too theoretical in the sense that BBT au block farming* inahitaji *a lot of mechanization*. Sasa hivi ukimchukua tu kijana uliyemchukua mtaani umfundishe miezi minne halafu umpe kazi kubwa kama hii *I don't think* kama tutafanikiwa. *I wish* tungechukua mashamba karibu na wenyeji wenyewe tukawa-*identify* wale vijana ambapo maeneo yale wanajihusisha na kilimo, wakapewa hiyo kazi, wakafundishwa, *because at least* wana *A, B, C* ya kilimo na itakuwa kwenye Mkoa ule au Wilaya ile. Kwa hiyo, hata kijana aki-*abscond,* wapo watakaoendeleza. Sasa tunawatoa Mikoa mingine, tunawapeleka mikoa mingine. Kesho hali yake ya kifedha imekuwa nzuri, anaamua kuacha lile shamba, unamfanya nini? Unamfanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, yangu ni hayo machache kwamba hebu *tu-rethink approach* ya hii *block farming* kwamba tumejiandaa vipi? Kwa gharama hizi zilizotajwa, kwa kweli sidhani kama ni *sustainable,* ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka. Nilimwita Mheshimiwa Jafari Chege, wakati huo Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota pamoja na Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka wanajiandaa.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nami nianze kwanza kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri aliyoifanya kwenye majimbo yetu, na pia kwa kukubali na kuridhia kuinua sekta ya Wizara hii ya Kilimo kwa kuiongezea fedha. Nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Mawaziri, watendaji wote, hasa Mkurugenzi wa Tume ya Umwagiliaji, ndugu yangu Raymond Mndolwa kwa namna ambavyo amejikita kuhakikisha angalau skimu mbalimbali ambazo zilikuwa ni mapendekezo ya Bunge zinaweza kufanyiwa kazi na zinatengewa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukurani hizi kipekee nichukue nafasi hii kukushukuru sana Mheshimiwa Waziri, nimeona kwenye bajeti ya mwaka huu, zipo *schemes* za wilayani kwangu Wilaya ya Rorya, kwa muda mrefu tumekuwa tukiziombea ziingie kwenye mpango mkakati na umeezingiza. Ikiwemo *scheme* ya Rabong nichukue nafasi kukushukuru, ikiwemo Chereche, Ryangubo, Rwang'enyi pamoja na *scheme* ya Mto Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani hizi Mheshimiwa Waziri, yapo mambo ambayo ningetamani nishauri kwa maana ya Mkoa wetu wa Mara. Mheshimiwa Waziri, utakubaliana na mimi pamoja na kwamba Mkoa huu ndio Mkoa anaotoka Muasisi wa Taifa hili, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, pamoja na kwamba mkoa huu ndio anaotoka Muasisi aliyekuwa anaAsisi sekta na Wizara unayoiongoza ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia utakubaliana na mimi kwamba Mkoa wa Mara ukiuzungumzia kwa sasa ni mkoa ambao hauna zao la kimkakati, hauna zao la kibiashara na ni mkoa ambao hata mazao yanayolimwa ya chakula haya-*sustain.* Ni mazao ambayo yanalimwa kwa ajili ya chakula cha kujilisha wenyewe na sio mazao yanayokwenda kwenye sekta kwa maana ya kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, nimekuwa nikishauri hapa ndani ya Bunge, sio kwamba tunapungukiwa baadhi ya mambo yanayoweza kutufanya na sisi tukawa na mazao ya kimkakati na mazao ya kibiashara kama ilivyo mikoa mingine. Nadhani ni uamuzi wa Wizara na *intervention* ya Serikali *a very serious interventions* ambayo inaweza ikatusaidia sisi kama mkoa kutupa *direction* ya namna njema ya kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mara utakubaliana na mimi Mheshimiwa Waziri, tuna zaidi ya hekta milioni mbili lakini tunazalisha hekta laki mbili mpaka laki tatu peke yake. Mazao tunayolima mengi yao ni mahindi na tukilima yale mazao ni mazao ya chakula peke yake. Hatulimi mazao kwa ajili ya kufanya kwa maana ya kujiinua kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia utakubaliana na mimi ni mkoa ambao tuna *irrigation scheme* zaidi ya 42, lakini zinazofanya kazi hazifiki hata 10 peke yake. Ni mkoa ambao umezungukwa na ziwa, kwa mfano wilayani kwangu asilimia 77 nimezungukwa na ziwa lakini hakuna mazao yanayolimwa ambayo unaweza ukasema haya ni mazao ya kibiashara ya kumkomboa mwananchi kwa ujumla wake na yakatangaza ule mkoa kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Mheshimiwa Waziri, katika ziara hizi unazozunguka, kwanza upe Mkoa wa Mara kipaumbele, tengeneza *a very serious intervention* ya kuja kwenye Mkoa wa Mara na kutengeneza ushauri kuona namna unavyoweza kukaa na wadau wa sekta ya kilimo na wananchi wanaofanya shughuli za kilimo ili kuinua mazao ya kibiashara ili leo tunaposimama sisi kama mkoa tuwe tuna zao la kibiashara tunalotambua kama mkoa, kuwe kuna zao la kimkakati lakini pia utengeneze *strategies* nzuri ya kuona namna unavyoweza kuwakwamua wakulima hawa wanaolima mazao madogo madogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niombe sana Mheshimiwa Waziri, hili ulione kwa jicho pana sana. Kwa sababu ukanda ule sisi Mkoa wa Mara ndio maana unaona hakuna tunachoweza kusimama. Siwezi kuzungumzia mbolea, siwezi kuzungumzia pembejeo na wakati hata kilimo kinachofanywa bado ni kidogo sana. Tunafanya *small scale agriculture* ambayo tungeweza kufanya *large scale* ili wananchi waweze kunufaika. Sasa nikuombe kwa kuwa umeanza kuzunguka maeneo mengi na haujafika Mkoa wa Mara, nikuombe uje *in a very serious* ili tukae tuweze kuona namna ambavyo tunaweza Kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba unafanya haya nikuombe Mheshimiwa Waziri, la kwanza kwenye zile *scheme* 46 pamoja na kwamba naona zimetengwa fedha lakini bado hazizidi *scheme* 10, nenda uone namna ambavyo zile *scheme* zote arobaini na kitu unavyoweza kuzipa fedha ziweze ku-*produce* ili wananchi waanze kulima kilimo cha biashara. Naona sasa *scheme* zinatumika kulima kilimo cha chakula peke yake. Pia, haya unayaweza naona maeneo mengine umekuwa ukifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, uone namna ya kutengeneza mahusianao mazuri ya *private sector* ili ziweze kuwekeza kwenye mazao ambayo yanweza yakai–*boost* kutenegeneza mazao ya kimkakati na mazao ya kibiashara na hili unaliweza kama ambavyo umekuwa ukifanya mikoa mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, utengeneze Mkoa wa Mara kuwe kuna soko rasmi la kuuza bidhaa. Leo sisi tunauza bidhaa zetu kwenye magulio na haya masoko ya kawaida. Hatuna soko rasmi ambalo wananchi wanauza bidhaa ambalo lita–*motivate* wananchi kuzalisha zaidi wakijua kuna mahali pa kuuza. Leo wakizal;isha inabidi wavuke waende Kenya kutafuta soko ambalo linaweza likawanufaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani sisi kama mkoa ungeweza kutengeneza namna nzuri ya kutengeneza soko zuri moja wapo katika ukanda ule. Kwa bahati nzuri ukanda wote wa ziwa hakuna soko kubwa ambalo linauza mazao ya chakula kwa ujumla wake. Ona namna mkoa ule kwa sababu uko mpakani uweze kutusaidia tuweze kupata masoko mazuri ya kuuza bidhaa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la nne, utakapokuwa umekuja ona namna ambayo tupate ghala la chakula ambalo litawafanya wakulima badala ya kuuza bei ya chini mazao yao wanapolima, waweze kuhifadhi wakisubiri bei nzuri ili na wao waendelee kutengeneza *motivation.* Pia, ninaamini kwa kufanya hivi utaweza kuwa *motivate* wakulima wengi pamoja na vijana ambao kimsingi wameamua kujiajiri kwenye sekta ya kilimo lakini hawana uwezo na hawana soko la uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine Mheshimiwa Waziri *in a very serious* kama nilivyosema, lazima utakaposimama hapa…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:**… leo utuambie katika ukanda ule ni zao gani la kibiashara ambalo umeweza kuainisha na zao la kimkakati kwenye mkoa mziama wa mara. Tunayo mazao tunayolima ambayo yanakubali ardhi ya upande ule, Kahawa inakubali, tumbaku inakubali, mkonge unakubali. Pamba imekuwa ikilimwa kwa muda mrefu na wewe ni shahidi, lakini haya mazao haya yamekufa kwenye Mkoa wa Mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani tukianza kuzungumza Mkoa wa Mara, hakuna zao tunalosimama nalo kama Mkoa. Sasa hatuwezi kwenda kwa *style* hii. Kama nilivyosema ni mkoa anaotoka muasisi ningetamani unavyosimama na

wewe Mheshimiwa Waziri, ujivunie Wizara unayoiongoza muasisi wa sekta uya kilimo ni Mwalimu Nyerere. Kwa hiyo, sisi tungeona Mkoa wa Mara, unatunyenyuaje kwenye sekta ya kilimo, kwenye maeneo yote na sio hivi tunavyozalisha kwenye mazao ya chakula peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazalisha mahindi tani laki mbili mpaka laki tatu kwa mwaka na wakati mahitaji ni zaidi ya tani 600,000 mpaka 700,000. Kwa hiyo, hata hiyo nusu yenyewe hatufiki hata hilo zao moja lenyewe hatuwezi kufika. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri,

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:**…utakapokuja kusimama jioni hapa uweke mpango mkakati wa namna utakavyokuwa kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, nakushukuru sana naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Chege kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani aweze kuchangia.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana niweze kupata nafasi hii ya kuchangia kwenye Wizara hii ya kilimo, Wizara muhimu sana kwa ustawi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt, Samia Suluhu Hassan na wasaidizi wake wote katika Wizara hii ya kilimo kwa sababu tangu ameingia madarakani ameonesha utashi wa moja kwa moja wa kumkomboa mkulima, kumuondoa mkulima wa kitanzania kutoka katika kuwa mtu ambae tunamtoa sadaka

pale ambapo tunapata changamoto bila kujali tunamuumiza kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda niende moja kwa moja kwenye ninachotaka kuzungumzia. Nitazungumzia huu mradi wa *BBT* au jenga kesho iliyo bora ambayo kimsingi inaangalia zaidi ushiriki wa vijana na wanawake katika kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Mbunge mwakilishi wa Vijana na nimeingia katika Bunge hili kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi na ahadi namba sita ya mwanachama yeyote wa Chama cha Mapinduzi, ni kujielimisha kwa kadri ya uwezo wangu na kutumia elimu yangu kwa maslahi ya wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, baada ya Mheshimiwa Bashe, kuja na jambo hili la Mradi huu wa *BBT* nilichukua jukumu la kujielimisha na kugundua jambo hili si jipya. Watu wengi waneweza kuona ndoto za Mheshimiwa Bashe na wasaidizi wake ni kama Ndoto za Alinacha au Hekaya za Abunuwas lakini sisi sio wa kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo hayo yalianza kufanyika katika Nchi ya Malaysia mwaka 1956, chini ya mradi ulioitwa *FELDA* au *Federal Land Development Authority*. Mradi huu kadri tunavyoongea leo unachangia asilimia 18 ya *GDP* ya nchi hii. Leo hii tunapozungumza ni moja ya mradi ambao unamiliki sekta kubwa sana ya uzalishaji katika nchi hiyo, ni mradi ambao umeifanya Malaysia iwepo katika nchi ambazo zinaongoza kwa uzalishaji wa *palm oil* duniani. Lakini ni mradi ambao umekwisha ondoka katika kupewa *grants* za Serikali na leo hii tunazungumza unapewa mikopo na Benki ya Dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Bashe, kwa sababu pamoja na uwepo wa

wimbi kubwa la watu wasio na imani na mradi huu hajarudi nyuma. Nimpongeze kwa sababu amechukua *initiative* ya kutuamini vijana na wanawake wa Kitanzania kwamba tukishikwa mkono na kuwezeshwa na Serikali, tunaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme nasikitishwa sana kwa sababu kama sisi Wabunge ambao ni wawakilishi na kwenye majimbo yetu tuna vijana, sensa iliyofanyika mwaka 2022, inaonesha zaidi ya asilimia 34 walioko katika nchi hii ni vijana lakini sisi Wabunge hatuwaamini vijana, nani atuamini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili si jipya na katika haya nina machache ya kushauri na ninaamini tukienda pamoja Mheshimiwa Bashe, Mheshimiwa Rais, pamoja na wasaidizi wao tunakwenda kufanikiwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala zima la *recruitment,* namna ambavyo vijana hawa wamepatikana. Yalitolewa matanzangazo na vijana waliomba kupitia mitandao na takwimu zinaonesha zaidi ya vijana 20,000 waliomba. Lakini wengi wa hawa walioomba wanatokea katika Jiji la Dar es salaam kuliko majiji mengine au mikoa mingine ya nchi hii. Hii inaonesha kwamba ilikuwa kama *survival for the fittest.* Watu wa Dar es salaam wana mtandao kwa karibu zaidi ndio maana wameweza kuomba wengi zaidi na kuchaguliwa kwa wingi zaidi. Kwa hiyo, nimuache Mheshimiwa Bashe na wasaoidizi wake, kipindi kijacho wanapokuja kuchukua vijana hawa wahakikishe wanawachukua vijana kwa namna ambayo itatoa fursa sawa kwa vijana wote wa nchi hii kuweza kuomba na kupata fursa hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee mimi niombe, mashamba haya yanapoanzishwa basi wajitahidi kuhakikisha kwamba yanaanzishwa katika kanda zote za nchi hii na hawa vijana wanapokuwa *posted* wawe *posted* katika Kanda zao. Tukiwapeleka mbali kama tunavyofanya sasa hivi

ina *risk* vijana kuweza kutelekeza mashamba yale na kurudi nyumbani pale mambo yanapokuwa magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana tuhakikishe kwamba tunakuwa na mashamba haya katika kanda mbalimbali lakini hata kule tusipoweza kuanzisha mashamba haya, basi tuanzishe vitalu nyumba ili tutoe fursa sawa kwa vijana kushiriki katika kilimo kutoka kila sehemu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto moja wapo kubwa zaidi katika mradi huu ni suala la ardhi. Wenzetu wa Malaysia waliweza kwa sababu inamiilikiwa na *Crown*. Kwa hiyo, wenyewe ilikuwa ni rahisi sana kwa Mfalme na wasaididzi wake kutoa ardhi na kuwapa watu. Kwetu sisi jambo hili ni tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, naomba sana pale ambapo wizara inakuja kutujibu, ituambie namna bora ambayo inafikiria itaweza kutumia ardhi ndogo tuliyonayo kuwasaidia vijana wengi ambao wanazidi kuongezeka siku kwa siku. Takwimu za Sensa zinaonesha pamoja na kwamba asilimia 34 ni vijana lakini asilimia 44 ni wale walio chini ya miaka 18 na hawa tunawategemea ni vijana wa kesho. Wizara ije utuambie ni namna gani inafikira kutumia ardhi ndogo tuliyonayo ambayo haiongezeki, kuwasaidia hawa tulio nao na hawa ambao wanakuja ku-*graduate* na kuwa vjana wa kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu unaonekana utakwisha mwaka 2030, ninaiomba sana Wizara, iangalie namna ya kutengeneza uendelevu wa huu mradi. Kama kule ambako tumejifunza wao wameanza tangu mwaka 1956, mpaka leo tunavyozungumza mradi huu upo na unaendelea na umejenga mabilionea wengi sana kutoka Malaysia. Naomba pia Serikali iangalie namna gani ya kuendelea kutengeneza uwezekano wa Mradi huu kuendelea hata baada ya mwaka 2030 ili vijana wa Kitanzania waendelee

kunufaika, vijana wa kitanzania waendelee kuvutiwa na kilimo, waendelee kuweza kusaidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilikuwa naomba kwa vile bajeti inayotumika au iliyotengwa katika mradi huu ni kubwa lakini bajeti kubwa zaidi imeenda kutengeneza *foundation*. Nilikuwa naishauri Wizara iangalie namna ya kupeleka mradi huu kwanza kwa mwanzo katika mikoa ambayo ina vyanzo vya maji vya uhakika ili tuweze kupunguza gharama za mwanzo za mradi na fedha nyingi zaidi iende kutumika kwa vijana moja kwa moja kuliko kutengeneza miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia Mheshimiwa Bashe, aangalie namna ambayo ata-*link* mradi huu na vijana wanaotoka vyuo na vyuo vikuu na a–*link* na vijana wanaotoka JKT ili kuweza kutumia mashamba haya kuweza kuwasaidia vijana hawa ambao tayari Serikali imekwishatumia fedha nyingi kuwaelimisha, tayari Serikali imekwishakutumia fedha nyingi kuwapa mafunzo hawa JKT na wao waje walisaidie Taifa lao waweze kuwa na kesho iliyo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee niombe, changamoto kubwa ya mkulima wa kitanzania ni suala la soko, niombe sana katika mradi huu Mheshimiwa anapokuwa anaangalia namna ya kutengeneza basi ahakikishe vile vyote vinavyozalishwa vinaweza kupata soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nakuomba sana… naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ng’wasi Kamani, ahsante sana muda wako umekwisha Mheshimiwa. Namwita Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, wakati huo Mheshimiwa Masache Njelu kasaka, anajiandaaa.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie hoja ya Wizara ya kilimo ambayo iko mezani kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza Mawaziri, Bashe na Mheshimiwa Mavunde, kwa kazi nzuri ambayo wanyoifanya. Ni Mawaziri wachapakazi, wabunifu na ni wasikivu na wanafikika kwa urahisi. Kipekee nimpongeze na nimshukuru Mheshimiwa Rais, kwa maono yake na jinsi anavyopeleka fedha nyingi kwa sekta hii ya Kilimo na amepelekea sasa hivi bajeti yetu kuongezeka mpaka hiyo bilioni 970. Tunakupongeza sana Mheshimiwa Rais na ni matarajio ya wakulima sasa kwamba sekta hii sasa italeta manufaa ambayo sisi Wabunge kila mwaka tulikuwa tunalilia kwamba bajeti ya sekta ya kilimo iongezeke. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda nitajikita kwenye uchangiaji ukurasa wa 169. Ukurasa wa 169 wa bajeti umezungumzia suala la kuongeza thamani. Nitazungumzia uongezaji wa thamani wa zao la Korosho, na kwenye korosho wenzangu waliotangulia kuchangia wamezungumzia changamoto. Kwenye Korosho kuna changamoto nyingi na zimekwisha tajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye korosho kuna changamoto ya kupungua kwa uzalishaji, tumeona kwa kipindi cha miaka mitatu sasa hivi uzalishaji unapungua mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye korosho kuna bei ndogo kwa mkulima ambayo haina tija, ambayo sasa hivi kwa muda wa miaka miwili kwenye minada yetu mkulima hapati bei ambayo inatija kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye korosho tumeshuhudia utitiri wa makato na tozo ambayo hatimaye inapunguza bei kwa mkulima. Pia, kwenye korosho ni zao

pekee ambalo lina *export levy*. Hili nazungumzia kwa sababu *export levy* baadae inapunguza bei kwa mkulima, sio kwamba inalipwa tu na mfanyabiashara lakini anayeumia baadae ni mkulima anapokwenda sokoni kwamba bei yake inapunguzwa .

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Wizara kwa kuja na mwarobaini, inasema kwamba zimetengwa fedha bilioni 10 ili Bodi ya Korosho ipelekwe kwenye *private sector* kwa ajili ya kujenga kiwanda cha kubangua korosho. Huu ni mpango mzuri na suluhisho la kuuza korosho ghafi. Kwa sababu tukiendelea kuuza korosho ghafi wakuilima wetu hawafaidiki lakini tukiuza korosho karanga tutapata bei nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikupongeze Mheshimiwa Bashe, kwa wazo lako sasa la kuingia kwenye ubanguaji. Lakini tamko hili Mheshimiwa Bashe, nikushauri kwamba hii ni vita ya kibiashara. Kwa sababu kuna nchi duniani hawapendi Tanzania wauze Korosho karanga, wanataka kila mwaka wauze korosho ghafi kwa sababu ni ajira kwa wananchi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanachukua korosho yetu na kupeleka nchini kwao na wanatengeneza ajira. Kwa hiyo, hili tamko ambalo umelitoa na kwenye mkutano wetu wa wadau wa korosho ulisema msimu wa 2025/2026 utakuwa ni mwisho wa kupeleka korosho ghafi, ina maana korosho yote itabangulia hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakuomba sasa tuwe na maadalizi ya kutosha. Tusipokuwa na maandalizi ya kutosha tutavurugwa, kwa sababu kama nilivyosema kuna nchi ambazo hawako tayari kuwekeza Tanzania kwa ajili ya kubangua korosho. Wanataka kila mwaka tupeleke korosho ghafi kwa sababu inatoa ajira kwao. Kwa hiyo, wao kwa gharama yoyote hawako tayari kuona Tanzania sasa inaanza ubanguaji. Kwa hiyo, tufanye *vetting* wakati wa kuwapata

watu hao watakaoingia kwenye *private sector* wawe na nia ya kuwekeza na kubangua Tanzania. Kwa sababu tuna uzoefu wa viwanda 12 vya zamani, tulifungua viwanda 12 lakini baada ya muda mfupi vikafungwa. Haya vile viwanda vilibinafsishwa mpaka leo viwanda vile havifanyi kazi ni magodauni tu. Kwa hiyo, lazima tuwafanyie *vetting* ambao tutakuwa nao katika uwekezaji, la sivyo kutakuwa na changamoto kama ilivyokuwa zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile, hawa wawekezaji lazima tuwape motisha. Tupunguze kodi ya mitambo wakati wanapoingia ili kupunguza gharama ya uwekezaji. Tukifanya hivi tutapata wawekezaji ambao ni *serious,* watakuwa na mtaji mkubwa na wataingia kwenye ubanguaji *serious.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Mheshimiwa Waziri, nikushauri kwamba wakati hao wawekezaji wanaendelea na shughuli zao za uwekezaji basi tuwe na *forum* za kuasikiliza ili pale wanapopata changamoto waweze kusikilizwa. Kwa mfano; sasa hivi kuna changmoto ya upatikanaji wa kosrosho kwa wabanguaji wa ndani, tuna mfumo wa soko la awali ambao unalalamikiwa, ni vizuri Waziri ukakaa na hao wenye viwamda ukatafuta mfumo ambao hautashusha bei kwenye minada, mfumo ambao hautapunguza bei kwa mkulima ili na wao wapate korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie kwenye suala la umwailiaji. Nimeona hapa umesema kwamba umeingia mikataba 22 kwa ajili ya kuanza umwagiliaji katika mabonde mbalimbali, hili ni wazo zuri. Kipekee kuna Bonde la Ruvuma *Basin,* ambalo linaanza Songea, Namtumbo, Tunduru, Masasi, Mtwara. Bonde hili bado hatujalitumia ipasavyo, lina *kilometer square* 60,000. Kwa hiyo, naomba yule mkandarasi ambae amepewa kazi ya kufanya usanifu aanze songea mpaka Kilambo – Mtwara Vijijini. Tukifanya hivyo tutatoka na Mradi ambao utasaidia Ruvuma *Basin.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu gani? Mto Ruvuma una changamoto na ukiangalia jiografia ya Mto Ruvuma kwamba mto uko kwa chini na maeneo ya umwagiliaji yapo kwa juu. Ni lazima tuje na *designing* ya kujenga mabwawa mengi ili yatumike wakati wa umwagiliaji. Kwa hiyo, usanifu lazima ufanywe kutoka Songea kama nilivyosema hadi Wilaya ya Mtwara ili maeneo yote haya yafaidike na mradi huu. Tukitumia vizuri bonde hili tutaweza kunufaisha uzalishaji wa mazao ya mpunga lakini na mbogamboga na kuweza kuwasaidia wananchi wetu ambao sasa hivi wana utegemezi wa zao moja moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Songea wanategemea mahindi lakini Mtwara watu wengi wanategemea korosho. Lakini tukifanya upembuzi yakinifu na bonde hili likatumika ipasavyo basi tutawanufaisha watu wetu. Kuna maeneo ya Lipeleng'enye na kule Chikwedu kwa Mzee wangu Mkuchika, kuna changamoto ya mafuriko, lazima tujenge ukuta wa kutosha ili kuhakikisha sasa maji ya Mto Ruvuma hayawezi kuathiri mashamba ya hao wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye maazimio ya mkutano wetu wa wadau tulikubalina kwamba tuunde tume ya ufuatiliaji kwenye korosho nafikiri tutafanya kazi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa muda wako umekwisha

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Nilimwita Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka wakati huo Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, anajiandaa.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nami kwa kuweza kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye Wizara hii, moja kati ya Wizara muhimu sana kwenye ustawi wa nchi yetu, kwa namna ambavyo inaendelea kufanya kazi vizuri. Lakini pia niwapongeze Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri hakika anafanya kazi vizuri sana na sisi kama vijana wameendelea kutuheshimisha kwenye taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo ambazo tunawapa Wizara na Wizara hii ukizingatia kwamba ndiye mkombozi wa wananchi wengi, hasa wakulima wadogowadogo kwa ajili ya kuhakikisha kwamba ustawi wa chakula katika nchi yetu unaendelea kuwa imara zaidi. Na ustawi wa chakula katika nchi yetu unategemea sana wakulima hawa wadogowadogo ambao takribani wanachukua asilimia 70 ya Watanzania wote. Hivyo tuweke jicho la kipekee kwa wakulima wadogowadogo hawa. Tunashukuru Serikali kwa kweli, tumeona ilileta ruzuku ya mbolea ambayo imepelekea wakulima wetu wadogo hawa uzalishaji wao kwenda vizuri zaidi na uhakika wa chakula kwa wananchi umekuwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mbolea hii kuwekewa ruzuku kumekuwa na changamoto ya mbolea hii kuweza kufika kwa wakati. Mbolea kwa wakulima wetu imechelewa sana kwenye msimu uliopita. Mbolea ya kupandia imeweza kufika mwezi wa 12 mpaka mwezi wa kwanza, hali ambayo ilisababisha wakulima wetu wengi, hasa wadogo hawa, kuweza kupata changamoto ya kuweka mbolea hii ya kupandia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai na nitoe wito sana kwa Serikali ihakikishe mbolea hii ya ruzuku inafika kwa wakati kwenye maeneo husika ili wananchi wetu wengi hawa waweze kunufaika, na hasa ukizingatia na maeneo tunatofautiana kutokana na msimu. Sisi watu wa Nyanda za

Juu Kusini tunajua kwamba msimu wetu ni kuanzia mwezi wa 11 na 12 ndipo tunapanda; lakini maeneo ya kaskazini huko pia wana msimu wao, na ile mbolea iweze kufika kwa wakati ili wakulima hawa waweze kunifaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la bei yake; mbolea hii imakuja kwenye *package* ya kilo 50. Wakulima wetu wanauwezo wa hali tofauti ya kununua mbolea hii. Tuiombe serikali kupitia Mheshimiwa Waziri iongee na wale mawakala wanaoleta mbolea hii ili waweze kuweka kwenye parkage tofautitofauti, kuanzia kilo 50,20,10 mpaka kilo tano, ili hata mkulima ambaye analima bustani nyumbani kwake, anayelima matuta matano nyumbani kwake aweze kununua mbolea hii na aweze kunufaika nayo kwa uzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili mbolea hii kwenye maeneo mengi imeweza kufika kwenye makao makuu ya wilaya. Sisi ndani ya Wilaya yetu ya Chunya ilifika makao makuu ya wilaya; na sisi kama unavyojua, kwa jiografia, kwa ukubwa wa Wilaya ya Chunya ukienda kwenye Kata za mwisho za Kambi Katoto na Mafyoko kule ni takribani kilometa zaidi ya 200 kutoka Makao Makuu ya Chunya Mjini. Na bahati mbaya sana mbolea hii wale mawakala hawakuweza kuifikisha kule, kwa hiyo ilipelekea sasa upatikanaji wa mbolea hii kuwa ni wa gharama kubwa ambayo wananchi wetu wengi walishindwa kuipata kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai kwa Wizara, kwenye Wilaya yetu ya Chunya na baadhi ya maeneo mengine ipeleke mbolea hii. Si makao makuu ya wilaya peke yake bali na kwenye baadhi ya maeneo ya *centers* zile kubwa kubwa ili wananchi wetu hawa wengi waweze kunufaika sawasawa na mbolea hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie suala la zao la tumbaku. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na

Serikali kwa ujumla chini ya Mama yetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kweli wameweza kusikia kilio cha Wabunge. Zao la tumbaku ambalo lilikuwa ni kilio kwa wakulima sasa hivi limekuwa neema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masoko sasa hivi yanafunguliwa, huko sasa hivi ni chereko chereko, sasa wanamwimba Mheshimiwa Bashe, wanamwimba Mheshimiwa Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa sana ambayo wanaifanya. Naomba sana, kampuni ambazo zimeletwa kwenye msimu huu, ambazo zinaendelea kufanya kazi ziendelee kufanya kazi vizuri na zilindwe. Vilevile, ikiwezekana kampuni nyingine pia ziweze kuja ili ushindani uweze kuwepo na baadaye mkulima aweze kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana wanaposhindana sokoni kwa wakulima ndivyo bei inavyokuwa nzuri zaidi na wakulima wetu hawa wanaweza kunufaika. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, kwenye upande wa tumbaku, kama yalivyokuwa mazao mengine, tumbaku ni moja kati ya zao ambalo halijapata mbolea ya ruzuku. Niombe sana kupitia Wizara hii na Serikali kwa ujumla ione namna ya kuweka ruzuku ya mbolea kwenye zao hili la tumbaku ili hawa wakulima wetu nao waweze kunufaika kama ambavyo wakulima wengine wa mazao wanaweza kunufaika kupitia kilimo hiki hili litaweza kutusaidia sana. Lakini bei yake, wakati msimu huu wa mbolea unaendelea; mbolea waliyoleta mara ya kwanza ilikwisha. Walipoleta mbolea mara ya pili walileta mbolea kwa wakulima wa tumbaku ikiwa ina nembo ya mbolea ya ruzuku, hali ambayo imeweza kuleta mkanganyiko mkubwa sana kwa wakulima wetu. Hii ni kwa sababu mifuko ina nembo inayoonesha kwamba hii mbolea ni ya ruzuku lakini wao wanauziwa kwa bei ambayo si mbolea ya ruzuku. Hali hii imewanyong'oneza sana

wakulima wetu kwa sababu sasa hivi imeleta hali ya sintofahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri anapokuja kuhitimisha uje utupe na majibu. Kwamba ile mifuko ambayo imekuja ina nembo ya mbolea ya ruzuku je, wakulima hawa watalipa kwa bei ya ruzuku au watalipa kwa bei ambayo itaendelea kuwanyonya wakulima wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu nizungumze ni suala la *block farming* au *BBT*. Sisi Wilaya yetu ya Chunya ni moja kati ya wanufaika wa mpango huu wa *BBT* kwa sababu tuna eneo la takribani hekta 47,000 ambalo limeshatengwa kwa ajili ya mpango huu. Mpango ni mzuri na tunapongeza Serikali kwa kuja na mpango huu tuna Imani kubwa sana mpango huu ukitekelezeka vizuri utakuwa ni mkombozi kwa nchi yetu na kuifanya Tanzania kuwa *hub* ya chakula kwa nchi zote za Afrika Mashariki na ikiwezeanika mpaka nchi zote mpaka Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linavyokuwa linakwenda lazima pia tuweze kutoa maangaliazo ambayo tunakuwa tunayaona. Moja kati ya mambo ambayo sisi tunaishauri Serikali, Serikali imeweka utaratibu mzuri wa kuwachukua vijana na kwenda kuwapekea kwenye kambi, mpango ni mzuri. Lakini, mnapochukua vijana hawa na kwenda kule kwenye kambi kule pia tuweze kuangalia vijana ambao wao tayari wamesha jiajiri kwenye kilimo hiki, tuweze kuwapa kipaumbele. Hawa vijana ambao tutawapa kipaumbele wataweza kutusaidia sana kwenye maeneo yale pale ili na wao waweze kunufaika. Hata benki huwa wanamkopesha…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana…

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** …mtu ambaye tayari anafanya biashara, sisi wale ambao tayari wameshaaanza kulima tukiwawezesha hii itaweza kuwasaidia na wao watazalisha kwa wingi zaidi na baadae tuwachukue hawa ambao tumewapeleaka…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Njelu Kasaka muda wako umekwisha

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Nilimuita Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda wakati huo Mheshimiwa Deogratus Philip Mwanyika anajiamndaa.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Kilimo. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai lakini pia nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo amekuwa akiifanya katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niwapongeze Wizara kupitia Waziri wa Kilimo na timu yake yote kwa kazi kubwa ambayo wamekuwa wakiifanya kwa manufaa ya nchi yetu. Niwapongeze pia Wizara kwa ruzuku mbalimbali katika mazao ya kilimo ambayo wameendelea kuitoa. Lakini pia niwapongeze kwa kurudisha *export levy* katika msimu wa mwaka jana; *export levy* ambayo ni msaada sana kwa wakulima, hasa wa korosho ambako ndiko zao lenye *export levy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo nimeenda kuangalia miongoni mwa malengo ya Wizara ni pamoja na kupunguza umasikini kwa asilimia 50 kwa wakulima ifikapo 2030. Ni wazo zuri, ni mpango mzuri. Lakini

napata shida kidogo; ni namna gani tutafikia kupunguza umaskini kwa wakulima hawa kwa *trend* ambayo tunaenda nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kurudisha *export levy* kwenye zao la korosho tulifarijika sana, na tunaendelea kushukuru; faraja yetu ilikuwa ni kwamba, kumbe sasa zile tozo mbalimbali ambazo zinapunguza kiasi cha fedha ambazo mkulima wa korosho anapoenda kuuza zao lake zinaenda kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tunashukuru kwamba tunapata pembejeo kwa ile asilima 50 ambayo inaenda kwenye tasnia ya korosho; lakini ile 50% ambayo inaenda kwenye mfuko mkuu wa Serikali tuombe sasa. Ili mkulima asibebeshwe mzigo mkubwa au apate bei ambayo italeta manufaa kwake na kupunguza umaskini, kama ambavyo tumetarajia kuupunguza, basi tunaomba zile tozo kwa mfano za *CBT, TARI, task force* zichukuliwe na Serikali ili mkulima anapoenda kuuza korosho yake basi aweze kupata angalau kitu kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mikorosho gharama ambazo mkulima anazitumia kuanzia kuandaa mashamba, palizi na shughuli zote mpaka aje kuvuna gharama zake ni kubwa mno. Gharama zile zinamfanya mkulima azidi kudidimia siku hadi siku. Kwa mfano kuna mwaka ambao korosho bei ilipanda kidogo kwenye soko, ikafikia kwa kilo shilingi 3,000 hadi 4,000. Ukienda yale maeneo ambayo yanalima korosho hali ilikuwa nzuri tulichangamka, watu walijenga nyumba bora na walikuwa wanapeleka watoto shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi imekuwa ni kinyume, wakulima wa korosho wamedidimia kwa sababu gharama za uzalishaji zimekuwa kubwa sana, hali ambayo inazidi kudidimiza. Ndiyo maana nachelea kwamba, je kweli

tutaweza kupunguza hiyo asilima 50 ya umaskini kwa hali ambayo tunaiona sasa hivi? Lazima mkakati wa dhati uwepo wa kuhakikisha kwamba zao hili linaenda kumuinua mkulima. Bila mkakati wa dhati itakuwa ni hadithi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ili kuthaminisha korosho hizo sasa hivi akina mama wengi wanabangua korosho zao ili wauze zikiwa katika hali ya thamani kubwa zaidi, lakini wanakosa namna ya kupata masoko. Korosho wanazo, wanamuuzia nani wanashindwa. Niombe, Serikali itakapokuja kuhitimisha ituambie mkakati wa kuwasaidia wakulima ambao wanabangua korosho zao ukoje ili wapate masoko. Wanashindwa *branding,* korosho zinabakia ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona Serikali imetuambia kwamba, hadi kufikia Aprili 2023 imepeleka Marekani tani 74.19 zilizobanguliwa zenye thamani ya shilingi milioni 455.7, ni jambo zuri la kushukuru. Lakini sasa tuone ni namna gani Wizara itabeba, badala ya wabanguaji wakubwa peke yake tuwafikie wale wabanguaji wadogo ambao na wenyewe wanatamani siku moja korosho zao walizobangua wanaziuza na wana uhakika wa soko. Lakini pia wanauza hata huko nje. Wizara tukifanya hivyo tutakuwa tunawasaidia sana wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, tunashukuru kwamba Serikali ilitupatia pembejeo za ruzuku kwenye msimu uliopita na kule nyuma pia. Lakini msimu wa mwaka jana, baada ya kuona changamoto zilizojitokeza kwenye msimu wa mwaka 2020/2021 mwaka jana Wizara ilitoa mwongozo wa namna ya ugawaji wa pembejeo zile za ruzuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo ule ulileta shida kidogo katika utekelezaji wake. Nishauri Wizara, kwamba tunapoandaa miongozo hii tujaribu kushuka kulechini tukaone hali halisi. Mengi yanatendeka kwa kukaa mezani, hatujui uhalisia ulivyo kule chini kwa wazalishaji wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo ule badala ya kumnufaisha mkulima halisi wa korosho ambaye tulimtegemea ulienda kuwanufaisha wale ambao walikuwa wananunua kangomba. Wananunua ndio wao…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ashante sana Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachania kwa maandishi naunga mkono hoja. Ahsante *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana nilimwita Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika aweze kuchangia.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kusema namshukuru sana Mheshimiwa Bashe kwa kutupa bajeti ambayo imekuwa ni nzuri. Lakini niseme wazi, napata tabu sana kusema naunga mkono kwa asilimia mia. Kama nitaunga ni kwa sababu tu bajeti hii bado inaendelea kuwapa ruzuku ya mbolea wakulima; lakini nina matatizo makubwa sana na maeneo ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeiangalia sana bajeti hii, na nimeangalia fedha tulizotumia kwenye eneo la umwagiliaji. Kuna skimu za kila aina hapa; skimu 42 mpya, kuna *block farms* zimeanzishwa, kuna mabonde ya umwagiliaji, kuna skimu nyingine 30 za hekta 69,000. Skimu zote hizi ukiziangalia kwa ujumla wake watu wa njombe hatumo. Kwa hiyo inanipa shida kuelewa *allocation* ya

*resources* hizi muhimu kwa watu wa Njombe na mikoa mingi ya Nyanda za Juu Kusini, hatumo. Sasa, kinachonisikitisha zaidi…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba ukiangalia kwa karibu zaidi watu wa Njombe tuna zao la chai. Mwaka 2015 tulikuwa na chai *vision* ya kuweza kuzalisha chai na ku-*recruit* watu wakulima wadogo wadogo wa chai 2,500. Lengo hilo limefanikiwa, wameweza kulima takriban hekta 2,300 na tume-*recruit* wakulima wadogowadogo takriban 300.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Njombe Vision kilikuwa na kujenga kiwanda, kiwanda kimejengwa, ni kiwanda kikubwa, kimejengwa na kampuni ya *Uniliver* kama *package* ya kusaidia wakulima wadogowadogo. Kiwanda hiki kinapokea majani kilo 50,000 *capacity* yake. Lakini wakulima wadogowadogo hawa wameshindwa kupeleka majani kufikisha kiwango cha *capacity* ya kiwanda, wanaweza kupeleka majani tani kilo 15,000. Na watu wa Lupembe wameongezea, tumefika angalau kilo 30,000, bado tuna *deficit* ya kilo 20,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kiwanda hiki kinatishiwa kufungwa kwa sababu *capacity* yake ni kubwa na uwezo wa kuleta majani ni mdogo. Kitakachotuwezesha pekee, ili kiwanda hiki kiweza kuendelea na wakulima wadogowadogo kuendelea ku-*supply* majani na wao kuongeza kipato na ajira ni kama tunaweza tukaongeza uzalishaji wa majani ya chai mabichi. Na itakayo tuwezesha ni umwagiliaji pekee. Katika mazingira kama haya nipende kusema nilitegemea sana kwamba, kwa kweli bajeti hii ingeangalia maeneo kama hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na turudi nyuma tuangalie; katika *principle* za uchumi ni vema ku-*consolidate the game*. Watu ambao wamejituma wamefia mahali wameanza, wadogowadogo wanauwezo, wamejiwezesha wenyewe, tuka wa-*support* kwanza kuliko kuchukua *resources* nyingi na kuzitupa na kuzituma kila mahali. Hakuna ubaya kuwa na *block farms,* lakini tuangalie tu-*consolidate* pale ambapo tumefanya vizuri kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ukisoma kwenye mpango mzoma bajeti ya Mheshimiwa Waziri kwenye maeneo hayo ya chai si kwamba ameyaacha kabisa, anachosema wataendelea kufanya utafiti. Hivi, ni utafiti gani wa umwagiliaji wa chai unataka kuufanya? Mwaka 2019 Halmashauri ya Njombe ilianzisha mpango wa umwagiliaji wa chai kama *pilot project*. Mimi nilipoingia Bungeni mtu wa kwanza niliyemchukua na kumpeleka Njombe alikuwa ni Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Prof. Mkenda. Walikwenda, tukaangalia maeneo yale na ile *project* ni nzuri sana, ya *block farming* ya wakulima wadogowadogo. Hatuongelei *large scale farming* hapa, wakulima wadogowadogo wa kawaida akina mama, akina dada na akina kaka. Ile program ilitakiwa sasa i-*run* kwenye zile hekta 2,500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika mazingira kama hayo kuna sababu gani ya Wizara kutoliangalia eneo hili na muhimu sana la umwagiliaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ukiangalia Mheshimiwa Bashe anasema yeye anaangalia bajeti yake inaangalia ilani ya chama inaangalia mpango wa miaka mitano. Lakini kwenye ilani ya chama akisoma vizuri *page 38* mpaka 41 kifungu 37 “D” kinasema; Serikali kupitia Wizara ya Kilimo ita-*focus* zaidi kuongeza uzalishaji wa majani ya chai na kuongeza tija kwa wakulima wadogowadogo wa chai. Sasa unawezaje kuacha hawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuliongelea hilo kwa sababu ya muda, lakini niseme, chai ni ubora, Tanzania bado chai yetu haina ubora. Bodi ya Chai inatakiwa iongeze nguvu kwenye kusimamia ubora wa chai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwa haraka kwenye mbolea. Sisi tunaishukuru sana Serikali na wakulima wa Njombe wanaishukuru sana Serikali kwa kuendelea kutoa mbolea ya ruzuku, na tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa mpango huu mkubwa. Nipende kusema kwamba, tulitegemea kwamba dosari za mpango ule uliopita zingeangalia ili kuweza kuboresha mbolea ifike kwa wakati, kama walivyosema wenzangu, lakini kwa Njombe tuna kitu tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni wakulima wakubwa, Wananjombe ni watu wanaojituma, ni watu hodari wa kilimo na hili halipingiki mahali popote. Msimu wetu wa kulima ni tofauti na maeneo mengine. Mbolea ya kupewa mifuko mitatu kwa eka haitutoshi, hiyo mbolea ni kwa ajili ya mahindi pekee yake. Ukienda kwenye viazi tunalima misimu mitatu kwa mwaka mmoja, Oktoba, Novemba yaani tunavuna Desemba. Tukipanda Februari tunavuna mwezi Juni. Halafu wananchi wa Njombe wamejiongeza, wanalima kilimo cha kumwagilia cha asili ambacho na chenyewe mwezi Juni wanaanza kuvuna Mwezi Septemba. Tungetaka tuongezewe mifuko ya mbolea angalau sisi tupate kwenye kilimo cha viazi pekee yake mifuko minne mpaka sita, ingefaa kwa kila eka ili tuweze kuendelea mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kusema kwenye hili unaona kunatokea uchakachuaji na hatuwezi kuwa-*protect* wachakachuaji, lakini ukweli ni kwamba *demand* ya mbolea kwa maeneo yale ni kubwa mno kuliko *supply* na haiji kwa wakati. Hiyo inasababisha watu wasiwe waaminifu kuingia katika *schemes* za kutaka kutengeneza na kuuza mbolea ili kujipatia fedha. Namuunga mkono Waziri kusema kwamba

sasa tutafanya hili jambo liwe jinai na isiwe jinai tu, tulifanye kabisa liwe ni uhujumu uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa parachichi kwa sababu muda unaniishia. Nimeona tuna mpango wa kuongeza uzalishaji wa parachichi na wapongeza wakulima wa Tanzania na hasa wa Njombe maana yake ndio wazalishaji wakubwa wa parachichi katika nchi hii. Tunategemea tumefika tani 29,000 na tumepata karibu milioni 52, lakini tunategemea kwenda kwenye tani 50,000 *by* mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufikia hapo bado tunahitaji mambo mengi sana ya kufanya lakini mojawapo Njombe tunaomba kwenye viatilifu tuangaliwe kama vile ambavyo korosho wanapewa, ruzuku kwenye pamba…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwanyika.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** …na sisi tupate ruzuku kwenye madawa ya ukungu ili tuweze kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na nitaomba maelezo mazuri kwa nini Njombe …

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Martha Gwau, wakati huo Mheshimiwa Bryceson Magessa Tumaini, Mheshimiwa Daktari Florence George Samizi na Mheshimiwa Luhaga Mpina wanajiandaa.

**MHE. MARTHA N. GWAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii uliyonipa ya kuchangia Wizara hii muhimu sana ya Kilimo, ambayo kwa wananchi wetu

tunaowawakilisha ndio shughuli kubwa wanazozifanya kwa kujipatia kipato, nimshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kabla sijaendelea nisiwe mchoyo wa fadhila kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuishika Wizara hii, lakini pia kwa kuona umuhimu wa Wizara hii na kuiongezea bajeti mwaka hadi mwaka wa fedha. Kwa hiyo nimpongeze sana. Pili, niipongeze Wizara chini ya kaka yangu Mheshimiwa Bashe na Naibu Waziri Mheshimiwa Mavunde, lakini na watendaji wote wa Wizara kwa juhudi kubwa na mikakati mingi wanayokuja nayo kwa ajili ya kumkwamua mkulima wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu leo utakua kwenye mambo mawili; suala zima la kilimo cha alizeti na suala zima la mbolea. Tanzania tuna wakulima nadhani wa aina tatu. Kuna wale ambao ni *small scale farmers* ambao ni *majority* ya watu wetu, ndio hao wanajishughulisha na kilimo kidogo kidogo. Pia tuna wale *middle* ambaye Kaka yangu Bashe amekuja na hii *program* ya *BBT,* mimi naweza nikasema kama hao ndio *middle farmers.* Vile vile tuna wale *large farmers* ambao wao wanakuja na mitaji yao na teknolojia yao. Sasa leo nijikite kuwaelezea au kuwatetea hawa *small scale farmers* ambao ndio mama zetu, baba zetu, wajomba zetu na watu wetu wote waliopo mikoani mwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nielezee zao la alizeti. Zao la alizeti ni kati ya mazao ya kibiashara yanayolimwa katika Mkoa wangu wa Singida. Pamoja na mazao mengine ya kibiashara lakini zao la alizeti ni zao letu moja la kibiashara. Tulipata heshima ya Waziri Mkuu kuja kuzindua mikoa ya kimkakati ambayo Singida ilikuwa kati ya hiyo mikoa ya kimkakati itakayolima zao la alizeti. Nimshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna uongozi wa mkoa chini ya Mkuu wetu wa Mkoa Mheshimiwa Peter Serukamba na Wakuu wa Wilaya zote tano wakihamasisha na wakisaidia wananchi kuhamasisha kulima zao hili la alizeti, kwa sababu Serikali imetusaidia mbolea, ruzuku pamoja na mbegu. Kwa hiyo wao wanafanya uhamasishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetoka kwenye kulima hekari laki nne na sasa tumelima laki sita na *projection* ya mwakani tutalima mpaka hekari milioni moja na tutakuwa na uwezo wa kulisha zaidi ya asilimia 40 ya mafuta kwa Nchi hii ya Tanzania katika Mkoa wetu mmoja wa Singida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushauri kwa Mheshimiwa Waziri, pamoja na juhudi nyingi wanazofanya na mikakati mingi, zao hili la alizeti sasa wakulima wetu wa Singida wanakata tamaa kulima. Wanakata tamaa kwa sababu bei ya mafuta ya alizeti imeshuka na zao la alizeti limeshuka kwa sababu Serikali haijaweka kodi kwa mafuta yanayotoka nje. Sasa *how can you compete* na Mheshimiwa Waziri kaka yangu *slogan* yake ni kumkomboa mkulima wa Tanzania. Ukombozi wa mkulima wa Tanzania, moja lazima iwe kulinda bei ya zao lake analolilima kwa sababu, nimesikiliza hotuba yake mwanzo mwisho kaongelea masoko ya ndani, ya nje na mambo mengi mazuri. Bahati mbaya sijasikia Mheshimiwa Waziri kaka yangu akiongea jinsi gani atalinda bei za mkulima huyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunapowahamasisha watu, Serikali wanapoweka mikakati mizuri ya kupata mbolea za ruzuku wananunua, lakini mbegu bora, sasa zao kama halina soko hawa watu wanakata tamaa, wanavunjika moyo. Kwa hiyo kabla Waziri hajaruhusu kodi kutowekwa kwenye mafuta ya nje, kutoa au kutokutoa, je, hivi wanawaza *implication* kwa hawa wakulima itakuwaje? Kwa hiyo nadhani ni mikakati ambayo Wizara inabidi ifanye kabla haijaruhusu kwa wakulima hawa kuvunjika moyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, Mheshimiwa Waziri aje na mikakati, atueleze na hawezi kushindwa kwa sababu *he is the one of the best Ministers,* ataweza kuwalinda wakulima wetu na kulinda bei za wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine cha pili hapo hapo, ni ushauri kuwa, wakulima wetu wauze *final product* badala ya kuuza mbegu. Kwa sababu Mheshimiwa Waziri amekuja na wazo la *BBT,* hawezi kushindwa kwa wakulima hawa kutengeneza au kujenga kiwanda labda kila halmashauri ili wakulima hawa wauze *final product,* badala ya sasa hivi wananuza magunia ya lumbesa ambayo wanalaliwa tu au wanalanguliwa na watu ambao wanaenda kufaidika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kama kuna kiwanda wakakamua mafuta watauza mafuta, lakini watauza mashudu nao watapata kipato kizuri. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nashauri tu katika hili zao la alizeti naomba aliangalie kwa sababu Mkoa wa Singida kiuchumi kwa kweli zao la alizeti ndio zao ambalo wanalitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa mwisho ni suala zima la mbolea. Tuna mbolea na Serikali waliweka ruzuku kwa mbolea, lakini nashauri kwa nini hii ruzuku isitolewe kwa mbolea ya viwanda vyetu vya ndani? Nasema hivi kwa sababu viwanda vya ndani vina *economic benefit* ya kupewa ruzuku. Mbolea zote zinazoagizwa sisi tunafanya kama tuna *export job,* kwa sababu ukitoa ruzuku kwa mbolea za nje ni kama una-*export job* badala ya kufanya *job creation*. Tukiweka ruzuku kwa mbolea za viwanda vyetu vya ndani, ina maana tunaruhusu hivi viwanda viajiri watu wengi, lakini tunaruhusu uchumi u-*circulate* kwa sisi kwa sisi hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna faida ya kuweka ruzuku kwa viwanda vyetu vya ndani, mojawapo ni *accountability*. Mheshimiwa Waziri amekuja na ule mfumo wa zile namba za kugawa mbolea. Sasa kama viwanda vyetu vya ndani vitapelekwa ruzuku moja kwa moja kiwandani, ina maana tutakuwa na uwezo wa kusema Mkoa wa Singida peleka tani kadhaa na tutafanya *accountability,* kwamba hizo tani zimepelekwa na kweli zimewafikia wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine tutaweza kufikisha mbolea kwa wakati. Mbolea nyingi wananchi wanalalamika hazifiki kwa wakati. Ule msimu wanataka kulima, mbolea inakuwa haijafika, lakini tukitoa ruzuku kwa viwanda vyetu vya ndani kuanzia mwezi Julai wanaanza kusambaza hizo mbolea kwa wakulima wetu wa vijijini. Kwa hiyo itafika mahali mwezi Desemba mbolea zishawafikia wakulima. Tofauti na sasa, wakulima hawapati mbolea kwa muda muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine tutapata kodi kwa Serikali kwa sababu uzalishaji wa viwanda vyetu vya ndani utakuwa mkubwa na wakulima watakuwa na *choices*. Wataambiwa bei hii ya mbolea ya nje, lakini bei hii ni mbolea ya ndani ambayo tayari ina ruzuku. Kwa hiyo, nashauri hayo kwa Waziri ayachukulie kama chachu, lakini ayachukue kama atatengeneza ajira na atakuza uchumi. Kiwanda cha Dodoma mfano, wakiajiri watu 3,000 na uchumi wa Dodoma utabadilika na wananchi maisha yao yatabadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Bryceson Magessa Tumaini aweze kuchangia.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii uliyonipatia ya kuongea

katika bajeti hii ya Wizara ya Kilimo. Pia nampongeza sana Mwenyezi Mungu na kumshukuru kwa kutupa nafasi hii ya kuzungumza tena leo katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Waziri wa Kilimo, Naibu Waziri, wataalam, Katibu Mkuu kwa kutupatia bajeti hii ambayo tunaizungumzia leo. Nilivyokuwa napitia nimegundua kwamba ukuaji wa sekta hii sasa uko 3.9. Hapo nyuma ulikuwa 4.9, maana yake kuna mahali fulani ukuaji kama unashuka hivi. Sasa unashuka kwa sababu gani? Nafikiri Waziri atakuja kutuambia, lakini mchango kwa pato la Taifa umekuwa 26.9 na tulikuwa tumekwenda 29, inawezekana kuna sekta imekua inaanza kuchangia zaidi kuliko kilimo. Ikumbukwe tu kwamba sisi Watanzania wengi tumeajiriwa kwenye sekta hii. Kwa hiyo, naamini kabisa ni sekta ambayo inabidi iangaliwe kwa umakini iwe na ukuaji mkubwa, ikikua maana yake na uchumi wetu utakuwa unakua zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nataka nijikite, naona zile taarifa za kimataifa na za Kitaifa zimezungumziwa sana, nataka nijikite kwenye Halmashauri yetu ya Geita ambayo inaitwa *Geita DC*. Mwaka 2020 kwenda 2021 sisi tulipanga kulima hekta takribani laki 115.4, lakini tuna hekta laki 327, maana yake tunalima kama asilimia 50 tu. Kuna kitu cha kufanya hapo. Tulitarijia vile vile tuweze kuvuna mazao ya wanga takribani tani laki 364.34 na mazao ya mikunde takribani tani 87,902 kwa kulima hekta 46,245. Hili limefanyika mwaka 2021 na tulipata mazao na ukamilishaji wake asilimia kama 99.9. Mwaka uliofuta makadirio yalikuwa ni hayo hayo na wakapata mafanikio hayo kama asilimia 99.9. Maana yake ni kwamba inawezekana makadirio tunayojiwekea sio makubwa sana kwa sababu eneo kubwa bado halijalimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni nini hapo? Inawezekana changomoto hii ya ukuaji wa sekta yetu tunayoiona ni kwa sababu kuna sehemu kubwa kule kwenye

maeneo bado haijalimwa. Sasa naishauri nini Serikali? Naishauri Serikali kwamba kwenye mazingira haya tuliyonayo ziko changamoto kadhaa ambazo nazijua nikizitaja kwenye Geita *DC* zitakuwa ni changamoto ambazo zinaweza kuwa hata ndani ya nchi. Kwa mfano, sisi Jimbo la Geita na Jimbo la Busanda tuna takribani jumla ya kata 37, tuna Maafisa Ugani 23. Unaweza ukajua kama Maafisa Ugani ni 23, kuna kata 14 hazina Maafisa Ugani. Sasa hawa wanaendaje, maana yake ni kwamba hawa wanakwenda bila kuelekezwa nini cha kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano, ukichukua tarafa kwa maana ya Tarafa ya Busanda, kuna kata 11, Maafisa Ugani wako saba. Tarafa ya Butundwe Maafisa Ugani wako tisa, Bugando wako watano, Kasamwa wako wawili jumla ni 23. Tuna kazi kubwa ya kufanya hapo kwamba hawa Maafisa Ugani sasa waongezwe kwenye maeneo yetu. Pia vipimo vya udongo ambavyo mwaka jana tulisema udongo utafitiwe, hakuna kipimo hata kimoja kilichokwenda, maana yake wakulima wetu wanalima kibubu hivi, hawajui udongo una hali gani na kitu gani kinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha tatu ambacho nilikisema ni pembejeo kwa maana ya mbegu na mbolea. Hii mbolea mfumo uliowekwa mwaka jana na ruzuku iliyowekwa na Rais, nimpongeze Mheshimiwa Rais imeleta uchangamfu wa sekta hii, lakini utaratibu uliotumika, wakulima wengi hawakupata mbolea. Kwa nini? Umbali, kwa hiyo ni ombi langu kwamba sasa mbolea hii ipelekwe kwenye kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ambayo naiona ni kwamba hata wale Mawakala ambao walifanya mwaka jana, wanaonekana sasa hawakwenda vizuri na mfumo wa Serikali, wengine wameanza kwenda TAKUKURU kuhojiwa. Kwa hiyo nina mashaka kwamba utaratibu wa mbolea wa mwaka huu huenda Waziri akapata

Mawakala wachache kwa sababu ya hofu hiyo. Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri waliangalie hiki tunalifanyaje kwenda kwenye kata zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kwenye mbolea hii hii, wale waliokuwa wameandikishwa mwaka jana wako wakulima wengi hawakuandikishwa. Ningeomba sana hawa waandikishwe ili kusudi kila mmoja aweze kufaidika na hii mbolea ya ruzuku na uzalishaji wetu ukue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, nimeona kuna upembuzi yakinifu wa skimu kadhaa katika Kata ya Nyakagomba, Kata ya Nyachiluluma, Kata ya Bukondo na Kata ya Magenge. Naamini kabisa hili kama atalifanya kwa wakati huenda tukaona matokeo mapema, kwa sababu tuna takribani hekta 7,200 kwenye maeneo haya ambayo zikiwekewa umwagiliaji watalima mara tatu badala ya kulima mara moja. Kwa hiyo, niombe sana huu upembuzi yakinifu usichukue muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wabunge na nchi nzima tuna matarajio kwa bajeti inayotolewa na Mheshimiwa Rais hapa tuone matokeo mapema na hayo matokeo najua kwa sababu ndio tunaanza yanaweza yakachukua muda mrefu kutokea. Kwa hiyo, niwaombe sana tujitahidi kufanya kadri inavyowezekana matokeo yaanze kuonekana. Kila anayesimama atakuwa anaongelea hili kwa sababu ndio tunaanza na matokeo yanazidi kuchelewa kuoneka, ianze kuonekana nini kinafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ambalo nataka kusema ni kuhusu hizi *block farming* ambazo wenzangu wamezisema. Kule Mkoani Geita sina uhakika *block farming* iko sehemu gani. Kwa hiyo kila unayemuuliza anakwambia hiki ni kitu gani. Niwaombe sana hii *vocabulary ya block farming* hii ije kule Geita watu watambue ni kitu gani kinatakiwa kufanyika,

kwa sababu sasa hivi inaonekana tu iko mahali. Najua inawezekana ni kwa sababu ya mafungu, lakini namwomba Mheshimiwa Waziri atembelee kule wamfahamu, wajue *block farming* ni nini kwa sababu sasa hivi *definition* yake kule kwetu wanaweza kukwambia ni uvuvi, kumbe *block farming* ni mashamba. Nimkaribishe sana Waziri aje eneo hilo… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Magessa na muda wako umekwisha, lakini unayo hiari ya kuunga mkono hoja kama ulikua hujamalizia.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga hoja mkono. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya tunaendelea, nilimwita Mheshimiwa Daktari Florence George Samizi, wakati huo Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina na Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu anajiandaa.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia hotuba hii ya Kilimo ambayo ndio uti wa mgongo kwa kuwa tumeona asilimia 65 ya wananchi wetu ni wakulima. Nami nianze kwa kuunga mkono hoja. Pia niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayofanya, lakini kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake nzima kwa jinsi ambavyo wanaitendea haki Wizara hii ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona jinsi ambavyo utekelezaji wa mbolea katika majimbo yetu ulivyofanyika kwa ufanisi mkubwa sana. Ukisoma taarifa ya Mheshimiwa Waziri inaonyesha kabisa kwamba upatikanaji wa mbolea

umepatikana kwa asilimia 126, zaidi ya lengo ambalo waliokuwa wamejiwekea la kuingiza mbolea tani 650,000. Hii imetokana na kwa sababu waliingiza tani 617,000 kutoka nje, lakini 75,000 zilitoka ndani ambayo ni takribani kama asilimia saba tu ilitoka ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na mwenzangu aliyepita kusema mbolea ni usalama wa nchi na mbolea ni usalama wa chakula. Tumejionea wenyewe jinsi tulivyopata magonjwa ya mlipuko wa *Covid* na tuliingia kwenye adha kubwa ya kukosa mbolea lakini vita ya Ukraine na Urusi ndio imekuwa wimbo wetu kwamba imesababisha tumekosa mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ni muda muafaka sasa kuwekeza zaidi kwenye viwanda vya ndani ili kuepukana na changamoto hiyo. Hii ni pale tu ambapo tutaamua kupeleka ruzuku kwenye viwanda hivi, kwanza ili tuweze kuwapa motisha lakini kama mwenzangu alivyochangia tunaenda kupata hizi *trickle down effect*. Tutapata ajira, hela yetu itabaki humu humu ndani, pesa itazunguka ndani, tutapata ajira, watalipa kodi, lakini wananchi wetu watafaidika *CSR* ni hapa hapa ndani na wawekezaji wengine wa nje watafurahia kuja ili sasa tuwe na uhakika wa mbolea kutoka nchini mwetu ili hii asilimia 92 inayoagizwa kutoka nje, basi iwe ya viwanda vya ndani. Tunayo Minjingu, tunayo *intercom,* wawezeshwe kwa kuwapa motisha ili na wawekezaji wengine waweze kuvutiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, tutaweza kuuza malighafi maana yake samadi tunayo nchini, gesi tunayo, *phosphate* tunayo, chokaa tunayo, kwa hiyo tutafaidika pia kuweza kuuza haya *material* yetu katika viwanda vyetu vya ndani na Serikali sasa itafanya kazi zingine kwa sababu kwanza watumishi ni wachache, kwa hiyo uratibu wote

tutawaachia wafanyabiashara kwa sababu Serikali *basically* haifanyi biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye hoja ya umwagiliaji. Ninapongeza Serikali kwa ajili ya umwagiliaji, taarifa imetuambia mabadiliko ya tabianchi yamechangia kuleta matatizo mengi. Ninaishukuru Serikali nimeona sasa hivi na mimi nimewekwa kwenye upembuzi yakinifu, niiombe Serikali kama kweli tunataka kupata kubadilisha kilimo hiki cha umwagiliaji basi tuende kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri ameonesha kabisa yeye ameshaingia mikataba 48 katika mikataba 69 ambayo ni asilimia 70. Kama ameingia mikataba ya shilingi bilioni 234 ni ukweli usiopingika kwamba miradi hii haijatekelezeka, na hii inathibitika kwenye taarifa ya *CAG* ambayo inasema Serikali imepeleka shilingi bilioni 48 tu sawa na asilimia 18 kwenye miradi ya umwagiliaji. Ndiyo maana hapa kila mtu anasema sijaona skimu hata mimi sijaona skimu. Mheshimiwa Waziri Kaka yangu Mheshimiwa Bashe nakushukuru nimepangwa kwenye upembuzi yakinifu kwenye skimu za Kigina, Muhambwe, Kumbanga, Nyendara. Ninakuomba skimu ya Nyendara naomba ifanyiwe kazi mapema, kwa sababu ilijengwa ikafikia nusu na sasa imekuwa ni majanga. Tumeshapata matukio ya vifo vifo sita pale maana *it's incomplete work,* watu wanatumbukia kwenye ile skimu, niombe kama haiwezekani kuisha tufunike wananchi wa Muhambwe wamesema bora tufunike iwe hamna ili watu wasife, kuliko wananchi kutumbukia kwa sababu skimu ile haijaisha. Skimu ile ili iishe inahitaji shilingi milioni 300 mpaka 500 tu. Imefikia asilimia 80, niwaombe katika mpango huu nami niwekwe kwenye mkakati ili wananchi wangu wa Nyendara, wananchi wangu wa Kata ya Misezelo waweze kuwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuiombe Serikali sasa kwa hali hii hatuna sababu ya kuendelea kutumia nguvu nyingi sana

kusema kwamba Serikali imeongeza bajeti. Tutumie nguvu nyingi sana kuwaambia wananchi mnaona skimu, mnaona hiki, mnaona hiki itakuwa kazi rahisi sana kuliko kutumia nguvu nyingi kuwaambia bajeti imeongezeka. Wananchi wetu wanataka kwenda kuona uhalisia wa hii bajeti kwenye maisha yao ya kila siku kwa maana waweze kuzalisha kwa sababu ndiyo kazi yao ya kila siku. Kwa hiyo, naamini Mheshimiwa Bashe katika hili mtakwenda kunisaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninaipongeza Benki ya Kilimo nimeona imetoa mikopo kwa wananchi lakini wananchi wa Muhambwe hawajafaidika kwa sababu bado benki hii ina pesa kidogo. Naomba Serikali iiongezee mtaji ili na wananchi wa Muhambwe waweze kufaidika kupata vitendeakazi. Hatuna matrekta, hatuna magari, tunalima bado kwa jembe la mkono, ninaiomba benki hii iweze kuongezewa fedha ili sasa iwafikie wakulima wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona kwenye taarifa wakulima wadogo wadogo wamekopeshwa shilingi bilioni 60 tu ni ndogo sana kwa wananchi wetu. Kwa hiyo, niiombe Serikali iwasaidie wakulima wadogo wadogo kwa kuongeza mtaji kwa benki hii ili wananchi wetu waweze kujikwamua na waondokane na hiki kilimo ambacho wanaona kwamba ni shida kwa sababu hawana vitendeakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba mradi wa *BBT* unakwenda kuleta mabadiliko kwa vijana wetu, lakini niungane na wenzangu, wale watu waliokuwa wanalima hiki kilimo ambao walikuwa wanahangaika wenyewe na wametulisha kwa miaka mingi waangaliwe pia kule kule waliko ili nao waweze kusaidiwa. Vijana wasaidiwe lakini na wale watu waliotutunza miaka yote wasaidiwe. Changamoto zao tunazifahamu nao tuwalenge kule kule waliko ili waweze kusaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu liko mpakani, ninaiomba Serikali kwa sababu mazao yetu mengi na hasa muhogo tunawauzia nchi jirani, niombe kusaidiwa maghala ili tuweze kutunza kwa sababu wale wa nchi jirani wananunua mashambani kwa hiyo wanawaibia wakulima. Niombe maghala ili wananchi wangu waweze kutunza mazao na tuwe na masoko ya ujirani mwema kwa sababu tutawauzia ile mihogo nchi jirani kwenye soko la pamoja. Nikipata maghala, nikipata soko, nikapata na vitendeakazi basi wananchi wangu wa Jimbo la Muhambwe watakwenda kufaidika na watakwenda kuzalisha kwa kiwango cha hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi naamini kwa haya machache, naunga mkono hoja kwa sababu kilimo ni uti wa mgongo wa Jimbo la Muhambwe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimuita Mheshimiwa Luhaga Mpina wakati huo Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu anajiandaa.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hii Wizara ya Kilimo katika makadirio yake ya mwaka 2023/2024. Niwapongeze sana Wizara kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea huu mradi wa upembuzi yakinifu katika Kijiji cha Mwakasumbi pamoja na Mwalukoli katika Jimbo la Kisesa, kazi nzuri sana lakini na namna bajeti inavyoongezwa ya kilimo ni jambo ambalo wakulima tunafurahia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba leo wafugaji ambao wamekwazwa na madhila yale ya wahifadhi wote leo wako hapa ambao Mheshimiwa Spika

aliomba vielelezo hivyo viletwe wamekuja wenyewe na vielelezo. Kwa hiyo leo jioni tunakabidhi vielelezo hivyo vilivyoombwa na Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa bajeti. Katika utekelezaji wa bajeti hapa, bajeti ya maendeleo ya Wizara ya Kilimo katika mwaka huu wa fedha ni shilingi bilioni 569.97. Fedha zilizotolewa mpaka sasa hivi na Serikali ni shilingi bilioni 470.75. lakini katika fedha hizo, shilingi bilioni 361.5 ni za umwagiliaji ambazo mpaka sasa hivi zilizotolewa ni shilingi bilioni 85 tu sawa na asilimia 23. Sasa unaipataje asilimia 40, unaipataje shilingi bilioni 470 wakati fedha za umwagiliaji shilingi bilioni 361 ambazo ni sawa na asilimia 63 ya fedha za maendeleo zimetolewa asilimia 23 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba fedha kwa ajili ya kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji mpaka sasa hivi imeshabadilishiwa matumizi. Zaidi ya shilingi bilioni 200 na kama imebadilishiwa matumizi, fedha za maendeleo, fedha zilizotengwa kwa ajili ya shughuli za umwagiliaji zimebadilishiwa maendeleo, zimepelekwa wapi? Kwa idhini ya nani? Waziri ana uwezo wa kubadilisha fedha za maendeleo zilizoidhinishwa na hili Bunge akazipeleka kwenye shughuli zingine. Tuambiwe kwa umakini juu ya hizi takwimu zilivyokaa na Waziri atakapokuja hapa ili tuweze kujua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni suala la utoaji wa mbolea ya ruzuku. Ukiangalia taarifa ilivyowasilishwa kwamba mpaka sasa hivi tayari mbolea tani 449,795 zimekwishatolewa na wanufaikaji 801,000 lakini ukienda kwenye ile jedwali alilosema jedwali la nane lina takwimu nyingine. Mbolea iliyopokelewa na kusambazwa mpaka sasa hivi ni tani 342,729 badala ya hiyo 400. Kwa hiyo kuna mkanganyiko mkubwa sana wa takwimu. Sasa hizi takwimu ni za kupika? Sasa kama zina uhalisia kwa nini zinatofautiana ukurasa hadi ukurasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, kama tuliandikisha wakulima 3,050,000, wakulima walioenda kunufaika na mbolea ni 801,000 peke yake, hawa wakulima wengine 2,200,000 walipata wapi mbolea? Kama tulijua kwamba mfumo huu wa utoaji wa mbolea ya ruzuku hatuwezi kuwafikia wakulima wote kwa pamoja, kwa nini tulileta mfumo ambao unapelekea mbolea kuipata mpaka upitie mfumo wa ruzuku ya mbolea? Hawa wananchi wengine wamelimaje kama hawakufikiwa? Kama tulikuwa na lengo la kusajili wakulima milioni saba na leo tumesajili milioni tatu, hawa wakulima wengine wanaendeshaje kilimo chao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto nyingi sana katika zoezi hili la utoaji wa mbolea ya ruzuku. Moja, mfumo wa mtandao wa mbolea za ruzuku uliokuwa ukitumika una changamoto nyingi. Moja, unaruhusu *double scanning* mpaka *multiple scanning*. Pili, mtambo huu hauwezi kuruhusu *sub-agent*. Mfumo unachelewa ku-*left* na hivyo mkulima anaweza aka-*draw* zaidi ya mara moja. Sasa kama una mfumo umeandaliwa wa namna hii, unaweza kwenda kufanya mpaka *double scanning* waharamia wengine wa kimtandao wanaweza kuiba fedha yoyote ile wanayoitaka kwenye huu mfumo, Wizara inaandaje mfumo na kuuleta kwa wananchi wenye changamoto za namna hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo ambao unaweza ukaiba fedha za nchi tukaenda kulipa mbolea hewa, unawezaje kuingia mfumo huo? Sitaki kuamini kwamba Serikali Mtandao kwa maana ya *e-GA* kwamba hawana uwezo wa kuwasimamia Wizara ya Kilimo, lakini nataka kuamini kwamba Wizara ya Kilimo walianzisha mfumo huu wa utoaji wa mbolea ya ruzuku bila kuwashirikisha *e-GA* na yawezekana kabisa hawana *clearance* ya *e-GA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuendesha mfumo bila kupata *clearance* ya *e-GA* ni kosa kisheria na matatizo yake

yanaenda kuzalisha matatizo makubwa ya uhujumu uchumi. Sasa Wizara inaweza namna gani kwanza huyu *vendor* alipatikanaje? Huyu *vendor* aliyetengeneza huu mfumo alipatikanaje? Alipitia zile *procedure* zinazotakiwa? Au alipatikana kwa kuteuliwa tu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili huu mfumo uliwezaje kuingia kwenye *operation* bila kupata *clearance* ya *e-GA* na tukawa na mfumo ambao una matatizo namna hii? Umepeleka matatizo makubwa kwa wakulima wetu. Wakulima wetu huko wanaambiwa mbolea ipo, tunaambiwa mbolea ipo lakini mbolea hawakupata wakulima wetu. Wakulima wameteseka kupata mbolea, wengine wamefia kwenye foleni. Mbolea zingine zimeibiwa, wameenda hawa mawakala 721 wamekuja kuambiwa kwamba tunawafutia leseni kwa sababu eti kwamba wamefanya *double scanning*. Sasa *double scanning* unawezaje kuifanya katika mfumo *proper?* Unawezaje kufanya *double scanning* kwenye mfumo *proper* halafu unamwambia nimekufutia leseni, halafu unamwambia jieleze kwa nini nisikufutie leseni wakati umeshamfutia tayari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria inakwambia toa notisi ndiyo umfukuze, huu mkanganyiko wa kuvunja sheria za nchi unaruhusiwaje kufanyika kwenye Taifa letu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bei elekezi. Wizara ilianza na bei elekezi ambayo haikufanyiwa uhakiki, hawakuhakiki bei elekezi inayotolewa kwa ununuzi wa mbolea na kusambaza mbolea, matokeo yake tumeenda kuwauzia wakulima kwa bei kubwa ambayo haina sababu yoyote kwa matamko tu ya wafanyabiashara. Wizara haikufanya uhakiki wa bei ya mbolea katika viwanda na katika masoko. *TFRA* haikufanya uhakiki huo matokeo yake leo mbolea eti ilipofika Machi baada ya kugundua kwamba sasa mahitaji ya mbolea yameisha nchini, yamepungua sana nchini, ilipofika Machi, *TFRA* inatoa bei elekezi ya shilingi

72,911 kwa mfuko wa *urea* wa kilo 50 kutoka shilingi 116,650 baada ya kuona mahitaji sasa hayapo. Wanashusha bei na *price* haiwezi ikashuka kama jiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *price volatility* na *price elasticity* haiwezi kuruhusu mshuko wa namna hiyo, maana yake ni kwamba hapakuwa na usimamizi mzuri kwenye bei, matokeo yake pamoja na kutoa bei ya ruzuku, lakini ukweli ni kwamba tumeenda kutoa ruzuku kwenye bei *fake*. Sasa ukitoa ruzuku kwenye bei *fake* huwezi kupata *value for money*. Tumewachangia wananchi kulipia, tumetumia *billions of money* za fedha za Watanzania kwa bei ambazo hazina uhakiki, kwa bei ambazo hazina ukweli, matokeo yake tumepoteza fedha nyingi na hatuambiwi, bei mpaka sasa hivi wakandarasi wanatudai shilingi ngapi, mpaka sasa hivi tumetumia shilingi ngapi kwa ajili ya ruzuku ya mbolea na kwa nini tunafichwa vitabu vyoote havizungumzi gharama ya mbolea, mpaka sasa hivi ni shilingi ngapi Tanzania tumelipa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, tunakushukuru sana Mheshimiwa Luhaga Mpina kwa mchango wako na muda wako umekwisha. Nilimuita Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu aweze kuchangia.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja ya bajeti ya mwaka 2022/2023 Wizara yetu ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa dhamira yake ya kukibadilisha Kilimo cha Tanzania akiamini kabisa kwamba tukiboresha kilimo cha Watanzania maana yake ndiyo unaboresha uchumi wao na ni *majority* ya Watanzania ambao wanafanya kazi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nichukue nafasi hii kumshukuru tena Mheshimiwa Rais, nimshukuru zaidi Mheshimiwa Waziri Bashe kwa namna ambavyo watu wa Ikungi tulipokuwa tuna changamoto ya njaa ya upungufu wa chakula wakatuletea chakula cha bei nafuu. Tulipata chakula kile kilitusaidia sana na kwa hakika leo tunaenda kufanya mavuno chakula kile kimetusaidia tunashukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kutupa kibali kupata *NFRA* wasogeze chakula pale kwenye Wilaya yetu na wananchi wale nilikuwa kwenye ziara siku mbili hizi wanatoa shukrani nyingi na wanamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo nichukue nafasi hii kushukuru kwa bajeti, kwa maana ya wasilisho la Mheshimiwa Waziri ambalo aliwasilisha pale jana, ni bajeti nzuri imeonekana kila mwaka inapanda, maana yake ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba kilimo kinakua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaenda mbali ninahitaji nionyeshe tu kwamba kuna *document* kubwa yenye heshima ambayo nchi hii tumeipitisha, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020/2025 inaeleza wazi na inakazia sana suala la kilimo. Ukienda kwenye ile Ibara ya 35 inaeleza wazi kuhusiana na kilimo, imeweka tamko. Imeweka tamko kwamba kilimo cha kisasa ndiyo msingi katika kujenga uchumi na kina nafasi ya kimkakati katika kukuza ustawi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi kwenye ilani imeeleza wazi kwamba makadirio mpaka 2025 tunapaswa tufikie Pato la Taifa tufikie asilimia 28 ya Pato la Taifa. Ukiangalia katika wasilisho la Mheshimiwa Waziri tumewasilisha vizuri kwamba sasa tumefikia asilimia 26.1 maana yake tunaenda vizuri miaka miwili na nusu ijayo huenda tukafikia asilimia 28 ambayo iko kwenye lengo la Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri mnaenda vizuri niwapongeze sana wewe na wataalam kwa kazi nzuri ambayo mnaifanya kwa sababu ni jambo ambalo litaenda kufanya vizuri, wananchi wengi zaidi ya asilimia 65 wanafanya kilimo. Maana yake ukiwagusa asilimia 65 ni kama watu milioni 40 wanafanya kazi ya kilimo katika nchi yetu. Kwa hiyo, nilitaka nianze na hilo ili kwanza kuonesha kwamba tunaona matokeo ya kweli yanaenda vizuri na ambayo kwa kweli tukiyasimamia vizuri na ushauri ambao tunatoa Wabunge huenda tukabadilisha kilimo chetu na kikawa kilimo chenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye eneo ambalo ni mkazo uliowekwa kwenye Ilani ya Uchaguzi. Ilani ya Uchaguzi imesema ni kusimamia kikamilifu hifadhi ya matumizi endelevu ya maji, ardhi ya kilimo na kuongeza miundombinu ya umwagiliaji. Nataka nianze kwenye eneo la umwagiliaji. Ninaamini kabisa tabianchi imeathiri sana kilimo cha Tanzania, siyo kilimo cha Tanzania, cha maeneo mengi Afrika, kama tutaendelea na hali ya kusubiria huruma ya Mungu kuleta mvua peke yake hatutakisogeza kilimo hiki. Kila mwaka tutakuja na sababu kwamba mwaka jana hatukufikia lengo kwa sababu mvua hazikunyesha za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, ninaona kwamba kuna *package* nzuri kwenye eneo la skimu za umwagiliaji. Niombe huenda tunaweza kuweka fedha nyingi, kwanza tunaiona dhamira ya Wizara tunaiona dhamira ya Waziri, tunaiona dhamira ya watendaji lakini tunapelea kwamba fedha hata Wabunge wote wanaomba hapa skimu za umwagiliaji, lakini nani anaenda kuzitunza zile skimu kule chini? Skimu nyingi zimekufa, skimu nyingi hazisimamiwi vizuri. Skimu nyingi hazitoi matokeo lakini kama haitoshi kuna baadhi ya maeneo hata hawajui maana ya skimu zenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo maana yake tunaenda ku-*dump* fedha, tunaziacha pale, hakuna usimamizi. Nikuombe Mheshimiwa Waziri tutafute *mechanism* nzuri ya kusimamia skimu ya fedha nyingi tunazopeleka kwa wananchi kule chini. Ninaamini tukifanya hivyo tutaleta matokeo tunayoyatarajia kwa sababu tusipofanya hivyo tutakuwa hatuna maana yoyote, tunawekeza fedha hakuna uendelevu wowote, maana yake hatuna matokeo ambayo tunayalenga. Tuna maeneo ya mito mingi, tuna maji yanapita kila mahali lakini tusipoyazuia maji na kuyatumia vizuri maana yake kilimo chetu hakiwezi kubadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili Mheshimiwa Waziri nikuombe sana tunajua kwenye Wizara yako umeniangalia katika skimu ya Mang'onyi pale, lakini Mheshimiwa Naibu Waziri mliniambia kwamba mtafanya. Niombe wakati wa ku-*wind up* nataka kusikia watu wa pale Mang'onyi wanataka kusikia Wizara inasemaje. Mwaka huu wa Fedha tujengewe ile skimu tuboreshe kwa sababu sasa hivi tuna soko la mboga mboga katika Mgodi mkubwa wa Shanta ambao uko pale Mang'onyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri baada ya kuwa nimeeleza eneo la skimu ambalo litaleta matokeo nieleze kidogo kwenye eneo la *transformation* ya kilimo katika nchi yetu. Tukitaka ku-*transform* kilimo cha nchi yetu tunahitaji mambo matatu. Tunahitaji utaalamu kwa maana ya *technology* au elimu, tunahitaji uwekezaji au fedha lakini tunahitaji pembejeo ambazo zinafaa katika maeneo yetu. Mambo haya matatu tukifanya vizuri tutakibadilisha kilimo chetu. Leo ukienda kwenye utaalam ni Maafisa Ugani wangapi ambao wana uwezo wa kumsaidia mkulima pale kijijini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Maafisa Ugani wengi Mheshimiwa Waziri, wakulima wana uwezo mkubwa kuliko Maafisa Ugani uliowapeleka kule vijijini. Maafisa Ugani

wamefanana na wananchi lakini wengine wamezidiwa uwezo na wananchi, kuna haja ya kuwasaidia, kuwabadilisha mtazamo wa kazi wanazozifanya. Uwekezaji kama nilivyosema tunaiomba Serikali iongeze fedha za kutosha kwenye sekta ya kilimo ambayo watu milioni 40 wanafanya kazi hii, tukifanya vizuri eneo hili tutaweza kubadilisha kabisa kilimo na uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu ni eneo la mbolea, viuatilifu, na mbegu. Eneo hili tukiongeza utafiti, tukaongeza mbegu za kutosha zinazofaa, zitamfanya mkulima awe na matokeo makubwa kwenye eneo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, nchi hii imekuwa sasa, kutoka Mtwara mpaka Kigoma watu wanataka wote walime zao moja linaitwa korosho, haiwezekani. Hatuwezi kuwa na kilimo cha korosho nchi nzima. Hata mazingira au hali ya hewa hairuhusu. Maana yake hata *concentration* ya namna ya kusaidia kilimo haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani leo kila mtu anataka kulima alizeti nchi nzima. Haiwezekani mtu atoke kule Tandaimba, anataka kwenda mpaka kule Mwanza alime alizeti, haiwezekani Mheshimiwa Waziri! Tufike mahali tuwe na kanda maalum kwamba hii kanda ni ya alizeti. Kama ni Singida, tu-*concentrate* pale Singida na mikoa ambayo inaweza kutoa alizeti. Leo hii mahindi hayawezi kulimwa nchi nzima. Mfano, kama Singida leo, hatuwezi wote kulima mahindi. Tutalima mtama, tutalima uwele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Parseko Kone, aliwahi kuwa Mkuu wa Mkoa wa Singida, alizuia kabisa kilimo cha mahindi kwenye maeneo ambayo hatuwezi kulima mahindi, akasema lazima watu walime mtama. Mtama ukizalishwa kwa wingi, nao ni nafaka, itauzwa, tutanunua chakula kingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuwe wakali, tuwasimamie wananchi, tuwasaidie ili Ilani ya CCM iweze kutekelezwa vizuri, tuwe na usalama wa chakula na mwisho wa siku pato la Taifa liongezeke kupitia sekta hii ya kilimo. Tusipofanya hivyo Mheshimiwa Waziri, tutakuwa tunayumba kila siku, kila mmoja anakuja na *proposal* yake. Lazima sisi kama nchi, tukubaliane kwamba kanda hii ni chakula hiki, kanda hii ni zao hili, mwisho wa siku nchi ikikusanya, tutasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndio nilitaka niyaseme…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kuunga mkono hoja, nawatakia kila la heri.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Miraji Mtaturu. Nilimwita Mheshimiwa Selemani Kakoso, wakati huo Mheshimiwa Mariam Ditopile, na Mheshimiwa Timotheo Mnzava wanajiandaa.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Awali ya yote, naipongeza Wizara kwa kuleta bajeti ambayo inamatumaini kwa Watanzania, lakini yapo maeneo ambayo nataka niishauri Serikali. Nianze kwenye eneo la miradi ya umwagiliaji. Ili nchi iweze kwenda mbele, ni lazima tuwekeze kwenye miradi ya umwagiliaji. Jimboni kwangu mimi ipo miradi ya umwagiliaji ambayo mpaka sasa bado haijakamilika. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri aangalie ule mradi wa umwagiliaji wa skimu ya Karema uweze kukamilika, kwani kila

bajeti inayokuja huwa tunaambiwa kwamba inakwenda kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Waziri aliangalie hili, ahadi zilizotolewa na Mawaziri ni nyingi kwenye mradi ule wa skimu ya Karema, sambamba na ile skimu nyingine ya Kabage ambayo ilianzishwa na Serikali. Kwa hiyo, tunaomba mkakamilishe ile miradi. Yapo maeneo mengine nchini kama tutawekeza kwenye miradi ya umwagiliaji, nchi itakuwa na usalama wa chakula, tutakuwa na uhakika wa uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo napenda kuchangia ni suala la mbolea ya ruzuku ya Serikali. Kwenye eneo hili, Serikali ilitoa fedha na tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuongeza fedha za ruzuku ambazo zimeenda kuwasaidia wananchi, lakini zipo kasoro kubwa sana ambazo zilijitokeza. Mwaka huu kuna baadhi ya wakulima ambao wamekula hasara kwa sababu mbolea zilizopelekwa zile ambazo tulikuwa tunakusudia kwamba zingeenda kuwafanyia kazi wananchi hazikuwa na ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali, mbolea zile ambazo zilikuwa na mashaka, tunaomba sana mziangalie, msije mkafanya makosa makubwa kama yaliyojitokeza, kupeleka mbolea mbazo hazina ubora uliokusudiwa. Hili ni jambo la kufanyiwa kazi na wataalam wafanye kazi ambayo inaweza kupambanua mbolea ambazo zinaweza zikawa na tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kilimo cha tumbaku. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwanza kwa ushawishi wa kuleta makampuni ya ununuzi wa tumbaku. Amefanya jambo jema, wananchi wengi sasa wanaanza kupata manufaa makubwa. Hata hivyo, kuna kasoro ambayo tunamwomba Mheshimiwa Waziri akalifanyie kazi. Mbolea za ruzuku zililoletwa hazijawagusa wakulima wa zao la tumbaku.

Hawa wanatumia mbolea za *CAN*, *UREA*, *SA* na hizo ni miongoni mwa mbolea ambazo zilitolewa ruzuku na Serikali, lakini hawajanufaika na kitu chochote. Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri alifanyie kazi. Ahakikishe mbolea hizi zimewafikia, tena kwenye msimu huu huu ambao wamelima, ziwanufaishe na wao. Ni muhimu sana kwenye eneo hili mlifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili uweze kufanya maboresho makubwa kwenye zao la tumbaku, ni vyema Mheshimiwa Waziri mkaweka fedha ambazo zitakuwa zinafanya maboresho ya kuongeza idadi ya ma-*classifier* wanaoteua zao la tumbaku kupitia Bodi ya Tumbaku. Eneo hili linachelewesha masoko sana. Leo hii Mkoa wa Katavi una *classifier* watatu tu. Mahitaji ni zaidi ya *classifier* sita ambao wana kazi ya uteuzi wa tumbaku. Sasa nazungumzia mkoa mmoja tu, lakini hata ambao natoka, Mkoa wa Tabora, una uhitaji mkubwa, Mkoa wa Shinyanga una uhitaji mkubwa, Mkoa wa Ruvuma na pengine mikoa yote inayolima zao la tumbaku.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri aelekeze mawazo ya kuboresha Bodi ya Tumbaku kwa eneo ambalo wanateua wateuzi ambao ni wa Serikali. Hili tunaomba Mheshimiwa Waziri akalifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri tuweke mkakati wa mazao yale ya kibiashara. Mazao ya kibiashara ndiyo yanayoleta fedha za kigeni hapa nchini, lakini kwa ujumla bado Serikali haijawekeza kwa kiwango kikubwa sana. Mazao haya ni kama yako yatima, yanajiendesha yenyewe bila nguvu ya Serikali. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri aje na mkakati wa kufanya maboresho ili

mazao haya ya kimakakati yaweze kutoa tija kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kakoso kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri, wakati huo Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava pamoja na Mheshimiwa Josephat Mathias Gwajima anajiandaa.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa hii. Kilimo siyo lelemama. Kwa kuanza, naomba nimnukuu Mheshimiwa Waziri ukurasa namba mbili kwenye utangulizi namba nne. Anasema; "Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuanza utekelezaji wa mageuzi kwenye sekta ya kilimo kwa kuwekeza katika miradi ya muda mrefu na maeneo ya msingi ya kutatua changamoto za kilimo kuanzia shambani hadi sokoni na kuitekeleza dhana na falsafa ya msingi kabisa kwenye kilimo kuwa "kilimo ni uwekezaji wa muda mrefu."

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumnukuu Mheshimiwa Waziri, mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni. Tupo hapa Wabunge ambao tulikuwepo Bunge lililopita na Mabunge mengine nyuma. Tangu Mheshimiwa Rais Dkt. Samia aingie madarakani kwenye Serikali ya Awamu ya Sita, na kumteua Mheshimiwa Bashe, kwa mara ya kwanza bajeti ya mwaka 2022 tulipongeza kwamba kilimo kimepewa fedha za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni mashuhuda. Leo hii nilikuwa napiga hesabu ya asilimia mpaka ikabidi niwaulize wenzangu, fedha za miradi ya maendeleo, tuliwatengea shilingi bilioni 569, zimekwenda shilingi bilioni 470. Pamoja na kasoro ambazo amezitoa mwenzangu, najua majibu mazuri

ya Mheshimiwa Waziri yatakuja. Ni asilimia 82 na nukta. Haijawahi kutokea! Jamani, tupigeni makofi na tumpongeze sana Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri kwa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Bashe amekuta kilimo kipo *ICU (Intensive Care Unit),* ameomba pesa kwa ajili ya madawa amtibu mgonjwa huyu, mwelekeo tunauona. Nchi hii tatizo kubwa ni kwamba tunao wakulima ambao kwa asilimia kubwa ni *peasants.* Hatuna *farmers,* tuna *peasants.* Sasa hawa mpaka uwanyanyue, na ubaya zaidi Mheshimiwa Waziri kwenye Wizara yake ana sera na mipango, lakini Waziri huyu hammiliki mkulima. Mkulima yuko Halmashauri kule kwenye TAMISEMI, ndiyo maana amekaa anabuni mambo ambayo sasa mwanga tunauona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe moyo Mheshimiwa Waziri, hata unaposikia hapa watu wanasema, ooh, itakuwaje? Umetupa *forum* ya kuongea, kwa sababu umedhubutu na unafanya. Leo tunaongelea kwamba kwa nini tunaingiza sukari? Kwa nini tunaingiza mafuta? Kwa nini tunaingiza unga wa ngano? Tumeona hizo nchi tunazotoa hayo mazao wamefanyaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge wa vijana, Mheshimiwa Ng'wasi, ametoa mfano wa nchi ile aliyoitaja, namna gani imeweza kuendelea kupitia mashamba haya makubwa. Kwa hiyo, kwa kweli napongeza hatua hizi, tena nampongeza sana Mkurugenzi wa Tume ya Umwagiliaji, Ndugu yangu Raymond. Kwa kweli moyo wa kilimo sasa upo kwenye tume yako. Ameongea Mheshimiwa aliyetangulia kuchangia kwamba tumepeleka fedha nyingi kuweka miradi ya umwagiliaji, weka mfumo mzuri wa usimamizi hii miradi iweze kuwa endelevu. Tunaona hatua nzuri ambazo mnazifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kabla ya kwenda kwenye ushauri wangu kwanza, naomba niongelee Mkoa wangu wa Dodoma. Mimi kwa niaba ya Wabunge wenzangu wa majimbo, napenda kuwashukuru sana Wizara, mmetupendelea Dodoma. Sisi ndio tuna-*pilot* Mradi wa *BBT* pale Chinangali, na hapa ndiyo imeibuka sasa naiwaza hata Dodoma yenye utalii. Leo hii kutokana na jitihada zenu tunaenda sasa kuzungumzia kitu kinaitwa *Agrotourism*. Leo kwenye shamba lile la Chinangali nimeona Mheshimiwa Waziri mpango wako, pale kutakuwa kuna kiwanda cha *wine,* pale kutakuwa kuna *restaurant,* na uzuri umewaza kuweka *private sector. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Msalato ikikamilika, mtalii akitoka nje, anashuka pale, anakuja Ikulu kuangalia, maana Ikulu tuna hadi wanyama mle, na pia atapita kwenye shamba lile kufanya *Agrotourism.* Vile vile ataenda Kondoa, tunayo michoro ya Kolo, tunayo Mkungunero kule, halafu ndiyo hapo ataenda Tarangire na Serengeti. Kwa kweli naunga mkono na ninawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na miradi ya *BBT* kugusa kule Chinangali, Bihawana, Membe na Chemba kule Gwandi, pia miradi ya umwagiliaji tumeipata Chamwino zaidi ya mmoja. Tumepata kule Bahi, Mpwapwa, Dodoma Mjini, Chemba, hata Wilaya ya Kondoa imeguswa, lakini cha kusikitisha tu, kule Kondoa mmegusa Kisese tu ambayo ni *Kondoa DC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina salamu kutoka kwa wananchi na vijana wa Kondoa Mjini, wanasikitika, mbona wao hujawakumbuka Mheshimiwa Bashe? Wanafahamu kwamba Diwani wao wa *Kondoa TC* ndiye Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii. Naomba kule kwenye Halmashauri ya Kondoa Mji tunayo *Mongoroma Irrigation scheme* kwenye Kata ya Seria ambayo ina zaidi ya ekari 3,000. Tunayo *Mlangu Block Farm* Kata ya Seria zaidi ya ekari 1,000; tunayo

*King'ang'a Irrigation Scheme,* Kata ya Kingare zaidi ya ekari 3,000. Ukija kujumuisha, naomba ukawaguse vijana hawa wa Halmashauri ya Kondoa Mji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafanya kazi kwa ukaribu kupitia Kamati, mimi nimshauri tu Mheshimiwa Waziri kuhusu mbegu. Naomba angalia namna ya kuwahusisha wakulima wadogo kwenye kuzalisha mbegu, na pia kwenye sekta binafsi. Huyu *ASA* nashauri abaki kwenye utafiti, abaki kuwa mdhibiti wa ubora wa hizi mbegu. Hebu kundi kubwa hili la *private sector* ulipe; tunao wawekezaji wazuri sana ambao wataweza kuwekeza na kuzalisha mbegu zilizo bora, wewe ukabaki kwenye kufanya tafiti na kudhibiti ubora wa hizo mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona pia kupitia uwekezaji mkubwa wa kwenye umwagiliaji. Leo hii kwa sababu hawa Maafisa Ugani wanasimamiwa na Wakurugenzi. Tumeona changamoto, wamepeleka vifaa lakini ufanisi wa vile vifaa hatuuoni, kwa sababu hauna usimamizi. Umeenda mbali Mheshimiwa Waziri, umewaza kupitia hii Tume ya Umwagiliaji, umeajiri wataalam 320, umeenda kujenga ofisi 121, na pia tumeona mmekabidhiwa magari pale na Mheshimiwa Rais. Hii yote umeona namna gani unaweza kuongeza usimamizi ili sasa uende ukawaguse wakulima wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaambie wakulima wadogo, mimi ni mkulima mwenzenu, hamjaachwa kuwa wanyonge. Ndiyo maana katika malengo ya Wizara hii, ni kupunguza umasikini kwa asilimia 50 ifikapo 2030? Nani wa masikini? Ni nyie. Mipango ipo dhabiti, na ndiyo maana Mheshimiwa Waziri ametafuta mfumo mzuri wa kuwafikia na kuwasimamia, na kwa kweli tunamuunga mkono na tunajua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala hili linaongelewa kuhusu hii *BBT.* Jamani niwaambie, tunataka kuzalisha ajira

mpya milioni tatu. Mnasema tukawafuate wale ambao wako kwenye kilimo, tunataka kutengeneza. Naomba nitoe ushuhuda. Mimi nilimaliza chuo mwaka 2009, nilienda kujiajiri kwenye kilimo. Nilikuwa msomi wa *degree* na nilikuwa mtoto wa kishua. Kwa jina langu tu ningeweza kutumia mazingira yangu kupata ajira, lakini nami nasema, natamani nijirudishe umri nyuma. Kipindi kile angekuwepo Rais Samia na Waziri Bashe, nami ningekuwa mnufaika wa hii *BBT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mtu alitengeneza *terminology* ili kuvutia *education,* akasema *education is sex*. Mheshimiwa Bashe na Msaidizi wako Mavunde na wote Katibu Mkuu, Naibu Katibu na timu nzima, *you are making agriculture sex,* ili sisi vijana ambao ni kundi kubwa tuvutiwe na kilimo tuweze kwenda kuinua maisha yetu na tuweze kwenda kuanzisha matajiri wazawa ndani ya nchi yetu, ambao ni matajiri kupitia kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo pia. Nilimwita Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, wakati huo Mheshimiwa Gwajima anajiandaa.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nitoe mchango wangu kwenye bajeti hii muhimu sana. Nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema ambaye anatujalia uzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nitumie nafasi hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kwa namna alivyotoa jicho la uhakika kwenye sekta ya kilimo. Kipekee nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na watendaji

wote wa Serikalini wakiongozwa na katibu Mkuu. Kiukweli Mheshimiwa Bashe, sisi vijana tunajifunza kwako na kwenu, na tuna imani kubwa na ninyi, na tunaridhika na kazi nzuri mnayoifanya. Kwa sababu hiyo nitakuwa na mambo madogo tu mawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza ni la umwagiliaji. Kipekee sisi wananchi wa Korogwe tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri. Tumeimba muda mrefu habari ya Bonde la Mkomazi. Tumekuwa na hadithi nyingi, wewe ni shahidi tangu ukiwa Naibu Waziri na mwenzako Mheshimiwa Mgumba, lakini mwaka jana 2022 uliniahidi ukasema, mdogo wangu tunatenga fedha, tunarudia upembuzi yakinifu na usanifu, na mwaka unaofuata tutakwenda kwenye ujenzi. Hakika mkataba umesainiwa na nimeona kwenye bajeti ukurasa wa 25 umenihakikishia kwamba kwenye bajeti hii ujenzi wa skimu hiyo unakwenda kuanza kwenye mwaka wa fedha unaokuja. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninawashukuru Mawaziri hawa kwa usikivu wao. Nimekaa nao kawenye vikao akaniambia nimwandikie, nikamwandikia. Kwenye bajeti, nimeyaona mabonde yale ya Magoma. Ukarabati wa skimu ile ya Chekerei, skimu ya Magila na eneo lile la Mayuni kule Mapangoni nimeona, nawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili la umwagiliaji sina cha kuchangia, zaidi nawashukuru sana. Tunaomba tu kazi hizi ziende kwa *speed* ili tuweze kuwanufaisha wakulima wetu na wananchi wa Korogwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni eneo la kilimo cha zao la mkonge. Sisi watu wa Mkoa wa Tanga ndio tunaongoza kwa uzalishaji wa Mkonge kwenye nchi hii. Unaposema Mkoa wa Tanga unaongoza kwenye uzalishaji, anayeongoza ni Wilaya ya Korogwe hasa Korogwe Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa namna walivyorudisha matumaini ya wananchi wa Korogwe na Mkoa wa Tanga na Tanzania kwa ujumla kwenye zao la mkonge. Tulijengewa dhana kwamba mkonge ni zao la wakulima wakubwa wenye fedha nyingi, wenye maeneo makubwa ya kulima, lakini imani mliyoijenga kwa wananchi wa Mkoa wa Tanga, imani mliyoijenga kwa wananchi wa Korogwe na wakulima wa mkonge, imewarudisha watu wa Tanga na watu wa Korogwe kwenye kilimo cha mkonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri mwaka 2020 nchi yetu tumezalisha Mkonge tani 37,022, lakini katika hizo wakulima wadogo walizalisha tani 26,000. Mwaka 2021 tumealisha tani 39,484, wakulima wadogo wamezalisha tani 24,000. Mwaka 2022 uliopita, tumezalisha tani 48,351, wakulima wadogo wamezalisha tani 22,000. Kwa miaka hii mitatu iliyopita, jumla kama nchi tumezalisha tani 124,858.39, na katika hizo wakulima wadogo mchango wao ni tani 73,420 sawa na asilimia 58.8. Kwa takwimu hizi huwezi kubeza mchango wa wakulima wadogo kwenye uzalishaji wa zao la mkono. Kwenye hotuba yako umesema na kwa mujibu wa takwimu za Bodi ya Mkonge wakulima wenye mkonge mdogo ambao haujapita miaka miwili wakulima wadogo sasa hivi wenye mkonge mdogo hawajaanza kuvuna, wana hekta 3,545. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema nini? Uzalishaji huu moyo huo wa wakulima wadogo ili uende vizuri naomba tuzingatie mambo mawili. Jambo la kwanza; mkonge kama mkonge majani hayani maana, maana ya mkonge ni nyuzi baada ya kusindika. Wakulima wadogo wanachangamoto kubwa sana ya mashine za kusindika mkonge kule Korogwe na *AMCOS* zile tano kuna mashine za kuchakata mkonge za Sasalana nilisema mwaka jana tunashukuru wamejirekebisha wanakwenda vizuri. Lakini wakulima wana uhitaji wa mashine ukiangalia uzalishaji huu, ukiangalia idadi ya eneo la

mashamba mapya waliyokuwa nayo wakulima wetu na kazi wanayoifanya sasa baada ya miaka miwili kutakuwa na *crisis* kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Mheshimiwa Waziri, alihaidi kwenye Bunge hili kwamba wanakwenda kununua mashine mbili kubwa za kuchakata mkonge wa wakulima kila tukiulizia tunaambiwa manunuzi bado ningetamani baadae ukija utuambie kwenye eneo hili Mheshimiwa Waziri mmefikia wapi? Lakini Mheshimiwa Waziri, wakulima wadogo kupitia *AMCOS* zao walitaka kuchukua mikopo kwenye taasisi za kifedha lakini mpaka leo taratibu zimekuwa ngumu wanakwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana tumesema hapa Mheshimiwa Waziri kwani hii Benki ya Kilimo ni kwa ajili ya kina nani? Kwanini Benki ya Kilimo iisiingie kusaidia *AMCOS* zetu hizi? Benki ya kilimo isibaki na wakulima wakubwa tu tuwasaidie *AMCOS*, tutumie benki ambazo ziko tayari, tuwe na madirisha. *AMCOS* zikopeshwe wakulima wapate mashine ili waende wakasindike mazao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo jingine bodi imegawa mashamba na nimesoma vizuri kwenye hotuba yako mmesema mmeishagawa hekta zaidi ya 3,829. Ombi langu na watu wa Korogwe tunaomba kwenye kugawa mashamba pamoja ya kwamba ardhi hii ni ya nchi nzima wapeni kipaumbele watu wa Korogwe kwenye yale maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwisho ni kwenye mkonge. Mwaka jana tumesafirisha nje tani 32,627 sawa na asilimia 67.5 lakini kwa miaka mitatu iliyopita nyuzi za mkonge zinakwenda nje ni zaidi ya asilimia 71 ya uzalishaji wa mkonge wote. Kupeleka nyuzi za mkonge nje ni kuuza ajira za watu wetu, kupeleka nyuzi za mkonge zote hizi asilimia 71 nje ni kupunguza kodi tunapata kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Serikali Mheshimiwa Waziri tunao watalamu wa uchumi, tunao watu wanafanya *economic intelligence* hivi tunashindwa kwenye kujifunza tunakopeleka mkonge? Wanazalisha nini? kwa ajili ya soko lipi? Tukafanya mikakati ya kuwavutia wawekezaji kuja kufunga mashine na viwanda Tanzania vya kuchakata mkonge, tusafirishe matunda ya mwisho siyo kusafirisha nyuzi. Tukisafirisha nyuzi tunapoteza ajira za watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimwia Waziri, mwaka jana kwenye hotuba ukurasa wa 165 na 166 ulisema vizuri sana kuhusu kuielekeza Bodi ya Mkonge kuongeza nguvu ya kuvutia matumizi ya magunia na nyuzi za mkonge naku–*discourage* bidhaa zile nyingine zinazoharibu soko la mkonge. Bahati mbaya mwaka huu kwenye hotuba yako sikuiona na bahati mbaya sana kwenye nchi yetu kuna viwanda nane vinavyoshulika na mazao ya mkonge kwa maana ya nyuzi za mkonge. Lakini leo tunapozungumza viwanda hivi nane vinavyofanya kazi vizuri ni viwanda vitatu tu kati ya viwanda vile nane na idadi ya uzalishaji wake ninayo hapa. Mheshimiwa Waziri siyo jambo zuri viwanda vinaendelea kufa, vinaendelea kupungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulijifunza kwenye *COVID*, ikitokea tuna majanga tujifunze kwenye vita ya Urusi, ikitokea kuna majanga masoko ya nje hayafanyi vizuri hatma yetu ni nini? Hatma ya wakulima wetu ni nini? Ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili moja ya jambo linalo–*discourage* uzalishaji wa vifaa vya mkonge kwenye nchi yetu ni sheria tulizokuwanazo na usimamizi wa sheria tuliyonayo. Sheria ya Forodha ya Afrika Mashariki ina ruhusu msamaha wa kodi kwa nyuzi za plastiki…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** …ni vizuri watu wa uvivi inawasaidia lakini tukazikague ili zitumike kwa matumizi yaliyokusudiwa na zisiende zaidi ya hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. nilimwita Mheshimiwa Josephat Mathias Gwajima, aweze kuchangia.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuchangia lakini pia nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo siku kwa siku anaendelea kuongeza bajeti ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nilitishwa sana, wakati Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Magu Mheshimiwa Kiswaga anachangia alisema maneno yafuatayo; nayanukuu alisema kwamba; "Watu wa Jimbo la Magu wamelima mpunga au mahindi na hapo katikati mvua imekatika kwa hiyo, mahindi yamekauka kwa namna yeyote ile watahitaji mahindi ya msaada mwaka ujao kwa sababu watakuwa na njaa" nanukuu alivyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliposikia maneno hayo nilitishika sana na kuogopa sana lile eneo ambalo Mheshimiwa Kiswaga, Mbunge wa Magu analitamka liko eneo mita 300 kutoka kwenye Ziwa Victoria narudia tena mita 300 kutokea kwenye Ziwa Victoria mahindi yamekauka na watahitaji chakula cha msaada mwaka ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme mita 300 ni nini? Kiwanja cha mpira kina mita 100. Mita 300 ni viwanja vitatu vya uwanja wa mpira ukiviunga kwa pamoja. Kwa hiyo, wananchi wana mashamba mita 300, mahindi yamekauka, mpunga umekauka, mwaka kesho Serikali itahitaji kuwapa

chakula cha msaada au mahindi ya msaada watu wanaoishi kati ya maji yenye uwezo ambayo maji wanaweza wakatumia kwa ajili ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tukubali *there is a problem that we must addresses the country* lazima tukubali asiyekubali anatatizo binafsi. Sasa basi kwa kusema maneno haya nataka kusema kwamba *unless* tumefika kwenye *agricultural revolution* kwa maana ya kuhamisha kilimo chetu na kuingia kwenye kilimo cha umwagiliaji hatutafaulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme dunia inakabiliwa na majanga mbalimbali yanayosababisha mabadiliko ya tabianchi na pia mabadiliko ya tabia za wanadamu. Kwa mtu yeyote anayejua *projections* za dunia, shida ya mvua, mabadiliko ya hali ya hewa yataendelea kuendelea miaka ijayo kwa wingi sana ni kitu gani ambacho kinatuzuia kuwekeza kwa nguvu nyingi sana kwenye suala la umwagiliaji kiasi kwamba tufike wakati tuhame kabisa kwenye kilimo cha kutegemea mvua tutegee umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nani atakaye kuelewa ukisema kwamba mwaka kesho Serikali inategemea kutoa chakula cha msaada kwa watu wanaolima mita 300 kutoka Ziwa Victoria wapate cha msaada? Ni kitu gani hiki kinaendelea? Ni kukosa maono ya muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme watu wanasema hivi kuna namna mbili ambayo kiongozi yeyote tukiwemo Wabunge anatakiwa kuona mambo. Namna ya kwanza *a leader must see far more than others* kiongozi lazima aone mbali kuliko wengine, *a leader must see more than others* kiongozi lazima aone zaidi ya wengine, *a leader must see before others* kiongozi lazima aone kabla ya wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunaona tayari kwamba mwaka kesho tutahitaji chakula cha msaada kwa watu wanaoishi mita 300 kutoka kanda ya Ziwa ya Victoria na wana mashamba pale. *Then what do we say?* Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo rafiki yangu Bashe ushauri mamlaka tuwekeze sana kwenye kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya vizuri *so far so good, so far so good,* lakini nilikuwa nakushauri tuwekeze sana, sana kwa sababu mabadilikoo ya hali ya hewa ukiangalia vita duniani mabadiliko ya jiografia, mabadiliko ya kisayansi yanategemewa kuwepo tena na tena. Kwa hiyo, na sisi tuone kwa mbali tuweze ku–*invest* kwenye umwagiliaji kwa kuwa nchi yetu na Mikoa yetu imezungukwa na maziwa ya kutosha, huo ni ushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nikuhusiana na Benki ya Mbegu za Asili. Mwaka 1980 watu walianza mchakato wa kuanza Benki ya Dunia ya Mbegu za Asili na kufikia 2008 kule Norway karibu na *north pole* wakakamilisha kutengeneza benki ya mbegu ya asili ambayo ina mbegu zote za chakula duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipata bahati ya kuingia kwenye hiyo benki ya mbegu nikaona *literature* moja, nilikuwa *interested* kujua kwanini benki ya mbegu? *Literature* moja inasema benki ya mbegu kwa sababu watu wana wasiwasi yanaweza kutokea majanga duniani yakaharibu mbegu ama kwa vita ama kwa silaha za *nuclear* wao ni watakuwa sehemu ya kuuza na kusaidia mbegu duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya pili kwanini benki ya mbegu duniani? Wakasema ni kwa sababu wanahisi kwamba siku zijazo mbegu itakuwa ni biashara kubwa kuliko biashara zote duniani. Hili nalithibitisha kwanza mbegu tulizonazo sasa hivi nyingi ni *genetic modified seed* zinatoka

Ulaya zamani ukipanda yale mazao unayo yavuna unayafanya kuwa mbegu ya mwaka ujao hizi mbegu *genetic modified seeds* ukipanda yale mazao, ukiyapanda hayawezi yakaota tena inabini ununue na ununue na ununue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utumwa wa mbegu unakuja duniani, narudia tena utumwa wa mbegu unakuja duniani na *genetic modified seeds* ni nini? Ni mbegu ambazo zimetengenezwa ki–*genetic* zimewekewa *RNA information* zina taarifa ndani yake mlaji aweje? Kwa ajili ya nini? Kwa jili ya mambo yajayo waswali wanasema anaekulisha anaamua hatma yako, anaekulisha anaamua utaishi muda gani? Utakuwa na akili gani? Utakuwa na afya kiasi gani? na Taifa lako litakuwaje hapo badae? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri, nashauri sana Wizara ya Kilimo tuweke fedha kwenye taasisi zetu za utafiti tuwe na utafiti wa mbegu zetu za asili na tuwe na benki ya mbegu zetu za asili hapa Tanzania ili ikitokea janga lolote tutatumia mbegu zetu za asili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Josephat Mathias Gwajima, ahsante sana, tunakushukuru. Sasa namwita Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga Sanga wakati huo Mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa ni Mhandisi Ezra John Chiwelesa.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga na Wabunge wenzangu kwamba aijawahi kutokea, nampongeza sana Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuongeza bajeti ambayo haijawahi kutokea mwaka jana bajeti iliongezwa nyingi, mwaka huu yaani ndiyo yameongezwa ma-bi na ma-bi na ma-bi. Kwa hiyo, tunampongeza sana Mama. Vilevile tunampongeza Bashe

pamoja na Naibu wake na Katibu Mkuu na watendaji wake wote kwa kazi nzuri wanayoitendea haki Wizara hii ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu uliyopita tulipopata fedha za ruzuku kule Njombe na najua na wenzangu wengine, Wabunge wenzangu tunakupongeza sana. Mpango huu ndiyo umeongeza mazao ya kilimo mbalimbali kwa sababu baadhi ya wakulima walikuwa wanashindwa kununua mbolea kwa sababu ilikuwa bei juu kutoka shilingi 140,000, shilingi 150,000 leo shilingi 70,000, shilingi 60,000 mfumo ulio uweka tunakupongeza sana. Ombi letu sisi watu wa Njombe mfumo huu uboreshwe, uongezwe mawakala zaidi kwa sababu baadhi ya mawakala walikuwa wachache kwa hiyo hawakufikisha sawa sawa foleni ya wananchi ilikuwa ni kubwa. Kwa hiyo tunakuomba uboreshe mfumo, uongeze zaidi mawakala ili waweze kusambaza mbolea za ruzuku kwa wakati unaostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekitiki, vilevile lakini kwa Njombe nimpongeze sana Mkuu wa Mkoa Anthony Mtaka kwa namna alivyoungana na wewe kuhakikisha watu wote waliyojaribu kuchanganya mbolea na michanga walikamatwa. Waliyochanganya mbolea feki walikamatwa kwa hiyo tunampongeza sana Anthony Mtaka kwa kushirikiana na wewe kuhakikisha kwamba watu wanaofanya ujanja pamoja na Mkuu wetu wa Wilaya Kisa Gwakisa waliweza kusimamia vizuri zoezi hili la Njombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile lakini nitaendelea kumpongeza pia Anthony Mtaka sisi Njombe katika Mkoa wetu Wilaya na Makete ndiyo inayozalisha sana ngano. Kwa hiyo tuna washukuru kwa kuunga mkono jitihada za Mkuu wa Mkoa, kwamba sasa Wilaya ya Makete ndiyo kuwe habu ya kulisha Tanzania na nchi ya Tanzania zao la ngano kwa hiyo tunakupongeza sana Waziri kwa kukubali wazo hili na tunampongeza Mama lakini pia Mheshimiwa Waziri Bashe,

mtulie vizuri. Wenzangu wamesema hapa wewe ni kijana, wewe ni kijana kweli ubunifu huo unaoendelea nao ndani ya Wizara yako wako watu wengine wanakubeza. Hao wewe songa mbele ndiyo unapatia. Kwa hiyo sisi tunakitakia kila la kheri uweze kufanikisha vizuri katika mpango huu ambao Mama amekutengea fedha nilizosema hapa ma bi na ma bi sasa yanakwenda kuwa na ma ti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho hili siyo liko kwenye Wizara yako Mwigulu Waziri wa Fedha nilimuona hapa. Nikuombe sana Mwigulu mwaka jana mwezi wa nane Rais alipokuja ulikuepo na wewe Bashe ulikuwepo mkumbushane wananchi wa eneo la kituo cha polisi cha Makambako Mjini fidia ambayo unagharimu shilingi milioni 235 na Rais alihaidi pale kwamba fedha hizi zitolewe. Nimuombe Mwigulu sasa muda umefika aweze kutoa fedha hizi ili wananchi hawa waishi kwa amani kwa sababu wanaishi kwa tabu sana nyumba zao zimebomoka, hawawezi kufanya kitu chochote wanategemea uwalipe fidia ili wakaweze kuishi mahala pengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna zao la parachichi Njombe. Mheshimiwa Bashe tukuombe utakapokuwa unamaliza hapa kutoa majibu ya haya Wabunge tuliyochangia unipe na majibu haya sisi Njombe ndiyo wakulima wakubwa wa parachichi Mkoani Njombe. Zao hili kama nyinyi Serikali maana watu wanao nunua wanatoka sehemu mbalimbali muwe na tamko la Serikali kwamba soko lake liko wapi? maana wananchi sasa wamejikita sana kuvunja mashamba yao ya miti na kulima maparachichi sasa isije ikatokea kama Mbunge mwenzangu mmoja amechangia hapa kwamba nchi nzima sasa wamesema walime korosho na sisi hapa isije ikatokea tukalima zaidi parachichi wakati soko kamili hatujapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyo akija hapa utuambie soko kamili la parachichi liko wapi? na uhakikishe kinajengwa

kiwanda cha parachichi katika Mkoa wetu wa Njombe, cha parachichi ili wananchi wawe na kizazi na kiza kwamba wataendelea kulima parachichi lakini vinginevyo Bashe na timu yako leo nisingependa sana nichangie nakupongeza sana wewe pamoja na Naibu wako pamoja na Katibu Mkuu pamoja na Wizara yote kwa ujumla mshikamane. Sasa kwa mwaka huu wa Kilimo wa 2023/2024 mtakapokuwa mnatuletea mbolea Njombe mtuletee kwa wakati lakini la pili muongeze mawakala kama nilivyosema. Vinginevyo Bashe nakushukuru, endelea na kazi nzuri unaifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sanga, ahsante sana kwa mchango wako. Nilimwita mchangiaji wetu wa mwisho Mheshimiwa *Engineer* Chiwelesa.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Nashukuru kwa kunipa nafasi namimi pia niungane na wachangiaji waliyopita kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kunyanyua kilimo cha nchi hii. Maana tunajua vipaumbele ni vingi lakini unapoona umeamua kuelekeza pesa polini ukakate mapoli hatimaye upate chakula na urudi mijini watu wafurahie ni uamuzi wa busara na ni uamuzi wa kijasiri lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Bashe na msaidizi wake na Watendaji wote wa Wizara hii kwa maono makubwa ambayo Bashe amekuwepo nayo maana amejipambanua kama Mkulima na maono haya yanatimia kwa sababu amepata Mheshimiwa Rais kumshika mkono na tunaona mambo yanaenda na pesa hizi ambazo zinatoka na zinaendelea kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile pia niishukuru Serikali hata sisi Biharamulo kwa mara ya kwanza katika historia tumeenda kujengewa skimu ya *irrigation* siyo jambo dogo hili kwa hiyo neema hii na sisi imetuangukia. Ukurasa wa 207 wa Hotuba yako Mheshimiwa Waziri, tutajengewa Mradi wa

Mwiruzi hekta karibu karibu 1,300 kwa hiyo hili jambo kubwa kwa wakazi wa Biharamulo tukushukuru. Hata hivyo sasa baada ya hayo nijikite mimi kwenye mambo mawili au matatu, mawili kama muda utapatikana yatakuwa matatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kutaja zao la kahawa bila kuitaja Kagera kwa sababu *history* inaonyesha mnamo karne ya 16 wenyeji wa Mkoa wa Kagera ndiyo waliyoingiza kahawa Tanzania wakitokea Ethiopia. Kahawa aina wa robusta na kwenye mauzo mpaka sasa kwenye andiko hili nililonalo la Tanzania *coffee industry development strategy* ya 21 – 25 la Bodi ya kahawa ukurasa wa 19 nimepitia nikawa naangali uzalishaji wa kahawa na *trend* ilivyo. Kahawa aina ya robusta kwa sehemu kubwa inazalishwa Kagera na *percentage* ya uzalishaji ya asilimia 44 *so far* kati ya asilimia 100 sasa tukija kuangalia *expansion* na *project* hii ambayo inafanyika kuna habari ya kugawa miche ya kahawa. Tumeona watu wa robusta tulicho pangiwa katika miche milioni 20 tumepangiwa kuwa tunapewa miche milioni tano tano sasa unajiuliza wewe unaezalisha 44 *percent* unapewa *five million* mwenye *fifty six* anapewa *fifteen million* sasa hiyo unajiuliza nikuirudisha Kagera chini au kuinyanyua Kagera ili iweze kuendelee kufanya kazi kama kweli unataka kuturudisha kwenye zao la kahawa kama vinara wa kahawa ebu hata miche inayopangwa tupewe *forty four percent* kama *share* yetu ambayo tunamiliki katika soko ili hiyo iwasaidie wakazi wa Kagera waweze kunyanyuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo ukiangialia gharama ya uzalishaji wa hii miche ni kubwa sasa Mheshimiwa Waziri mimi nilitaka nikuombe na nitoe ushauri, wenzetu ya Uganda wanachokifanya wanatumia *tissue culture*. Tuko kwenye *volume mass production* ya miche ya kahawa ndiyo inabidi twende nayo. Mheshimiwa Waziri sasa tukuombe najua wewe ni mbunifu, umekuwa kinara wa ubunifu kama ulivyoanzisha *BBT* rudi maabara nyanyuka na *tissue culture* hii tukimbizane na wenzetu Waganda itatusaidi

kututoa hapa tulipo. Pesa kubwa unayotengwa cha kwanza haitokuwa na magonjwa ya kahawa kwa hiyo itatusaidia tutapata *mass production* ya miche lakini hakutakuwa na ugonjwa hata tunapo otesha hii miche itastawi na itakuwa kwa ajili ya manufaa ya hao wananchi hilo nikuombe uliangalie halafu tupewe *share* yetu ya *forty four percent* ukishamaliza kuzalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile pili hata migomba Mheshimiwa Waziri. Migomba ya Kagera tumeta ugonjwa sana wa mnayauko rudini maabara ulitupeleka Kibaha maabara nzuri sana pale iliyojengwa rudi pale weka *tissue culture* hata kwenye habari ya migomba ili iweze kutusaidia kwa hayo nikuombe uweze kutusaiodia ili sasa Kagera turudi kwenye hadhi yetu ya kahawa na migomba hatimaye uchumi huu ambao Mama Samia anaunyanyua na sisi uweze kutugusa. Iko habari ya Tumbaku Mheshimiwa Waziri, niliongea hapa kwa ajili ya wakulima wa tumbaku wa Biharamulo tunapeleka tumbaku kilomita 250 kwenda kuuza kwenye Mkoa wa Kitumba wa Kahama. Tunakuomba wakulima wa Biharamulo wana wasiwasi kwanza kama vile kuwapeleka Kahama wanaanza kuwa na wasi wasi kama wanaenda kuibiwa. Kwa sababu wanasema ikishafika pale akapangua *grade* hawezi kuibeba airudishe nyakaura au airudishe Kalenga au airudishe Nyanza matokeo yake anakubaliana na bei pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti sasa nimuombe Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anamaliza naomba tumbaku ya Biharamulo inunuliwe Baharamulo isitoke nje ya Wilaya yetu. Hilo nakuomba utusaidie na uweze kuisimamia lakini Mheshimiwa Waziri niliomba pia habari ya mbolea ya ruzuku ya tumbaku najua *World Bank* na *IMF* wanapinga hiyo hasa kwenye mbolea ya *NPK* tusaidie tafuta jinsi ya kusaidia maana wakulima wote ni wa kwako. Tafuta jinsi ambavyo unaweza najua wewe ni *intelligence* sina haja ya kukufundisha lakini naamini liko jambo unaweza ukafanya

hata wakulima wa tumbaku wakanufaika hujawahi kushindwa jambo Mheshimiwa Bashe, hilo naomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tuliomba pia kwenye habari ya mbolea wamesema hapa wenzangu mbolea isiyo na ubora. Tangu Serikali ya Awamu ya Nne kumekuwa na malalamiko makubwa sana juu ya *quality* ya mbolea inayozalishwa hapa nchini sina haja ya kutaja kiwanda. Sasa nikuombe hata wewe mwenyewe *at some extent* nimekusikia ukiongelea habari ya mbolea isiyo na ubora mpaka ukaifutia ruzuku, sasa tuombe huwezi kufikia huko mtaani hili ni Bunge wananchi wale waliyopelekewa mbolea isiyo na ubora wamepata hasara na ile mbolea wameilipia. Utakapokuwa una *wind up* tusikie kauli ya Serikali juu ya mwenendo mbovu uliyopigiwa kelele wa kiwanda hiki tupate kauli humu ndani. Wananchi wa Tanzania wanaopewa mbolea feki au mbolea mbovu isiyo na *quality* waendelee kuumia au mbadilishe mtafute jinsi ya kuwasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile pia katika kitu kingine ambacho niliomba na nilijibiwa kwenye Bunge la mwezi wa pili tunaomba mbolea isogezwe karibu. Mimi nina watu leo wako Kalenge kilomita 70 na unamwambia aje Biharamulo Mjini kuchukua mbolea mifuko miwili au mifuko mitatu kwa sababu mlitujibu kwamba mnapeleka katika ngazi ya *AMCOS* tunaomba mbolea safari hii zifike vijijini na wananchi wazipokee kulekule kwao hiyo itawasaidia wananchi wasihangaike na hatimaye tutawapunuguzia hata uchovu na usumbufu mwingine wa pesa ambao wanakuwa wanaupata pale wanapoenda kuchukua mbolea mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo na kwa sababu ya muda naomba kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa uchangiaji na kabla sijahitimisha ninaomba kutambua Wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ambao ni viongozi wa vyama vya msingi vya ushirika, karibuni sana, karibuni sana Bungeni. Ninahairisha Shughuli za Bunge mpaka jioni saa kumi kamili. *(Makofi)*

*(Saa 7.04 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 10.00 Alasiri)*

*(Saa 10.00 Alasiri Bunge Lilirudia)*

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano na yako majina hapa ya wabunge ambao tutaendela kuwasikiliza michango yao. Tutaanza na Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix ajiandae.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nianze kwa kusema ninaunga mkono hoja. Ninampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri lakini pia ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuongeza fedha kwenye Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono mapema kwa sababu najua muda hautoshi; lakini nataka kutoa ushauri ambao Mheshimiwa Waziri usiutafsiri kama napinga lakini nataka kuliboresha jambo hili ili liwe na nyama nzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naangalia kwenye takwimu mbalimbali za kidunia, nikaangalia nchi gani duniani inaongoza kwa kuuza nanasi; na nimekwenda huko kwa sababu kwetu Geita tunalima nanasi, na inauza nanasi za kiwango gani na wanunuzi wakubwa ni kina nani.

Mheshimiwa Spika, Costa Rica wanauza nanasi nje zaidi, wanauza tani 2,900,000, na kupitia nanasi wanapata 1.7 *USD billion*. Anayefatia pale chini ni Philippines, halafu anafuata Indonesia ambaye anauza tani milioni mbili na kitu, ambaye anafata *1.4 billion*. Anakuja Philippines. Afrika nzima mtu anayeuza nanasi kwa wingi ni Nigeria, ambaye anauza 1.5 *million tones;* na katika hapa anapata zaidi ya dola 700,000,000.

Mheshimiwa Spika, kwa nini nimechukua eneo hili, na ukiangalia sasa kwenye *market share* Costa Rica anauza asilimia 51 ya mananasi kwenye nchi hizo za Ulaya. Anafuatia Philippines kama nilivyosema na hao wengine. Kwa nini nimechekua takwimu hii? Tuliwahi kutoa ushauri humu Bungeni, yapo mazao ambayo si kipaumbele na hayajawahi kuwa kipaumbele lakini yana uwezo wa kutuletea mabadiliko makubwa kwenye uchumi wa nchi. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, takwimu hizi ambazo ninazitoa ni takwimu ambazo kwetu sisi hakuna muujiza. Kinachowasumbua wakulima walioko Geita leo kwa nini hawauzi nanasi nje, ni kwa sababu wanalima matunda ya kula hawajasaidiwa kutafuta mbegu ambayo wanaweza ku-*export*. Sasa kama tunataka kuleta mapinduzi katika eneo hili, ni mfano mzauri sana Mheshimiwa Waziri ukapeleka *block farming* katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, nimefanya hii *study* nikaenda kwenye andiko moja la mtu mmoja wa Nigeria ambaye alikuwa *sponsored* na *Rockefeller;* wamegundua kwamba ili waongeze mauzo ya nanasi na mihogo nchini Nigeria na Ghana wakaingia kwenye *block farming*. Walichokifanya wao, cha kwanza umefanya wewe, umetafuta ardhi, *thats fine;* walichofanya cha pili wakatafuta *credit facility,* nani atakwenda kutoa *credit* pale, na hii ni *MOU* ya mkulima na yule anayeenda kutoa fedha. Utapewa fedha unayoitaka kwa *MOU*. Lakini la tatu huyo anayekupa *credit* amekuwa *connected* na masoko, kwa hiyo hautakuwa na tatizo na soko.

Mheshimiwa Spika, sasa sisi ambacho tungeweza kukifanya, wakulima wa nanasi, hao ambao ni kama *neglected*, wanalima madawa sijui ya kienyeji sijui nini, na Ulaya wanapokea nanasi zilizokaushwa sio nanasi mbichi. Sisi tunashindwa wapi hapa? Miaka michache nyuma *avocado* ilikuwa inalimwa nchi nzima lakini ilikuwa haiuzwi nje. Kuna mtu akaleta *specie* ya *avocado* akajua hii *specie* ina soko Ulaya akaenda Ulaya, leo tumeangalia kwenye takwimu Mheshimiwa Waziri, nchi inakata kata deni kutokana na mauzo ya *avocado*. Kwa hiyo kinachosumbua sasa ni aina ya *specie* ambazo ziko sokoni.

Mheshimiwa Spika, na wakulima wetu wala hawahitaji nguvu nyingi. Nimesema hapa kwamba kule Geita wako tayari, Costa Rica wanalima hekta 40,000 peke yake, wanapata 1.7 *bilion USD*. Kule Geita ambako mimi natoka, takribani Jimbo zima la Musukuma wanalima nanasi. Kwa hiyo *you could make it a block farming* halafu wewe ukapeleka *credit* ukapeleka mbegu inayopuzwa Ulaya, ukapeleka wanunuzi wa masoko yale, uka-*transform* kile kilimo kuwa kilimo cha kisasa tukapata fedha nyingi kuliko hata fedha ambazo zinapatikana kwenye pamba na mazao mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, Mheshimiwa Waziri alinifata nilipochangia kwenye hotuba ya Waziri Mkuu, akaomba ku-*share* na mimi jambo hili. Sina mgogoro na *block farming,* shida yangu ni moja tu. Tanzania leo, amesema hapa muhamasishaji mmoja*, almost 30 percent* ni watu chini ya miaka 18. Ukiwapa watu leo wenye miaka 25, ukawapa hati ya miaka 60 hao wenye miaka 18 *ten years to come* wenye miaka 15 watakuwa na miaka 25. Kama *project* unataka iwe *sustainable* walichokifanya Nigeria wamewa-*connect* hawa na wale wanunuzi na wakawapa hekta mbili za mkataba. Na yule anapopewa ana-*access* kwenye fedha, anauza, baada ya miaka ile anayopewa kimkataba ame-*graduate* anakwenda kufanya kutafuta mashamba kwenye maeneo yake mengine.

Mheshimiwa Spika, sisi kwa *population* tuliyonayo hawa tulionao wote wakifikia huo umri wa kuhitaji kukopeshwa, kama hii ndiyo *source* ya ajira, na mimi nafurahi; Mheshimiwa Waziri kwa sababu unataka kutengeneza ajira 1,500,0000; *market seekers* wa kila mwaka wanaotafuta kazi wanaoingia kwenye kutafuta kazi kila mwaka wanafika takriban 800,000. Sasa ukianza kumilikisha ardhi kwa miaka 60 nataka nikwambie *after* hii miaka mitatu hautakuwa na ardhi ya kumpa mtu yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ziko nchi Jirani tunazo, ardhi nzima inamilikiwa na watu. Nahofia tunaeza kuelekea huko. Kuna nchi ambayo ukienda hata kupata heka moja hakuna, Serikali haina ardhi. Sasa mimi umeshanipa miaka 60 na kuna mtu anategemea kweli, Kanyasu atakuwa mkulima maisha yake yote, yaani mimi nina miaka 25 leo umenipa hati nilime miaka mitano, halafu niendelee kuwa mkulima hadi nifikishe miaka 50 ambayo ninayo leo, kweli? Inawezekana? Zamani mimi nilikuwa mvuvi, nimesomea uvuvi, nime-*practice* uvuvi miaka 10 nimeacha sasa hivi Mbunge.

Kwa hiyo, hao mliowapa miaka 15 ijayo wamejaa humu Bungeni, watakuja kuwa Wabunge. Sasa una uhakika gani kwamba una mkataba hawatabadili kazi? Mheshimiwa Waziri ni ushauri tu lakini naunga mkono. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsannte sana. Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, atafuatiwa na Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya ajiandae.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipatia nafasi hii na mimi iwe mchangiaji kwa jioni hii ya leo. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kunijalia afya ili niweze kusimama katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba kipekee nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa jitihada zake za kuhakikisha kwamba kilimo kinapewa msukumo kwani ni ukweli usiopingika kwamba zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania wanategemea juhudi zake katika shughuli za kilimo. Ndio maana hakukosea kwa kuhakikisha kwamba bajeti inaongezeka ili kuweza kuwakomboa watanzania walio wengi, ambao ni zaidi ya asilimia 75.

Mheshimiwa Spika, lakini pia naomba niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wasaidizi wake wote kwa jinsi ambavyo wanajitahidi Kwenda kufanya mapinduzi katika suala zima la kilimo, na hili sisi sote tumekuwa tukisema tunataka Pato la Taifa linachangiwa na kilimo lionekane bila kutumia tochi, lionekane kwa wazi. Kwa sababu katika kilimo pekee ndipo ambapo wabilionea wa Kitanzania wataonekana bila kupepesa macho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kupongeza maeneo hayo mimi nakusudia kuongelea eneo moja na muda ukiruhusu nitaenda maeneo mengine mawili. Nimejikita katika

suala zima la mbegu na leo nimechagua mbegu aina tatu tu. Mbegu ya mahindi, mbegu ya soya na mbegu ya michikichi. Kwa nini nimechagua mbegu ya mahindi? Kilimo chetu kimepewa majina mengi, kilimo cha kufa na kupona *which I don't believe* kwamba kilimo ni kufa na kupona. Inawezekana kwa sababu wakati ule ilikuwa kwamba unapolima ni kama vile *either* uishi au ufe, sasa, kilimo kinatakiwa kiwe ni kilimo cha kibiashara ambacho kinapaswa kiwakomboe wananchi kutoka katika wimbi la umasikini na kuwa matajiri.

Mheshimiwa Spika, ili uwe na uhakika juu ya mavuno yaliyo sahihi, kwa maana *yield per acre*, ni pale uinapokuwa unajihakikishia kwamba unakuwa na mbegu iliyo bora, maana ukisia mbegu iliyo bora una uhakika wa kuvuna vizuri. Kwa hiyo ukikosea katika kusia mbegu usiyo bora kwa vyovyote vile utarajie kwamba hata mavuno yake hayatakuwa na tija.

Mheshimiwa Spika, siamini kama katika nchi ya Tanzania kuna sehemu yoyote, mkoa wowote Tanzania ambao hawali ugali, hawapo. Ndiyo maana nimechagua mahindi nikiwa najua kwamba takriban Watanzania wote wanategemea chakula kinachotokana na mahindi. Ndiyo maana ninamuomba Mheshimiwa Waziri; na hii inawezekana ikawa ni kasumba, kwamba wakoloni wametuwekea mipaka na sisi tunaishi kwa hiyo mipaka ilhali hakuna kitu cha maana ambacho kinatutengnanisha. Walifanya hivyo ili waweze kututawala kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amekiri yeye mwenyewe katika ukurasa wa 25 kipengele cha 58, kwamba tuna uhaba wa mbegu za mahindi na mbegu zingine. Lakini ni ukweli usiopingika kwamba kwa sisi wa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, ziko nchi ambazo wanafanya vizuri katika suala zima la kuzalisha mbegu iliyo bora. Wenzetu Malawi, Zambia na Zimbabwe wanafanya vizuri sana. Sasa nimuombe

Mheshimiwa Waziri, hizi *colonial boundaries* isiwe kwamba mwananchi wa Kalambo anapoenda kununua mbegu ya mahindi ambayo ana uhakika inafanya vizuri ionekane kama vile amebeba madawa ya kulevya sio sahihi hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, tuache wananchi hawa watu-*facilitate* ili wawe na uhakika na mbegu ambazo wanapata kwa sababu zinafanya vizuri kwa majirani zao. Ninaamini, kwa bahati nzuri tuna mashirikiano ya karibu sana akatika nchi hizi za Kiafrika, hakuna sababu ya kufanya sheria zikawa ngumu sana pale ambapo mwananchi anaingiza mbegu kwa ajili ya kwenda kulima, mbegu ambazo alitakiwa awe amwekuwa *supplied* na Serikali. Serikali wamekiri hawana uwezo kwa sasa wa kutosheleza soko la mbegu kwa mahitaji. Niweze ku-*facilitate,* waingize, tena kwa kusindikizwa badala ya kukimbizwa.

Mheshimiwa Spika, vile vile vimeongelea suala la mbegu za michikichi na soya kwa sababu naamini pale mabapo unasonga ugali kwa vyovyote unategemea uwe na kutoweo ambacho radha yake inakuwepo pale ambapo yametumiaka mafuta kiasi kwa mujibu ambavyo wataalamu wanatushauri; kwamba ni vizuri mafuta yakatumika japo kwa kiasi. Amesema na wenzangu wamesema nchi kama Malaysia wamefanya vizuri baada ya kuchukua mbegu ya michikichi ambayo walichukua Kigoma, wakaenda wakafanya utafiti ukaongezea kidogo, leo wanazalisha *palm oil* nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, sasa nimuombe Mheshimiwa Waziri, zipo jitihada ambazo zinafanyika kuhakikisha kwamba miche bora ya michikichi inapelekwa Kigoma lakini haitoshi. Mwambao wa Ziwa Tanganyika, maeneo ya Katavi, Rukwa kote michikichi inakubali, hata Mbeya, ukienda Kyela kule inafanya vizuri. Ni wakati muafaka kwa Wizara kuhakikisha kwamba mbegu zilizo bora zinatafutwa na zinapelekwa kwa wananchi kwa bei ambayo ni *affordable*. Hata Serikali lile

tatizo ambalo inapambana nalo kwamb ainafika kipindi wanafikiri kufunga Ziwa Tanganika kutakuwa na *alternative way* ya wananchi wetu; kwamba, *ok,* tuna michikichi, tutazalisha mawese, wakati tunafunga Ziwa Tanganyika. Lakini kama hakuna maandalizi namna gani wananchi wetu wawe na kazi nyingine mbadala ya kufanya wakati mmefunga ziwa haiwezi kutuletea tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nimekuwa nikisema na leo naomba nirudie. Kuna uhakika wa soko la dunia kwa zao la soya; kwa maana ya mafuta, lakini hata *soya cake* ambayo inapatikana kama makapi baada ya kukamua mafuta. Hiki ni chakula kizuri sana cha mifugo. Sasa Wizara mshirikiane. Mikoa ambayo zao la soya linakubali ni pamoja na Kagera, Ruvuma, Rukwa na Katavi. Tatizo tulilonalo ni kwamba, hatuna mbegu; na wenyewe wamekiri. Wenzetu Zambia wanazalisha mbegu bora kabisa ambayo imefanyiwa majaribio mazuri na inafanya vizuri duniani. Lakini hii kama haitoshi hata Malawi wana mbegu nzuri sana. Mimi *I am a living example,* haya ninayoyasema siyasemi kama *theory,* nafanya, nalima zao la soya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninachoomba ni *support* ya Serikali kwa mikoa hiyo ambayo nimeitaja. Serikali ikiamua kuwekeza; na hii *importation* ya *cheap products* ambazo hatuna hata uhakika juu ya *quality* yake itakuwa imekwisha. Kazi nzuri imeanza lakini tunahitaji tufanye kazi kwa juhudi Zaidi. Tumechelewa, *it's our time* tuhakikishe kwamba Tanzania tulishe Afrika, Afrika Mashariki na dunia kwa ujumla. Ili tuwe na uhakika na hilo, naomba kupongeza; kuna *scheme* ya umwagiliaji kule Legezamwendo. Lakini hebu tazama, kamoja hakatoshi. Iko *potential* kubwa hebu tujaribu kutizama kwa ujumla ili tuweze kusaidia Taifa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mheshimiwa Aloyce John Kamamba ajiandae.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi ya pekee kukushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kutoa mchango wangu kwenye hotuba ya Waziri wa Kilimo. Awali ya yote nimpongeze kwa kazi kubwa na nzuri ambayo yeye mwenyewe Mheshimiwa Bashe na Naibu wake Mheshimiwa Mavunde wanaifanya, hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, Baada ya kutoa pongezi, kwa kuwa muda ni mfupi naomba niende moja kwa moja kutoa mchango wangu kwenye hotuba yako hasa kwenye mazao ya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeipitia hotuba ya Waziri wa Kilimo. Nimeenda kwenye jedwali kwenye mazao ya biashara. Yapo mazao saba yanayotuingizia fedha nyingi za kigeni nayo ni tumbaku, kahawa, chai, korosho, pamba, pareto na mkonge.

Katika mazao haya saba kwa msimu huu wa kilimo wa 2022/2023 zao ambalo limeingiza fedha nyingi za kigeni ni zao la kahawa, limetuingizia fedha USD 204,670,147 likifuatiwa na tumbaku ambayo imetuingizia USD 154,084,169 likifuatiwa na pamba ambayo imetuingizia USD 147,135,803 na zao ambalo ni la mwisho na limetuingizia kiwango kidogo ni pareto ambalo limetuingizia USD milioni 5,484,927. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zipo nchi ambazo uchumi wake umekua kutokana na mchango wa kahawa. Brazil ndio nchi ulimwenguni ambayo kabisa ni mkulima na mzalishaji mkubwa na imetajirika kwa sababu ya zao la kahawa. Katika Afrika tunazo nchi, ipo Uganda imetutangulia mbele, lakini ipo Ethiopia. Ukienda kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2020 – 2025 inasema hivi; "Ifikapo mwaka 2025 zao hili la

kahawa kwa mwaka tuwe tuna uwezo wa kuzalisha tani 161,000," lakini mpaka sasa hivi ndiyo tumefikia tani 80,000 na ndizo hizi zimetuletea hizi fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe ushauri mkubwa kabisa kwa kulinganisha na majirani zetu. Ukiangalia tukijilinganisha na Nchi jirani ya Uganda ambayo sisi katika nchi yetu kahawa inalimwa katika mikoa 16 ukitafuta *arable land,* ardhi inayofaa kwa zao hili ni zaidi ya mara tatu ya ardhi ambayo inalimwa kahawa Uganda, lakini wao wenyewe kwa mwaka huu, kwa msimu huu wameingiza *USD* milioni 800, kiwango hicho ni kikubwa tukijilinganisha.

Mheshimiwa Spika, zipo jitihada ambazo bado kama nchi tunatakiwa tufanyie kazi. Ni zao pekee hili la kahawa ambalo linaweza likawa na mchango mkubwa kwenye ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Bado kuna nafasi kubwa ya juhudi ambazo zinatakiwa zifanyike, nchi inatakiwa iwekeze, pamoja na kwamba, imekwishaandikwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ukiangalia kwenye uzalishaji kwa miaka hii miwili, mitatu, tukianzia na msimu ule wa 2019 na 20 tulizalisha tani 73,000, mwaka uliofuatia tani 70,000, msimu uliofuatia 66,000 tulishuka, lakini sasa tumepanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali inatakiwa ichukue hatua madhubuti kwanza ili tuweze kuwa na malengo makubwa. Tuwe na malengo makubwa ya kuhakikisha kiwango cha uzalishaji wa kahawa ambayo ndio zao namba moja ambalo limetuingizia fedha za kigeni ni lazima Serikali iwekeze. Sehemu za kuwekeza kwanza ni lazima uwe na uwezo wa kuzalisha mbegu bora katika mikoa yote ambayo inalima kahawa kwa kuitumia *TACRI.* Uganda kwa mwaka huu wenyewe wanaenda kuzalisha miche bora milioni 171, Ethiopia wanaenda kuzalisha miche bora ya kahawa milioni 362, sisi milioni 20, kiwango hicho ni kidogo, hakiwezi kuleta mapinduzi ya kilimo cha kahawa na kikachangia kwenye uchumi wetu. Kwa hiyo, zinahitajika jitihada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima tuwe na malengo makubwa tutoke kwenye milioni 20 twende hata kwenye milioni 200 halafu tuigawe hiyo miche, tupanue mashamba, tuwawezeshe wananchi ambao tayari wanajishughulisha na kilimo hiki cha kahawa, tuwawezeshe vijana kufungua mashamba mapya na tuwape mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ya pili, naomba nichangie tena kwenye zao la chikichi. Kwanza nampongeza Waziri na sisi watu wa Kigoma tunamshukuru sana kwa sababu, kwenye bajeti hii tumeona chikichi kwa mara ya kwanza imeenda kupata ruzuku, inaenda kuwa mkombozi. Itaenda kuokoa bilioni 470 ambazo Serikali inatumia kwa ajili ya kununua mafuta ya kupikia na kuyaleta humu nchini. Yafuatayo yanatakiwa yafanyike ili kuhakikisha uzalishaji wa chikichi unaongezeka.

Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Kandege ambavyo amekwishazungumza ukitoka Kigoma, Katavi mpaka Rukwa ule ukanda wote ni wa hali ya hewa ambao unaweza ukakuza zao la chikichi, ule mpango wa Waziri sasa wa *BBT* wa zile *block farms* ndio wakati wake sasa. Serikali ije kuyafungua mashamba hayo, iwatayarishe vijana na iwape mashamba hayo wayasimamie, itachukua muda mfupi tu tutaweza kujitegemea kwa mafuta na tutakuwa tumeokoa fedha hizi za kigeni ambazo tunazitumia katika kuingiza mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zao la tatu ni tangawizi, nalo linalimwa katika Jimbo langu la Buhigwe. Tunavyo vijiji zaidi ya kumi ambavyo sasa hivi vinashughulika na kilimo cha tangawizi. Tangawizi ni mojawapo ya viungo muhimu sana, kwa hiyo, tunaomba katika bajeti hii Waziri ajitahidi na aoneshe namna gani Serikali inaweza kuboresha miundombinu ili kuongeza kipato cha wakulima wa tangawizi na hasa kwa kuwaletea viwanda vya kuchakata zao la tangawizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Shukrani. Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Aloyce John Kamamba na Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei ajiandae.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii. Vilevile kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambazo anaendelea kuzifanya. Nimeongea mara nyingi hapa, sisi Manyoni Mashariki tumepata miradi mingi sana ikiwepo hii miradi ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nichukue nafasi hii kumshukuru sana Waziri, ndugu yangu Mheshimiwa Bashe pamoja na Naibu Waziri, ndugu yangu na mdogo wangu Mheshimiwa Mavunde, kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya, lakini bila kuwasahau watendaji wetu wa Wizara ya Kilimo hususan, Bodi ya Korosho, lakini Bodi ya Umwagiliaji na Katibu Mkuu. Mheshimiwa Bashe ametusaidia sana kwenye kilimo cha korosho Manyoni. Najua kuna mambo mengi ameyafanya, sasa hivi kilimo chetu cha korosho Manyoni kinaenda vizuri sana. Sasa hivi anajenga maghala, lakini ametupelekea pikipiki, lakini kuna vitu vingi sana ambavyo amevifanya kwa hiyo, namshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo nina ajenda kubwa mbili ambazo ningependa kuchangia kwenye Wizara ya Kilimo. Eneo la kwanza nitachangia upande wa skimu za umwagiliaji na eneo la pili nataka niishauri Serikali jinsi gani tunaweza tuka-*transform* Tume ya Umwagiliaji. Wachangiaji wengi wameeleza hapa kuhusu umuhimu wa Tume ya Umwagiliaji kwa hiyo, naomba nichangie eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upande wa skimu za umwagiliaji; kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, alimtuma Naibu

Waziri, Mheshimiwa Mavunde alikuja Manyoni pale Chikuyu kwenye Skimu ya Umwagiliaji wa Chikuyu. Ile skimu ilikaa miaka mitatu wananchi hawajalima, lakini alikuja akatoa maelekezo na nimshukuru sana Mkurugenzi wa Tume ya Umwagiliaji walikuja wakaikarabati ile Skimu ya Umwagiliaji ya Chikuyu, lakini bahati mbaya mwaka huu tena ule mto ukaenda kubomoa sehemu fulani ya ile skimu.

Mheshimiwa Spika, nimeona kwenye bajeti ya Waziri kwamba, ameweka vilevile kukarabati hii Skimu ya Chikuyu. Nimwombe tena Mheshimiwa Waziri, tukamalizie ile kero ili tuwape matumaini wakulima wa hapo chikuyu.

Mheshimiwa Spika, Tarafa ya Kintinku, Tarafa ya Bahi na Tarafa ya Kilimatinde sisi tunategemea kilimo cha mpunga na kilimo cha mpunga kinahitaji umwagiliaji. Nimeona kwenye bajeti ya kilimo wameweka ukarabati wa Skimu ya Ngaiti, Skimu ya Maweni, Skimu ya Lusilile, ya Udimaa hata ya Msemembo. Nimwombe sasa Waziri, ukarabati huu uende kufanyika, hawa wananchi asilimia 100 wanategemea kilimo cha umwagiliaji. Bila kuwepo miundombinu ya umwagiliaji ambayo ni mizuri maana yake tunatengeneza njaa kwa hawa watu.

Mheshimiwa Spika, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri pamoja na mdogo wangu Mheshimiwa Mavunde wajitahidi wakawasaidie hawa ndugu zangu wa Ngaiti, Maweni, Mtiwe, Chikuyu, Msemembo, lakini Udimaa na Lusilile hizi skimu zao mwaka huu zikatengenezwe, zikakarabatiwe ili angalau mwaka unapoanza wa kilimo waweze kulima.

Mheshimiwa Spika, lingine, Waziri mwaka jana alikuja na bajeti ya kusema kwamba, anaenda kuanza kufanya *feasibility study* ya Mradi wa Bwawa la Mbwasa. Nimefurahi kwenye bajeti hii vilevile Waziri ameeleza hapa kwamba anaenda kufanya mapitio ya ile *feasibility study* ambayo

ilishafanyika muda mrefu sana, lakini vilevile anaenda kuanza kujenga Bwawa la Umwagiliaji la huu Mradi wa Mbwasa.

Mheshimiwa Spika, huu mradi wananchi wameusubiri kwa muda mrefu sana. Nakumbuka Mheshimiwa Naibu Waziri Mavunde alipokuja wananchi walimuuliza na aliwaahidi kwamba, Serikali ipo mbioni kuhakikisha kwamba, huu mradi unaanza kujengwa. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri auchukue huu Mradi wa Umwagiliaji wa Mbwasa kwa sababu ni mradi ambao utawaokoa sana wananchi wa Manyoni, hususan Tarafa ya Kintinku ambako wanategemea zaidi kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine, tuna bodi yetu ile Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko, nilitegemea sasa tunapoongelea kilimo cha mpunga katika hizi tarafa tatu, Tarafa ya Bahi, Tarafa ya Kintinku na Kilimatinde, tuwe tuna uwekezaji wa masoko angalau katika hizi tarafa tatu. Hatuna masoko ya uhakika ya mpunga, tuna madalali tu na walanguzi ambao wanaingia kwenye eneo lile la Kintinku, Bahi na hata Kilimatinde.

Mheshimiwa Spika, nimwombe Waziri, tuna Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko, awa-*task* hawa watu waweke miundombinu pale, maghala, lakini watuanzishie masoko ili wananchi wetu wawe na uhakika wanapouza mpunga wanauza kwa bei ambayo itakuwa na manufaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni kuhusu hii Tume ya Umwagiliaji. Watu wengi wamechangia kuhusu hii Tume ya Umwagiliaji. Niseme kweli na nimekuwa nikichangia sana, hatuwezi kuendeleza kilimo cha Tanzania kama hatutawekeza kwenye hii Tume ya Umwagiliaji. Ni eneo ambalo kwa kweli, tunahitaji kuwekeza. Nimshukuru sana Mheshimiwa Rais mwaka huu, kuanzia Rais Dkt. Samia alipoingia madarakani bajeti ya Wizara ya Kilimo imepanda

sana, mwaka jana ilikuwa bilioni 700, mwaka huu tuna bilioni zaidi ya 900, lakini vilevile bajeti ya umwagiliaji imepanda, mwaka jana tulikuwa na bilioni 262, mwaka huu tuna bilioni 373, haya ni mapinduzi makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunahitaji kufanya vitu viwili. Eneo la kwanza ambalo naliona na ningependa kushauri, kwa nini hii Tume yetu tusii-*transform?* Hapa ukisikiliza Wabunge wengi wameongelea suala la umwagiliaji, *we need a giant institution,* tunahitaji kuja na kitu tofauti na tume, kwa nini tusifikirie kuja na *authority, National Irrigation Authority?* Kama tulivyokuja na *RUWASA, TARURA, TANROADS,* iwe *giant?* Tuipe meno, tuipe fedha, ili iweze ku-*manage* suala la *irrigation* kwa Tanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitegemea kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri angeeleza kwamba, lini anakuja kuanzisha *National Irrigation Authority* ambayo sasa itaenda ku-*spear head* masuala ya umwagiliaji. La pili, tunapofikiria kuanzisha hii *authority,* lazima tufikirie kwenye *financing frame work,* fedha tutapata wapi? Ukiangalia kwa kiasi kikubwa vyanzo vya fedha vya hii tume ni zile tozo za wakulima kutoka kwenye skimu, skimu ambazo hatujazikarabati. Nashauri, tunahitaji kuja na mfumo mzuri wa kutafuta vyanzo vya mapato, mbona tunatoza maeneo mengine kwa nini tusitoze asilimia tatu kwa wakandarasi ile asilimia tatu ikaingia kwenye hiyo Tume ya Umwagiliaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kwa kweli katika haya Mheshimiwa Waziri, alichukue hili, hasa hasa la kwenye suala la ku-*transform* Tume ya Umwagiliaji. Sisi Wabunge wengi tunategemea kwamba, kama tuta-*invest* kwenye suala la *irrigation,* umwagiliaji, tunaweza kwenda ku-*transform* kilimo cha Watanzania, lakini kama tutakuwa hatuna uwezo wa kuwekeza kwenye kilimo cha umwagiliaji uwezo wa ku-*transform* kilimo utakuwa ni mdogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nirudie tena kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwanza kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya, lakini nimshukuru sana Mwenyekiti wa Bodi ya Korosho, amefanya mambo makubwa sana Manyoni. Nimshukuru sana vilevile Mwenyekiti wa Bodi ya Mazao Mchanganyiko na Mkurugenzi kwa kazi kubwa ambayo anaifanya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya naunga mkono hoja na nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei na Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke ajiandae.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuchangia hoja iliyopo mbele yetu, hoja ya Wizara ya Kilimo. Kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa fedha nyingi ambazo amepeleka katika jimbo letu, lakini kwa bajeti hii ametukumbuka pia, ametupelekea fedha. tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwapongeze pia Mheshimiwa Waziri, msaidizi wake Naibu Waziri na watendaji wote kwa kazi kubwa na hasa ikizingatiwa kwamba, Wizara yao ni Wizara ambayo inachangia kutoa huduma kwa zaidi ya asilimia 65. Tunawashukuru na tunawapongeza sana Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja. Naunga mkono hoja kwa sababu tu kwanza niliomba kwenye skimu za umwagiliaji mwaka jana na kweli mwaka huu wameweza kutuingiza kwenye ukarabati wa skimu ambazo zilikuwa na matatizo. Zipo Skimu za Mughwazi, Skimu

ya Ruhwiti na Katengela, hizi zimetengewa fedha kwa ajili ya ukarabati, sisi Kakonko tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zipo pia skimu ambazo ni mpya zinakwenda kuanzwa kwa ajili ya upembuzi yakinifu. Ipo Skimu ya Ruhuru, Skimu ya Mgunzu, Skimu ya Kanyonza na Skimu ya Churanzi, hizi ni skimu mpya, tunashukuru fedha zimewekwa kwenye bajeti. Sasa niombe fedha zikishapitishwa, nina hakika bajeti ya Waziri itapita, watuletee fedha ili kazi iweze kuanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze vilevile kwa kuzungumzia suala la mbolea. Mbolea ni muhimu sana kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, kilimo kinafanyika, lakini nizungumze kwamba, mbolea na mbegu bora hazipelekwi katika majimbo yetu kwa wakati. Wilaya yetu ya Kakonko tunapata mvua kuanzia mwezi Septemba, lakini mbolea inakuja kufika mwezi Desemba, wakati huo mahindi yanabeba, mbolea ile haiji kutusaidia. Hii inakwenda sambamba na ubora wa mbolea hiyo, katika Wilaya ya Kakonko na mimi mwenyewe ni mkulima, tumepata mbolea lakini ubora wake sio sahihi. Hili nililiwasilisha katika ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nikatoa taarifa kwamba, mbolea tuliyopata na ambayo nimeitumia hata kwenye shamba langu, shamba halina mabadiliko yoyote.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba, Wizara ilituma wataalam, wakaja kuchukua sehemu ya mbolea ile iliyobaki, lakini vilevile wakachukua udongo, sijapata majibu. Kwa hiyo, niombe atakapokuwa anahitimisha tuweze kupata majibu sahihi, kuna Mbunge mwenzangu amechangia hapa suala la ubora wa mbolea tunayoipata haiko sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la bei ya mazao. Wilaya ya Kakonko moja ya zao letu ambalo ni la kimkakati ni alizeti. Alizeti ni zao la mkakati kwa Wilaya ya Kakonko likienda sambamba na zao la chikichi pamoja na muhogo,

tatizo hatuna uhakika wa bei. Tuombe Serikali itusaidie kupata bei inayolingana na mazingira yetu, ili wananchi waweze kufaidi vizuri zao hilo la muhogo, ikiwa ni pamoja na zao la alizeti, ikiwa ni pamoja na zao la chikichi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla naomba nitoe sasa ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, nina hakika Wabunge wametoa ushauri, wametoa maoni mbalimbali, haya yote hayawezi kufanyika bila kuwa na wataalam. Kwa hiyo, moja niombe Serikali iajiri watumishi na watumishi hao wapelekwe katika vijiji vyetu, wapelekwe katika mashamba yetu na wasimamiwe, ili waweze kufanya kazi ya kuwafikia wananchi, kutoa ushauri wa kitaalam. Nina hakika baada ya muda si mrefu Serikali yetu, nchi yetu inaweza ikapata chakula cha kutosha na kupata akiba kwa ajili ya matumizi mengineyo ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu pia ni kuhakikisha kwamba mashamba yale ambayo yamepelekwa kwa ajili ya vijana maarufu kwa jina la *BBT,* hebu yapelekwe kwenye Mikoa ile ambayo ina mvua za kutosha. Asubuhi wamechangia kwamba imeletwa Dodoma, kwetu Kigoma limechukuliwa eneo dogo sana, ninaomba maeneo yale ambayo yana mvua za kutosha kama Mikoa ya Kigoma, Rukwa, Katavi, Ruvuma, Mbeya na Njombe, tupeleke huko,nina hakika mvua zipo za kutosha, ardhi ya kutosha na hivyo haitakuwa shida, vijana wetu wataweza kupata huduma hiyo nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ni kuhakikisha kwamba mbolea mbegu pamoja na viuatilifu vinapelekwa kwenye Majimbo yetu na kwenye Mikoa yetu kwa wakati, isiwe tunahitaji mbolea ya kupandia inakuja tunamalizia palizi. Tunahitaji mbolea ya kukuzia inakuja mahindi karibu

yanaiva. Niombe sana pembejeo zipelekwe mapema katika Mikoa yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia yapo mazao ya kimkakati ya chikichi na alizeti tuhakikishe kwamba nayo yanapewa bei ya kutosheleza kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, ninashauri kwamba Serikali ihakikishe kwamba inalinda bei ya mazao mbalimbali ambayo yanalimwa katika nchi yetu. Hii ni pamoja na kuhakikisha kwamba mazao yanahifadhiwa ikiwa ni pamoja na kujenga maghala ambayo yatasaidia wananchi wetu kuweza kuhifadhi mazao na kuyauza kwa wakati ambao utakuwa unastahili na ambapo wataweza kuongeza bei yao.

Mheshimiwa Spika, nishukuru tena kwa nafasi ambayo umenipa, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, atafuatiwa na Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mheshimiwa Hamis Mwagao Tabasam ajiandae.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa fursa hii ya kuchangia kwenye bajeti hii ya Wizara ambayo ni muhimu sana kwetu. Nianze kwa kusema kwamba tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Makamu wake, Waziri Mkuu na kipekee kwa hapa, Waziri wa Kilimo, wametutendea haki kwa kuongeza fedha ambazo zinaenda kusaidia Watanzania wengi sana kama zitatumika ilivyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kusema kwamba mkakati unaotekelezwa sasa hivi na Wizara hii ya Kilimo ni mkakati ambao ni tofauti sana na miaka yote ambayo tuliwahi kuutekeleza. Ni tofauti sana na ninaona kwamba lawama nyingi zinazojitokeza kwa wakulima na hata kwetu sisi Wabunge zinatokana na ukweli kwamba hatukuwa

tumeidhinishwa vizuri, hatukuwa tumepata miongozo ya kutosha ili kuweza ku-*communicate* na wale watu wetu kule vijijini wakaelewa ni kitu gani kinakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo najua kwamba tunajifunza kwa kufanya na tunapojifunza kwa kufanya tunafanya makosa, kunatokea makosa na ninaamini kwamba kiongozi mwerevu ni yule ambaye sasa anachukua yale makosa na kuya-*address* ili huko mbeleni yale makosa yapungue tuweze kuona mkakati huu ukifanikishwa.

Mheshimiwa Spika, kusema kweli huu mkakati ni mkakati ambao ulihitaji uhamasishaji mkubwa na maandalizi mapema, ninaomba sasa kwamba Serikali iendelee kuwaandaa mawakala. Kule kwetu Vunjo tulikuwa na mawakala watatu tu kwenye Kata 16 zenye watu 255,000 ni wachache sana, kwa hiyo watu walikuwa wanatembea mbali kutafuta na mara nyingine wanakuta kwamba wale mawakala wameishiwa na mbolea au wana mbolea aina moja kwa hiyo unaenda unarudi. Kwa hiyo, kusema kweli ni mkakati ambao tunauunga mkono lakini sasa Serikali ijiandae vizuri kwa kutengeneza huo mfumo wa kugawa hii mbolea ya ruzuku, ninaamini kwamba itaendelea kwa sababu bei za mbolea duniani bado ziko juu kiasi, lazima tujue kama alivyosema mmoja wetu, kwamba tuna-*subsidize* au tunatoa ruzuku kwa bei tunayojua, tusitoe ruzuku kabla hatujajua kwamba bei ya kufikisha zile mbolea hapa Tanzania zitakuaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kule kwetu Vunjo na Kilimanjaro kwa ujumla, natumaini tumenufaika kidogo sana kwa miradi ambayo imetekelezwa. Kitu cha kwanza ambacho ninataka niulize ni kwamba, vigezo vilivyotumika kugawa miradi mbalimbali ya umwagiliaji, miradi ya mabwawa, miradi ya maghala na miradi ya uhifadhi wa mazao imefanyika namna gani na vigezo gani vimetumika? Kwa sababu la sivyo, tutabaki kusononeka wenyewe, tunasema hapa kuna

upendeleo. Kwa sababu ili kuondoa masuala ya upendeleo au siyo upendeleo, lazima kuwe na *criteria* na *rules* ambazo zinam-*guide* yule anayesema sasa napeleka ghala Songea au sehemu nyingine *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nashangaa kwa sababu kwa mfano kule kwetu tuna magulio au masoko ambayo toka kabla ya uhuru yapo, yamezeeka. Mama anakwenda ananyeshewa mvua wakati wa mvua, jua linampiga, hakuna hata paa, hakuna *allocation* yoyote iliyofanyika kusema kwamba hebu tusaidie wale watu wa kule Vunjo kwa mfano kwenye Masoko ya Himo, Mwika, Mombi, Kisambo, Marangu Mtoni na kadhalika, wakapata angalau mahali pa kujiepusha.

Mheshimiwa Spika, inavyotokea ni kwamba mkulima anapokwenda na mazao yake, mahindi au mbogamboga, akishindwa kuuza siku ile basi lazima ama aviache, avitupe au arudishe nyumbani ambapo hakuna walaji. Kwa hiyo, inakuwa kwamba kungekuwa na miundombinu hii ya maghala ambayo naamini kwamba haya ambayo yanatengenezwa sasa hivi na Mheshimiwa Bashe yana viwango vya kuweza kuhifadhi mbogamboga hizo, ndizi hizo baadaye zikauzwa kwa wale wachuuzi wanaojitokeza inakuwa ni vigumu sana kusema kwamba tumesaidika vya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana ikiwezekana hiyo iangaliwe na ninaamini kwamba soko linakuwepo lakini wale madalali wanaokuja kununua kutoka Dar es Salaam lazima waweze kuhifadhi mahali yale mazao. Nashukuru pia Mheshimiwa Bashe ameona umuhimu wa ku-*emphasize* kwenye huu mkakati wake kwamba analenga kuongeza zaidi uzalishaji wa mazao ya chakula, maana yake nafaka, mbogamboga na matunda ambayo yana tija lakini ni *very delicate* haya mazao, ni *perishable,* ukiweka baada ya siku

mbili, tatu, yanaharibika kama hayakuhifadhiwa sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naambiwa kwamba tani milioni 2.75 zinazozalishwa za mazao haya ya matunda na mbogamboga ni asilimia Nne tu inachakatwa. Kwa hiyo ina maana nyingine inaharibika na wale wanaobahatisha zinanunuliwa na wenzetu wa mpakani ambao wana *chain* nzuri ya kuweza kuhifadhi na kusafirisha haya mazao kupeleka sokoni, sisi tunabakia hapa kusema kwamba watu wanao-*export* maparachichi yetu ni majirani zetu! Ukweli ni kwamba kama hatujajenga miundombinu ya kufikisha mazao yetu sokoni yataishia kwa majirani, kwa sababu wale wana miundombinu, wanazo *quality cold rooms* za kusafirisha haya mazao ambayo ni *perishable* ambayo yanaharibika kwa haraka. Kwa hiyo, naomba katika mchakato huu Mheshimiwa Waziri aone namna gani atatusaidia kwenye kulinda hiki tunachozalisha kwa wingi kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naona wenzangu wamekuwa wanasema huwezi kutekeleza mkakati mmoja unaofanana kwenye nchi kubwa namna hii kwenye Kanda zote na Mikoa yote, *it's impossible*. Huwezi kusema kwamba labda uanze kulima korosho kila mahali au kahawa kila mahali, haitawezekana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaamini kwamba kwa mfano mwenzangu mmoja alitoa mfano wa Malaysia, lakini nataka kusema kwamba kweli kule kwetu Kilimanjaro ambako hatuna ardhi, mkakati wetu unataka *intensive farming,* kumuwezesha mkulima azalishe kingi kwenye kaeneo kadogo na azalishe kwa mwaka mzima, *which means* umwagialiji ni kitu cha msingi sana, azalishe kwa mwaka mmoja lakini atumie eneo dogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo mengine kusema kweli huhitaji hata mbolea. Kwanza maeneo mengi

hayajatumika na mmomonyoko wa udongo haujaharibu sana kwa hiyo ukifanya *extensive farming,* ukawapelekea hizi *tractors* na mashine zikasaidia *mechanization,* utaongeza tija yao *extensively,* maana yake kwa kutumia maeneo makubwa. Kwa hiyo ninataka kusema kwamba kusema kweli tuangalie, bila kufanya vile tutapata matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kingine ninacholalamika ni kwamba kule kwetu nimetafuta kila mahali kwenye hii *document* ya Mheshimiwa Waziri nione *BBT* kule Vunjo imefikaje. *BBT* iko wapi Vunjo? Huwezi kugawa vitalu kwa miaka 66 kwa mtu yuleyule! miaka 66 si atauza na yeye kwa sababu lazima *i-rejuvenate.* Kusema kwamba hii ingekuwa ni *seed* mtu anapewa kwa mwaka mmoja wa pili anakuwa amechota faida ya kutosha anapeleka ku-*invest* mahali pengine, anamwachia mwingine, wanapeana vijiti, nae anazalisha, akishakaa miaka miwili anaenda inakuwa ni *rotation.* Hata kama unasema unampa mtu mmoja, mimi sijui nani atapewa, lakini naamini kwamba hiyo kitu ambayo hata *criteria* ya kusema unachagua eti watu waombe, mtu aombe wakati hajawahi kuona shamba unamwambia omba! Kwa sababu ana uwezo wa kuingia kwenye kishkwambi anaomba, pengine hata siyo yeye atakwenda kufanya kazi. Halafu ukweli ni kwamba kwenye hivi vitalu hata ikiwa ni eka tano, watahitaji wafanyakazi pia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kimei, muda wako umekwisha.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamis Mwagao Tabasam, Mheshimiwa Aleksia Asia Kamguna ajiandae.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwenye wingi wa rehema, kwa kunipa kibali cha kusimama ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja. Nami niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuamua kwa moyo wake wa dhati kufanya kilimo cha Tanzania kiwe cha kuwaletea wananchi chakula, kilimo cha kuleta ajira vilevile kiwe ni kilimo cha kibiashara, nampongeza sana Rais wangu. Pia nampongeza Makamu wa Rais, Dkt. Mpango, kwa uhamasishaji wa zao la mchikichi. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Bashe Waziri wa Kilomo, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Kilimo, hongera sana kwa kazi mnayoifanya. Nitakuwa sijatenda haki nisipompongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, kwa kazi kubwa anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu nitajielekeza katika maeneo mawili. Eneo la kwanza ni mchikichi, eneo la pili nitazungumzia mbolea. Kwa nini nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, tangu mwaka 2018 Serikali ilipoamua mchikichi kuwa zao la kimkakati Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuwa akija Mkoani Kigoma kuhamasisha kilimo cha zao la mchikichi na wananchi walihamasika wanaendelea kuhamasika na kwa sasa ni miaka mitano michikichi ile aliyokuwa akiihamasha na mchikichi alioupanda yeye mwenyewe katika eneo la JKT Bulombora tayari umeishaanza kuzaa matunda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Bashe, Naibu wako ameshafika Kigoma, ninakuomba ukimaliza Bunge hili uje ujionee maajabu yanayofanyika Mkoa wa Kigoma katika zao la mchikichi. Gereza la Kwitanga wanafanya vizuri sana, wana mashamba makubwa sana ambayo tangu kilimo cha

mchikichi kilipoanza kuhamasishwa wameweza kulima. JKT Bulombora wana mashamba makubwa sana na wanaanza kuzalisha michikichi kuwagawia wananchi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Bashe tunakuomba ufike Kigoma.

Mheshimiwa Spika, wananchi wamehamasika, wamelima, bado kuna changamoto kwenye miche ya michikichi, mahitaji bado ni makubwa. Lakini niishukuru Serikali kwa kutenga ruzuku kwa ajili ya miche ya michikichi. Ninakuomba sasa Mheshimiwa Bashe ufike Kigoma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Benki ya *TIB.* Wananchi wamekuwa wakihamasishwa kwenda kuomba mkopo *TIB,* lakini ni ukweli usiofichika kwamba masharti bado ni magumu. Ninaiomba Serikali kupitia Waziri wa Ardhi, waweze kupimiwa mashamba yao ili waweze kupata hati miliki, mashamba yao yaweze kuwadhamini, hatimaye waweze kukopesheka, bila hivyo bado masharti ni magumu. Kwa hiyo, ninaomba Serikali ihamasishe, Waziri wa Ardhi, wananchi wapimiwe mashamba yao wapate hati miliki ili waweze kukopesheka kupitia hati miliki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuzungumzia kuhusu mbolea. Ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuweza kuwapatia wananchi mbolea. Tuliipata mbolea ambayo wananchi wameweza kupata kwa shilingi 70,000. Kwa kweli tunashukuru, kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kigoma ninamshukuru sana Mama kuweza kutupatia mbolea ya ruzuku. Bado kuna changamoto.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Bashe nikushukuru kwanza, yalipokuwa yakitokea matatizo madogo madogo wakati wa ugawaji wa mbolea kila tulipokupigia simu ulipokea simu na ulitoa maelekezo na watendaji wako waliweza kufanya kama ulivyowaelekeza.

Mheshimiwa Spika, mwanzoni mbolea zilikuwa zinapelekwa Makao Makuu ya Wilaya. Ninakuomba sasa Mheshimiwa Bashe, mbolea ziende kwenye Tarafa na kila Kata ili kila mwananchi atakapohitaji mbolea iwe karibu yake. Kwa sababu wananchi wamepata mateso sana kwa ajili ya ufuatiliaji wa mbolea kutoka vijijini kuja Makao Makuu waliweza kupata shida sana, walilazimika kulala mjini siku mbili, tatu, wakipanga foleni kusubiri mbolea, pia walilipia nyumba za wageni ili waweze kujihifadhi wakati wanasubiri mbolea. Naomba marekebisho yafayike ili waweze kunufaika kwa kupata mbolea bila kupata shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vipo vifungashio, mara nyingi mbolea inafungwa kwenye mifuko ya kilo 50 na kilo 25. Wale wakulima wadogowadogo na hasa akina mama wengine ambao hawana uwezo wa kununua mfuko wa kilo 50 au kilo 25, naomba uhamasishe iweze kuwepo mifuko inayofungasha kilo 20, kilo 15, kilo 10, kilo tano hadi kilo mbili ili mbolea iweze kuwafikia hata wananchi wa kipato cha chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimuombe Waziri, yapo malalamiko ya mawakala waliofanya kazi ya kusambaza mbolea zaidi ya miaka mitano na wamekaa kwa matumaini kwamba ipo siku watalipwa pesa zao, Mheshimiwa Waziri nataka nikuulize; je, watu hao watalipwa pesa hizo wanazozidai? Kama hawatalipwa waambieni ukweli waache kusubiri wakati uwezekano wa kulipwa pesa hizo haupo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno hayo nakushukuru sana, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hamis Mwagao Tabasam, atafuatiwa na Mheshimiwa Aleksia Asia Kamguna, Mheshimiwa Assa Nelson Makanika ajiandae.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi kupata nafasi ya kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema aliyekujalia wewe kuwepo leo hapo na kumjalia Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuiona nafasi ya bajeti hii ya Kilimo kama chachu ya maendeleo na sehemu ambayo tunakuja kukabiliana na suala la njaa, ameongeza asilimia 29 katika bajeti hii, tumpigie sana makofi, *Insha Allah! (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo nataka nishukuru kwanza. Namshukuru sana Waziri wetu Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa. Tumekwenda kwake kwa ajili ya kumwomba mahindi ya njaa kwa ajili ya kupunguza bei. Hali ya chakula Sengerema ilikuwa ni ngumu, gunia moja la mahindi liliuzwa mpaka shilingi 130,000 na baadaye tulikwenda kwa Mheshimiwa Bashe, Waziri wa Kilimo na akakubali kutupatia tani 2,000. Ametuokoa sana, Mungu akujalie sana Mheshimiwa Waziri Bashe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, naomba nishukuru kwa suala la ndege waharibifu. Tumekwenda kwake kumwomba ndege kwa ajili ya kunyunyuza dawa ya kuwaua ndege waharibifu wa mazao kule Sengerema, akatutumia ndege. Ila ndege ile ilipokuja kwetu ilitokea Kilosa, na baadaye ndege ile ilikwenda kutua Mwanza halafu ikaja kupuliza dawa. Ikimaliza kupuliza dawa, ndege ile inarudi kwenda kutua Mwanza. Sasa naziangalia zile gharama za ile ndege, kwamba kama wanapulizia dawa, kwa mfano, wanapulizia dawa Bunda, lazima ije Mwanza halafu irudi kule Bunda.

Mheshimiwa Spika, nataka kutoa ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri wetu wa Kilimo. Pamoja na msaada wake, sasa waende mbali Zaidi, wafikirie kupata *helicopter* ambayo

itaweza kutua mahali popote katika suala la umwagiliaji. Kwa sababu kuua ndege waharibifu kwa kutumia gharama kubwa kama hizi, kwamba kama Kahama hakuna uwanja wa ndege, kwa mfano, labda Ngara hakuna uwanja wa ndege, ndege mpaka ikatue Bukoba halafu ijazwe dawa, irudi Ngara, hili ni jambo ambalo tunaona kama Wizara inatumia gharama kubwa sana. Kwa hiyo, watumie *helicopter*.

Mheshimiwa Spika, vile vile miradi iliyopo, na wao wataweza kusafiri na ile ndege. Siku ikihitaji kumwagilia, itamwagilia; lakini msafiri na *helicopter,* miradi ni mingi, mtazeeka. Sasa hivi Mheshimiwa Bashe umechoka kweli kweli nakuona, *alhamdulillah* unafanya kazi, lakini lazima ujionee huruma. Utaacha hii nafasi, unachoka, wanakuja wengine tena. Kama kuna suala la kununua ndege, peleka maombi, leta hapa, bajeti imeongezeka, wakuruhusu ununue helikopta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naanza kuchangia. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, suala la umwagiliaji. Miradi ya umwagiliaji ndiyo pekee inaweza ikalinusuru Taifa hili. Ni kwamba, tumeona kilimo chetu sasa hivi kwa kutumia hali ya hewa ya mvua, mvua zinabadilika. Leo kanda ya ziwa mvua zinanyesha mwezi wa Tatu, wakati mahitaji yetu ya kupata maji, ni mwezi wa Tisa, wa Kumi, na wa Kumi na Moja. Tungekuwa tuna miradi ya umwagiliaji; na ninakushukuru kwenye bajeti hii umeiangalia sana kanda ya ziwa. Ushauri wangu kwa Wizara, Wizara hebu njooni tumwagilie maeneo yetu yanayofanyika katika *irrigation* kwa kutumia *pipeline* kutoka ziwani.

Mheshimiwa Spika, wenzetu Misri wanatumia maji haya haya ya Ziwa Victoria, lakini yanapita katika mto. Sisi wenye ziwa hatupati thamani ya maji haya, kwa sababu hii miradi ya *irrigation* pia ukichimba bwawa tunategemea mvua

inyeshe, maji yajae ndiyo ukamwagilie, wakati ziwa tunalo. Kwa nini usipandishe maji katika milima, halafu ukafungulia mabomba watu wakamwagilia?

Mheshimiwa Spika, mfano, kwangu kuna mradi wa Isole, alikuja Mkurugenzi wa Umwagiliaji, Mr. Ray tumezunguka naye Sengerema, ameona ile miradi. Tunayo miradi mitano ya *irrigation*. Kuna Isole/Kishinda, pia tuna mradi mwingine ambao uko Rwenge, Rwenge - Kagunga - Shimaka; tuna mradi mwingine ambao unaanzia Sima, huo uko katika sehemu inaitwa Ishokeya. Huo ni mradi mkubwa sana wa *irrigation,* aliuona Mr. Ray kule. Vile vile tuna mradi wa Ibanda - Igaka ambao tunashirikiana na mwenzangu kutoka Geita, Mheshimiwa Kanyasu. Huu mradi umetangazwa, tunashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, pia tuna mradi wa Katunguru ambao na wenyewe ulikuwa umekwama. Tunakushukuru Mheshimiwa Bashe, leo kuna Mchina yuko kule anamalizia kazi. Sasa kuna na mradi ambao ulikuwa unataka *design* na kujengwa, ni mradi ambao unatoka Kashindaga – Butonga - Nyamizeze – Nyamazugo. Kule sisi tuna mradi wa maji na kuna matenki kule. Ukijenga tenki kubwa mlimani, sisi tutamwagilia kwa maji ya ziwa. Sasa tunakuomba miradi hii kwa sababu Mkurugenzi wako alipita kule, tuone kama safari hii na sisi Sengerema tutabahatika kupata nafasi hiyo.

Mheshimiwa Spika, la pili ni suala la ushirika. Ushirika tumeona kwenye hizi gharama za kupanga bei za pamba. Bei za pamba, Mheshimiwa Bashe unapanga pamoja na watu wako wa Wizara ya kilimo, lakini mnapanga na wanunuzi wa pamba, Wakuu wa Mikoa wanakwenda pale. Kwa nini sisi Wabunge tunaotoka kwenye mikoa inayolima pamba tusiwemo katika upangaji wa bei? Mnaficha nini? Hivi mkitualika sisi tukaja pale hizo siku tatu au nne, tukakaa tukaangalia hicho mnachokifanya, ili tuwe mabalozi, turudi kwa wananchi, lakini mnawachukua watu wanakwenda

kuwa mabalozi wa pamba, wameshastaafu, sisi tuko kazini; mnatuachaje sisi kuwa mabalozi wa pamba? Mimi nakushangaa, sijui unafeli wapi mdogo wangu katika jambo hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni sula la ushirika. Ushirika mnawatengea pesa pale, naona shilingi 20kwenye kila kilo. Sijui kuna *AMCOS,* sijui kuna nani mnawatengea, sasa huu ushirika uliofilisika; ushirika kama Nyanza, wakati unaanzishwa mwaka 1972, wakati huo Mwanza kwa Mkoa mzima wa ilikuwa na wananchi 760,000. Leo wananchi tuko 3,600,000. Ushirika huu umeshindikana, umeshakufa, unaung'ang'ania wa nini Mheshimiwa Bashe? Mwisho tuje tugombane humu ndani, una tu-*lock* sisi kuendelea. Tuna *Ginnery* Buyagwi iko pale, inatakiwa ukarabati, wewe mwenyewe ulikuja ukaona.

**MHE. BALOZI DKT. BASHIRU A. KAKURWA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**TAARIFA**

**SPIKA:** Mheshimiwa Tabasam, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Bashiru Ally Kakurwa.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, taarifa iwe na afya.

**MHE. BALOZI DKT. BASHIRU A. KAKURWA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpa taarifa mzungumzaji kwamba suala la ushirika ni sera ya CCM na iko kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Tabasam unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Namheshimu sana bosi wangu, lakini kama kuna

kitu kiko *ICU* tukiacha kusema kwamba mgonjwa huyu ana hali mbaya, kwa sababu tu kiko ndani ya sera, sasa hii ni hatari. Kwa hali hiyo, tunavyozungumza, sisi ushirika tunautaka, lakini uwe ushirika wenye manufaa. Kwa mfano, kama ushirika wa *KACU,* walijiondoa *SHIRECU,* lakini leo *KACU* ndiyo kanunua mbolea, viuatilifu na kila kitu. Kaenda kukopa, ni ushirika ambao hauna deni.

Mheshimiwa Spika, ushirika wetu wa Nyanza, tuna *godown* Dar es Salaam, leo zinaweka marumaru badala ya kuweka pamba; zinaweka mabati na nondo; tuna *godown* ziko Mwanza, Mheshimiwa Bashe alikuja akaona, leo wanaweka *cement* na magodoro. Pia tuna ofisi zetu za Nyanza, hata mimi nina ofisi kule ndani, zilikuwa ni ofisi za ushirika, lakini leo tunapangishwa sisi kama ofisi. Kuna mabenki na kila kitu. Kwa hiyo, ule ushirika hauwezekani tena.

Mheshimiwa Spika, leo Mwanza hawalimi pamba. Nyamagana sasa hivi ni Jiji, hawana hata nafasi ya kwenda kutengeneza makaburi. Hawa wanatakiwa ushirika wa nini tena? Ilemela hawana hata sehemu ya kulima pamba, ushirika wa nini? Ushirika sasa unatutaka sisi watu wa Sengerema na Buchosa, unamtaka mtu wa Misungwi, Kwimba, Ngudu na Magu. Pia ushirika huu wa Nyanza unavyouona, pesa wanazo kule, tumeomba tuletewe *CEO* pale, tuweze kuja kugawana sisi. Huyo Mrajisi anachukua pesa karibu Shilingi sita kwa kila kilo ya pamba; ya nini? Huyo Mrajisi anafanya kazi gani, wakati ushirika umekufa? Leo Nyanza hajanunua pamba miaka 23. Sera ya CCM*;* miaka 23! Pamba inanunuliwa na wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, washirika tumekaa sisi wenye ushirika wetu, tuna hali mbaya Mheshimiwa Bashe. Unashindwaje kuvunja hii? Nakamata kule kwenye fungu lako, ukurasa wa 15 kwenye ushirika, nitakukamatia kule mdogo wangu. Sina jinsi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Najua kabisa wewe ni mzalendo, lakini kama hutakuja kusema unakuja kuugawa ushirika wa Nyanza, watu wamebakia kuwa walaji tu pale, wanakula pesa za Nyanza. Wewe mwenyewe njoo uje useme hapa, Nyanza inafanya kazi gani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Tabasamu, kengele ya pili ilishagonga. Ahsante sana.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, naomba sekunde moja nimalizie mchango huu.

**SPIKA:**Ahsante sana. Kuna wenzio wameomba kuchangia nao, sasa inabidi uunge mkono hoja.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO**: Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Shukurani. Mheshimiwa Aleksia Asia Kamguna, atafuatiwa na Mheshimiwa Assa Nelson Makanika na Mheshimiwa Nancy Hassan Nyalusi, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi. Awali ya yote, hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupatia uhai. Nampongeza Mheshimiwa Samia kwa kazi anazozifanya yeye na wasaidizi wake pamoja na Mawaziri na Watanzania wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nimesimama kwa ajili ya kuchangia kwenye hii bajeti ya kilimo kama inavyojieleza yenyewe, katika ukurasa wa 11 aya ya 26, amesema kwamba, upande wa mazao mwaka 2020 mazao yalipatikana kwa asilimia tano, mwaka 2021 ilikuwa asilimia 3.6 na mwaka 2020 tena

katika upande wa kipato ilikuwa ni asilimia 15.4 na mwaka 2021 ilikuwa ni asilimia 14.6.

Mheshimiwa Spika, katika Tanzania idadi yetu ni milioni 61.74, lakini walio wengi ni wakulima ambao ni asilimia 65. Wakulima hawa ukiwaangalia sana kwa haraka haraka ni watu ambao kidogo ni wenye shida nyingi na changamoto nyingi. Wao wamesema kwamba katika ukurasa huo, aya ya 26, wanasema kilimo kilipungua na mapato pia lilipungua kwa sababu ya Uviko-19 pamoja na vita vya Ukraine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naenda mbali zaidi, siyo vita tu na Uviko-19, mmeacha kitu kikubwa tu; migogoro ya wakulima na wafugaji. Migogoro ya wakulima na wafugaji pamoja na tembo, hao ndio wamefanya wakulima warudi nyuma. Kwa sababu Uviko vijijini walikuwa hawavioni, wakulima wadogo wadogo walikuwa wakiendelea na kazi, lakini wakilima kule vijijini watu wa mifugo wanaingia wanakula; tembo wanaingia wanashambulia yale mazao; lakini wanaposhambulia, tembo ana mtetezi wake ambaye ni Wizara ya Maliasili na Utalii, anakwambia wewe mazao yako yameliwa kwa sababu umelima kwenye *shoroba.* Mtu wa mifugo, Wizara yake inamtetea pia, inasema kwamba, mtu wa mifugo kazi yake, amewaandalia chakula, kutengeneza manyasi, ambayo ameyapanda. Sasa yale manyasi hayatakua ndani ya miezi mitatu au miezi sita. Sidhani kama mtu ana ng'ombe 100 atalisha kwenye robo heka, itamuchukua muda. Je, huyu mkulima katika kipindi hiki atakuwa Halimi, ataishije? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkulima anaonekana kama hana mtetezi, ni mkiwa. Kama tembo anatetewa na maliasili, kama mfugaji anatetewa na Wizara ya Mifugo: Je, huyu mkulima anatetewa na nani? Katika hotuba yake sijaona sehemu yoyote ameainisha kwamba mkulima tumsaidie katika hatua hii na hii, katika hali hii. Jamani, hicho kilimo kitaendaje? Umetenga hela nyingi sana kwa ajili ya skimu za wakulima,

lakini zile skimu zitaenda kufanya kazi gani kama mtu analima, halafu mazao yake yanaliwa na tembo, mazao yake yanaliwa ni mifugo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza Wizara ya Kilimo kama inavyosema, imwangalie mkulima, mnamteteaje mkulima huyu ambaye ni yatima? Hatuwezi tukapanga bei wakati kile kilichovunwa hakipo. Sasa tunaomba Wizara ya Kilimo imtetee mkulima ambaye ni yatima. Kwa mfano, hususan Mkoa wa Morogoro, mnajua kabisa ule ni Mkoa wa kimkakati, kama Wizara ya Kilimo mngesimama, tungeweza kulisha Tanzania nzima, lakini kwa kuwa tumebaki yatima, Morogoro itakuwa ni masikini kuliko ilivyokuwa hapo awali, kwa sababu haina mtetezi.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara hii iangalie, kama wao wameweka nyasi, hao watu wa mifugo, na maliasili wanasema tunalima kwenye shoruba: Je, ninyi mnatuteteaje wakulima? Naomba mnapomalizia hapa unijibu kwamba, ninyi mmejipangaje katika kumtetea huyu mkulima ambaye ni yatima? Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili nazungumzia kuhusiana na usalama wa chakula. Katika Tanzania, zamani kulikuwa na *National Milling,* watu wanachukua vyakula wanaweka dawa kwenye magunia na kwenye mifuko, lakini walikuwa wanakoboa *National Milling,* kumbe vile vyakula vina dawa ndani yake. Sasa hivi unakuta kila kona vimezagaa viwanda vya kukoboa mahindi: Je, usalama wa huyo Mtanzania uko wapi? Kwa mfano, kule Dar es Salaam Manzese, unakuta unaenda, kuna viwanda, lakini kuna maji kwenye kikopo. Sasa yale maji yatasafisha yale mahindi jamani? Matokeo yake unakuta kwamba, watu tunakula sumu na wanapata magonjwa mengi kama ya kansa kwa sababu hatudhibiti hivyo vyakula. Tunaomba Wizara ya Kilimo msimamie, ili tuweze kupunguza haya magonjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kuna kilimo hiki cha mbogamboga, tunapulizia dawa. Hizi dawa katika kupulizia, hamjawaelimisha wale wakulima wadogo wadogo. Wakipulizia dawa baada ya siku mbili mtu anaziuza zile mboga; akishaziuza, walaji wanakula, hatujui mle ndani kuna nini? Matokeo yake magonjwa tena yanaongezeka. Kwa hiyo, naomba Wizara ya Kilimo mliangalie hilo, kwamba wakulima ni watoto yatima.

Mheshimiwa Spika, mkitaka tuendelee, kwanza mkae ninyi Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo ili mjue kwamba mtatatuaje tatizo la wakulima na wafugaji kwa Tanzania nzima hususan Mkoa wa Morogoro? Pia mkae muone kwamba mtatatuaje hilo tatizo la sumu ambazo nafikiri Watanzania wengi tunakula sumu, baada ya kuwa tunakula sumu, tunatumia hela nyingi sana katika kujitibia, basi mtafute namna ya kusimamia hiyo miradi yetu ambayo tunawawezesha wakulima wadogo wadogo, tusiwaache, lakini tuwasimamie hatimaye nao waweze kujikwamua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo, machache, naunga mkono hoja. Nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Assa Nelson Makanika, atafuatiwa na Mheshimiwa Nancy Hassan Nyalusi, na Mheshimiwa Godwin Kunambi, ajiandae.

**MHE. ASSA N. MAKANIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Wizara hii ya Kilimo ambayo ni muhimu sana, Wizara ambayo ina mchango mkubwa sana katika Taifa letu. Asilimia 26.1 ya pato la Taifa linatokana na Wizara hii. Wizara hii ni muhimu sana kwa sababu inatoa ajira ya wastani wa asilimia 65, lakini siyo hivyo, viwanda vyetu na malighafi zake asilimia 65 zinategemea Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nimshukuru Mheshimiwa Rais, anafanya kazi kubwa sana, lakini nimshukuru pia Mheshimiwa Waziri Mkuu, anafanya kazi kubwa sana katika Mkoa wetu wa Kigoma na hasa katika zao la chikichi. Mheshimiwa Waziri Mkuu amefanya jambo kubwa sana la chikichi ambapo pamoja na ukuaji mkubwa tunaupigia kelele, lakini jambo la kudhibiti vipimo vya mafuta ya mawese ni jambo kubwa sana katika Mkoa wetu wa Kigoma. Tunatuma salaam hizo za shukrani kwake na kwa Serikali yote na pia kwa Kamati ya Ulinzi na Usalama, kwa kazi kubwa ambayo wanaendelea kuifanya katika Mkoa wetu wa Kigoma. Hivi sasa vipimo vya lita 30 ambavyo vilikuwa vinamnyonya mkulima wa Mawese, vinaonekana kama bangi katika Mkoa wetu wa Kigoma. Hilo tunalishukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ni kijana, kaka yangu Mheshimiwa Bashe, namshukuru sana kwa kazi anayoifanya. Pamoja na mambo mazuri sana aliyoyafanya katika Wizara yake, natambua Benki ya Kilimo *(TADB)* imetoa mikopo shilingi bilioni 169, lakini shilingi bilioni 108 zimekwenda kama *direct landing.* Siyo hivyo tu, bado ametoa shilingi bilioni 60 kwa ajili ya kwenda kwa wakulima wadogo wadogo. Kwa hilo tunamshukuru sana na tunaendelea kuipongeza Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. hapa liko jambo moja tu ambalo tunamwomba Mheshimiwa Bashe, sisi kama vijana, naye ni kaka yetu atusikie. Hapa kuna changamoto kubwa sana. Kwenye benki hii ya kilimo, hebu uwape mtaji kaka yangu wafanye kazi.

Mheshimiwa Spika, wakulima wanahitaji mitaji. Benki hizi usipoziwezesha, hawawezi kupata manufaa makubwa na benki hii. Mheshimiwa Bashe nitakupa mfano mmoja. Hivi sasa hii Benki ya *TADB* inaweza kukopesha wakulima wetu kwa asilimia tisa, lakini wakulima bado wana mizigo mikubwa, ndio maana tunaomba uweze kuiongezea pesa ili angalau

asilimia ishuke nane mpaka saba ili mkulima asiwe na mzigo mkubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini si hivyo Mheshimiwa Bashe, wapo watu ambao wanaingia kama ma-*middle men* kwenye hii benki ya kilimo, ambao ukiangalia kama Mkoa wa Kigoma, ili hizi *AMCOS* ziweze kukopesheka lazima kuwe na mtu anaitwa *PASS*. Huyu *PASS* ndiye atakuwa mdhamini wa mkulima ili mkulima aaminike, watu hawa jaribu kuwa *Cut off*. Kwa sababu huyu *PASS* ana *percent* yake kwenye mkopo ambao mkulima atachukua. Ukiwaondoa hawa *PASS* unamuondolea mkulima mzigo mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye kahawa Mheshimiwa Bashe, umefanya jambo kubwa sana katika Mkoa wetu wa Kigoma. Umeweza kufanya jambo la msingi sana mpaka wanunuzi wamekwenda kwa mkulima *direct.* Wamenunua kahawa na angalau kwa Mkoa wetu wa Kigoma bei si haba, tunakushukuru sana kwa jambo hilo. Lakini mzigo umeutoa ulikokuwa mwanzo umeuhamishia kwenye pembejeo. Hivi sasa lita moja ya dawa ya kutibu kahawa iliyokuwa inanunuliwa kwa shilingi 15,000 hivi sasa ni 50,000. Huo ni mzigo mkubwa sana Kaka yangu Bashe, uweze kuangalia namna gani tuweze kumpunguzia adha mkulima huyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *my brother* nitazungumzia jambo lingine, jambo la mkulima na pembejeo. Wabunge wengi wamezungumza katika hali hii ya mbolea ya ruzuku na nimekusumbua sana kipindi cha mbolea hii. Mheshimiwa Bashe, nia ni njema ya suala hili na tunaipongeza sisi Wabunge ambao tunatoka kwenye majimbo ya vijijini. Lakini ziko dosari ambazo zimeingia hapa katikati zilitaka kuchafua nia hii, na jambo hili Mheshimiwa Bashe, tutafurahi zaidi ukilifanyia kazi kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano tu mdogo ili niweze kumalizia, naona na muda unakwenda. Mheshimiwa Bashe, kwenye hii *program* ya mbolea ya ruzuku wapo watu wanne, kuna Serikali, kuna *supplier,* kuna *agency* ambaye ni wakala lakini kuna mtu wa mwisho ambae ndiye mkulima.

Mheshimiwa Spika, sasa tunapata shida kubwa sana ambapo tunaona mkulima anapiga kelele. Mbolea muda mwingine inamfikia kwa bei ya juu sio hiyo ya ruzuku. Wakulima wa Mkabogo kule jimboni kwangu, wakulima wa vijiji vya kule Kalinzi wameweza kufikiwa na mbolea kwa bei ya 120,000 mpaka shambani, wakati ili hali hii mbolea ni shilingi 70,000. Ukiangalia hapa katikati ni kwa sababu hawa mawakala wana sababu kuu mbili.

Mheshimiwa Spika, sababu ya kwanza; wao wanaweza kutoa ile mbolea kwa mkopo. Maana yake ninyi mnamlipa *supplier* mnamwacha *agent*, huyu *agent* hana mtaji mkubwa wa kuweza kupeleka mbolea mpaka kwenye tarafa na vijiji lakini angekuwa na mtaji mkubwa angeweza kufikisha mbolea hii hadi kwenye vijiji.

Mheshimiwa Spika, sasa, changamoto kubwa unakwenda kumlipa *supplier cash* unamwacha *agent* huyu aende akazungushe mbolea kwa pesa yake, matokeo yake mbolea haifikishi. Ukiangale pale Kigoma Mjini *agent* alikuwepo mmoja. Kigoma mjini hakuna mkulima sisi vijijini ndio tunalima lakini hakukuwa na wakala hata mmoja, kitendo ambacho kimeongeza hii nia njema ikaonekana kuwa nia mbaya lakini tunaamini kwa jambo kubwa ambalo unaendelea kufanya, ukaifanye hii kazi kwa ustaarabu mkubwa sana ili wakulima wetu waweze kunufaika na hali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisimalize bila kuunga mkono hoja, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nancy Hassan Nyalusi, atafuatiwa na Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, Mheshimiwa Augustine Holle Vuma ajiandae.

**MHE. NANCY H. NYALUSI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja hii iliyoko mezani.

Mheshimiwa Spika, nina mambo matatu; jambo la kwanza ni pongezi na Shukurani. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa maono na msukumo Mkubwa ambao ameuweka kwenye wizara ya kilimo. Pia tunampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na viongozi wote wa Wizara kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi wananchi wa Mkoa wa Iringa, tunaishukuru Serikali sana kwa mpango wa ujenzi wa kiwanda cha kuchakata parachichi katika Wilaya ya Mufindi, Kata ya Nyororo. Tunamuomba Mheshimiwa Waziri anapokuja kuhitimisha atuambie ni lini ujenzi wa kiwanda hicho utaanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo langu la pili, ni ruzuku ya mbolea. Tunaishukuru sana Serikali kwa ruzuku ya mbolea, wananchi wanafurahia sana kwa jambo hilo. Tunaishukuru tena Serikali kwa sababu mwaka huu wametenga tena pesa kwa ajili ya mbolea ya ruzuku. Lakini msimu uliopita kulikuwa kuna changamoto nyingi ambazo zilitokea. Naomba kutoa mapendekezo yafuatayo ili kuweza kutatua changamoto hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza, tunaomba mbolea zifike kwa wakati kabla ya msimu haujaanza. Kwa sababu mwaka jana mbolea ya kupandia ilichelewa hadi mahindi yamekwisha ota mbolea ya kupandia ndio inafika ambayo ilileta usumbufu mkubwa sana kwa wananchi na kero kubwa sana. Mheshimiwa Waziri tunaomba utusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, tunaomba ziwekwe *center* ambazo wakulima wataweza kupata m,bolea kwa wepesi. Kwa sababu kwa mfano kule kwetu Mkoa wa Iringa, mwananchi alikuwa anatoka Mauninga karibuni kilometa 100 anafuata mbolea Iringa Mjini, ni mateso makubwa sana. Mwananchi anatoka Maduma anakwenda mpaka Mafinga Mjini ndio apate mbolea, ni mateso makubwa sana. Tunaomba ziwekwe hizo *center* na pia Mheshimiwa Waziri, mfumo wa ugawaji wa mbolea uendane na uhalisia wa maisha ya watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mapendekezo mengine ni usajili wa wakulima. Mheshimiwa Waziri, tunakuomba uanze usajili wa wakulima mapema kwa sababu suala la usajili sio dharura. Unaweza kuanza kuwasajili sasa hivi ili kuondoa usumbufu ambao ulikuwa unajitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la nne; ni Mamlaka ya Mbolea Tanzania, Mfumo wa Mamlaka ya Mbolea Tanzania, tunakuomba Mheshimiwa Waziri, ukaufanyie mapitio. Kwa sababu una mapungufu mengi ambayo mawakala wanalalamikia. Kwa hiyo, tunaomba ukafanye mapitio kwenye mfumo huo ili kutoa haya mapungufu na kuwaondolea mzigo mawakala. Mheshimiwa Bashe, tunaimani kubwa na wewe na tunaimani kwamba utatatua changamoto hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ya tatu; ni stakabadhi ghalani, Serikali ina mpango wa kuingiza zao la mahindi kwenye mfumo wa stakabdhi ghalani katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Lakini Mheshimiwa Waziri anapohitimisha tunaomba atwambie amejipangaje? Kwa sababu tumeona kwamba kwenye zao la choroko na dengu kulikuwa kuna usumbufu mkubwa na changamoto nyingi. Je, amejipangaje kwenye huo mpango wake wa kuingiza zao la mahindi kwenye stakabadhi ghalani? Kwa sababu wakulima

wana hofu na wanahitaji kuondolewa hofu hiyo ili waweze kupata faraja katika jitihada zao za uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, atafuatiwa na Mheshimiwa Vuma Agustine Holle, Mheshimiwa Jumanne Kibera Kishimba ajiandae.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nami nishiriki kutoa mchango wangu, ushauri wangu, kwenye sekta hii muhimu kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Taifa letu limepita katika kipindi tofauti na katika kila kipindi tulikuwa tunashuhudia kauli mbiu mbalimbali kuhusiana na hii sekta ya kilimo. Wakati wa Hayati Baba wa Taifa tulianza na kilimo cha kufa na kupona, ikapita tukaja na Kilimo uti wa Mgongo, ikapita, tukaja na Kilimo Kwanza ikapita. Sasa tumemaliza maneno yote ya kiswahi tumekuja na maneno ya kiingereza, bado kilimo kipo pale pale ni changamoto kwa Taifa letu, tunasema (*BBT) Build a Better Tomorrow* (Jenga Kesho Iliyobora). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mwandishi mmoja wa kiingereza anaitwa Shakespeare aliwahi zungumza kauli hizi mbili; ya kwanza alisema *if wishes were horses, baggers would ride them* (Kama matamanio yangekuwa Ngami hata omba omba wangeweza kuendesha. Lakini akaaza kuchanganya msemo mwingine tena akisema *wishes are weak salad to dine with* (matamanio ni sawa na kachumbali iliyochacha haifai kwa kitoweo). *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, tukiendelea kuwa na matamanio kama Taifa kwenye sekta ya kilimo na bila kuwa na jitihada, bila kuwa na utayari, bila kuwa na *commitment* kwenye sekta ya kilimo, nina wasiwasi hata hii ya *BBT (Build a Better*

*Tomorrow)*. Namwamini sana Kaka yangu Mheshimiwa Bashe na Ndugu yangu Mheshimiwa Naibu Waziri, katika hili wazo ni jema lakini nitashauri hapa tuboreshe kidogo Ili tusiishie tu kuwa na matamanio, matamanio tukumbuke ni sawa na kachumbari iliyochacha haifai kwa kitowewo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nia ni njema na dhamira ya Serikali ni njema kabisa, naomba nishauri kuboresha eneo hili la ajira hasa kwa hawa vijana hii programu ya *BBT.*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri kaka yangu Mheshimiwa Bashe, naomba unisikie kwa makini eneo hili. Mimi ni mkulima na bahati nzuri na kifahamu kilimo hasa cha zao la mpunga, nililipa ada ya elimu ya sekondari kwa kuuza mchele na mpunga. Nitaeleza kidogo hapo *am not speaking from without, am speaking from within.* Sizunguzmi habari ambayo siifahamu, nazungumza habari ambayo ninaifahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunawachukua vijana na ninaomba nishauri kufikiri kimakakati kwenye eneo la *BBT*. Kijana yeyote ni *desperate* anataka pesa ya chap chap, kijana yeyote anataka maganikio ya haraka. Ukichukua kundi la vijana ukawapeleka mahala tukaandaa mashamba ya *block farming,* zao ambalo litachukua miaka minne, kijana anakimbia, habaki ataondoka. Kwa sababu matamanio yake apate fedha ya chap chap.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwenye eneo hili, twende kwenye maeneo husika ambayo vijana wanajishughulisha na kilimo. Usichukue watu wapya, usichukue watu wa Dar es salaam, usichukue watu wa mjini uwapeleke wakalime, kilimo ni *tiresome work* sio kazi ya mzaha mzaha ni kazi ya kujituma kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, twende Mororgoro kule Mlimba tukatazame vijana wanajishughulisha na kilimo pale

tukawawezeshe wale. Wale wakiwezeshwa, kijana mkulima wa Mlimba anaelima mpunga akalima vizuri, akanunua *V8,* akajenga nyumba bora anaendesha, vijana wengine watajua kilimo kinalipa. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini hawa watawachukua Dar es Salaam, wamenyoa *punk,* tunawaweka mahala wakalime kilimo ni *tiresome work,* sio mchezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe kwanza kufikiri kimkakati jambo moja, aina ya mazao tutakayokwenda kulima yawe ya muda mfupi. Nimeona pale Dodoma ili zabibu ivunwe sio chini ya miaka minne. Nani atakaa miaka minne asubiri hii zabibu? Nina wasi wasi na matokeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zabibu yenyewe haina soko hapa Dodoma, wananchi mazao yanaoza. Twende tukaimarishe mazao ya muda mfupi. Mahindi, mpunga, kijana ndani ya muda wa miezi minne, au sita ana fedha mfukoni. Mje Mlimba pale mfanye kilimo, muende na maeneo mengine. Mazao ya muda mfupi haya ndio yatakayowasaidia vijana wengi kuvutiwa na kilimo kwa sababu watapata pesa ya chap chap. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine tunazungumzia kilimo cha biashara, ili kilimo biashara kiweze kufanikiwa :-

Mheshimiwa Spika, moja; lazima uwe na ardhi inayofaa kwa kilimo. Sasa na hii ningependa kusikia unapokwenda kuhitimisha, namna gani wizara ya Kilimo inashirikiana na sekta ya ardhi katika kuhakikisha mwananchi wa kitanzania anakopesheka?

Mheshimiwa Spika, leo hii mkulima wa Mlimba ana eneo la heka 50 hakopesheki benki hana *title*, hawezi kuwa na kilimo biashara. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa

kuwaasa benki zote washushe riba. Ninashukuru benki wameitikia sasa hivi benki mikopo ni *single digit* asilimia 9. Pia nimekopa juzi *CRDB* nimekopa wa-*vester* mikopo mizuri lakini sasa nani anakopesheka? Nimekopesheka kwa sababu nilikuwa nina *collateral* nina hati. Sasa mkulima wa kawaida asilimia zaidi ya 70 ya wakulima hawana hati miliki. Sasa kilimo biashara itakuwa nikauli ile ile isiyotekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namna gani tunaunganisha sekta ya kilimo na viwanda na Biashara? Hii lazima unapokuja kwenye *winding up* nipate majibu, unieleze namna gani viwanda na biashara inashirikiana na kilimo katika kuanzisha *agro based industries.* Hilo nalo ni jambo lingine kwenye suala la zima la masoko. Kwa hiyo, najaribu kueleza haya yote na ni muhimu Mheshimiwa Waziri, ukayaeleza ili tuone kama watanzania kwamba ni kweli tunaona tuko tayari kwenda kuwa na kilimo biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho najua kengele ya pili imegonga, ni ya kwanza naenda ya pili? Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nazungumzia hoja ya zao la bidhaa ya mchele. Duniani takribani watu bilioni 3.5 wanakula mchele lakini leo hii *NRFA* hawajajenga hata ghala moja la kuhifadhi mpunga. Mahindi kule Marekani ni chakula cha mifugo. Mahindi yanagharama kubwa kuyahifadhi kuliko mpunga, mpunga hauhitaji dawa yoyote utakaa hata miaka kumi. Adui wa mpunga ni maji tu, mje *NFRA* na mpango sasa muanzishe maghala ya kuhifadhi mpunga. Hilo ni jambo lingine natoa ushauri kwenye eneo hilo. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kwenye suala la umwagiliaji. Unajua nasikitika sana kwenda sehemu kame na kuanza kuchimba visima vya maji tutengeneze mabwawa, gharama ni kubwa. Hii nchi Mungu aliibariki jamani yaani hoja yangu tunataka ku–*achieve* nini? Yaani tunapokuwa na mpango wa jambo fulani tunataka ku–*achieve* nini? Ushauri

wangu kaka yangu Mheshimiwa Bashe, nakuomba nenda maeneo ambayo uwekezaji wa umwagiliaji ni rahisi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana, kengele ya pili imekwishagonga.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga hoja mkono. Ahsante sana. (*Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Vuma Augustine Holle, atafuatiwa na Mheshimiwa Jumanne Kibera Kishimba, Mheshimiwa Zubeiri Mohammed Kuchauka ajiandae.

**MHE. VUMA A. HOLLE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia kwenye bajeti hii ya Wizara muhimu, Wizara ambayo imebeba maisha ya watanzania walio wengi. Awali ya yote nipongeze Serikali Kupitia Mheshimiwa Rais, kwa kuendelea kuongeza bajeti ya Wizara ya Kilimo. Ni wazi kwamba kwa kufanya hivyo wanagusa watanzania walio wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaenda moja kwa moja kwenye mchango wangu. Jambo la kwanza; Jimbo la Kasulu Vijijini lina kata 21, kata 10 kati ya 21 wanalima pamba. Ukienda kwenye Kata ya Asante Nyerere, Kata ya Rungwe Mpya, Kigembe, Pwaga, Shunguliba, Nyamidaho, Kitagata, Kurugongo na Lusesa, kata kumi, kata zote hizi ni wakulima wa pamba.

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali tangu mwaka 2019 mpaka leo 2023 imeweka baridi kwenye sekta ndogo ya pamba. Baridi kivipi? Kuna madai ya *key players* kwa maana ya makampuni ya ununuzi wa pamba lakini na makampuni

ambayo yana–*supply* pembejeo wanadai Serikali zaidi ya bilioni 102 kwa zaidi ya miaka minne sasa Serikali inadaiwa, imeshikilia pesa hiyo haijawalipa fedha zao. Kwa kufanya hivyo, kumefanya sekta ndogo ya pamba iweze kuathirika na kusinyaa. Wananchi kule ndio ambao wanateseka kwa sababu hawa ndio *key players. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumefanya vikao mara kadhaa na hata hapa Bunge lako liliazimia kwamba Serikali inapaswa kulipa fedha hizo. Tunataka tujue wakati waziri akija hapa kwenye majumuisho atueleze ni lini Serikali italipa fedha hizi za *key players* hawa kwenye sekta ndogo ya pamba ili kuchangamsha sekta hiyo *otherwise* hatutakubaliana. Hilo ni jambo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nichangie kuhusu Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko, Mheshimiwa Waziri, unisikilize kwa umakini, *CPB* ilikuwa ni taasisi ambayo inaenda kufa kabisa *it was a loss-making company.* Sasa hivi imeanza kutengeneza faida na inakwenda vizuri, lakini ziko taratibu ambazo bado zinaishika. Tumewasikiliza kwenye Kamati yetu ya *PIC* mara kadhaa. Hawa *CPB* wanafanya biashara kama wafanyabiashara wengine, wana–*competitor* wengi tu kwenye kuuza unga, kwenye kuuza sijui nini, kwenye kuuza mafuta, kwenye yote wanayoyafanya wana *competitors* wengi.

Mheshimiwa Spika, sasa kuna changomoto ya kwanza ni kuhusu mtaji. hawa watu kwa sababu wanafanya biashara na wanapata faida wala hawahitaji Serikali ichukue mtaji iwape ila iwawekee utaratibu mzuri wakitaka kukopa fedha.

Mheshimiwa Spika, *CPB* wakitaka kukopa fedha kwa ajili ya biashara wanatakiwa kwenda kuomba kibali. Yaani bodi ya *CPB* haina mamlaka wala nguvu ya kuweza kwenda kukopa, yaani kwenda kukopa benki mpaka waombe kibali

kutoka Wizara ya Fedha, mchakato ambao huwa unakwenda mpaka miezi mitano au sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sasa wakati kuna *competitor* wengine wakitaka mtaji wao wanakwenda benki wanakopa wana-*invest* kwenye biashaara sisi taasisi yetu hii lazima kwanza tusubiri miezi sita. Yaani bodi ilishapanga kukopa, imepitisha inaenda kwanza Wizara ya Fedha, unasubiri sijui miezi mitano au sita ndipo majibu yaje wakope.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kuisaidia taasisi hii. Kama tutataka kumsaidia Mheshimiwa Waziri taratibu hizi zirekebishwe, hawa watu wawe na uwezo wa kwenda kukopa. Bodi ikshaidhinisha wawe na uwezo wa kukopa, wakikopa tutakuwa tunafungua minyororo ambayo tumewafunga na tutakuwa na spidi nzuri sana kwenye ku-*compete* na wengine ambao wako kwenye soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa ubunifu wake wa wakugusa sasa wakulima wadogowadogo kupitia bajeti yake ya mwaka huu. Nimesoma kwenye ukurasa wa 138 wa bajeti yake; kwamba anakwenda kujenga miundombinu kweye kila halmashauri. Kila halmashauri itachimbiwa kisima kirefu, kwa kuanzia, kwa hiyo watachimba visima 184. Pia amesema atawawezesha wakulima, yaani kila kisima kimoja kitatumiwa na wakulima 150, kila mkulima atapewa eka mbili. Kwa hiyo zaidi ya ekari 69,000 zitaendelezwa, hii ni hatua kubwa sana. Hata wale ambao walikuwa wanalalamika kwamba *BBT* haijachukua vijana wao, sasa unakuja mradi ambao kila halmashauri, kwa kuanzia, ina uwezo wa kuwa na watu au wakulima 150 ambao watawekewa utaratibu mzuri na hatimaye waweze kujiajiri, huu ni mwanzo mzuri. Ninaamini kila mwaka utakuwa unazidi kuongeza fedha ili badala ya kuchukua wakulima 150 uende mpaka 500 na zaidi katika kila halmashauri ili kuhakikisha kwamba wakulima tunawasaidia; hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Benki ya Kilimo, Benki ya Kilimo tulishasema hapa pia, lilishaweka Azimio la Bunge; kwamba wapewe bilioni 100 ili kuwea ku-*bust* mtaji wao waweze kuwafikia watu wengi. Kila mtu anasema Benki ya Kilimo inafanya vizuri, wengine wanasema hatujakopeshwa; ni kwa sababu wanania ya kukopesha lakini mtaji ni mdogo.

Mheshimiwa Spika, mimi najifikiria, kwa nini Benki ya Kilimo, yaani iwe chini ya Wizara ya Fedha, *why?* Hili Serikali mkalifikirie vizuri. Yaani kwa nini isiwe Wizara ya Kilimo huko huko? Yaani Benki ya Kilimo iko Wizara ya Fedha, sidhani kama kuna ulazima sana Benki ya Kilimo iende kuripoti kwa Waziri wa kilimo.

Mheshimiwa Spika, hii inaweza kusaidia sana kuepusha baadhi ya *delaying communication* na maamuzi, wala hakuna shida yoyote. Tunashudia kuna baadhi ya Wizara hapa zinamiliki vyuo; kwa nini wasiseme kwamba chuo cha kilimo ki-*repot* kwenye Wizara ya Elimu? Mbona kina-*report* kwa Wizara ya Kimo wenyewe? Chuo cha Biashara kina-*report* kwenye viwanda na biashara; kwa nini kisi-*report* kwa Wizara ya Elimu? Kwa hiyo hii nayo inawezekana. Wizara ya Kilimo wapeni benki yao ili kupunguza hizo *delaying za communication* kati ya Wizara na Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba niunge mkono hoja. Ahsante sana.

**SPIKA:** ahsante sana Mheshimiwa Jumanne Kibera Kishimba atafuatiwa na Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga ajiandae.

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniaptia nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Kilimo. Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuongeza bajeti kwa *29 percent* kwenye bajeti yetu ya kilimo,

ambayo itatusaidia sana hasa sisi ambao tunatoka katika maeneo ya kilimo. Mwaka huu tunakabiriwa na ukame mbaya sana ukilinganisha labda wa mwaka 1974, kwa hiyo tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tunahitimisha Wizara ikiwemo na kamati moja, mimi leo nitaanzia Wizara ya Mifugo na uvuvi ambayo ilianza mwanzo.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri Mwanasheria Mkuu wa Serikali yupo hapa; tunaomba, kwa wafugaji wetu ambao ng'ombe wao wamekamatwa kwenye hifadh,i wanapokuwa wametolewa hukumu wapelekwe kwenye mnada kwenda kuuzwa kihalali badala ya mtindo wa sasa hivi ambapo watu wa kule hifadhi wanapiga mnada wao. Wapelekwe mnadani kama sheria ya Serikali ilivyo na mnada wa Serikali ndio unaotambulika, itawasaidia sana. Wafugaji wetu watapata kinachobaki na wao Serikali watapata kinachobaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la kufunga Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria. Sisi maeneo yetu uchumi wetu pia unategemea maziwa haya. Maziwa haya yakifungwa tutakuwa tumeingia kwenye mgogoro mkubwa sana hata sisi watu wa Kahama na Shinyanga, hasa wakati huu ambao ni mgumu sana kwetu.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze Wabunge wa Kigoma kwa mchango mzuri sana ambao walionesha wakati wa kutetea. Lakini kikubwa, na hoja yangu ya msingi hapa ni kwamba lazima wataalamu wetu watumie muda mrefu sana wa kufikiri. Ng'ombe anazaa mtoto mmoja kwa mwaka, mbuzi anazaa mtoto mmoja kwa mwaka, na kondoo pia, lakini hatujawahi kuona shortage inatokea. Ni lini tumepata shida kwamba nyama ya ng'ombe hakuna au ng'ombe hakuna; na hata sasa hivi tunazozana kupunguza ng'ombe?

Mheshimiwa Spika, samaki anazaa watoto laki mbili mpaka milioni moja; tunahakika wamekwisha? Ni uongo wa mchana. Kinachoendelea hapo ni kwamba gharama ya uvuvi imepanda. Leo *drum* moja la *petrol* ambalo ni lita 200 unahitaji zaidi ya shilingi 800,000 mpaka 1,000,000. Sasa kama una ma-*drum* matano unaondoka kwenda kuvua huna darubini, hujui samaki walipo, umeondoka na gharama ya shilingi milioni tano, unategemea utapata samaki wa milioni nane? Haiwezekani, ni *report* za uongo.

Mheshimiwa Spika, je, hawa wangekuwepo siku Yesu alipowakuta akina Simon na Petro wamekosa samaki wangelifunga Ziwa la Galilaya? Uvuvi ni kubahatisha; haiwezekani kazi ya kubahatisha, hakuna uvuvi duniani asili yake ni kubahatisha. Hata siku ya Bwana Yesu alikuta akina Simon na Petro wamekosa Samaki ndipo akawaombea wakapata. Sasa angekuwepo mtaalamu wetu angelifunga Ziwa la Galialaya? Haiwezekani, hatuwezi kuwa na wataalamu ambao ni wavivu wa kufikiri, watatuingiza kwenye migogoro mikubwa mno. Mnaona tunazozana hapa suala la herein, tunazozana kweli wananchi mpaka wanauliza, kwa nini ninyi huwa hamleti mijadala ya kutupa nyasi za kulisha ng'ombe? Ninyi mijadala yenu yote ni kuja kwetu kuja kutukamata. Hakuna mawazo mapya yanayotoka kwenu? Wananchi wanahitaji mawazo mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakwenda kwenye suala la kilimo. Ni kweli kwenye jimbo langu nina viwanda zaidi ya sita vya pamba na vinategemea pamba, lakini kwa bei inayoonesha, ya mwaka huu, labda tu tumuombe ndugu yangu Mheshimiwa Bashe mbegu za pamba na viuatilifu vya pamba viuzwe madukani kama zilivyo mbegu za mahindi na mazao mengine, itatusaidia. Kwa sababu sasa hivi mwananchi atakatwa shilingi 490 mpaka 500 kwa kilo moja, Mheshimiwa Bashe ni huruma na huruma, lazima ufanye huruma ngumu sana. Mwananchi anapata kilo 200 kwenye

ekari moja shilingi laki mbili; akikatwa huyu mtu, na hali ya chakula ilivyo, ni lazima kufikiria sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, ruhusu watu wanaoweza kununua mbegu zao wanunue ili wao wakati wanauza pamba yao wawe huru kama mazao mengine. Kwa nini mimi mnanilazimisha nikaungane kwenye *group* lingine? na kwa nini mimi nimlipie mtu ambaye mimi sihusiani naye? Mimi nimelima pamba kidogo, sikutumia dawa, sikutumia mbolea, nimelima na wanangu, naendaje kumlipia mtu mwingine aliyetumia mbolea na dawa? Haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *trend* hii ikienda zao la pamba tunakwenda kulinawa, *a hundred percent* tunakwenda kulinawa; kwa sababu mazao ni mengi mno Kanda ya Ziwa. Alizeti leo heka moja mtu atapata shilingi laki saba au nane kwa nini akalime pamba yenye matatizo mengi na migogoro mingi? Halafu ndiyo iwe na sheria kali. Kwa hiyo namuomba sana Mheshimiwa bashe aliangalie kwa mapana sana suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la mbolea hii ya kupima. Mheshimiwa Waziri yeye ana bucha; sasa nashangaa; wewe Mheshimiwa Bashe kwenye bucha lako unapima nyama watu wanaenda kula; sasa unamkataza mtu kupima mbolea ikaende ardhini, inawezekana kweli? Yaani haieleweki ni kwa nini. Na ukiisoma hiyo sheria ya kupima mbolea ni miaka miwili jela? Sasa, mwananchi hana hela laki moja na nusu, anataka kulima mchicha, sasa anafanyaje? Au unataka kuweka kwenye *garden?* Kwa nini mbolea iwe na thamani kuliko chakula? Wote tunaona, sukari tunapima.

Mheshimiwa Spika, karibu na kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu pale kuna nyama za kuku ziko nje, tena zimechomwa na Waheshimiwa Wabunge wote mko pale. Sasa iruhusiwe

kula nyama iliyochomwa iko nje lakini mtu anayechukua mbolea kusaidia mwenzie anakamatwa matokeo yake wananchi wanauziana kwa magendo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri aruhusu, hizi sheria mengine za kikoloni kwa sasa hivi hatuzihitaji tena. Kama mama ametoa fedha zote hizi tunaendeleaje na sheria mbaya za kikoloni?

Mheshimiwa Spika, Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Viwanda na Biashara anafahamu vizuri. Kuna sukari ambayo inatengenezwa kutoka kwenye viazi vya kienyeji; na hoja hiyo imeletwa mara nyingi sana kwenye Kamati wakati mimi bado niko kwenye Kamati ya Viwanda na Biashara; na sukari hiyo ni sukari ambayo inatumika kwenye soda na vitu vingine, hata kwa chakula, na ni nzuri mno, lakini inapigwa vita na watu wa viwanda vya sukari. Kwa sababu wananchi wakianza kulima viazi hivi vya kawaida wakatengeneza sukari teknolojia hii itawaondoa wao kwenye miwa.

Mheshimiwa Spika, leo mmesikia mabadiliko makubwa yaliyotokea China, China nusu wanatengeneza gari za umeme. Si na sisi tutatupa gari zetu huku? Kwa nini wao wazuie wananchi wasilime viazi ambavyo vinaiva miezi miwili, havihitaji dawa na havihitaji kitu chochote ili wakatengeneza sukari, lakini baada ya makapi yale yakawa ni chakula? Sasa kwa nini watu wakatae kibabe, kwamba wamekataa?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Khenzile ni shahidi, anafahamu, wafanyabiashara wamekuja mle wanalia, kwamba jamani ruhusuni viazi hivi vya kawaida.

Mheshimiwa Spika, maana sisi hata kwa kienyeji viazi ukivikausha ukaja ukavichemsha inayotoka ni sukari, wala haina hata ubishi. Kwa hiyo ni kiasi cha Wizara ku-*promote* ili kuondokana na hili la kulalamikia mazao ya kila aina.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia nimshukuru sana Mheshimiwa Bashe, umetusaidia sana hasa wakati wa njaa. Ametusaidia mahindi ya kutosha na kila wakati tulikuwa tukihitaji msaada wowote amekuwa akitusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba ajiandae

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi jioni hii ili nami nichangie bajeti iliyo mbele yetu. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan. Namshukuru Mheshimiwa Rais kwa mambo matatu kwenye wizara hii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka hebu sogeza kidogo hicho kisemeo, enhe namna hiyo.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Rais kwenye wizara hii kwa ambo makubwa matatu. Jambo la kwanza ni kutupatia pembejeo za korosho bure kwa msimu uliopita, jambo la pili kwa kutupatia mbolea za ruzuku kwenye msimu huu uliopoita, na jambo la tatu tulipatiwa mahindi ya msaada pale wanyama pori walipotupeleka kwenye njaa kwa hiyo ninamshukuru sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kushukuru Mheshimiwa Rais kwa kutupatia viuatilifu vya bure. Lakini wako wajanja wenzetu ambao wanatumia hizi lugha za kisasa "kutumia fursa." Kwa kweli Mheshimiwa Waziri hangaika na hawa watu wanaotumia fursa kwa kutupatia viuatilifu vilivyokosa ubora.

Jambo hili limetushushia uzalishaji wa korosho kwenye mkoa wetu wa Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo kubwa lilionisimamisha leo hapa, kuna dude moja hivi sijapata kulielewa linaitwa *COASCO.* Niko kwenye Bunge hili mwaka wa nane, hii taasisi inayoitwa *COASCO* sijajua inafanya kazi gani. Na Mheshimiwa Waziri hata ukileta semina leo watu wa *COASCO* hapa wakaja kutoa maelezo mimi nitakuwa mtu wa mwisho kuelewa.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano nina *AMCOS* zangu tano Liwale mwaka juzi walifanya vibaya, likaitwa hilo dude la *COASCO* likaja. Wamefanya kazi pale takriban kwa wiki tatu hivi kama siyo mwezi. Lakini *findings* walizozikuta pale mpaka leo ni makabati ya kwao wao, hatujui kinachoendelea. Viongozi wa *AMCOS* wanafahamu, lakini wanachama wa *AMCOS* zile hawajui chochote mpaka leo. Sasa sijaelewa hiyo *COASCO* imewekwa pale kwa ajili ya kulinda au kuchunguza? Yaani sijaelewa. Kwa kweli Mheshimiwa Waziri hebu hiyo semina ije pengine na mimi nitaweza kuelewa; lakini nilisha sema nitakuwa wa mwisho.

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hivyo; ziko *findings* ambazo ukiwauliza watakuambia hizi tumempelekea Mkuu wa Wilaya, hizi zingine tumewapelekea *TAKUKURU;* lakini mbona huu ni mwaka wa tatu sasa *AMCOS* zile bado watu wanalalamika? Kuna *AMCOS* mimi kule kwangu mizani na matrekta vimeuzwa. *COASCO* wamekwenda kufanya uchunguzi lakini *findings* zile hawajaweka wazi mpaka leo. Hawa watu *COASCO* kama kuna sheria ya kuunda hiyo *COASCO;* kwanza mimi sielewi wamewekwa pale kwa kazi gani, sheria inasemaje, wamewekwa pale *COASCO* kwa sababu ipi?

Mheshimiwa Spika, Kama *AMCOS* tano wamezikagua leo mwaka wa tatu bado zinahangaika! Ukienda *TAKUKURU*

huelewi chochote ukienda kwa Mkuu wa Wilaya anakuambia *findings* ziko TAKUKURU.

Mheshimiwa Spika, lakini hilohilo jambo la *COASCO* nalipeleka moja kwa moja mpaka kwa Mrajisi wa Vyama vya Ushirika. Kwa sababu moja ya swali ambalo nilimuuliza Mrajisi wa Vyama vya Ushirika wa Mkoa wa Lindi, nilimuuliza wewe kama mlezi wa *AMCOS* kuna *AMCOS* zina matatizo moja mbili tatu umezifanyia nini? Ananiambia suala lao liko *COASCO*. Nikamwambia mrajisi kuna matrekta yameuzwa, wanachama wanalalamika matrekta yameuzwaje? Anasema matrekta haya yameuzwa lakini fedha zilingia kwenye *account* ya *AMCOS;* lakini fedha zile zimetoka kwenye *account* ya *AMCOS* zimefanya nini yeye haimuhusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ina maana kwamba Mrajisi wa Vyama vya Ushirika uwezo wake ni kujua tu kwamba matrekta yameuzwa fedha zimeingia kwenye *AMCOS, AMCOS* wamefanya nini yeye hajui. Nako kuna shida, nako huko kwenye vyama vya ushirika nako kuna shida. Mimi kwa ufahamu wangu Mrajisi wa Vyama vya Ushirika yeye ndiye msimamizi wa vyama vya ushirika, kama kuna chama cha ushirika kina mgongano labda kati ya viongozi na wanchama yeye anaingia kati.

Mheshimiwa Spika, unajua nini kilichofanyika; wakati hawa *COASCO* wameleta ripoti walikuja na Mrajisi wa Mkoa akaitisha mkutano wa wanachama, alikwenda pale akasoma tu zile *findings* za *COASCO* akasoma akaondoka akasema mkutano huo sitaki maswali. Hao ndio viongozi wetu.

Mheshimiwa Spika, na mimi nikashangaa sana mimi nikajua hiyo *COASCO* sikujua kwamba iko chini yake Mheshimiwa Waziri. Kwa sababu yeye kwa sifa aliyo nayo

kwa utendaji na weledi wake kuwa na hili dude liko pale limuharibia… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka, kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo kwa sababu kiu yangu ilikuwa ni *COASCO*, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt Mwigulu Lameck Nchemba, Mheshimiwa Angeline Mabula, ajiandae.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa maoni yangu na mchango wangu kwenye bajeti hii ya Wizara ya Kilimo. Niungane na Wabunge wenzangu wote waliotangulia kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada kubwa anazozifanya na kuuona umuhimu sana wa Wizara hii ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi humu ambao tunatokea maeneo ya majimbo ambayo yana wananchi wengi wakulima tusipozungumzia sekta hii ya kilimo tutakuwa tumewasaliti wakulima.

Mheshimiwa Spika, niungane na Wabunge wengine waliompongeza sana Mheshimiwa Bashe na Naibu wake Mheshimiwa Anthony Mavunde, Kaka yangu na wasaidizi wao wote kule Wizara. Kwa kweli wanajitahidi wanafanya kazi vizuri na wana maono nazuri. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikisoma malengo ya Wizara, Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake ameandika ni kuongeza tija na uzalishaji katika Sekta ya Kilimo. Ili kuongeza tija, maana yake nini? Maana yake tunaangalia mkulima sasa kwa ekari, akipanda ekari moja atapata mavuno kiasi gani. Hili jambo ni muhimu sana tukaliangalie ili kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata matokeo ya kile ambacho wanakifanya.

Mheshimiwa Spika, tutafikiaje hapo sasa? Ili tuweze kufikia kwenye tija ni muhimu sana kuboresha huduma za ugani kule kwenye vijiji. Sasa hapa maana yake tunaenda pamoja na kuangalia idadi ya watumishi walioko pale. Kule Ludewa nashukuru sana Wizara hii tumeongezewa watumishi, tulikuwa na watumishi 41, tumeongezewa Maafisa Umwagiliaji watatu na maafisa wengine watatu. Kati ya hao *graduates* ni tisa. Kwa hiyo niishukuru sana Serikali kwa kutuongezea watumishi kwenye Sekta ya Kilimo watumishi sita na kwenye Sekta ya Mifugo watumishi 10.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sasa hivi maana yake tija tunayoitaka anayozungumza Mheshimiwa Waziri itakuwa ni rahisi kuweza kuipata. Maana yake wale watumishi sasa wataenda kuwaelimisha wakulima. Sasa ili wapate tija lazima tunaangalia hata muda ambao wanapanda, je wakulima hawa wanapanda kwa wakati? Kwa hiyo tunatarajia watumishi hawa ambao wameletwa waweze kwenda kuhakikisha kwamba wakulima wetu wanapanda kwa wakati, lakini vile vile wanatumia mbegu bora.

Mheshimiwa Spika, sasa hapa kwenye eneo la mbegu, ningependa sana kuishauri Serikali, mbegu bado kwa mkulima wa kijijini, bado ni ghali sana. Kwa hiyo Serikali ingefaa iweze kuwekeza fedha kwa kushirikiana na vyuo vikuu vya kilimo na taasisi mbalimbali za utafiti, ili waweze kuandaa mbegu ambazo mkulima atazipata kwa gharama nafuu kuliko hali ilivyo hivi sasa. Kwa sababu wakati tunakua

tuliona wazazi wetu, mbegu kama alipanda mwaka jana, mwaka huu anachagua anarudia tena. Hii ilikuwa inawapunguzia gharama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi zile mbegu za asili tumezipoteza. Kuna Mbunge mmoja alisisitiza hapa kwamba kuna umuhimu wa kuja kuhangaika pia kuhakikisha kwamba hizi mbegu tunaweza tukaziandaa na kuzihifadhi. Kwa hiyo, eneo la mbegu bado ni ghali, kwa hiyo Serikali iwekeze, ishirikiane na vyuo vikuu vya kilimo na taasisi za utafiti kuhakikisha kwamba mbegu inashuka bei na ikiwezekana tuweke ruzuku pia kwenye mbegu na yale madawa ya kuua wadudu na yenyewe tuweke ruzuku ili yapatikane kwa bei nafuu sana.

Mheshimiwa Spika, niishukuru sana Serikali kwa kuweka ruzuku kwenye mbolea. Kule Ludewa tulipata shida kidogo kutokana na changamoto ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezieleza, lakini nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake. Kuna mtaalam mmoja anaitwa Mablanketi, nafikiri aliniunganisha Naibu Waziri mpaka tuligombana, lakini baadaye alifanya kazi nzuri tukaweza kupata lori zaidi ya 15 zenye mifugo 600 kila moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kutokana na ruzuku ile ya mbolea leo lazima niwe muungwana niweze kuishukuru sana Serikali. Nami niombe tu zile changamoto za kukosekana kwa maghala, mawakala kule wilaya za pembezoni yaweze kutatuliwa mapema.

Mheshimiwa Spika, vile vile nipongeze sana Serikali kwa kuifufua ile *TFC* na kuipa fedha iweze kuagiza mbolea. Nimesoma kwamba awamu ijayo mbolea itakuja mapema na hii kwa kweli sisi kule Mkoa wa Njombe alizungumza ndugu yangu Mwanyika. Tunalima mara kwa mara viazi vinalimwa misimu miwili au mitatu, lakini kuna kilimo cha bustani

vitunguu, nyanya, mboga mboga. Kwa hiyo muda wowote mbolea zinahitajika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nitaomba hawa watu wa *TFC* waweze kuleta mbolea mapema iweze kupatikana muda wote. Vile vile kuna wazee ambao hawana uwezo wa kumudu kununua mbolea ya mfuko 70,000. Wao wakipata hela kidogo wanakwenda ananunua kwenye kilo. Naomba pia hilo liweze kuzingatiwa kwa sababu hali za wananchi wetu hazifanani, tusiwalazimishe wote kununua mbolea kilo 50 na kuendelea.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ni muhimu sana, Ludewa tumepata mahindi mengi, tumelima hekta 51,000, tunaomba masoko yaweze kuandaliwa kwa sababu tutakuwa na mavuno mengi. Tani laki tano hazitoshi, naomba Serikali ionge fedha.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

## MCHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, kutokana na suala la muda nalazimika pia kuchangia kwa maandishi na mchango wangu utajikita kwenye zao la korosho pekee kutokana na anguko lililotokea msimu uliopita.

Mheshimiwa Spika, ili kuhami zao la korosho linaloyumba kila mwaka nashauri yafuatayo; kwanza Serikali ikubali kupunguza makato kwa mnunuzi na mkulima (kwa rejea ya msimu uliopita ni wastani wa shilingi 1,130 kwa kilo) ili kuhami bei ya soko.

Pili, Serikali ifute ushuru wa shilingi 110 inayoitwa ya maendeleo ya korosho huku ukweli ukiwa ni fedha za kulipia pembejeo kwani tayari Serikali ile ile iliwatangazia Watanzania kupitia Bunge na sheria ikapitishwa ya kurejesha fedha za *export levy* asilimia 50 kwa wakulima.

Tatu, Serikali ifute ushuru wa shilingi 81 ya magunia na ieleze ziliko fedha za magunia za misimu ya mwaka 2019/2020, 2020/2021, 2021/2022 ambazo wasambazaji wa magunia ya mwaka 2017 hawajalipwa hadi leo na deni linazidi kuwa kubwa.

Mheshimiwa Spika, nne, Serikali ifute ongezeko la ushuru wa shilingi 20 kwa watunza maghala na kufanya kuwa shilingi 52 hadi itueleze wakulima sababu za msingi za ongezeko hili kubwa la ushuru.

Mheshimiwa Spika, tano, Serikali ipeleke haraka muswada wa sheria kupunguza makato ya *export levy* kutoka asilimia 15 ya *FOB* hadi asilimia tisa *(single digit)* kuhami bei ya soko na Bodi ya Korosho iharakishe mchakato wa kuandaa mapendekezo kwenye kikao kijacho cha wadau kutazama kama bado haya makato yana tija kwa wakulima na ikibainika hayana tija, yafutwe.

Mheshimiwa Spika, sita, Serikali ianzishe mfumo maalum wa ruzuku ya kufidia soko la korosho *(subsidies)* ili ikitokea soko limeyumba, Serikali iwe na uhakika wa kumuokoa mkulima. Tunaweza kutenga sehemu ya mapato ya *export levy* kwa ajili hii.

Mheshimiwa Spika, saba ni muda muafaka wa kuanza kutazama upya muundo wa vikao vya wadau wa zao la korosho ambao ndio hupitisha makato kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kupata wawakilishi kwenye kikao cha wadau upoje na wawakilishi wa wakulima ni asilimia ngapi ya wajumbe wote?

Mheshimiwa Spika, kuhusu pembejeo na kushuka kwa uzalishaji wa korosho; zao la korosho linashuka uzalishaji mwaka hadi mwaka toka tani laki tatu mwaka 2017/2018 hadi tani laki mbili mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kushuka huku kwa uzalishaji ambako pia kwa mwaka huu makusanyo halisi ni tani laki 1.7; moja ya sababu ya kushuka huku kunatokana pamoja na mambo mengine kama utaratibu usiofaa wa pembejeo, pembejeo zisizozingatia hali ya hewa ya eneo, usambazaji wa pembejeo *fake*.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwanza utaratibu wa awali wa mkulima kuchangia pembejeo anayoitaka, kwa kiasi anachokitaka urejeshwe huku Serikali ikifidia bei ya ziada kupitia *export levy*. Hii itasaidia sana mkulima kupata pembejeo aitakayo kutokana na hali ya hewa.

Mheshimiwa Spika, pili, Kamati ya Pamoja ya Ununuzi wa Pembejeo chini ya *MAMCU* ivunjwe, tuendelee na utaratibu wa zamani kwani kamati hii imetumia fursa hii kujineemesha huku ikiingia mikataba na wazabuni wasio na uwezo, wenye pembejeo *fake* na pembejeo ambazo hazijawahi kutumika kwenye korosho na zinazoshusha uzalishaji. Kasi ya pembejeo mpya kujaa sokoni ni kiashiria kimojawapo

Tatu, *export levy* isitumike kuchangia pembejeo na tuifute shilingi 110 ya maendeeo ya korosho kama tulivyoshauri hapo juu.

Mheshimiwa Spika, nne, Serikali itoke hadharani iseme hatua alizochukuliwa msambazaji wa pembejeo *fake*

zilizokamatwa Masasi, Nachingwea, Tandahimba na Newala ambaye alijinasibu kushirikiana na vigogo wa Serikali huku akikimbizwa China kupisha joto la mijadala na aliporejea hakuna hatua alizochukuliwa.

Mheshimiwa Spika, tano, Serikali ieleze ziliko pembejeo *fake* ambazo kila mwaka zimekuwa zikikamatwa kila msimu wa korosho unapofika.

Mheshimiwa Spika, mwisho ila sio kwa umuhimu, ni vyema Serikali itoe athari za makisio ya pembejeo *vs* uzalishaji iliyotolewa na Mkurugenzi wa Bodi ya Korosho ya tani laki nne na tukaagiza pembejeo kulingana na makisio hayo. Hii bakaa ya tani laki 230 ambayo Serikali inalipa bila mshirika (mnunuzi) tunatoa wapi.

Mheshimiwa Spika, kwa msimu wa mwaka huu wa 2022/2023 *indirect charges* kwenye kila kilo moja ya korosho ambazo zimeathiri bei ya soko zipo kama ifuatavyo; hizi analipa mnunuzi *(*mkulima *in fact);* makato ya maendeleo ya zao la korosho (pembejeo) shilingi 110; ushuru wa watunza maghala shilingi 52; deni la magunia shilingi 81; usafirishaji shilingi 120; *export levy* ambayo ni sawa na asilimia 15 ya *FOB* shilingi 380; *ICD* shilingi 120; Ushuru wa Bandari shilingi 100; vibali shilingi 10; *offload* shilingi 10; *provisional income tax* shilingi 70; *forwarding charges* shilingi 10; na *other charges* shilingi 50.

Mheshimiwa Spika, kwa vyovyote vile gharama hizi mwisho wake zinarudi kwa wakulima, hivyo nashauri tufanye marejeo ili kuwaongezea *morale* wakulima na wanunuzi pamoja na kupata mbegu bora. Ahsante kwa nafasi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha ushauri na maoni yangu kuhusu mbolea ya ruzuku kwa Mafinga na Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kwamba kwa kuwa sisi tunalima mwaka mzima, basi mbolea ipatikane

mwaka mzima na kwa ujazo tofauti. Ukienda mpaka wa Namanga utaona bidhaa zinazovuka, kati ya bidhaa kubwa inayovuka ni pamoja na viazi ambavyo asilimia kubwa vinalimwa mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya na Songwe.

Mheshimiwa Spika, tunazungumza kuhusu kuongeza ajira, eneo hili linatoa ajira kuanzia wakulima, wauzaji wa pembejeo lakini pia sekta ya usafirishaji kuanzia kufikisha pembejeo shambani na kusafirisha viazi. Yawezekana ni gharama kubwa na yawezekana mwelekeo ni kutoa ruzuku kwa ajili ya mazao ya chakula, kama hivyo ndivyo, basi walau hata kama haitakuwa 50%, basi iwe ruzuku hata ya 25%, kwa mfano mbolea ya shilingi 150,000 basi ipatikane japo kwa shilingi 100,000.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujazo, wapo wakulima wanalima kilimo cha kumwagilia na cha mabondeni kwa maana ya vinyungu, hawa wanahitaji mbolea kwa matumizi ya awamu tofauti, kuna wakati anahitaji mbolea ya ujazo wa kilo tano, kilo kumi, kilo 20 na kadhalika. Hii itawapunguzia usumbufu ambapo kwa sasa wakulima wetu wanalazimika kuchanga fedha na kununua mfuko mmoja na baadae kuanza kugawana kwa kupima kwenye visadolini.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Wizara kwa wasilisho la bajeti na ninaomba kuchangia kama ifuatavyo; kwanza tuokoe zao la mkonge na viwanda vyake.

Mheshimiwa Spika, katika kitabu cha hotuba ya Waziri ukurasa wa 11-14 imetaja mchango wa kilimo katika pato la Taifa kuwa ni 26.1% na kwamba kilimo kinachangia 65% ya malighafi za viwanda. Zao la mkonge ni moja ya zao ambalo linaweza kuchangia asilimia za mchango wa kilimo katika pato la Taifa. Mawazo ya aina hii nimeyawasilisha pia katika bajeti ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Spika, katika ilani yetu ya Uchaguzi ya CCM ya 2020-2025 imetaja kuzalisha ajira milioni nane, ni wazi kuwa ajira hizi kwa kiasi kikubwa zitatokana na mnyororo wa thamani kuanzia katika malighafi za kutoka mashambani/kilimo hadi viwandani *(agro-processing industry)*. Ajira hizi pamoja na viwandani itaendelea hadi sokoni. Ni masikitiko makubwa sana kwamba wakati tumeamua kufanya zao la mkonge kuwa zao la kimkakati, hakuna jitihada za makusudi za kulinda viwanda vya kuchakata zao la mkonge kwa maana ya kulinda soko. Ndani ya Serikali hakuna ufuatiliaji wa maagizo na maelekezo ya Waziri Mkuu ya Septemba, 2021 na rejea yake Novemba, 2021 kwamba Wizara inayohusika na mazingira kwa maana ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira izuie *importation* ya kamba za *plastic* ambazo kwa kiasi kikubwa mbali ya kuvuruga soko la kamba za kitani, lakini pia zinaathiri mazingira.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo ni matarajio yangu kwamba ikiwa Wizara ya Kilimo mnayo dhamana ya kukuza kilimo na kuongeza mchango wa malighafi za viwandani, basi pia mnao wajibu wa kuwa kiongozi wa kulinda viwanda ambavyo vinatumia malighafi za kilimo. Hivyo kama Wizara ya Kilimo mnayo nafasi kubwa ya kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhakikisha kuwa zuio hilo linasimamiwa ili kuwalinda wakulima na kulinda viwanda na ajira za Watanzania kama sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Pili ni kuhusu vijana waliohudhuria mafunzo ya kilimo nchini Israel, je, wamesahaulika, tumewatelekeza au hawana tija? Kwa miaka kadhaa kama Taifa tumekuwa tukiwapeleka baadhi ya vijana waliomaliza *SUA* kwenda kuhudhuria mafunzo ya miezi takribani kumi na moja, hata hivyo wakirudi hatuwatumii, hatujui wako wapi? Kwa nini vijana hawa tusingeanza nao kwenye *BBT* hata kuwafanya ndio viongozi wa wengine? Katika hotuba ya Waziri ukurasa wa 75

amezungumzia mpango wa mashamba makubwa ya pamoja, nashauri kwa kuwa tayari tuna vijana waliopata maarifa ya hali ya juu ya kilimo huko Israel tuone kwa namna gani tutawatumia, sio sahihi na ni kupoteza rasilimali watu na fedha kuwaaacha hawa vijana wanaelea tu.

Mheshimiwa Spika, swali dogo, je, Wizara inawatambua, wako wangapi, wako wapi na wanafanya nini? Ndio maana baadhi ya watu wanaona *BBT* ni siasa, haya siwezi kuyasema Bungeni *live* bali nawaletea kwa maandishi, je, kama *BBT* sio siasa? Kwa nini hatuwatumii hawa vijana, wako *idle* wakati *skills* wanazo, kwa nini tutafute wapya ambao pengine kujiunga kwao na *BBT* ni kwa sababu wako *desperate*, hawana kazi, kwa sababu wamekosa ajira, hawana mbadala ndio maana wakakimbilia *BBT*.

Mheshimiwa Spika, je, *BBT* ni siasa au *business as usual* kama tulivyoshuhudia ya Kilimo Kwanza na kadhalika? Kama sio siasa basi ni matarajio yangu kwamba tuta-*make maximum use of the available resources* wakiwemo hawa vijana waliopata mafunzo Israel. Na ninatamani sana Waziri katika majumuisho aseme jambo kuhusu hawa vijana. Labda hii programu haikuwa na baraka za Wizara, labda kwa utaalam wenu mnaona haiwahusu, lakini iwe ni kilimo au yeyote aliyeratibu programu hii, bado mwisho wa siku ni Serikali katika ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ushauri wangu kwa Wizara, Waziri atuambie hatma ya hawa vijana, vinginevyo kwangu mimi nitaona hata *BBT it is business as usual, it is politics.* Na kuthibitisha kwamba kama Serikali tunawatambua hawa vijana soma hii meseji; "Kwanza Waziri wa Kilimo Josephat Hasunga wa Songwe aliwahi kuja Israel na akaahidi mambo mengi tu endapo tutarudi Tanzania, pili, Naibu Waziri Anthony Mavunde mwaka jana alihudhuria mahafali. Tatu kuna siku alikuwa Dodoma Mavunde alisema *BBT* itakuchua wanafunzi waliotoka Israel sijui wamemsaliti akina nani huko juu! Nne

Naibu Waziri Katambi aliwakaribisha Bungeni kama wageni wake siku fulani Bunge lililopita."

Mheshimiwa Spika, kuhitimisha suala hili, ni wazi Wizara na Serikali kwa ujumla inawatambua vijana hao, basi tuone namna ya kufanya, kuwatumia ili wawe na mchango katika kilimo chetu.

Mheshimiwa Spika, mafuta ya kula na kuondolewa kwa ushuru kutoka 35% hadi 0% je imesaidia kukua kwa kilimo cha mbegu za uzalishaji mafuta ya kula au tumenufaisha ma-*tycoon* wa biashara ya mafuta ya kula?

Mheshimiwa Spika, suala hili pamoja na kuwa ni la Viwanda na Biashara pamoja na Hazina, lakini ukweli unabaki pale pale kwamba wenzetu wa Kilimo wanao wajibu wa kwanza kuhakikisha Taifa linajitosheleza kwa mafuta ya kula na hata kuuza nje. Lakini kwa mshangao na masikitiko makubwa mwaka wa fedha tunaoumaliza huu wa 2022/2023, Serikali iliondoa ushuru wa *the so called* mafuta ghafi kutoka 35% hadi 0% kwa mwaka mmoja kwa waagizaji kutoka nje. Maamuzi haya baadhi yetu tuliyapinga na kushauri kwamba hata kama ni ahueni basi walau iende kwa hatua na kwa awamu, kwa kupunguza hata hadi 15%.

Mheshimiwa Spika, ilitolewa hoja kwamba ingesaidia kupunguza bei ya mafuta ya kula, tukiwa *honest* wala haikuwa na mashiko, sana sana tumewanufaisha wafanyabiashara wakubwa, kwa sababu kwanza hawaingizi *crude* kama walivyodai, wanaingiza *refined* na kufanya *packaging,* matokeo yake tumewaumiza wakulima wetu wa alizeti, je, sisi kama Wizara ya Kilimo tumekuza kilimo au tumekirudisha nyuma?

Mheshimiwa Spika, ni wazi kuwa azma ya Taifa hili kujitosheleza kwa mafuta ya kula ina safari ndefu sana kwa sababu wafanya maamuzi wanaangalia maslahi binafsi na

sio maslahi ya walio wengi ambao ni wakulima wetu. Leo hii *morale* ya kulima alizeti imeshuka mno kutokana na bei ya alizeti kuwa ndogo. Kuna kichaka watu wanajificha ooh tumeondoa ili kupunguza makali ya bei, makali ya bei yamekuja kupungua baada ya wananchi kuanza kuvuna alizeti zao, kwa hiyo kuondoa ushuru kutoka 35% hadi 0% hakujawa na faida sio kwa mlaji wa mwisho wala mkulima wa alizeti. Kama Wizara mnapaswa kuwa na wivu na kutetea kilimo na hasa kwa mazao ambayo yatalisaidia Taifa kuondokana na kuagiza baadhi ya bidhaa kutoka nje kama ilivyo kwa mafuta ya kula. Yafaa sote kwa pamoja tuwe na dhamira moja na tuone aibu kuendelea kuagiza mafuta ya kula nje ya nchi, na ndio maana mwaka jana nilishauri, washirikisheni JKT, mtaona matokeo *in just two years.*

Mheshimiwa Spika, napongeza jitihada za Mheshimiwa Waziri Mkuu zinazoendelea kule Kigoma za kilimo cha michikichi. Ninaamini tukiwawezesha JKT tutavuka, lazima tufike wakati tuwe na uthubutu, tuwe wakweli wa nafsi, sio sawa kama Taifa kuendelea kutumia zaidi ya USD milioni 300 kuagiza mafuta ya kule, tuone aibu kama Taifa. Tukiwekeza katika JKT sio tu kwamba tutaokoa fedha za kigeni, lakini pia tutauza mafuta katika nchi jirani za DRC, Malawi, Zambia na hata Burundi na Rwanda. Nchi hizi zinategemea mafuta ya kula kutoka Malaysia, tukizalisha tunalo soko la ndani lakini pia soko hata ndani ya *EAC* na baadhi ya nchi za *SADC*.

Mheshimiwa Spika, kule Chita, nashauri Serikali ikajifunze kilimo cha mpunga chini ya JKT, ni aibu sisi kutoa vibali eti kuagiza mchele tani 90,000; haya ni mambo tunapaswa kuyakataa kwa vitendo, hata programu ya *BBT* awamu ya pili, kama tuna dhamira njema na ya dhati, nashauri mngehusisha vijana waliopata mafunzo JKT na usimamizi ungefanywa kwa ushirikiano wa ofisi hizi tatu, Kilimo, Kazi na Ajira na JKT.

Mheshimiwa Spika, usalama wa mbegu na mbegu bora; katika ukurasa wa 119 wa hotuba ya Waziri ameeleza kuhusu suala la utafiti wa mbegu bora, ninashauri tuwe na mpango maalum wa kuhakikisha Taifa linajitosheleza kwa mbegu bora na salama. Mfumo uliopo kwa hakika sio salama katika suala la usalama wa chakula na usalama wa Taifa. Nashauri pia tuhusishe vyombo vyetu hasa JKT katika kufanya tafiti za mbegu bora, mimi naamini kwamba *innovation* mara nyingine inatokea kwenye vyombo vya ulinzi na usalama hasa majeshi, simaanishi kwamba tuwaachie wao, hapana, tuwashirikishe, tushirikiane na ndio maana nawasihi ndugu zangu wa Kilimo mkatembelee Chita, kipo kitu mtajifunza.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri wa Kilimo, Naibu Waziri, Katibu Mkuu kwa hotuba nzuri ya bajeti iliyobeba maudhui ya mabadiliko makubwa katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwezesha bajeti ya kilimo kupanda kwa asilimia 29 na kuruhusu mradi mzuri, mkubwa wa kuwawezesha vijana na wanawake kunufaika na kilimo wa *BBT*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mpango wa *BBT* awamu hii ya kwanza, vijana zaidi ya 800 wako vyuoni wanapatiwa mafunzo. Faida za mpango huu wa *BBT* ambapo wanawake na vijana wanufaika wa mpango huu watapata ni kama ifuatavyo; ardhi iliyopimwa, hivyo watawezeshwa kumiliki ardhi; mafunzo juu kilimo cha biashara; mikopo ya kutunisha mitaji yao. Kutakuwa na dirisha la utoaji mikopo; itaondoa unyanyapaa wa vijana kwa kilimo na vijana watalima, watapata ajira na kutajirika.

Mheshimiwa Spika, ili mradi huu uwe endelevu, napendekeza watakaohusika katika kuwagawia hao vijana na wanawake maeneo, wazingatie kutenga eneo kwa wanawake na vijana wazawa wa maeneo hayo ili kuondoa malalamiko yanayoweza kutoka kwa wenyeji wa hayo maeneo.

Pia napendekeza TAMISEMI iagize Halmashauri zote nchini zibaini na kutenga maeneo ili tuwe na benki ya ardhi ya kutosha, kusudi ifikie wakati mradi huu utakapoweza kuendeshwa katika Halmashauri zote nchini na hivyo wanufaika kuwa wengi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo cha vanila kinawanufaisha watu wengi duniani huko inapolimwa, mkoani Kagera kilimo cha vanila kina zaidi ya miaka 20. Lakini hadi leo hakuna soko la uhakika. Mnunuzi ambaye tena ndiye mwanzilishi wa zao la vanila Kagera, Shirika la Mayawa wana changamoto kubwa. Vanila za wakulima walizonunua tangu mwaka 2021, baadhi ya wakulima hawajalipwa hadi Leo. Mayawa walipata mkopo wa *TADB* wakalipa baadhi ya wakulima na wengine hawakulipwa. Hivi sasa Meneja wa Mayawa bodi imemsimamisha kazi. Wakulima wanalalamika, wanaumia hawajalipwa sasa mwaka wa pili.

Mheshimiwa Spika, Mayawa wanasema wao vanila walizonunua tangu mwaka 2021 wamekosa mnununuzi na hivyo hawajauza. Hivyo katika msimu wa mwaka 2022 hawakununua vanila na hata katika mwaka wa 2023 hawatanunua vanila.

Mheshimiwa Spika, ili kuwaokoa wakulima naomba Serikali imsaidie Mayawa kutatua changamoto hii, watafutiwe mnunuzi wa vanila kavu. Katika msimu wa mwaka jana alikuwepo mnunuzi mkubwa mmoja anayeitwa *NEI*. Kwa sababu alikuwa peke yake aliwawekea wakulima masharti magumu ikiwemo wakulima kulazmishwa kuvuna vanila zote

kwa mara moja, hata zile ambazo hazijakomaa. Mnunuzi aliwapa muda mfupi wa yeye kununua. Sasa tunaingia katika msimu wa kuvuna mwaka huu, tunaomba Serikali ihamasishe na kuwezesha upatikanaji wa mnunuzi mwingine mkubwa wa vanila.

Mheshimiwa Spika, zao hili kwa sasa linalimwa katika mikoa mingi lakini hakuna miongozo, hakuna huduma za ugani na bei ya miche bado iko juu sana. Je, ni lini Serikali italipatia zao la vanila umuhimu unaostahili na kuweza kuwasaidia wakulima kwa kutoa huduma za ugani na kwa kupitia idara ya masoko Wizarani na *TANTRED* kuwatafutia soko wakulima hawa?

Mheshimiwa Spika, kuhusu mbolea ya ruzuku; tunaishukuru Serikali kwa kusambaza mbolea katika msimu uliopita. Mkoa wa Kagera ni kati ya mikoa ambayo matumizi ya mbolea bado yako chini sana. Mbolea iliyopelekwa mkoani Kagera kiasi kikubwa ilienda *Kagera Sugar* kwenye kilimo cha miwa. Mawakala wa usambazaji mbolea ni wachache mkoani kwani wanaogopa wasije wakaleta mbolea, ikakosa mnunuzi.

Naiomba Serikali kwenye maeneo na mikoa mingine kama Kagera ambapo wananchi matumizi yao ya mbolea yako chini, uhamasishaji juu ya matumizi sahihi ya mbolea na Serikali iwasambazie mbolea hadi kwenye vituo mbalimbali mkoani ili wakulima waipate mbolea kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, tunaipongeza Serikali kwa kuwapatia pikipiki Maafisa Ugani wote 342 walio katika mkoa wa Kagera. Hii itawawezesha kufanya kazi zao vizuri. Mkoani Kagera kuna upungufu mkubwa wa Maafisa Ugani, wapo 342 kati ya 732 wanaotakiwa. Tunaomba kupatiwa Maafisa Ugani wa kutosha waweze kusimamia na kutoa huduma za ugani kwa wakulima wa mazao mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Iringa ni mkoa wa kilimo hususani hata Manispaa ya Iringa. Sasa sisi hatuna eneo la kufanya *block farming* na Iringa Manispaa ndiyo lango la utalii Kusini na tunajengewa uwanja wa ndege ambao utaruhusu hata ndege ya mizigo kutua na kuchukua kama mboga mboga.

Mheshimiwa Waziri wewe unajua utalii ni pamoja na huduma nzuri ya chakula. Hivyo basi, rejea mazungumzo yetu, tunaomba sana sana tupewe eneo la Serikali lililokuwa la Kilimo au Utafiti Gingilanyi, katika Kata ya Nduli ili tutumie kama *block farming* kwa vijana wa manispaa ya Iringa, pia tunaweza tukatumia eneo lililokuwa Kituo cha Utafiti cha Kilimo kilichopo Ipogolo Kata ya Ruaha.

Mheshimiwa Spika, pia tunaeneo la umwagiliaji la Mkoga Kata ya Isakalilo. Tunaomba litengewe bajeti kwa ajili ya kuboresha ili kuwa na kilimo cha umwagiliaji na chenye tija.

Mheshimiwa Spika, tunaomba changamoto ya upatikanaji wa mbolea karibu na wakulima itatuliwe, kwanza, kwa kuweka mfumo madhubuti ambao utafanya kazi kwa wakati wote bila kukatikakatika, kuwa na wasambazaji wa kutosha mpaka vijijini hivyo kuimarisha utendaji kazi wa mawakala wadogo kwa kuondoa urasimu usio kuwa wa msingi kwa mawakala wadogo. Pia kuufanya mfumo usiruhusu *QR code* kuwa *scanned* zaidi ya mara mbili, iwe kama ilivyo kwenye *voucher* za simu au namba za LUKU ukiingiza mara moja haiwezi kuruhusu tena kuingiza au ku-*scan.* Pia zisitolewe zinazofanana kwa makampuni mawili

Mheshimiwa Spika, mbolea hii ya ruzuku ikiwezekana iwe na *limit* ya mifuko itakayotolewa. Labda Serikali iseme itatoa ruzuku kwa mifuko kadhaa tu. Wale wenye mahitaji

makubwa maana yake wana uwezo mkubwa hivyo waweze kununua kwa bei ya kawaida isiyokuwa na ruzuku. Wakulima wakubwa wengine huchukua mbolea ya kutosha wakulima wa Wilaya nzima hawa wanaweza. Mbolea ya ruzuku itolewe kwa mwaka mzima. Pia usajili wa wakulima kama wapo ambao bado hawajamaliza basi waendelee kutumia mpaka wamalize na usajili wa wakulima uwe ni endelevu.

Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mawaziri na viongozi wote wa Wizara ya Kilimo, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Kilimo kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Serikali katika utekelezaji wa ustawi wa jamii na maendeleo endelevu, na hii ni mojawapo ya nguzo kuu katika utayari wetu wa ushindani wa kimataifa *(national competitiveness)*. Bajeti hii inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Spika, kulingana na taarifa ya Wizara ya Kilimo, Tanzania ina hekta milioni 44 zinazofaa kwa kilimo cha

mazao, kwa wastani hekta milioni 10.8 tu sawa na asilimia 24 ndizo zinazolimwa kila mwaka. Sekta hii kwa mwaka 2021/2022 imechangia asilimia 26.1 kwenye Pato la Taifa, imetoa ajira kwa wananchi kwa wastani wa asilimia 65 na imechangia asilimia 65 ya upatikanaji wa malighafi za viwanda. Sekta ya kilimo ni mhimili wa uchumi wa nchi na inachangia pato la mkulima mmoja mmoja, kaya na Taifa kwa ujumla. Sekta ya kilimo na hususani sekta ndogo ya mazao imechangia asilimia 15.4 katika Pato la Taifa na zaidi ya asilimia 100 ya upatikanaji wa chakula kinachozalishwa nchini na kupelekea utulivu wa mfumuko wa bei kwa takriban asilimia 59.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kujitosheleza kwa chakula na kuchangia katika uchumi wa Taifa, takribani mazao yote yanazalishwa kwa tija ndogo katika eneo husika. Uzalishaji wa mahindi wa chini ya tani mbili kwa hekta moja ni asilimia 29 tu ya uzalishaji unaotegemewa wa tani sita kwa hekta moja. Uzalishaji huu wa chini kwa mazao yote kwa kiasi kikubwa unatokana na ukosefu wa ushauri wa watalaam wa kilimo ikiwemo matumizi yasiyo sahihi ya mbolea na pembejeo zingine. Katika hali hii, kilimo hakijamsaidia mkulima kwa kiasi kikubwa kunajinasua kwenye umaskini na kimeendelea kutoa mchango mdogo kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa mbolea nchini hadi Februari, 2023 ulikuwa tani 748,890 ambayo ilikuwa juu ya mahitaji ya tani 667,730. Pamoja na bei za mbolea kwenye soko la dunia kuwa juu, tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutoa ruzuku ya karibu asilimia 50 na kupelekea tani 300,179 kununuliwa kwa bei ya ruzuku. Hatua hii muhimu ni mafanikio makubwa katika safari ya kuleta tija kwenye kilimo nchini na napendekeza kuendelea na ruzuku ya pembejeo pamoja na kuanzisha *Price Stabilization Fund* kwa pembejeo hasa mbolea ili kuongeza tija kwenye uzalishaji wa mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iendelee kuimarisha usalama wa chakula nchini kwa kununua na kuhifadhi nafaka kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula. Kutokana na vita ya Urusi na Ukraine kunaashiria kuendelea kuwa na upungufu mkubwa wa nafaka na kwa kuzingatia gharama kubwa za uzalishaji wa karibu asilimia 100, Serikali ichukue hatua za makusudi kusaidia wakulima wapate bei nzuri ya *NFRA* badala ya kuuza kwa walanguzi na kutorosha chakula nje ya nchi. Kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu, kufikia mwaka 2030 biashara ya mazao ya chakula inakadiriwa kufikia dola za Kimarekani trilioni moja. Serikali ichukue hatua za makusudi kuboresha uzalishaji wa mazao ya chakula kutosheleza soko la ndani na nje. Uzalishaji wenye tija kwenye kilimo utaongeza upatikanaji wa fedha za kigeni na kupunguza pengo la urari wa biashara.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie fursa za Kiwanda cha Viuadudu cha Kibaha kuanza uzalishaji wa viuatilifu inayotokana na pareto ambayo inazalishwa hapa nchini na imekuwa inauzwa nchi za nje kama *semi-finished product* kwa bei ndogo ya kutupa. Viuatilifu kutokana na pareto ni suluhisho la soko la pareto na pia suluhisho kwa upotevu wa mazao kushambuliwa na wadudu *(post-harvest losses)*.

Mheshimiwa Spika, Serikali ianze mchakato wa kuanzishwa viwanda vya mbolea kwa kutumia madini *(calcium carbonate, agricultural lime, phosphates, natural gas etc.)* yanayopatikana kwa wingi hapa Tanzania, kuanza uzalishaji wa mbolea hapa nchini. Kutokana na athari za vita ya Urusi na Ukraine zinazoendelea, iwe fursa kwetu kwa kuanza kutumia rasilimali zinazopatikani nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha bajeti ya 2022/2023 Serikali ilitenga shilingi 834,382,834,000 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambayo sehemu kubwa ilielekezwa kwenye miundombinu ya umwagiliaji. Utekelezaji wa miradi hadi kufikia Februari, 2023 hasa utekelezaji kwa

fedha za nje uko chini sana. Sehemu kubwa ya miradi inategemea kuchukua miezi 24 na kuna matumaini ya utekelezaji kwenda kama ulivyotarajiwa. Matumaini pekee ni hatua zilizooneshwa kwenye bajeti ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji na Serikali iweke mikakati madhubuti kuhakikisha ufanisi wa utekelezaji wa bajeti hii ya umwagiliaji. Serikali iangalie utelezaji wa miradi ya mabwawa kuunganisha uratibu kwa mahitaji ya jumla kama vile mahitaji ya Wizara ya Mifugo na hata Wizara ya Maji, kunaweza kuwa na tija kuwa na chombo kimoja chenye nguvu zaidi.

Mheshimiwa Spika, pia mikakati hii iweke nyongeza za ujenzi wa mabwawa hasa maeneo yenye mafuriko makubwa ikiwa ni pamoja na kuzuia mafuriko. Pia napendekeza Serikali iweke msukumo mkubwa wa kuharakisha utekelezaji wa miradi iliomo kwenye mradi wa Bonde la Mto Songwe *(Songwe River Basin Development Programme - SRBDP),* wenye ofisi zake Kyela, Tanzania. Mradi huu unaotekelezwa kwa pamoja na Serikali za Tanzania na Malawi, ni muhimu sana kwa sasa kutokana hasa na ujenzi wa mabwawa ambayo pamoja na manufaa mengine, yatasaidia kupunguza mafuriko ya Bonde la Kyela. Mabwawa haya yamelenga kuzalisha umeme, kilimo cha umwagiliaji, shughuli za uvuvi na hata utalii ambao unahitajika sana katika Wilaya ya Mbeya na ukanda wote wa Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Spika, Serikali ichukue hatua za haraka kuleta Bungeni mapendekezo ya Sheria ya Kilimo ambayo pamoja na mambo mengine itawezesha usimamizi wa matumizi bora ya ardhi ya kilimo ambayo inaendelea kupotea kwa matumizi ya makazi. Pia kutokana na changamoto za tabianchi, kumekuwepo na uharibifu mkubwa wa mazingira, na ongezeko la upungufu wa vyanzo vya maji. Uharibifu unaotokana na shughuli za kibinadamu umepelekea misitu mingi kuharibiwa na uchomaji moto, ukataji mkaa, na hata kilimo kwenye vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali iongeze msukumo kwa Wizara za Maji, Kilimo, Maliasili na Mazingira kufanya kazi kama timu moja ili kukabiliana na janga hili kubwa ikiwemo ujenzi wa mabwawa makubwa katika maeneo yanayokumbwa na mafuriko. Kama ilivyo kwa athari za mafuriko ya Kyela, hata Ziwa Rukwa linaathirika sana na kujaa mchanga na udongo unaosombwa na mito kutokana na mmomonyoko wa udongo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya pamoja na msaidizi wake Naibu Waziri. Wote mnafanya kazi nzuri bila kuwasahau Makatibu Wakuu wa Wizara kwa kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita katika maeneo yafuatayo; nikianza na Maafisa Ugani; napongeza Serikali kwa kuwapa pikipiki Maafisa Ugani waweze kuwafikia wakulima. Tatizo maafisa hawa wako Wizara ya TAMISEMI pamoja na Waziri kuwa na nia njema na kilimo, lakini hawa Maafisa Ugani hawawajibiki katika Wizara yake. Niiombe Serikali waangalie mfumo wa utawala wa Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchimbaji wa mabwawa; kutokana na mabadiliko ya tabianchi na ukosefu wa mvua naungana na Serikali kuchimba mabwawa na kufanya kilimo cha umwagiliaji tuweze kupata mazao mengi ya chakula na biashara.

Kwa upande wa rasirimali watu; Serikali itoe kibali cha ajira kwa Wizara hii kwani kuna taasisi hakuna watumishi wa kutosha kama *TFC*, ni vyema Wizara ipewe kibali.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Hongereni sana.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, suala la kutumia jembe la mkoa halitaweza kuwasaidia wakulima wadogo wadogo. Ni muhimu sana Serikali sasa ipeleke matrekta kwenye vijiji kwa kuanzia na matatu kila kijiji. Tukiendelea kulima kwa mkono bado wakulima wadogo ambao ni wengi hawatafaidika na umaskini utabaki pale pale.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa vituo vya usambazaji mbolea tafadhali sana viwepo vijijini. Wakulima wanatapeliwa sana na wajanja ambao hutumia pikipiki kutoa kituo kikuu na kuongeza bei.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Hussein Bashe, Naibu Waziri Mheshimiwa Anthony Mavunde, Katibu Mkuu Ndugu Gerald Mweli, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Hussein Mohamed, wataalam wa Wizara, wakuu wa taasisi zilizo chini ya Wizara pamoja na wadau wa maendeleo kwa mchango mkubwa sana kwenye sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utahusu fursa za kilimo cha umwagiliaji katika jimbo la Moshi Vijijini, hali ya Vyama vya Ushirika na Kiwanda cha Kukoboa Mpunga kilichopo Kijiji cha Chekereni, Kata ya Mabogini jimbo la Moshi Vijijini.

Mheshimiwa Spika, mkoa wa Kilimanjaro una fursa kubwa sana za kilimo cha umwagiliaji. Hii ni kutokana na ukweli kwamba Kilimanjaro kuna mito mingi inayoanzia mlimani na kuishia bahari ya Hindi bila kutumika kikamilifu kwenye kilimo.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali ijenge skimu mpya na kukarabati zile skimu za asili ili haya maji yatumike kuzalisha mazao badala ya kuishia baharini.

Mheshimiwa Spika, katika jimbo langu la Moshi Vijijini ninaishauri Serikali ifanye yafuatayo; kwanza Serikali iwekeze kikamilifu kwenye kuboresha na kujenga upya skimu za asili. Kule Kilimanjaro kulikuwa na mradi wa *Rehabilitation of Traditional Irrigation Schemes*. Tangu mradi huu ufungwe, miundombinu ya skimu hizi imekuwa kwenye hali mbaya. Kwa ujumla miundombinu hii imechoka na maji hayawafikii tena wakulima wa kahawa, ndizi, mbogamboga na matunda kama maparachichi. Skimu hizi za asili zikiboreshwa (Kata za Kibosho, Kirima, Kibosho Kati, Kibosho Mashariki, Kibosho Magharibi, Kindi, Okaoni, Uru Shimbwe, Uru Mashariki, Uru Kaskazini, Uru Kusini, Kimochi, Oldmoshi Mashariki, Old Moshi Magharibi na Mbokomu) zitasaidia sana kuongeza tija kwa wakulima wangu wa Jimbo la Moshi Vijijini.

Pili, Serikali ijenge skimu mpya za umwagiliaji katika maeneo ya tambarare ambayo hukumbwa na mafuriko makubwa kila mwaka. Maji ya mafuriko yaelekezwe shambani kuzalisha chakula (mpunga na mazao mengine). Maeneo ya kuzingatia ni:-

a) Wizara ijenge skimu mpya Kata ya Arusha Chini katika Mto Ronga itakayohusisha vijiji vya Mikocheni na Chemchem ambako kuna takribani 2000 ha.

b) Wizara ijenge skimu mpya ya ziada Kata ya Mabogini ambapo kuna 1350 ha.

Mheshimiwa Spika, skimu hizi mpya zikijengwa, zitaongeza 3350 ha kwenye kilimo cha umwagiliaji na kuongeza uzalishaji wa chakula na kuchangia kikamilifu katika uchumi wa wananchi na Taifa.

Mheshimiwa Spika, mchango mwingine ni kuhusu mashamba ya ushirika na vyama vya *SACCOS* zilizopo kwenye maeneo mbalimbali ya Jimbo la Moshi Vijijini. Uongozi wa mashamba na baadhi ya *SACCOS* ni changamoto kubwa sana. Viongozi wengi wa ushirika hawana taaluma za kuongoza ushirika.

Mheshimiwa Spika, katika baadhi ya vyama jimboni kwangu kuna matumizi mabaya ya madaraka na rasilimali za mashamba mengi ya ushirika. Katika mikutano yangu ya hadhara, wakulima wametoa malalamiko kuwa wanaibiwa na viongozi wa ushirika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa fedha za kutosha zimetengwa kwenye idara ya ushirika, ninaishauri Serikali ifanye ukaguzi maalum katika mashamba na *SACCOS* zote na watakaobainika wamefuja mali za ushirika, wachukuliwe hatua za kisheria na vyombo husika. Hii ni pamoja na kurekebisha sheria na sera za ushirika Tanzania ili tuwabane wabadhirifu wa mali za ushirika.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa mwisho ni kuhusu Kiwanda cha Kukoboa Mpunga cha Kilimanjaro *Paddy Hulling Co. Ltd.*

Mheshimiwa Spika, kiwanda hiki kimesimamisha shughuli zake na kabla ya kufungwa, kiwanda hiki kilikuwa moja ya kiwanda kilichokuwa kimepata mafanikio makubwa sana. Kiwanda hiki kipo Chekereni – Moshi katika Kata ya Mabogini.

Mheshimiwa Spika, kiwanda hiki kiko kwenye eneo ambalo huzalisha mpunga mara mbili hadi tatu kwa mwaka. Kiwanda hiki hakifanyi kazi tangu Septemba, 2014. Kiwanda cha Kukoboa Mpunga kilikodishwa na Chama Kikuu cha Ushirika cha Kahawa *(KNCU)* na baada ya kushindwa kukiendesha, mkoa ulimshauri Msajili wa Hazina kukirudisha Serikalini ili atafutwe mwekezaji mwingine anayeweza

kukiendesha. Tayari Msajili wa Hazina amerejesha kiwanda hiki Serikali tangu tarehe 18 Oktoba, 2018 lakini bado hajapatikana mwekezaji, na shughuli zimelala. Kutokuwepo kwa kiwanda hiki kumeondoa fursa ya wakulima kupata bei nzuri ya mpunga na ajira kiwandani kwa wana Moshi Vijijini.

Mheshimiwa Spika, kiwanda hiki kinaweza kuwa ni chanzo cha kuongeza thamani na kusafirisha mchele wetu nje na kuwapatia wakulima kipato na taifa kwa ujumla. Naiomba Wizara isaidie kumpata mwekezaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ya kuendeleza kilimo na kuwaletea ustawi wananchi. Pili, nimpongeze Waziri Mheshimiwa Hussein Bashe pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Anthony Mavunde, Katibu Mkuu Ndugu Gerald Mweli na Naibu wake pamoja na watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nashauri mchango uliotolewa na Mheshimiwa Benaya Kapinga kwa kusema kuhusu utaratibu wa sasa wa kununua kahawa ufanyiwe kazi. Wakulima wanalalamika sana ikiwemo wa Wilaya ya Nyasa kutokana na kukopwa kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, shukrani kwa miradi ya umwagiliaji ya Chiulu, Lundo na Kimbande kuonekana katika mipango ya uendelezaji katika bajeti hii. Kuna mahali katika skimu za ukarabati Kimbande inasomeka kuwa katika Wilaya ya Mbinga. Ili mradi usipotee naomba Kimbande isomeke ipo Nyasa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri alinidokeza kuwa Skimu ya Lituhi imo kwenye mikakati ya bajeti hii. Nilipoenda kwenye mwenge kwa furaha kabisa nikawaeleza wananchi, wakakushukuru na kukuombea sana Mheshimiwa Waziri na pia Mheshimiwa Rais. Sasa Lituhi ambayo pia niliuliza swali humu Bungeni na ukanijibu wewe mwenyewe, imeyeyukia wapi? Nadhani imekumbana na changamoto za kiuandishi.

Mheshimiwa Spika, Nyasa ipo pembezoni, bado ni maskini lakini ina rasilimali za kuanzia kama hizi. Msimu uliopita hatukupata chochote, tunawaamini mwaka huu hamtatuacha.

Mheshimiwa Spika, namalizia kuwashukuru kwa kutuletea *Engineer* Faraja, yupo vizuri, akipewa nyenzo atafanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, nashauri pia bajeti yenu ishuke chini kiutekelezaji.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mchango wangu wa maandishi kama ifuatavyo; kwanza kuhusu miradi ya umwagiliaji Jimbo la Singida Kaskazini, Bwawa la Mgori limejaa tope na halina miundombinu ya umwagiliaji. Naishukuru Wizara kwa kutuma timu ya wataalam kuhakikisha bwawa hili linafanyiwa kazi ili liweze kusaidia uzalishaji kwani ni eneo lenye ardhi nzuri kwa kilimo cha umwagiliaji kwa mazao ya mahindi, vitunguu karanga na alizeti. Bwawa hili litanufaisha hekta 1000 endapo litapatiwa miundombinu ya umwagiliaji.

Aidha, katika Jimbo la Singida Kaskazini tunayo Mabwawa ya Ntambuko, Kisisi, Masoghweda, Endesh na Mikuyu ambayo yanafaa sana kwa kilimo cha umwagiliaji endapo yatawekewa miundombinu yake. Pia ardhi yake ni nzuri kwa uzalishaji wa mazao anuai hasa mahindi, alizeti, vitunguu na mbogamboga. Naiomba Wizara iyatembelee na

kuyafanyia upembuzi yakinifu na kuyajengea miundombinu yaweze kutumika kwa umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ina upungufu wa watumishi 93 wa Idara ya Kilimo, naomba kupatiwa watumishi ili kazi ziweze kufanyika ipasavyo; idara iwezeshwe usafiri wa gari ili iweze kufanya ufuatiliaji wa shughuli za kilimo kwa urahisi. Gari lililopo ni kuukuu na ni bovu. Pia tunalo shamba la mbegu lenye hekta 600; naomba Wizara iweke mkakati wa kuzalisha mbegu za mazao hususan mahindi na alizeti ili kuepuka gharama kubwa tunazopata kusafirisha mbegu kutoka maeneo ya mbali.

Mheshimiwa Spika, zao la pamba lirejeshwe katika mkoa wa Singida kwani tunacho Kiwanda cha Pamba Mkoani Singida ambacho kinahudumia mikoa ya Singida, Tabora na Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwa hai na salama. Ninapenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anazozifanya katika Taifa letu hili, kwa kuzidi kuiongeza bajeti ya Wizara ya hii ya Kilimo kwa mwaka wa 2023/2024. Haya yote ni kwamba Mheshimiwa Rais anawapenda wananchi wake wa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, pia ninapenda kumpogeza Waziri na Naibu wake, uongozi wote wa Wizara hii. Hakika maneno ya wazee wetu kwamba pumu imepata mkohozi Wizara hii imepata mtendaji hodari sana.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Wizara ya Fedha itoe pesa kwa Wizara hii ili mipango yote mizuri iliyoletwa iweze kutekelezwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Wizara kuimarisha masoko na huduma za masoko kwa wakulima na kuwasogezea masoko, sambamba na kuimarisha miundombinu ya kuyafikia masoko.

Mheshimiwa Spika, kuimarisha usafirishaji kutoka mashambani na kwenda katika maeneo ya masoko hasa barabara za vijijini zifanyiwe matengenezo ili ziweze kupitika kipindi chote.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Wizara iwajengee uwezo zaidi Maafisa Ugani ili kufanya shughuli zao na kumudu majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, Serikali iendelee kuongeza mashamba darasa ili kuwawezesha wakulima kuendelea kujifunza kupitia mashamba hayo.

Mheshimiwa Spika, pia wakulima wapatiwe ujuzi na maarifa baada ya mavuno ili waweze kutunza na kuhifadhi mazao yao wakati wakisubiri kupata soko la mazao hayo.

Mheshimiwa Spika, Serikali kuimarisha wigo wa kuongeza thamani ya mazao ili kuongeza tija kwa wakulima kwa kupata masoko ya ndani na nje.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa wananchi wengi wanazalisha mazao ya chakula, tunaomba Serikali izidi kuhamasisha wananchi wetu waweze kuzalisha mazao ya biashara ili waweze kupata kipato cha kujikimu katika maisha yao.

Mheshimiwa Spika, Serikali kuhakikisha inatafuta masoko ya kutosha kwa mazao ya wakulima ili kuepusha kupata hasara, mfano alizeti, ufuta, mbaazi na mbogamboga.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Spika, naongezea mchango wangu wa jana.

Mheshimiwa Spika, nianze na Kiwanda cha *TANICA* Kagera. Naomba Wizara kupitia Bodi ya Kahawa ilipie hisa ambazo hazijalipiwa zenye thamani ya shilingi bilioni 8.6 katika Kiwanda cha *TANICA* cha Mkoa wa Kagera. Pia nashauri Wizara itusaidie kutafuta wawekezaji zaidi kwenye kiwanda hicho ili kiweze kupata teknolojia mpya. Kiwanda hiki ni muhimu sana kwani kinaongeza thamani kwenye kahawa yetu, tusikiachie kife Mheshimiwa Waziri.

Pili ni Skimu za Kyamyorwa, Buhangaza na Kyota Wilaya ya Muleba; nashukuru sana, naona Tume ya Umwagiliaji imepeleka wafanyakazi Kagera na zaidi Wilaya ya Muleba. Aidha nawashukuru wamepewa vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, naumba sana Waziri, Skimu za Kyamyorwa, Buhangaza na Kyota, Wizara kupitia Tume ya Umwagiliaji itusaidie kukamilisha skimu hizi ambazo Serikali yetu imeweka pesa nyingi ya walipakodi lakini haina tija kwa wakulima wetu kwa sababu haijakamilika. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, nimechangia sana Bungeni kuhusu skimu hizi, nakuomba uzikamilishe kwa ajili ya watu wa Muleba na Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Building Better Tomorrow (BBT),* Muleba tuna eneo kubwa la Mwisa II zaidi ya hekta 80 ambazo ndio *busket food* kwa Wilaya ya Muleba na Mkoa Kagera kwa ujumla. Eneo hili linafaa sana kwa kilimo, sana mahindi, maharage na mchele. Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kupitia *NARCO* walipima eneo hili vitalu jambo ambalo linatishia usalama wa chakula mkoa wa Kagera. Nawaomba eneo angalau nusu yake litumike kwenye mradi wa *BBT.*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kumalizia nyongeza ya mchango wangu kwa Wizara ya Kilimo kwa kuwa wakati ninachangia ndani ya Bunge kwa kuwa muda ulikuwa hautoshi sikumaliza kuwasilisha mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, ninashauri suala la *BBT* liwekezwe zaidi kwenye mikoa na ukanda wenye uhakika wa mvua ili kuepuka gharama za ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji kwenye maeneo ambayo hayana nvua kabisa. Ninaomba pia kwa kuwa Mkoa wa Ruvuma umekuwa na uhakika wa mvua za kutosha, *BBT* ipelekwe huko mapema sana nina imani itafanya vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miundombinu; Mheshimiwa Waziri Hussein Bashe ameweka mpango mzuri sana wa kuweka miundombinu mizuri kwenye suala la utekelezaji na nitataja baadhi tu ya vifaa ambavyo ni pikipiki, vinasaba, nyumba, magari ambayo ametaja kuwa magari hayo yatawahusu Maafisa Kilimo wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu sijasikia maboresho ya miundombinu kama magari yakitajwa kwa Wakurugenzi wa Taasisi za Wizara ya Kilimo kwa maana ya maslahi yao. Hawa wakurugenzi wanafanya kazi nzuri sana na ndiyo maana Wizara hii imeonesha matokeo chanya katika utendaji wake.

Mheshimiwa Spika, iko haja na ni jambo muhimu sana kwa wakurugenzi hawa kuboreshewa maslahi yao ikiwa ni pamoja na kuwapa magari mazuri yenye uhakika na yatakayokidhi mazingira halisi ya utendaji wao maana hawa viumbe wanazunguka nchi nzima kuhakikisha ustawi wa Wizara, wananchi na uchumi wa nchi unakuwa kama ilivyo sasa. Aidha kwa kuwa hawa wakurugenzi wamekuwa

wakifanya kazi na makampuni makubwa yaani matajiri wakubwa ambao wana fedha nyingi ambazo zinaweza kuwaweka katika hali ya majaribu makubwa sana, ni imani yangu kuwa endapo maslahi yao yataboreshwa itasaidia sana kuwaongezea ari ya utendaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, nipende kuliambia Bunge lako tukufu kuwa katika hali ya kawaida nimeona gari la mmoja wa wakurugenzi akiwa ziarani Mkoani Ruvuma katika kufuatilia majukumu yake kwa zao la tumbaku kwa kweli lile gari linaonekana kuchakaa kabisa, nikajiuliza ndio gari analotumia Mkurugenzi kuzungukia nchi nzima? Kimsingi magari kama hayo ni hatari sana kwa usalama wa watendaji hao, hata hivyo viumbe hawa ni rasilimali ya Taifa na inapotokea wanapata ajali na kupoteza maisha mara nyingi tunakuwa tunasema maneno rahisi kabisa kwamba "Taifa limepoteza kiongozi muhimu sana na kwamba pengo lake halitazibika" *so what?*

Mheshimiwa Spika, hii ni hatari sana na ni hasara kubwa kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mbolea ya ruzuku mfumo uboreshwe kwani inaonesha kuwa mfumo wa mbolea ya ruzuku ina tundu. Aidha, mbolea sasa ipelekwe mpaka vijijini ili kumpunguzia mkulima gharama na adha mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wafadhila endapo nitamaliza mchango wangu bila kuwataja watu wafuatao na ninaomba majina yao yaingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, Watendaji Wakuu hawa wa taasisi ndani ya Wizara ya Kilimo wanastahili pongezi, wanafanya kazi nzuri sana hakika wanazitendea haki nafasi zao walizopewa nao ni hawa wafuatao; *NFRA* ni CPA Milton Lupa; Kahawa ni Ndugu Primus Kimaro; Korosho ni Ndugu

Francis Alfred; Tumbaku ni Ndugu Stanley Mnozya; *TFRA* ni Dkt. Stephan Ngailo na *CPB* ni Ndugu John Maige.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa nafasi hii ninaunga mkono hoja na ninaomba kuwasilisha.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kuendelea kuipanua na kuendeleza sekta hii ya kilimo ambayo ina mchango mkubwa wa pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri pia pamoja na timu yake yote kwa uthubutu waliouonesha pamoja na kuendeleza maono haya mazuri ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, Watanzania milioni 61 wote wanakula chakula kila siku, na kati ya hawa zaidi ya milioni 40 wanajihusisha na shughuli za kilimo kwenye maisha yao ya kila siku. Hivyo basi tunaona kabisa sekta hii ilivyo na mchango mkubwa kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee suala moja la mazao ya bustani *(horticulture)* ambayo inajumlisha mbogamboga, matunda, maua na viungo.

Mheshimiwa Spika, mazao haya ya bustani yanachangia sana kwenye kuingizia nchi yetu fedha za kigeni kwa kiasi kikubwa, lakini bado Wizara hayajayapa mkazo wa kutosha. Ukiangalia ukurasa wa 104 ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri utaona mwenendo wa uzalishaji wa mazao ya bustani kutoka mwaka 2018 hadi 2022. Ukiacha mazao mengine, zao la maua limekua limetelekezwa muda mrefu kama halina mwenyewe licha ya kwamba maua ni zao ambalo lina soko la uhakika duniani na lina mchango mkubwa kuingiza fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, mwenendo huu wa maua hauridhishi na hivyo naiomba sana Wizara iweze kutueleza wakati wanahitimisha mikakati iliyonayo kwenye kuendeleza zao la maua hapa nchini na hususan kwa mkoa wangu wa Arusha.

Mheshimiwa Spika, leo hii kwenye nchi jirani ya Kenya zao hili la maua linachangia zaidi ya dola milioni 900, ajira 100,000 na inagusa maisha ya zaidi ya watu 2,000,000. Lakini pia ukiachia zao la chai, maua ni ya pili kwenye kuchangia pato la Taifa katika nchi ya Kenya. Hivyo basi tunaona jinsi majirani zetu wanavyo ipa kipaumbele hii sekta.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Arusha ni miongoni mwa mikoa iliyokuwa inastawisha sana mazao haya ya bustani na ilikuwa inachangia pato la Taifa na fedha za kigeni kwa kiasi kikubwa, lakini tokea mashamba yalioyokuwepo ya mbogamboa, maua na matunda kufilisika na kutaifishwa mazao haya yameshindwa kuingizia taifa letu fedha hizi.Namuomba pia mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha atuambie mikakati ya kufufua mashamba haya kwa ajili ya mustakabali mpana wa Mkoa wa Arusha na nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Spika, tunaishukuru sana Serikali kwa mradi wa umwagiliaji Ruhuhu. Tunaomba utumike kutatua changamoto ya mafuriko Kata ya Ruhuhu hasa Vijiji vya Kipingu, Ilela na Ngelenge ambapo mpunga, mihogo na mahindi ya wakulima kuzama.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Bonde la Masimavalafu lenye ekari 5,000 nalo lipate mradi wa kilimo cha umwagiliaji. Bonde hili lipo Kata ya Ibumi, Kijiji cha Masimavalafu, Wilaya ya Ludewa.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, utangulizi; nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa nafasi hii uliyonipa nami niweze kuchangia hotuba hii muhimu ya Makadirio ya Mapato na Matumzi ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Awali ya yote naomba nipongeze hatua zinazochukuliwa na Serikali kuendelea kuongeza bajeti ya kilimo na suala la kilimo cha umwagiliaji kupewa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, nipongeze kwa uamuzi wa Serikali wa kujenga Bwawa na Skimu za Umwagiliaji katika Kijiji cha Mwakasumbi na Mwaukoli katika Jimbo la Kisesa. Suala hili nimekuwa nikilipigia kelele humu Bungeni kwa muda mrefu sana na ninaomba maeneo mengine yaliyobaki ya Mwandu Itinje, Mwasengela, Sakasaka, Tidabuligi na Mwabusalu nako maeneo hayo wananchi wanazisubiri kwa hamu kubwa skimu na mabwawa kwa kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kushindwa kukusanya maduhuli ya Serikali ambapo imeweza kukusanya kiasi cha shilingi milioni 679.57 sawa na asilimia 0.5 ya lengo la shilingi bilioni 126.1 zilizokadiriwa mwaka 2022/2023 hata mwaka wa fedha 2021/2022 mchezo ulikuwa ule ule Tume ilishindwa kukusanya mapato. Kitendo cha Wizara kutochukua hatua stahiki kwa uongozi wa Tume hii maana yake imebariki uzembe na ubadhirifu unaoendelea, hali hii inanipa mashaka makubwa juu ya uwezo wa Tume kusimamia majukumu na miradi mikubwa ya umwagiliaji ambayo tunaitengea mabilioni ya fedha kila mwaka. Hatua stahiki zichukuliwe ikiwemo kuwajibika kwa uongozi na Menejimenti ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa bajeti ya maendeleo; hapa kuna mkanganyiko mkubwa, fedha za maendeleo zilizoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2022/2023 ni shilingi bilioni 569.97; hadi kufikia Aprili, 2023 fedha zilizokuwa zimetolewa ni shilingi bilioni 470.75 sawa na asilimia 82.6 ya bajeti nzima ya maendeleo. Fedha hizo zimetolewa na

zimetumika kutekeleza miradi mbalimbali ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji na uhifadhi, kuimarisha utafiti na uzalishaji wa mbegu bora, kuanzisha mashamba makubwa ya pamoja na kugharamia ruzuku ya mbolea.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya maendeleo ya shilingi bilioni 569.97 fedha kwa ajili ya kuimarisha kilimo cha umwagiliaji ni shilingi bilioni 361.5 sawa na asilimia 63.4 ya bajeti nzima ya maendeleo. Kiasi kilichokuwa kimelipwa hadi Aprili, 2023 kwa ajili ya miundombinu ya umwagiliaji ni shilingi bilioni 85.15 sawa na asilimia 23.5 tu ya bajeti ya umwagiliaji. Fedha zilizopokelewa na kutumika zilifikiaje kiasi cha shilingi bilioni 470.75 wakati fedha zilizotolewa kwa ajili ya miundombinu ya umwagiliaji ni shilingi bilioni 85.15 tu kati ya shilingi bilioni 361.5?

Mheshimiwa Spika, hata tafsiri yake ni kwamba fedha kwa ajili ya miradi ya umwagiliaji imeshabadilishiwa matumizi na hapa kwa hesabu zangu ni takribani shilingi bilioni 200 hazijulikani zilipo na matumizi yake hayafahamiki. Waziri hana mamlaka kisheria kubadilisha matumizi ya vifungu na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Waziri atueleze fedha ziko wapi na zimebadilishiwa matumizi kwa ridhaa ya nani?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Tume ya Taifa ya Ushirika; Serikali iliahidi kwa muda mrefu kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Ushirika lakini utekelezaji wake umekuwa wa kusuasua, mwaka jana Waziri wa Kilimo aliahidi hapa Bungeni kuwa benki hii ingekuwa imeanza katika mwaka huu wa fedha unaomalizika. Taarifa iliyowasilishwa inaonesha mtaji umefikia shilingi bilioni 5.2 tu kati ya mtaji wa shilingi bilioni 15 unaohitajika ili kukidhi vigezo vya kuanzisha benki kama vilivyowekwa na *BOT* na hatujaelezwa benki hiyo itaanzishwa lini.

Mheshimiwa Spika, aidha ukaguzi uliofanywa na *COASCO* katika Vyama vya Ushirika 6,005 matokeo ya

ukaguzi huo yameonesha kuwa hati safi ni 5.65% huku hati zenye mashaka, mbaya na kushindwa kutoa maoni zikiwa 94.35% na mwaka jana hali ilikuwa vilevile na kwa maana hiyo hakuna mabadiliko yoyote yaliyofanyika na hii ni ishara ya kuota mizizi kwa ubadhirifu wa mali za umma na udhaifu wa mifumo ya udhibiti ya ndani hata Tume ya Maendeleo ya Ushirika ilipofanya ukaguzi ilibaini vyama vingi vya ushirika vinakabiliwa na madeni makubwa.

Mheshimiwa Spika, nimshauri mwaka jana na leo namshauri tena, Waziri aachane na mpango wa kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Ushirika na badala yake aimarishe mifumo ya usimamizi ya vyama hivi na kuondoa mianya ya upotevu wa fedha za wanachama na fedha za umma na kadhalika. Pia ili kuwezesha kupata mikopo kwa wingi na kwa urahisi lianzishwe dirisha la Vyama vya Ushirika katika Benki ya Maendeleo ya Kilimo *(TADB)*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utoaji wa mbolea ya ruzuku; huu utaratibu wa utoaji wa mbolea za ruzuku ulianzishwa na Serikali katika msimu wa kilimo wa 2022/2023 kwa lengo la kuongeza upatikanaji na kuwapunguzia gharama wakulima baada ya mtikisiko wa kiuchumi uliosababishwa na *Covid-19* na vita ya Ukraine na Urusi. Utaratibu huu ulitarajiwa kuondoa kasoro na dosari zilizokuwepo lakini badala yake hali imekuwa mbaya zaidi, mbolea kuadimika na kusababisha wakulima kukosa mbolea, wakulima kuuziwa mbolea *fake* ambayo imeenda kuua mazao na kuharibu afya ya udongo, mbolea kuchelewa kufika kwa wakulima, utoroshaji wa mbolea nje ya nchi, kuuziwa michanga badala ya mbolea, wananchi kusafiri umbali mrefu kufuata mbolea, kupoteza muda na wengine kupoteza maisha wakiwa kwenye foleni wakihangaika kutafuta mbolea.

Mheshimiwa Spika, utoaji wa mbolea ya ruzuku umekuwa na changamoto nyingi kama ifuatavyo:-

(i) Takwimu zilizotolewa na Waziri zina mkanganyiko mkubwa ambapo anasema hadi kufikia Aprili, 2023 mbolea za ruzuku zilizokuwa zimepokelewa na kusambazwa kwa wakulima ni tani 449,795 na wakulima walionufaika ni 801,776 lakini kiambatisho Na. 8 kinaonesha kuwa mbolea ya ruzuku iliyosambazwa ni tani 342,729 na wakulima walionufaika ni 782,553. Nini chanzo cha mkanganyiko huo wa takwimu au hizi takwimu ni za kupika? Waziri afafanue.

(ii) Wakulima waliosajiliwa ni 3,050,621 lakini wakulima walionufaika na mbolea ya ruzuku ni 801,776, nini kilichosababisha wakulima zaidi ya milioni 2.2 waliosajiliwa na kuahidiwa kupewa mbolea ya ruzuku wakose mbolea wakati nchini tuna ziada ya mbolea ya ruzuku tani 369,647?

(iii) Serikali ilifahamu kuwa haitawafikia na kuwasajili wakulima wote kwa mara moja, kwa nini ilianzisha mfumo wa utoaji wa mbolea ambao unalazimisha kupata lazima upitie mfumo wa mbolea ya ruzuku?

(iv) Mfumo wa kimtandao wa mbolea za ruzuku, hapa najiuliza kwa nini Wizara ya Kilimo ilianza kutumia mfumo huu ukiwa na changamoto nyingi kiasi hiki, na siamini kuwa Mamlaka ya Serikali Mtandao *(eGA)* inaweza kutoa kibali *(clearance)* kuruhusu mfumo huu kutumika nchini. Mfano mfumo huu unaruhusu:-

(a) Mfumo hauna usalama wala ukomo *(Security and Limit)*. Imewezekana kufanyika mikwaruzo ya kivunge cha mwitikio wa haraka *(QR code scanning)* zaidi ya mara moja *(double scanning) or multiple scanning)* kwa mauzo ya mfuko mmoja wa mbolea ambayo ingeweza kufanywa na waagizaji, mawakala, muundaji wa mfumo au haramia yeyote wa mfumo na kupelekea mauzo hewa ya mbolea kwa wakulima na madai hewa ya fedha kwa Serikali. Hapa ushahidi upo *TFRA* ilifutia leseni za mawakala 721 kwa makosa ya *double scanning* tarehe 17 Aprili, 2023.

(b) Mfumo huu hauwezi kung'amua kama mbolea imetumika kwenye shamba husika *(traceability)*. Hivyo mtu anaweza kuja kuchukua tu mbolea kwa namba ya mkulima halafu akaenda kuiuza nchi jirani kwa magendo ambao wanampa bei kubwa zaidi kuliko bei ya ruzuku. Hali hii imepelekea utoroshaji mkubwa wa mbolea nje ya nchi. Kesi za utoroshaji wa mbolea nje ya nchi zimekuwa zikiripotiwa mara kwa mara. Hata Mheshimiwa Waziri wa Kilimo alipofanya ziara Nyanda za Juu Kusini alikuta kesi za utoroshaji wa mbolea za ruzuku zimefurika kwenye Mahakama za Mikoa iliyo mipakani kama Songwe.

(c) Mfumo ulianzishwa bila kuzingatia kwamba huko mashambani mitandao ya simu inasumbua na inabidi wakulima wasafiri umbali mrefu kuitafuta mbolea sehemu zenye mitandao ya simu hali ambayo imekuwa ikiwaingiza hasara kubwa wakulima ya pesa za nauli, kulala *guest house* na gharama ya chakula.

(d) Mzabuni wa aliyeunda mfumo hatujaelezwa uwezo wake namna alivyopatikana, au alipatikana kwa kupewa mkataba bila kushindanishwa na wengine kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi ya Umma *(Public Procurement Act)*.

(e) Mfumo huu unachelewa ku-*left* na hivyo unamwezesha mkulima ku-*draw* zaidi ya kiwango alichonacho mfano anaweza kuchukua mbolea zaidi ya kituo kimoja na hivyo kupelekea hasara kwa mawakala.

(f) *QR Codes* zinaingiliana na kampuni nyingine mfano *QR Codes* za Kampuni X na Kampuni Y zinaingiliana na hivyo kusababisha mawakala kushindwa kutofautisha na hivyo kusababisha hasara na kudaiwa upande mwingine.

(g) Mfumo na matumizi ya *Agrodealer Tool* hauruhusu kufanya *Branch* au *Sub–Agent* na hivyo kulazimisha wakulima

kuja mjini sehemu moja kufuata mbolea na hautambui gharama nje ya eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Wizara ya Kilimo kuanzisha na kutumia mfumo bila kupata kibali *(clearance)* cha Mamlaka ya Serikali Mtandao *(eGA),* ni kwenda kinyume cha sheria ya Serikali Mtandao *(Electronic Government Act of 2019)* na wahusika wanapaswa wawe wanatumikia kifungo hadi sasa. Mfumo huu umeleta hasara kubwa kwa wakulima, mawakala na Serikali ikiwemo. Madai hewa ya fedha za ruzuku za mbolea, mazao kudumaa na kukosa mavuno na madeni makubwa ya mawakala na waagizaji wa mbolea makampuni, kutumia fedha zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge cha shilingi bilioni 150. Nani atafidia hasara hii, huu ni uhujumu uchumi, ni lazima tupate maelezo ya kutosha ili Bunge lichukue nafasi yake.

(v) Kufuta leseni za mawakala wa usambazi wa mbolea 721, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea *(TFRA)* iliwafutia leseni mawakala 721 wa usambazaji wa mbolea ya ruzuku kupitia matangazo ya magazeti ya Mwananchi na *The Guardian* ya tarehe 17 Aprili, 2023 ambapo pia maamuzi hayo yalipata kibali cha Waziri wa Kilimo alipoongea na waandishi wa habari nje ya Ukumbi wa Bunge Dodoma kupitia Kituo cha Televisheni cha Azam *(UTV)*. Tarehe 19 Aprili, 2023 *TFRA* iliwaandikia barua mawakala hao wajieleze kwa nini wasifutiwe leseni ya biashara ya mbolea kwa kosa la kuvunja sheria kwa kufanya udanganyifu wa ku-*scan QR Codes* zaidi ya mara moja *(multiple scanning)*. Jambo hili linaleta mkanganyiko mkubwa sana.

(a) Serikali kwa nini iandae mfumo unaoruhusu kufanya udanganyifu yaani *double scanning or multiple scanning*?

(b) Kwa nini *TFRA* iwafutie leseni mawakala 721 na kuwatangaza nchi nzima kuwa sio waadilifu halafu

iwaandikie barua ya kuwataka wajieleze; kwa nini wasifutiwe leseni huku ikiwa tayari imeshawahukumu?

(c) Kwa nini *TFRA* imekiuka Sheria ya Mbolea ya mwaka 2009 ambayo inataka kutoa notisi ya siku 30 na kupata maelezo ya mawakala hao kabla ya kuwaondoa? Hapa kuna nia ovu iliyokusudiwa na Wizara dhidi ya hawa mawakala.

(d) *TFRA* ilijuaje kama *double scanning* imefanywa na mawakala wakati mfumo ulioandaliwa hauna usalama *(security)* kiasi kwamba *multiple scanning* inaweza kufanywa na waagizaji, muundaji wa mfumo au haramia mwingine yeyote wa mifumo ya mitandao.

(e) *TFRA* hakufahamu changamoto hizo, *multiple scanning* anasubiri imebaki miezi miwili kuisha msimu wa kilimo ndio anaanza kuchukua hatua?

Mheshimiwa Spika, nani atawafuta machozi mawakala 721 ambao wamevunjiwa heshima kwenye umma na mitaji yao kuwekwa rehani? Uvunjifu wa sheria ukiruhusiwa uendelee namna hii utaleta matatizo makubwa kwenye Taifa, watu wote waliohusika kufanya dhuluma hii wawajibishwe na kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

(vi) Kutokufanyika uhakiki wa bei kabla ya kuanza kutoa mbolea ya ruzuku, Wizara ya Kilimo iliandaa mfumo wa kuanza kutoa mbolea za ruzuku bila kufanya uhakiki wa bei katika viwanda vinavyozalisha mbolea na matokeo yake pamoja na kushuka sana kwa bei za mbolea katika soko la dunia bado wakulima wanaumizwa kwa bei kubwa huku Serikali ikidaiwa pesa nyingi na makampuni yanayoingiza mbolea nchini ambazo zingeepukika kama ufuatiliaji wa bei za mbolea viwandani ungeendelea kufanyika mara kwa mara kama ilivyokuwa wakati wa *BPS*. Mfano, *TFRA* ilitangaza bei elekezi ya mbolea ya Urea kwa mfuko wa kilo 50 mwezi

Agosti, 2022 kwa wastani wa shilingi 124,734, mwezi Novemba, 2022 wastani wa shilingi 116,687 na mwezi Machi, 2023 wastani shilingi 72,911. Mbolea katika soko la dunia ilikuwa inashuka bei kila mwezi kwa nini *TFRA* haikutangaza bei elekezi?

Kwa nini bei imeporomoka ghafla baada ya msimu wa kilimo kukaribia kufika mwisho na mahitaji ya mbolea kupungua? Lakini pia bei haina tabia ya kushuka ghafla inashuka kwa *slope* ni *price elasticity or price volatility*.

Mheshimiwa Spika, bei elekezi iliyotolewa na *TFRA* ilitokana na matamko ya wafanyabiashara na hakuna uhakiki wa kiuchunguzi *(due diligence)* uliofanywa na Serikali kupitia *TFRA* kama sheria inavyoelekeza. Pamoja na bei ya soko la dunia kuendelea kushuka, lakini ziliendelea kutumika bei zilezile za juu mpaka msimu wa matumizi makubwa ya mbolea ulipomalizika Machi, 2023 ndipo *TFRA* ikatangza bei ndogo zaidi (wastani wa shilingi 76,421 na hivyo kufanya wastani wa ruzuku ambayo Serikali ilitakiwa kuwalipa mawakala kuwa shilingi 6,421 kwa mfuko wa kilo 50). Hiki kitendo cha kuacha kufuatilia bei za soko la dunia kama sheria inavyoelekeza kumeifanya Serikali kulipa na kudaiwa na makampuni madai na malipo hewa.

(vii) Kiasi cha fedha kilicholipwa hadi sasa kugharamia mbolea ya ruzuku hakijatajwa mahali popote na Waziri wala madai ya waagizaji wa mbolea, kwa nini Waziri anatumia nguvu kubwa sana kuficha taarifa hizo.

Mheshimiwa Spika, ushauri; *CAG* afanye ukaguzi maalum kuhusu utekelezaji wa utoaji wa mbolea ya ruzuku kwa haraka kabla ya Bajeti Kuu ya Serikali ya mwaka 2023/2024 ili kubaini mapungufu yaliyopo na Bunge kuchukua nafasi yake.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula na Mheshimiwa Antony Peter Mavunde ajiandae.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba unipe ruhusa ya dakika moja niwatakie kila la kheri Timu ya Wanachi kesho wanapofanya kazi kubwa ya kupeperusha bendera ya nchi katika hatua kubwa hiyo ya nusu fainali, ambayo ni hatua kubwa sana kwenye mashindano hayo ya hapa Afrika. Niwape pole wenzetu juzi walipambana kule Mtwara lakini wamekufa kiume, mashindano ndivyo yalivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumepokea hoja zote ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezitoa. Hoja ambayo inaangukia katika upande wa Wizara yetu, ya kwanza illikuwa masuala ya kikodi. Kama nilivyosema wakati tunajadili Wizara zingine za Kisekta ambazo masuala ya kikodi yalijitokeza. Nilisema kwamba tunaendelea na mchakato wa kuandaa hatua za kikodi ambazo tutazileta hapa Bungeni na masuala ya Kilimo na yenyewe yapo ambayo yatafanyiwa rejea na kuweza kuboreshwa ili kuweza kutengeneza mazingira rafiki ya kuweza kukuza kilimo chetu. Wizara ya Kisekta inahusika pamoja na sekta binafsi wanahusika katika kuandaa hatua hizo mpya za kikodi ambazo zitakuwa rafiki katika kukuza kilimo chetu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo lilijitokeza pia suala la Benki yetu ya Maendeleo ya Kilimo, Benki yetu ya Maendeleo ya Kilimo tumezipokea hoja ikiwepo ushauri wa namna ya kutunisha mfuko huo kwa kuhusisha taasisi za kifedha za ndani ya nchi pamoja na nje ya nchi. Tumepokea ushauri huo na tutakuja na tamko la kisera tutakapoleta hotuba kuu ya Serikali mapema mwezi ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaahidi Waheshimiwa Wabunge Benki hii ya Kilimo ni Benki yetu na ni *engine* katika hatua za

Mheshimiwa Rais za kuhakikisha tunakwenda kwenye kilimo cha kibiashara. Kwa hiyo tutakuja na tamko la kisera ambalo litakuwa linaendana na maono hayo ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, kwa maslahi ya muda, hoja ya tatu ambayo ilikuwa imetolewa imeongelewa na Waheshimiwa Wabunge na nimesikia Mheshimiwa Mpina akiliongelea na lilikuwa suala la fedha za maendeleo. Utaratibu wetu wa kibajeti tunaotumia hapa nchini ni *cash* bajeti. Tukishapata ridhaa ya Bunge hapa Bungeni tunapitishiwa makadirio ya mapato na matumizi, hatupitishiwi fedha kwamba ziko mahali hivi zianze kugawanywa kwenda kwenye kila Wizara. Tunapitishiwa makadirio ya mapato tunakwenda kukusanya na tunapitishiwa makadirio ya matumizi, tunapata ridhaa ya kwenda kutumia kwa kila miradi.

Mheshimiwa Spika, kwenye miradi ile ambayo wakati wake wa utekelezaji ni mfupi tunatumia *force account*. Pale kwenye *force account* tunatanguliza fedha tunawapatia wanaendelea kutekeleza, lakini kwenye miradi mikubwa kama ya barabara, miradi mikubwa kama ya umwagiliaji, tunachofanya tunafanya kwanza taratibu za mapitio ya taratibu za manunuzi kufuatana na bajeti iliyopitishwa. Tukishapitishiwa taratibu za kimanunuzi, mikataba inasainiwa, mikataba ikishasainiwa hatua ya kwanza ni kutekeleza taratibu za mkataba ambayo ni kulipa asilimia ya kwanza ya awali ambayo ni *down payment* kwa kila mradi.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo tunaanza kulipa *certificate* kufuatana na hatua za kiukaguzi wa utekelezaji wa mradi ambao umefikiwa. Hatuingii tu mkataba halafu tukampa fedha zote. Huu sio utaratibu kwamba kwa sababu bajeti ilipita ya bilioni 600 ama bilioni 300 basi baada ya kuingia mkataba tunaenda tunampatia bilioni 300. Huo utaratibu haupo na nimeshangaa sana kwa sababu aliyeongea Mheshimiwa Mpina ni Mbunge mzoefu na amekuwa kwenye Serikali. Ni Waziri mstaafu anajua kwamba

tunapotekeleza mradi hata kama bajeti ilipitishwa hatuendi kumpatia yule mkandarasi fedha yote ili aanze kuchukua kutoka kwenye ghala lake.

Mheshimiwa Spika, tunamlipa *down payment*, tukishamaliza kumlipa *down payment* tunaanza kumlipa kwa *certificate* kufuatana na ngazi ya mradi alivyotekeleza na pale ambapo inatokea ngazi ya mradi ambayo ametekeleza haijafika asilimia 100 haina maana kwamba fedha ile imepelekwa kwenye matumizi mengine. Maana yake fedha hiyo inaenda hatua kwa hatua za utekelezaji kadri *certificate* inavyokuja. Hivyo hivyo hata Bwawa la Mwalimu Nyerere tunavyojenga hatuiingii mkataba wa trilioni sita halafu baada ya kuingia mkataba tukawapatia wakandarasi trilioni sita. Kwanza fedha zenyewe hizo haziko tu mahali zimerundikwa zisubiri kwamba unavyosaini mkataba umpatie yule anayetekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miradi ya umwagiliaji ni miradi kama ya barabara na hata hii ya sasa ambayo tunatekeleza, tunatekeleza si vimiradi vya mzaha mzaha hivi, tumeamua kutekeleza miradi *seriously* ya umwagiliaji. Miradi hii kiwango cha chini kabisa cha muda wa utekelezaji itakuwa kwenye miezi 24 hivi. Sasa kama ni miezi 24 mkandarasi unaingiaje naye mkataba halafu uende ukampatie fedha yote ya utekelezaji wa mradi. Unampatiaje fedha ya utekelezaji wa mradi wa miezi 24, siku moja? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunatekeleza hivyo hivyo kwenye barabara, tunatoa kufuatana na *certificate*. Kwa jinsi Mheshimiwa Rais alivyodhamiria kwenye jambo hili la umwagiliaji, hatujakosa fedha ya kutekeleza miradi ya umwagiliaji na hii ni awamu ya kwanza na tutaendelea na awamu zingine na kwenye ile bajeti ambayo ameisoma Mheshimiwa Bashe bado tunamalizia majadiliano mengine na kuna miradi mingine mikubwa tunatarajia tuiseme wakati

tunatoa tamko la kisera na tamko la bajeti tutakapoleta hapa kwa ajili ya kupata ridhaa hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo wananchi pamoja na Waheshimiwa Wabunge, huu ni utaratibu wa *cash budget* wala hamna fedha ambayo ina ukakasi wowote kuhusu utekelezaji huu wa miradi hii ya umwagiliaji. Kinachofanyika ni taratibu za kutekeleza miradi mikubwa na miradi ya kielelezo. Tumedhamiria kwenye hii miradi ya umwagiliaji na tutaenda kwenye hiyo hatua ambayo tunaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni jambo ambalo si jema sana ile ambapo kila mtu ukikaa unawaza tu kudhania wanaotekeleza wanakosea. Halafu na wengine walishawahi kuwa na fursa pia kama Mpina hivi, haangalii hata yale ambayo yeye aliwahi kutekeleza na watu walikua wanamuongelea namna gani. Yeye kila wakati kuwaza kila Wizara inachotekeleza inakosea. Hii si sahihi, nadhani Mheshimiwa Rais tumtie moyo. Fikirieni tuna miaka 60 tangu uhuru, hivi kwenye hekta zaidi ya milioni 29, ni hekta ngapi zimeshajengewa miradi *serious* ya umwagiliaji. Sasa mwaka mmoja tu ambao ameanza tunakuja na *criticism* kibao. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, kengele imeshagonga.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. hapa ndio gari lilishaanza kushika gia, nimwachie Mheshimiwa Waziri wa Kisekta ila aendelee… *(Makofi)*

**SPIKA:** Usingeanza na mambo yako ya Yanga ungekuwa umekamilisha sasa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde na Mtoa Hoja ajiandae ajiandae.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa fursa hii kuchangia hoja ya Wizara ya Kilimo. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo anaisimamia Wizara hii na niwapongeze Waziri pamoja na timu yake kwa kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ni Wizara wezeshi na katika suala zima la utambuzi wa maeneo kwa ajili ya kilimo na shughuli zingine, Tume ya Mipango ya Ardhi ndio kazi yake. Ni jukumu lao kwanza la shughuli katika tume kuhakikisha kwamba wanaratibu na kuwezesha mpango wa matumizi ya ardhi yaweze kufanyika katika maeneo na kwa kipindi kifupi katika kutambua maeneo kwa ajili ya kilimo toka Mheshimiwa Rais alipowekeza na kujikita kwenye kilimo. Jumla ya hekta ambazo zimeshatambuliwa mpaka sasa ni 2,160,076. Zimetengwa kwa ajili ya kilimo kutoka katika vijiji 1,059, kati ya vijiji 2,765 ambavyo vimewekewa mpango wa matumizi. Mheshimiwa Josephine Genzabuke alizungumzia habari ya kuwawezesha wakulima na ndio hasa dhamira njema ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapowapimia wakulima maeneo yao maana yake kwanza tunaongeza thamani ya ile ardhi yao. Inapoongezwa thamani kwa kupewa ile hati, tunamwezesha pia kuondokana na migogoro, lakini tunampa uwezo wa kuitumia ile haki kwa ajili ya shughuli za kimaendeleo. Mpaka sasa tunavyozungumza jumla ya hati 1,318 zimetumika, zile hati miliki za kimila zimetumika katika mabenki kutoka kwenye halmashauri 10 katika mabenki ambayo yametoa jumla ya bilioni 60, milioni 164 zimetolewa kama mkopo kutokana na hizi hati miliki za kimila.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa maana nyingine Mheshimiwa Genzabuke alivyoliongelea, Serikali inaliangalia hili na tunajua wakulima wako zaidi ya asilimia 65 kwa sensa ya 2022. Kwa maana hiyo ni kwamba unapowekeza kwenye kilimo lazima pia umwangalie mkulima na kumwangalia kwake ni kuhakikisha kwamba ile salama ya miliki yake inakuwepo na ndio maana tunakazania katika suala zima la kuweka mpango wa matumizi ya ardhi katika maeneo, ili kila kipande cha ardhi kipangiwe matumizi. *Once* ukishakipangia jukumu lingine linakuwa ni la kukitumia.

Mheshimiwa Spika, wenzetu wa kilimo nawapongeza sana kwa sababu katika haya maeneo ambayo tumeyaainisha wanalo jukumu la kupima ule udongo kuona unafaa kwa kilimo gani. Kuna Mbunge mmoja amechangia akawa anasema tuwe tunaangalia na udongo unafaa kwa namna gani ili katika mazao tuangalie kikanda. Nadhani hili Wizara wameshalichukua na wanalifanyia kazi. Sisi kama Wizara ya Ardhi jukumu letu ni kuhakikisha maeneo yale yanapangiwa mpango, yanatengwa kwa ajili ya kilimo ili wao waangalie udongo uko namna gani. unafaa kwa kilimo kipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Rais katika hii *program* ambayo wanaendelea nayo ya *BBT* kwa vijana, lakini hili hajalianza leo, tuangalie pia hata kipindi kilichopita, Ofisi ya Waziri Mkuu imekwenda katika halmashauri 117 kati ya halmashauri 184, ikifundisha vijana na wamefundishwa vijana zaidi 12,000 kwa ajili ya kilimo cha kitalu nyumba. Kwa sababu tunatambua vijana wako mjini na vijijini na si wote watakaoweza kwenda vijijini kwa ajili ya kilimo ambacho kinakwenda kufanyika sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndio maana wanawekeza pia, Serikali inawekeza kwenye kilimo cha kitalu nyumba kwa maana ya ile *Green House*. Sasa hawa vijana 12,000 na zaidi ambao wameshapatiwa mafunzo hayo ni jukumu letu katika

halmashauri zetu kuhakikisha kwamba ujuzi ule wanaulea, walioko mjini wakaendeleza kilimo, wanaweza wakafanya kilimo cha *horticulture,* wakati wenzao wanaendelea huku katika vijiji na maeneo mengine, maana yake hawa huku tayari wanao na wanaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nataka kusema kwamba, Serikali inaangalia kwa uhakika namna ya kutumia vizuri ardhi yetu na kutambua na kwa kupima na kwa kuweka mpango madhubuti. Jukumu letu sasa kama halmashauri kama Wizara huko tuliko, tuone namna bora ya kuhakikisha mpango wa matumizi kwa wenye mamlaka za upangaji, tunaipa kipaumbele sekta ya kilimo ambayo ndio sekta inayochukua zaidi ya asilimia 65 ya Watanzania wamewekeza kule. Kwa hiyo hili tutalifanya kwa sababu tunajua ni jukumu letu kama Serikali kuwezesha Watanzania…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, Naibu Waziri wa Kilimo na Mtoa Hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema aliyetuwezesha kufika siku ya leo na kwa baraka zake tele tuko hapa siku ya leo. Pia kipekee kabisa nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa miongozo yao na maelekezo yao katika kutekeleza majukumu ndani ya Wizara ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kipekee kabisa naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri Hussein Mohamed Bashe, Waziri wa Kilimo pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Kilimo kwa ushirikiano mkubwa ambao wamekuwa wakinipatia katika kutekeleza majukumu katika Wizara ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa mbele ya Bunge hili naomba niseme namshukuru sana Mheshimiwa Waziri amekuwa kaka, amekuwa rafiki, amekuwa kiongozi, lakini amekuwa Mwalimu mzuri. Nimejifunza kilimo kupitia yeye na mimi kila siku asubuhi nikiamka saa 12 lazima nisikilize kwenye *YouTube* jambo lolote la Hussein Bashe kwenye kilimo imenifanya nimekielewa vizuri kilimo hivi sasa. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na hoja ya kwanza, hoja ya *BBT* kwamba ni kwa nini hatujaenda Mikoa yote? Tulitoa utaratibu mzuri kabisa ambapo tuliandika barua kwa Mamlaka za Mikoa za kuwataka kutenga maeneo maalum kwa ajili ya *program* hii kubwa ya vijana na wakina mama. Ipo mikoa ambayo ilifanya kwa uharaka na iliandaa maeneo na ikawa rahisi katika sehemu ya kwanza ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kutoa rai kwa Mikoa mingine yote ambayo maeneo yapo kwa ajili ya kilimo kwenda kutekeleza *program* hii ya *BBT,* Wizara tuko tayari kuja kuyaangalia maeneo hayo, tutatuma wataalam wetu na tuko tayari kuanzisha *program* hizi katika maeneo hayo. Lengo letu kubwa ni kuhakikisha tumeifikia nchi nzima kutokana na ikolojia ya kila eneo na hiyo ndiyo maksudi mazima ya *program* hii.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Shinyanga kwa mfano, ukiangalia hapa katika vitabu vyetu haimo lakini Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga namshukuru sana pamoja na Mheshimiwa Mbunge Katambi hapo walishirikiana kwa

pamoja na Wabunge wa Mkoa wa Shinyanga, tulizungumza na Mwekezaji pale Jambo ambaye yeye anazalisha *juice* na ana mahitaji makubwa sana ya maembe, Mkoa wa Shinyanga wanaweza kulima maembe. Ninavyozungumza hivi sasa wameshaandaa eneo na tumeshamuelekeza mtaalam wetu kwenda kupima afya ya udongo, tutakwenda kufanya *BBT* katika Mkoa wa Shinyanga na *off taker* tayari yuko pale ni Jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia Geita wameonesha utayari. Mkoa wa Geita kwenye kilimo cha mananasi na wenyewe wako tayari kwa ushirikiano wa Mkuu wa Mkoa na kwenyewe pia kule tutakwenda, bahati nzuri mananasi ya Geita Jambo ameshayapima na ana uwezo wa kuyatumia kutengeneza *juice,* kwa hiyo soko la uhakika lipo na pale tutakwenda kuweka mradi mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesikiliza hoja za Waheshimiwa Wabunge, wamechangia vizuri sana na kutoa ushauri mzuri sana, liko jambo nataka niliweke vizuri ili lieleweke vizuri. Hapa kuna hoja mbili, kuna hoja ya *program* ya *BBT* na kuna hoja ya mashamba makubwa ya pamoja *(block farms)* haya ni mambo mawili tofauti. Ni sawasawa na kwamba kila Wakili ni Mwanasheria lakini siyo kila Mwanasheria ni Wakili. Maana yake ni hivi katika haya mashamba. Mashamba makubwa ya pamoja siyo lazima yote kuwemo kuna *BBT*. *BBT* ni *program* ya uwezeshaji wa vijana na wakina mama ambao siyo lazima iwekwe katika mashamba makubwa yote ya Pamoja, lakini *BBT* ni mkusanyiko wa eneo kubwa kwa hiyo ni shamba moja au mashamba ya pamoja lakini siyo lazima ya kwamba kila kwenye *block farm* kuna *BBT,* na hapa ndiyo dhana ile ambayo nataka niiseme kwamba watu wanafikiri tumewasahau wakulima wengine na tumewalenga vijana peke yao na wakulima wengine tumewaacha kabisa, hapana.

Mheshimiwa Spika, katika mashamba haya makubwa watakwenda kulima wakina mama, wakina baba, wenye umri ambao siyo umri wa vijana na vijana pia watakuwemo. Kwa hiyo, hoja ya kwamba tumewaacha kabisa hapana. Kwa hiyo nataka niliweke sawa sawa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni suala la umwagiliaji. Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi imetuelekeza kwamba ikifika mwaka 2025 tuwe tuna eneo linalomwagiliwa la hekta milioni 1.2, Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Wabunge mwaka jana mkatoa hoja na ushauri kwamba nchi yetu imejaliwa mabonde, maeneo mazuri, kwa nini hatuongezi eneo la umwagiliaji?

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita ni Serikali sikivu, Mheshimiwa Rais alisikia hoja ya Wabunge juu ya maeneo makubwa ya kimkakati ya kufanya kilimo cha umwagiliaji na Tarehe 20 mwezi Machi, 2023 mbele ya Mheshimiwa Rais, tumesaini mikataba ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika mabonde 22 ya kimkakati ambayo tafsiri yake ni nini? Tafsiri yake ni kwamba tunakwenda kuimwagilia nchi nzima. Mabonde haya ya kimkakati inaanzia katika Bonde la Ziwa Victoria, zaidi ya hekta 20,000. Tunakwenda Bonde la Bugwema, Bonde la Suguti, tunakwenda Bonde la Mto Manonga Wembele, tunakwenda Bonde la Ruhuhu, Bonde la Tumbandiosi, Bonde la Makondeko, Bonde la Lukuledi, Bonde la Mto Songwe, Ifakara Idete, Kilombero, Mkomazi, Rufiji *Basin*, inakwenda mpaka Kasinde, Ngomai. Mabonde haya yote yanakwenda kutengeneza hekta 306,631 za umwagiliaji, ni nchi nzima tunakwenda kuigusa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hiyo tuliona kutokana na mabadiliko ya tabianchi lazima tuhakikishe tunafanya kilimo cha umwagiliaji. Kilimo cha umwagiliaji maana yake nini? Lazima uwe una skimu zinazokusaidia kufanya kilimo mwaka mzima zaidi ya mara moja. Ili uweze

kufanya hivyo lazima uwe na chanzo cha uhakika cha maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha huu 2022/2023 ambao unaishia, tumekwenda na Wakandarasi wako *site* tunachimba mabwawa 14 ya awali ambayo yatatupa mita za ujazo ya maji 131,535,000 ambazo ukizibadilisha ni sawa na maji lita bilioni 131. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyafanya hayo, kwenye bajeti hii ya mwaka huu ambayo Wabunge mtaipitisha hapa, tunakwenda kuchimba mabwawa mapya 100 ambayo yatakuwa yana mita za ujazo milioni 906 sawa na lita za maji bilioni 900. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatuishii hapo, tunakwenda kuchimba visima 150 katika Halmashauri 184. Wako wakulima ambao kwao wanahitaji visima tu kuweza kuongeza uzalishaji, tutafanya Wizara ya Kilimo. Tumejifunza kwa Wabunge wametuambia hapa ya kwamba yako baadhi ya maeneo hatuhitaji visima, hatuhitaji mifereji mikubwa. Tutapeleka pia na pampu katika maeneo ambayo ni karibu na vyanzo vya maji ili wakulima wetu waweze kumwagilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ilizungumzwa hoja hapa kwanini hatuweki nguvu nyingi kwenye mazao ambayo yatatuletea pia fedha za kigeni? Sasa nafikiri tu kuna baadhi ya Waheshimiwa hasa aliyeongea hoja hii Mheshimiwa Halima Mdee nafikiri hakuangalia vizuri humu ndani. Nitampa mfano wa mazao mawili tu, mchele na parachichi ambayo aliisema yeye. Kwenye mpunga, maeneo ambayo tunayategemea sana ni Mkoa wa Mbeya, Wilaya ya Mbarali. Pale Wilaya ya Mbarali tumefanya uwekezaji mkubwa wa miradi ya umwagiliaji. Mheshimiwa Mtega yuko hapa ni shahidi.

Mheshimiwa Spika, pale tuna mradi wa Bonokuva Gigolo, tuna mradi wa *Herman Chosi,* tuna mradi wa Ipolo Isenyela, tuna mradi wa Matebete, ambayo ni miradi ya fedha nyingi na hii yote itakwenda kusaidia upatikanaji wa mpunga wa uhakika kwa nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili kwenye parachichi ambayo aliisema. Kwenye parachichi tunafanyaje? Tumetafuta masoko ya uhakika ya parachichi. Tarehe 25 Novemba, 2021, Mamlaka ya Afya ya Mimea ya India walituruhusu kuingiza parachichi. Tunapeleka parachichi India, tutapeleka parachichi Hispania, tutapeleka parachichi China, Marekani tunamalizia hoja ya *phytosanitary* ili tupeleke kule nako parachichi. Serikali inafanyaje katika kuliandaa hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zao hili linahitaji pia *requirement* ya kimataifa, mojawapo ni usafi wa mazao. Ukienda Arusha, Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu tumepata ithibati ya kimataifa ya usafi wa mazao ambayo itasaidia kupeleka mazao yetu nje ya nchi, pale pia tumefunga mtambo mkubwa tunauita *micro plasma atomic emission spectroscopy* ambao unasaidia kupima usafi wa mazao na zamani mkulima wa Tanzania alikuwa analipa zaidi ya dola 10,000 kwa ajili ya kipimo hicho leo analipa dola 300 kwa ajili ya kupata hati ya usafi wa mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka niseme hapa haraka haraka ni kwenye mkonge. Wabunge mmesema hapa kuhusu mkonge, Wabunge wa Mkoa wa Tanga mmesema vizuri sana, tumesikia hoja zenu. Hoja kubwa ya mkonge ambayo inapelekea mkonge wetu kupata changamoto kubwa ni mkonge mwingi unaoza kwa sababu ya kukosa makorona. Wabunge wa Mkoa wa Tanga mwaka huu mtayaona makorona katika Mkoa wenu wa Tanga kuanza kuchakata mkonge. Tumeshaagiza na *procurement process* inaendelea, korona zile zitakuja na Wabunge wetu

wa Mkoa wa Tanga mtatembea kifuambele, wakulima wenu watapata sehemu ya kwenda kuchakata mkonge wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunataka mkulima wa mkonge wa Tanga aache kuuza *UG,* aache kuuza *SSUG,* aache kuuza *UF*. Tunataka mkulima wa mkonge wa Tanga auze *SL* na *3S*. Hii ndiyo mkonge wa daraja la juu kabisa ambao utampatia fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Nakushukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri zima kisemeo hapo.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimuite Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe na mtoa hoja, Waziri wa Kilimo aje ahitimishe hoja yake.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na nikushukuru wewe na Bunge lako Tukufu kutoa fursa kwa Wabunge wengi kuchangia na pale ilipohitaji hata ratiba ilibadilishwa ili Wabunge waweze kuchangia hoja hii ambayo ni kwa maslahi ya Watanzania wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wamechangia Wabunge 88 kwa ujumla. Kwanza nitumie nafasi hii kuwashukuru Wabunge na niwaambie mwaka jana tulivyo-*submit* bajeti yetu hapa mawazo na ushauri wenu ni sehemu ya kuandaa mpango wetu wa mwaka ujao kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu. Kwa sababu sisi hatuishi *in isolation,* kwenye Kijiji tunaishi na watu na tunathamini sana michango yenu. Nataka niwaambie tu kwamba maoni na ushauri na *critics* zote mnazozitoa kwetu sisi ni sehemu ya *lesson* na niwahakikishie tunazichukua tunaenda kuzifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zipo hoja zilizotolewa na Wabunge nyingi, inawezekana nisizijibu zote. Hoja ya kwanza ambayo nilitaka niseme ni je, tuna uhitaji ushirika? Jibu ni ndiyo. Je, tunahitaji ushirika wa namna gani? Tunahitaji ushirika unaoenda kumsaidia mkulima na wala siyo ushirika utakaomnyonya mkulima. Je, ushirika tulionao ni mtakatifu? Jibu ni kwamba ushirika tulionao una changamoto na ndiyo maana kuna Waziri wa Kilimo, kuna Tume ya Ushirika tuna wajibu wa kwenda kusimamia changamoto hizo. Je, upo ushirika unaowatendea haki wakulima kwenye nchi hii? Jibu ni ndiyo upo. Upo ushirika unaowaibia wakulima? Jibu ni ndiyo upo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hatuwezi kwenda kuua mfumo wa ushirika katika nchi kwa sababu tu tunao washirika ambao siyo waaminifu. Tutachukua hatua na nimhakikishie Ndugu yangu Mbunge wa Mbozi na Wabunge wa Kahawa wa *arabica,* ilituchukua miaka miwili kujadiliana na kuelewana na wenzetu wa *robusta,* leo changamoto zilizoko kwenye *robusta* zimepungua, ushirika una *compete* na sekta binafsi, wanashindana sokoni, tunawapa mitaji, wanaingia kununua na mkulima analipwa fedha yake *on time.* Tutakuja kwenu Mbozi na nimwambie Mwenisongole kwa macho yangu nimeona viongozi wa ushirika wa Mbozi walivyowaibia wakulima wa kahawa na mimi nilimkamata, nikamuweka ndani na timu ya Wizara ya Kilimo imeenda, imetuletea takataka zilizoko. Nikuhakikishie tunaenda kufanyia kazi, wakulima wa Songwe, Mbozi mpaka Mbinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii, Mrajisi wa Vyama vya Ushirika yuko hapa, ni marufuku Chama cha Ushirika kwenda kukopa fedha kabla ya msimu na kusema tunalipa malipo ya awali, halafu mzigo wa riba na gharama za uendeshaji mnaenda kumbebesha mkulima. Hii tabia ife na tutaenda na watu wetu kwenda kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ushirika ni lazima tuuwezeshe. Tunafanya sasa hivi *feasibility study* ya *TANICA*. Tutaenda kuipa *TANICA* shilingi bilioni nane ili kui-*capitalize* iweze ku-*compete* na kuweza kufanya *value addition,* hili linawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni *irrigation*. Je, kuna matatizo kwenye Tume ya Umwagiliaji? Mwenyekiti wa *PAC* ametoka. Nataka nimwambie, taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imekuwa ni sehemu ambayo sisi ni kama *instrument* ya kufanyiakazi. Hatutaki kuwa *hostage* wa matatizo ya mwaka 2017 na 2018, ingekuwa hivyo leo hii kwenye hii nchi kwani *TRC* haikuanguka? *ATCL* haikuanguka? Si zilianguka? Hakukuwepo na ubadhirifu au mambo matatizo yaliyokuwepo? Ni jukumu letu sisi kufanyia, kuchukua hatua juu ya matatizo yaliyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *irrigation* kwenye nchi yetu *as a country* toka mwaka 2000 hatukuwahi kuweka *emphasis* kwenye mifumo ya umwagiliaji na usimamiaji wa umwagiliaji katika nchi hii. Ndiyo ukweli! Tulitenga shilingi bilioni 20 na mimi nilikuwa Mbunge nakaa pale alipokaa Mheshimiwa Tabasam. Fedha haziendi, tunataraji kwamba zaidi ya Halmashauri mia moja na kitu, tunatenga fedha za usimamizi za umwagiliaji shilingi milioni 20. Hakuwezi kutokea muujiza! Ndiyo maana kuna hayo matatizo tuliyoyaona. Aliyaona Mkaguzi wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, tumechukua hatua gani? Hatua ya kwanza Tume ya Umwagiliaji sasa imeenda kuwa na ofisi kila Wilaya. Pili, Mheshimiwa Rais katupa kibali tumeajiri ma-*engineer* sasa hivi wana mwezi mmoja tumewapeleka katika Wilaya. Tatu, tumewanunulia vitendeakazi tumenunua gari 53 tunapeleka katika kila Wilaya. Nne, tumeongeza bajeti na sasa hivi hakuna mradi wa umwagiliaji unaofanyika bila *feasibility study*. Nchi yetu Mwenyezi Mungu kaijalia hekta

milioni zaidi ya 29 kwa miaka 60 tume-*invest only 2.7 per cent* ni aibu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mama Samia kafanya nini? Kasema wekeni *emphasis* kwenye *irrigation.* Kwanza hauwezi kuweka fedha za umwagiliaji bila kutambua maeneo ya umwagiliaji, Naibu Waziri amesema. Tuna maji Ziwa Victoria mita 300 wakulima wanasubiri mvua. Tumefanya nini? Tunafanya *feasibility study* kuanzia Mara mpaka Kagera. Kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu hata asipojenga Samia, atakuja kujenga mtu kwa sababu leo tunajenga *Stigler's* waliofikiri juu ya *Stigler's* na kufanya *feasibility study* na *detailed design* leo hawapo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sisi *plan* zetu kama Wizara siyo za kesho, niwaambie Wabunge kama mnafikiri tunawekeza kwenye umwagiliaji kujenga mifereji ya mita mia mia siyo Wizara hii, siyo Waziri huyu. Tunafikiri kufanya miradi ya umwagiliaji ili tumwagilie kiangazi na masika. Tuna mradi wa 55 *billion* hapo kwa Mheshimiwa Lukuvi. Ule mradi tunaujenga kwa miaka miwili. Mradi ule tu barabara za mashamba ni kilometa 98. Mradi ule mifereji ni zaidi ya kilometa 100. Halafu mnataraji eti kuna hoja hapa kwamba imetengwa shilingi bilioni 300 fedha kwa nini hazijatoka zote? Labda tubadilishe utaratibu tuleteeni pale Wizarani zikae shilingi bilioni 300 na nyie ndiyo mna mamlaka badilisheni Sheria ya Manunuzi hapa, kila kitu iwe *force account.* Haina shida mimi nitaziweka ofisini, bwana eeh, chukua *in advance.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utaratibu ni kwamba miradi yote tuliyoiahidi mwaka jana mpaka kufikia mwezi Aprili, asilimia 70 tumeshasaini na leo ninavyowaambia miradi ya mwisho tumeipandisha kwenye mfumo. Tunaenda Juni 30 hatutakuwa tunadaiwa mradi mmoja. Wakandarasi wote watakuwa *site* na miradi hii inajengwa kwa miezi 18 mpaka 24, mwaka kesho ndiyo ina kamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *phase two* tumesema miradi yote katika haya mabwawa 100 kwa kuwa tunajenga *irrigation scheme* sasa *phase two* kwenye fedha za mwaka kesho tunaanza kujenga mabwawa ili tulime mwaka mzima. Huu ndiyo mwelekeo wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, hapa ameongea Dada yangu Mheshimiwa Halima kasema tunafanya kilimo cha *iPad* na mimi namheshimu. *It is a very good statement,* ni kweli! Tunataka siku moja nchi hii na dunia hii watu waingie *google* wajifunze kilimo kilichofanywa Tanzania. Mimi nashangaa watu wanashindwa kuota, *this is the country* na mimi nataka niwaambie, sisi ndiyo *purity* ya nchi, kama sisi tunawaza kimaskini *we are in trouble*. Niwaambie ukweli! Kama sisi tunawaza kimaskini tena tuna tatizo kubwa mno ambalo linatukabili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna hoja ya *BBT*. Kwanza naomba ni-*clarify*. *BBT* ina-*compete* na wakulima wadogo waliopo? Jibu ni hapana. *BBT* imesababisha wakulima wadogo tuwaweke pembeni? Jibu ni Hapana. *BBT* imesababisha wakulima wadogo wasihudumiwe? Ruzuku ya mbolea ina-*target* wakulima wadogo. Tunavyopeleka Maafisa Ugani, tuna-*target* wakulima wadogo.

Mheshimiwa Spika, kwenye bajeti hii tumeweka fedha kwa ili kila Halmashauri tuchukue wakulima au mashamba 150, tutawachimbia kisima bure, tutawawekea pampu kwa kutumia *solar technology,* tutawawekea *tank* la kuanzia lita 5,000 na tutawawekea *irrigation kit* ya ekari 2.5. Huyu ni nani? Mkulima mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza nataka niwaambie Wabunge wenzangu, ukiona Taifa lolote asilimia 70 ya *population* wako shambani, ni Taifa masikini. Ndiyo *principle* za *economics*. Haiwezekani *the bigger population* iko

shambani ina-*contribute* asilimia 25 tu ya pato la Taifa. Ni *sign of poverty*. Kwa nini? Kwa sababu *productivity* ni ndogo.

Mheshimiwa Spika, tunachotakiwa sisi leo, kwa kuwa sisi tuko shambani, watoto wetu wasiende kulima hekta moja moja. Tujenge uwezo wa-*graduate* kutoka kwenye *agriculture,* waende kwenye *service industry* na maeneo mengine. *Economy* zote zilizokuwa duniani, watu wachache wako shambani, wengi wameondoka. Sasa kipato cha mkulima mdogo ni Shilingi ngapi? Haizidi *1.2* million Shillings kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa nini tumeenda kwenye *program* ya *BBT*? Kwanza nataka niwaambie Watanzania wenzangu, ni aibu kuhoji kwamba kwa nini tumemmilikisha kijana ardhi? Leo anakuja Mzungu kutoka Ulaya; juzi ofisini kwangu ilikuja kampuni moja kutoka China, inataka kuwekeza. *Condition* ya kwanza nimpe ekari 20,000; *condition* ya pili, nimpe *subleasing title* ya miaka 60; *condition* ya tatu, anataka barabara; *condition* ya nne, anataka umeme.

Mheshimiwa Spika, sasa nikimpa Mtanzania hekta 10, nimemwandalia shamba, nimemwekea *irrigation scheme,* nimempelekea umeme, nimempimia afya ya udongo, mnasema, kwa nini tumemilikisha? Wawekezaji wangapi katika nchi hii tumewamilikisha ardhi na hawaitumii? *What is wrong* kummilikisha mtoto wa Kitanzania ardhi? Nauliza hili swali, kuna dhambi gani? Mheshimiwa Halima usiingie kwenye historia ya kuhoji kijana wa Kitanzania ambaye kaenda kurithishwa ardhi…

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**WAZIRI WA KILIMO:** Umechangia, *give me space*.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Usiniwekee maneno.

**WAZIRI WA KILIMO:** Nimesema hivi…

**SPIKA:** Ngoja, ngoja, Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Halima, naomba ukae. Waheshimiwa Wabunge, kwenye ngazi hii, Waziri akiwa amesimama anahitimisha hoja, huwa hakuna taarifa. Kinachoweza kutokea, ukiona kilichojibiwa ni tofauti na ulichokuwa umesema wewe, utatumia kanuni nyingine, lakini kanuni ya taarifa haiwezi kutumika katika ngazi hii.

Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, *out of respect,* hoja imekuwepo tunawatoa Dar es Salaam. Hivi nimuulize *graduate* yeyote aliyemo humu ndani, alipomaliza Chuo Kikuu, *destination* ya kwanza ilikuwa wapi? Nawaulizeni! Mimi nimemaliza Mzumbe, nimeenda Dar es Salaam, sikurudi kwetu kijijini, Nzega. Nimeenda Dar es Salaam, nazunguka na bahasha ya kaki, na kula wali wa shilingi 700 *IFM*. Leo tunahoji, eti kijana aliyeko Dar es Salaam hawezi kulima! Nani kasema kwamba kijana aliyekwenda Dar es Salaam hawezi kulima? Nani? Tumemjaribu wapi? Hawawezi kulima kwa sababu tunataka kuwa-*subject* walime kwa teknolojia za 1960, 1970, 1980, *it is impossible. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini vijana hawalimi? Halafu tunasema sisi viongozi mbele ya Mungu, nami niko *honest, I will push BBT,* aidha nifanikiwe mimi na wenzangu, ama nikaanguke. Siwezi kusubiri, siwezi kuwa mmoja wa viongozi wanaowanyooshea vidole vijana wa nchi hii kwamba kwa nini hawataki kujiajiri? Tunao wajibu. Tuna *moral responsibility* ya kuwatengenezea vijana wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mazingira ya kujiajiri, na ndicho kinachofanywa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii nani anaweza kwenda kununua ardhi ya shilingi milioni mbili, milioni tatu hekta moja? Nani, kijana aliyetoka chuo kikuu? Nani anaweza kutumia Shilingi milioni mbili au milioni moja na nusu au milioni tatu kuweka *drip irrigation*? Yuko wapi huyo kijana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nimpe mfano, nami na-*focus* kwenye hoja ya Mheshimiwa Halima kwa sababu, *let me say,* nasema ukweli.

**MBUNGE FULANI:** Unachagua hoja!

**WAZIRI WA KILIMO:** *Yes,* nimechagua hoja.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hebu tusikilizane. Unapozungumza Waziri akiwa amesimama hapa mbele, unataka aongelee hoja anazojibu au muanze kujibizana? Tafadhali naomba utulivu, Waziri anajibu hoja za Wabunge. Yeye wakati ninyi mnachangia aliwasikiliza, mpeni nafasi na yeye ya kumsikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nataka nitoe hii takwimu. asilimia 74 ya Watanzania walioko mashambani, wana wastani wa ekari mbili. Asilimia 25 tunaowaita *medium size,* wana ekari tano mpaka 20. Tunaowaita *large scale,* wana ekari 20 mpaka 100. Hii ndiyo taswira. Wote hawa wanavuna mara moja kwa mwaka, wanasubiri kudra ya Mungu. Lazima tuondokane na hii hali. Hii hali hatuwezi kuondokana nayo kwa msimu mmoja, au miwili, au mitatu, *is a long-term process.* Lazima tufanye hii kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine niongelee suala la ruzuku ya mbolea. Nakiri kulikuwepo na changamoto za *distribution network.* Tunachukua hatua. Hatua ya kwanza, tunawekeza kwenye *TFC,* kampuni yetu wa Serikali. Kwenye bajeti tumeipa shilingi bilioni 40, mwaka jana 2022 tuliipa shilingi bilioni sita, mwaka huu tumeiongezea shilingi bilioni 40, na sasa hivi tuko kwenye *negotiation* na *funding* kutoka *JICA* ambazo zilikuwa ziende ku-*support* hiyo ruzuku, tutawapa dola milioni 25, itakuwa *capitalized.*

Mheshimiwa Spika, kwa nini tunai-*facilitate* kampuni hii? Tunai-*facilitate* ili tuwe na jicho la Serikali ambalo linaweza kutusaidia kwenye *price discovery* huko nje. Wata-*import* mbolea kutoka huko nje na watanunua kutoka huko nje, lakini *capacity* ya ndani tunaendelea kuijenga.

Mheshimiwa Spika, leo tuna hiki kiwanda chetu cha *INTRACOM* ambacho kinaendelea kufanya kazi, tunatarajia mpaka mwezi wa Kumi kitafika tani milioni moja. Kwa kuwa *program* ya ugawaji wa ruzuku ya mbolea; na kwa nini tunafanya hivyo? Hapa nitaijibu hoja ya Mheshimiwa Mpina.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mpina kahoji kachukua idadi ya wakulima tuliowasajili, kagawa kwa mbolea tulizotoa; nadhani ni katika kuelewa. Kwanza wakulima milioni saba wa nchi hii sio wote wanaotumia mbolea. Matumizi ya mbolea katika nchi hii kwa hekta moja sasa hivi, wastani ni kilo 19. *SADC minimum standard* ni *50 kg*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa nini kuna tatizo la matumizi ya mbolea? Elimu, hilo la kwanza; la pili, taarifa ya afya ya udongo; la tatu, ni *availability* na *affordability.* Kwa hiyo, Serikali inaweka ruzuku ili bei iweze kushuka. Siyo sahihi katika hoja yake, nami nimeichukua hoja yake hapa, ninayo, kanipa yeye mwenyewe kwa maandishi. Kuna mambo kama manne kayataja. La kwanza, kasema mfumo wa usajili na mfumo wa ruzuku haukupata *approval* ya Serikali, umeenda

kinyume na utaratibu. Nataka nimwambie, tumepata *approval* ya Katibu Mkuu Kiongozi, tunayo *approval ya e-GA;* tarehe 26 Juni, tulipata *approval* ya *e-GA,* na tarehe 16 Julai vilevile Katibu Mkuu Kiongozi aliwaandikia *e-GA* kuwasiliana na Wizara ya Kilimo kwa ajili ya kutengeneza mfumo wa ruzuku ya mbolea. Barua hii hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni vizuri, nami nataka nimshauri, na ninajua ameenda hadi *e-GA*. Namwomba kwamba kwa mila zetu hasa sisi tunaotoka huko maeneo ya wafugaji, ni vibaya sana mtu ambaye umefika katika *level* ya uongozi, kuongea mbele ya Baraza ku-*accuse* mambo ambayo huna *facts.* Nataka nimwombe, *next time* akiwa na jambo linalohusu Wizara ya Kilimo, mlango wangu uko wazi sana. Saa yoyote njoo, tutakusikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja yake ya pili ni kwamba, mfumo wetu ulikuwa haufai, kuna *double scanning*. Sasa tumegunduaje mfumo kwamba huyu mtu ka-*double scan* kama mfumo wetu hautoi taarifa? Mfumo wetu unatupatia taarifa, mtu yeyote atakaye-*temper* na *system;* na wizi uliokuwa unafanyika, na Bunge hili litumike, uko wa aina nyingi. Mkulima alikuwa akifika dukani, akichukiliwa namba yake ya kusajili na *Agro-dealer,* leo *allocation* yake ni mifuko kumi, akilipa mitatu, akiondoka, kwa kuwa *Agro-dealer* kabaki na ile namba, anaitumia tena ile namba, meseji inaenda kwa mkulima, mkulima anapiga *call center* ya Wizara ya Kilimo. Sisi tunafanya *tracing*.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi wanaendelea kuhojiwa. Kuna wengine wamefika, tumewakamata walikuwa wame-*double scan* mbolea za zaidi ya shilingi milioni 100, wanasema naomba nisamehewe, hiyo shilingi milioni 100 ifutwe, tuendelee. Nataka niwaambie, tulianza tukiwa hatuna mfumo wa kumtambua mkulima nchi hii. Tumeanza safari, sasa tumefika wakulima milioni tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie Bunge lako tukufu kuwaambia wakulima, tarehe 01 mwezi huu wa Tano, *TFRA* ilitangaza wakulima kwenda kujisajili na ku-*update data* zao. Nendeni mkajisajili, mwendelee kutoa taarifa zenu sahihi, mfumo utaendelea kuwa *updated,* na *process* ya kusajili wakulima ni ya mpaka mwaka 2025. Tutakamilisha kumjua mkulima jina, *GPS* ya shamba lake, afya ya udongo wa eneo lake, na kujua mazao anayolima, na kuwa na taarifa sahihi. Kwa muda mrefu tumehudumia wakulima tusiowatambua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, gharama za mradi wa *BBT*. Wastani wa shilingi milioni 16 kwa hekta. Kwanza, nilitaka niseme jambo moja. Hekta moja ni ekari 2.5, nasi hatuchukui mashamba yaliyoandaliwa, tunachukua mapori, ambapo tunaenda kusafisha. Kusafisha hekta moja ya pori, ni wastani wa *1.5 million shillings.* Gharama hizi za shilingi milioni 16, zinahusisha kusafisha, kupima afya ya udongo, gharama ya kupima shamba, ni wastani wa shilingi milioni mbili. Huyo anayekuja, hawezi kuzilipa hizo gharama. Sisi ndiyo tunaolipa gharama za upimaji wa haya mashamba. Tuna-*include* gharama za kupanda, tuna-*include* gharama za kupima afya ya udongo, tuna-*include* gharama za teknolojia itakayotumika, *whether* ni *sprinkler* ama ni *drip irrigation* kama kwenye maeneo ya mabonde kama kule Membe, tunakotumia *canal technology.*

Mheshimiwa Spika, siku ya mwisho tunapomkabidhi huyu kijana gharama ya hekta moja ambayo ni ekari mbili na nusu, ni karibu Shilingi 16,700,000. Ukigawa, haizidi Shilingi milioni saba kwa ekari. Ni muujiza gani? Mheshimiwa Halima analima pale panaitwa Ihanga, ndiyo mfano wangu leo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, yeye mwenyewe ameshindwa kuweka *the best technology* za *irrigation,* anatumia zile za vijungu, zile *traditional.* Mmenielewa! *This tells the costs* ya

*investment*. Mmenielewa lakini? *This tells the costs of investment* kwamba shilingi milioni 16 *is nothing*. Shilingi trilioni moja, tukichukua hekta milioni moja kwa ekari milioni 2.5; shilingi trilioni 16 tukiajiri vijana 250,000 na *scientifically* imedhibitika kwamba ajira moja ya shambani inatengeneza ajira sita kwenye *value* ya *addition*; gharama ya kutengeneza hizi ajira, ni shilingi milioni nane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii jamani ni *simple economics* siyo muujiza, ni namba. Je, tunatarajia kunaweza kukatokea changamoto? Inawezekana kabisa. Sasa hivi tunafanya mikoa mingapi? Dodoma, tunafanya Njombe ekari 80,000, tunafanya Singida, tunaenda Geita, tunaenda Shinyanga, kote huko tunaenda. Tumepokea maoni yenu kuhusu namna ya kuwapata vijana. Tutaenda kuyafanyia kazi. Hili tutaenda kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine la mabadiliko kwenye Tume ya Umwagiliaji, tunakuja na sheria, inaitwa *Tanzania Irrigation and Extension Development Authority.* Kwa sababu tunapeleka vitendea kazi, tunapeleka watu, lazima tuwe na mamlaka yenye kuwajibika kusimamia shughuli hizi.

Mheshimiwa Spika, kulitolewa wazo la kuwepo na mfuko wa umwagiliaji. Sheria ipo. Tumeanzisha *Irrigation Development Fund,* tumepata shida kwenye ukusanyaji wa maduhuli, na ziko sababu. Tumeamua kwenda kuzifanyia kazi hizo sababu, kwa sababu hatukuwa na mfumo wa *registration* wa *scheme* za nchi. Sasa hivi tunafanya *registration* ya *scheme* zote za nchi. Hatukuwa na mfumo wa kuwasajili wakulima walioko kwenye *scheme,* sasa hivi tunafanya shughuli ya kusajili wakulima walioko kwenye *scheme*.

Mheshimiwa Spika, niliombe Bunge lako Tukufu kwamba tusi-*condemn* vijana wa nchi hii. Tusiumie kwa nini mtu amemiliki ekari 10. Nchi hii ina jumla ya hekta milioni 44

zinazofaa kwa kilimo. Tulizotumia hazizidi hata milioni 15, bado ardhi ipo. Tuhangaike kuongeza tija ya uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, suala la mbegu, ni kweli, kama nchi tuna tatizo la mbegu. Mahitaji yetu ya mbegu ni jumla ya tani 670,000. Tunazalisha asilimia 10, Serikali inachukua hatua gani? Kwanza, tumeanza kuweka miundombinu ya umwagiliaji kwenye mashamba yetu yote ya mbegu.

Mheshimiwa Spika, pili, tunaihusisha sekta binafsi ya nchi yetu kwenye uzalishaji wa mbegu na tumeanza kuwapa mashamba. Tumewapa pale Mbozi, na mwaka huu wamezalisha tani 7,000. Tatu, tuna-*acquire land* kama Serikali ili tuweze kuwa na ardhi tunayoihitaji ili tujitosheleze kwa mbegu. Nchi yetu inahitaji jumla ya hekta 360,000 za kuzalishia mbegu.

Mheshimiwa Spika, lingine, tunawekeza kwenye utafiti, naongelea *issue* ya kuwepo kwa maabara za *tissue culture,* kwa watu wa Kagera kwenye eneo la kahawa. Tunapeleka pale maabara Maruku, tunaenda kuweka maabara kwa ajili ya *tissue culture* ya migomba na *tissue culture* kwa ajili ya kahawa.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine, tunapima afya ya udongo wa nchi. Niseme tu jambo moja. Hapa ndani, niwaambieni, hili ndiyo Bunge na sisi ndio Watanzania, na Watanzania wote wajue. Taifa letu toka tunapata uhuru, suala la kupima afya ya udongo, tulikuwa tunategemea makampuni ya mbolea na *donors*, haiwezekani. Serikali imechukua hatua gani?

Mheshimiwa Spika, kwanza, tumetengeneza mfumo wetu, tumeshaanza na sasa hivi kupima ramani kwa ajili ya kuangalia *acidity level* kwenye nchi yetu. Hiyo ni ramani ya nchi yetu na hali ya afya yetu ya udongo, lakini *database* hiyo tunaimiliki wenyewe, tunatengeneza mfumo wa

kuhifadhi taarifa za upimaji wa afya ya udongo ili tuweze kujua mbolea sahihi unayoipeleka Nzega *is a process* siyo jambo la usiku mmoja.

Mheshimiwa Spika, la tatu; uwekezaji kwenye *infrastructure* za umwagiliaji tutatumia maji ya Ziwa Victoria wala siyo aibu, tutatumia maji ya *Lake* Tanganyika wala siyo aibu tutatumia na tumeisha tangaza. Sasa hivi *feasibility study* zinaanza kufanyika na mwaka huu unaokuja katika mabonde yenye jumla ya hekta 306,000. Mwaka huu unaokuja kwa sababu *feasibility study* zinafanyika ndani ya mwaka huu wa fedha wa 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka kesho tutaanza kujenga hekta 300,000 katika kila bonde ndiyo muelekeo wa Serikali. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge, *transformation* ya *agriculture* naweza nikasema *with confidence* baada ya Mwalimu Nyerere mimi nakuwa mkweli. Baada ya Mwalimu Nyerere ni Serikali ya Awamu ya Sita ndiyo imeamua kwenda kuwekeza kwenye maeneo ya msingi ya kilimo ndiyo ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mwalimu kaondoka kaacha mashamba 17 ya mbegu ni yaleyale *sixty years* Mwalimu kaondoka kaziacha maabara zilezile. Leo ndiyo tunawekeza kwenye maaabara za utafiti, leo ndiyo tuna *expand* tunaanza kufungua mashamba kwa ajili ya kuweka miundombinu ya umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho *program* ya *BBT* inahusisha kwenda shambani, inahusisha kutoa *financing* kwa vijana walioko kwenye mashamba ambao hawamo ndani madarasa sasa hivi. Mwezi uliyopita tumewapa vijana *two hundred million* walioko mashambani ambao hawawezi kwenda kukopeshwa na taasisi za fedha. Tumeweka *eighty hundred million* katika mfuko wa pembejeo tutawapatia

hawa vijana ambao wanafanya shughuli za kilimo mashambani na wanaofanya *value addition. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongelee *issue* ya ngano na alizeti. Eneo la alizeti tumesambaza mbegu na nataka niipongeze taasisi yetu ya *ASA* mbegu walizosambaza safari hii *satisfied seed* zimeweza kuleta matokeo mazuri na uvunaji umeanza.

Mheshimiwa Spika, ninajua wakulima wa alizeti kuna anguko la bei, nataka niwaambie hivi tunampelekea Mheshimiwa Rais barua ombi la kututeulia Mwenyekiti wa *COPRA* Mamlaka inayosimamia *cereals* na *other produce*. Ambayo kwa mujibu wa sheria hii ndiyo itatoa masuala ya bei elekezi, tutatoa bei elekezi ya alizeti *clearly*. Hatua ya pili tunawasilia na wenzetu Wizara ya Fedha tumewaomba tuongeze kodi ya mafuta yanayotoka nje ya *refine* kutoka asilimia 25 kwenda asilimia 35 na wachajiwe *VAT* ya asilimia 18. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la ngano sisi tuna *import* ngano tani milioni moja kwa mwaka. Ili tujitosheleze ngano tunahitaji tani 50,000 za mbegu za kwenda kumpa mkulima alime tumechukua hatua gani? Tumeanza kuzalisha mbegu mama, sasa tunazalisha mbegu za *pre basic,* tunaenda kuzalisha *basic seed* 2025/2026 tutazalisha mbegu kwa ajili ya wakuwapelekea wakulima. Tumewaandikia makampni ya ngano yote kwamba waingie *MOU* na Serikali kwamba kabla ya ku–*import* watanunua ngabo ya ndani kwanza, wamekataa mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme mbele ya Bunge lako Tukufu, niseme mbele ya Wabunge na mbele ya watanzania kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu 2025/2026 tunaenda kuzalisha ngano mwenye mamlaka ya kuwapa cheti cha ku–*import* ngano ndani ya nchi ni Waziri wa Kilimo. Kama takuwa kwenye kiti viwanda vitageuka chuma chakavu

hawatoingiza hata kilo moja kama hawajanunua ngano ya ndani ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watanzania hawatokufa kwa kukosa ngano, haiwezekani unambembeleza mmefanya nao *trial*, tumewapa mbegu wao wenyewe kwenye maabara zao. Wamesema inafaa alafu wakati wa kusaini *MOU* wanasema hatutaki *over my dead body* watasaini mkataba, wasipo saini hatutowapa *phytol-sanitary* kuingiza ngano watajua watakachofanya na viwanda vyao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haiwezekani 1970, 1980 asilimia 80 ya ngano ya nchini, hii ilikuwa inapatikana ndani tulifungua mipaka. Kwa hiyo, hili walifahamu tutaufunga Mkoa wa Manyara, tunafanya *pilot* Njombe, tumeona matokeo ni mazuri, tutaweka *cluster* na sasa tumeishaamua kuwa na korido za mazao. Kuna mazao tutazalisha maeneo maalum maeneo mengine hatutoyaruhusu kuzalishwa ili tuweze *economies of scale. (Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, dakika mbili malizia.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kusema kitu kimoja, bila kuongeza tija kila siku tutakutana hapa bei ya mkulima mbaya, bei ya mkulima juu bei ya nini. Lazima tuongeze tija, lazima tumiliki mbegu zetu wenyewe, lazima tuwekeze kwenye umwagiliaji na ni lazima tuwekeze kwenye skimu za umwagiliaji siyo mifereji ya umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kufanya hivi tunahitaji kuwekeza kwa muda mrefu na huu ndiyo muelekeo sahihi kokote kule duniani. Lazima tufungue mashamba ya kuzalisha mbegu, lazima tuhakikishe tunaiwezesha sekta yetu binafsi ya ndani na kwenye bajeti tumeweka bilioni 10 ambayo tutawapatia wafanyabiashara wa kitanzania wanaobangua korosho, wanaoongeza *value addition* kwenye zabibu,

kuwanunulia vifaa kwa ajili ya kununua mazao ya wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, nataka niwaambie vijana wa kitanzania Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amedhamiria kuwafanya wamiliki nyenzo za uzalishaji na kuwamilikisha ardhi. Tutawekeza kwenye eneo la kuwamilikisha ardhi, tutawasapoti waweze kufanya shughuli zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho niwaambie Waheshimiwa Wabunge maoni yenu tutaendelea kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsanteni, natoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, tunaendelea.

Katibu.

**NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tuketi.

Katibu.

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 43 – Wizara ya Kilimo**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*…..........………...Sh. 6,594,823,000

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kifungu hiki kina Mshahara wa Waziri. Kuna majina hapa ya Wabunge, ambao wanataka ufafanuzi juu ya jambo mahususi na la kisera, Mheshimiwa Francis Isack Mtinga.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi hii. Katika mchango wangu juu ya zao la mkonge nilieleza kwa kirefu jinsi ambavyo uzalishaji na uingizaji wa nyuzi za plastiki zinavyo athiri na kutishia kuuwa zao la mkonge kama ilivyotokea miaka ya 65 mpaka 90 katika majibu ya Waziri na Naibu wake sijaridhishwa na sijasikia kabisa juu ya *commitment* ya Serikali katika kupiga marufuku uzalishaji na uingingizaji wa nyuzi hizi katika vifungashio vya vyakula. Naomba Serikali inipe *commitment* na kama sijaridhishwa nitashika shilingi ya Waziri. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu nimwambie Mheshimiwa Francis Isack kwamba hana sababu ya kuishika shilingi ya Waziri katika eneo hili. Kwa sababu tumeishakaa na wenzetu Wizara ya Viwanda na Biashara na wenzetu wa Wizara ya Mazingira wanafanyia mapitio ya baadhi ya kanuni ili tuone namna gani tunaweza kuchukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya kumlinda mzalishaji wa katani sasa hivi asilimia 50 ya gunia tunazonunua kwa ajili yaku–*export* korosho tunanunua gunia za katani za ndani ya nchi. Kwa hiyo, tutaendelea ku–*observe* na tunafanya kazi kwa karibu na wenzetu wa mazingira ili tuweze kutatua hili tatizo hasa zile kamba za katani za kushonea kwenye magunia. Kwa hiyo, ninaomba atupe tu muda tutaendelea kulifanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis Mtinga, naona umesimama.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya Mheshimiwa Waziri yanatia moyo kama ambavyo yametokea mara nyingi sijaridhishwa vizuri na majibu haya naomba Wabunge wenzangu waniunge mkono jambo hili tulijadili kwa muda mfupi.

**MWENYEKITI:** Hoja haijaungwa mkono. Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Katika mchango wangu nilioutoa jana nilieleza masikitko yangu kuhusu wakulima wa kahawa ya arabika ambayo, kahawa hii inalimwa katika Mkoa wa Mbeya, Songwe na Mkoa wa Ruvuma. Wanachajiwa shilingi 200 kwa kilo na bodi ya kahawa, wakisema hizo ni za kuendeleza zao la kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa robusta nchini wanachajiwa shiingi 100 na nilihoji kwa Mheshimiwa Waziri nilitegemea angenipa majibu. *Logic* ya hawa wakulima wa arabika kutozwa shilingi 200 na nilihoji Mheshimiwa Waziri aniambie mchango wa bodi kwa wakulima wa arabika ni nini? Kwa sababu hawa wakulima wanapokuwa wanaenda kununua miche bodi haipo, wanapo hangaika kupanda bodi ya hahawa haipo…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa George Mwenisongole, ile 200 ni kwa ajili ya bodi?

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo inachukuliwa na bodi na kwa ajili ya kuendeleza zao la kahawa.

**MWENYEKITI:** Kwa sababu kifungu hiki ulichosimama kinataka hoja moja tu na mahususi. Sasa hapo umesema kuhusu bei kwamba huku ni 200 kwingine 100 ndiyo maana

nakuuliza hili unaloendelea nalo la kuhusu bodi lina uhusiano na hiyo shilingi 200? Hiyo 200 ni bodi ndiyo inapewa?

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Ndiyo, bodi inapewa.

**MWENYEKITI:** Haya malizia hoja yako.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hao bodi wanachukua hiyo 200. Wakati wa robusta wanachajiwa 100 wa arabika wanachajiwa shilingi 200. Sasa nikahoji muendelezo *logic* ya hiyo bodi kuchajiwa hiyo shilingi 200 ni nini? Wakati awatoi msaada wowote kwa wakulima wanaendeleza kitu gani? kitu ambacho Waziri ajanipa majibu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa. Sasa hoja yako kwa Waziri ni nini?

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba hiyo shilingi 200 ni kubwa sana kwanini basi isiwe shilingi 100 kama wakulima wa robusta wanavyochajiwa au iondolewe kabisa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni *acknowledge* hoja ya Mheshimiwa George. Cha kwanza kinachochajiwa ni shilingi 100 na anayelipa ni mnunuzi ndiyo maana nimesema wakulima walioko Mkoa wa Songwe, Mbeya na baadhi ya maeneo na Mbinga wanakabiliwa na changamoto ya mfumo wa ushirika.

Mheshimiwa Spika, nime–*commit* hapa kwamba tutaenda kulifanyia kazi kwa sababu halina mahusiano na mkulima anaetakiwa kulipa ni mnunuzi na ni shilingi 100 ya kahawa ghafi *challenge* iliyoko upande wa Nyanda za Juu Kusini vyama vya ushirika vimehama kwenye *function* yake ya

msingi vimeamua kuwa mkulima, *aggregator*, *CPU owner* na *exporter* wenyewe. Kwa hiyo, kama wanafanya kazi ya *exportation* haitakiwi hiyo tozo achajiwe nani? Mkulima. Kwa hiyo, nimewahaidi hapa tunaenda kulifanyia kazi na wala siyo shilingi 200 ni shilingi 100. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa George Mwenisongole, haya naona ameketi kwa hiyo amekubaliana na hoja? Naona umesimama tena.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimelizika na majibu ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Cecil David Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa hii nafasi swali langu kubwa ni la kisera kama ambavyo umetuelekeza. Mheshimiwa Waziri katika hizi siku mbili alikuwa akitoa hotuba yake na sisi kama Wabunge tumechangia sana lakini hatukupata nafasi nzuri sana ya kwenda *deep* kwa sababu ya muda na tulikuwa watu wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *value addition* Wabunge wengi waliyochangia wamekuwa wanaleta malalamiko yao na ushauri sana kwenye masuala ya *value addition* eneo ambalo linahitaji Mheshimiwa Waziri atupe maelezo ya kina. Kwa sababu mpaka sasa tumeshuhudia kwenye zao la korosho halifanyi vizuri sana kwenye soko kwa sababu hatuliongezei thamani hapa kabla halijaondoka na kwenda nje na mnyororo mzima. Tunapata hofu mambo haya yasije yakatokea kwenye parachichi kwa sababu tunalenga kwenye ku–*export* zaidi badala ya kutumia hapa nchini au kuzipa thamani na kuzi–*export*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile pia tunaona kwenya kahawa hivyo hivyo sasa hii isije ikatuathiri lakini tuone na

muunganiko wako kwa maana ya Wizara ya Kilimo itakavyofanyakazi sambamba na Wizara ya Viwanda na Biashara kwenye masuala haya ya *value addition* pamoja na masoko. Kwa hiyo, tunataka Mheshimiwa Waziri atueleze kwa kina anakusudia kufanya nini kuongeza thamani ya mazao badala ya kuwaza masuala ya *export* kila mara ili kuweza kuyaongezea thamani yake hapa hapa nchini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukua hotuba niliyoisoma ukurasa wa 169 tumeongelea suala la *value addition*. Tunachukua hatua gani? Ni kweli anavyosema kwamba kutegemea kuuza *raw export* maana yake tuna *export* ajira na tunakuwa tunaathirika sana na *fluctuation* zinazotoke sokoni. Lakini tunapofanya *value addition* ni kweli inaongeza thamani ya lile zao na itamafanya mkulima siku ya mwisho aweze kupata bei nzuri ya soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hatua gani tunachukua? Mfano kwenye zao la korosho alilolisema mwaka huu tumeweka shilingi bilioni 10 na tumejiwekea lengo 2025/2026 korosho za nchi hii zote zitabanguliwa ndani ya nchi na Serikali inaenda ku–*support private sector* iliyopo kwenye eneo lile kwakuwapa *support* za *incentive* za kikodi, kwa kuwapa *infrastructure development* hiii ndiyo hatua tunayochukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye zao la parachichi kama alilotolea mfano tunaanza sasa hivi programu ya kujenga *common use facility* katika maeneo ya nyanda za juu kusini, kwa maana ya Mkoa wa Njombe, Mkoa wa Iringa na vilevile Kilimanjaro na tumeshamaliza hizo *detail design* na kazi hizo zimeishatangazwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa mwenyekiti, kwa hiyo tunaweka hizo *infrastructure* na hatutoendesha Serikali sisi tutajenga halafu tutazitangaza, tutawapa sekta binafsi za kitanzania waweze kufanya hizo kazi za kuongeza thamani ya mazao. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecil Mwambe, naona umesimama.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana anayoyatoa Mheshimiwa Waziri kwenye hili jambo lakini kama ambavyo nilisema toka mwanzo kwamba tunapanga hapa mipango mizuri sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecil Mwambe, kwa ngazi hii unaeleza kama umekubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Waziri, ama hujakubaliananayo? Halafu tunasonga na utaratibu mwingine.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naridhika na majibu yake *with doubt* tutatafutana nje na kuyajadili.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la zabibu ni miongoni mwa mazao ya kimkakati, lakini kwa bahati mbaya zao hili limekuwa halina bodi; na kutokana na kutokuwa na bodi kumekuwa na *irregularities* mbalimbali kuanzia kwenye kulima, uvunaji, masoko na hata uandaaji wa *wine*. Lakini pamoja na hivyo vile vile zao hili linakabiliwa na mvinyo unaotoka nje ambao unakuja kuharibu soko na uzalishaji wa zabibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ipo *cartel* kubwa kwenye zao hili la zabibu kutokana na kutokuwa na sheria zinazo-*regulate* namna ya kulikuza zao hili. Naomba

*commitment* ya Waziri, na Mheshimiwa Waziri naomba bodi, nimeomba muda mrefu, naomba unipe bodi ya zabibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Nilikuwa natafakari hapo kama hilo ni swali la kisera ama ni swali gani, maana kama na wewe umeshaomba mara kadhaa. (*Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Waziri nimeona unataka kusimama kutoa ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge, amekuwa mfatiliaji mzuri sana katika eneo hili. Ni kweli katika ulimwengu huu tulionao ukiondoa nchi ya Mexico, Dodoma peke yake duniani ndio una uwezo wa kuvuna zabibu mara mbili na zao hili lina tija sana. Lakini kwa hoja ambayo ameisema Mbunge, nataka tu nimuondoe hofu ya kwanza tumechukua hatua. Kwanza kabisa tumekutana na vyama vya msingi vyote 11 kwa lengo la kutengeneza mfumo mzuri kuanzia hapo kwenda mbele; kwa maana ya kuanza kuwa na muunganiko wa vyama halafu kuunda chama cha upili, chama kikuu ambacho tarehe 11 Novemba, 2022 tulikaa kikao. Tayari tumeshaanzisha *Dodoma Regional Cooperative Union (DORECU)* ambayo sasa ni safari ya kwenda huko ambako alipopasema Mheshimiwa kwenye bodi. kwa hiyo hatua tumezichukua.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nollo naona umesimama.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushika shilingi, sijaridhika. Ushirika ni kitu kingine, bodi ni kitu kingine. Natoa hoja.

**MWENYEKITI:** Hoja haijaungwa mkono. Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti,

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja ili iungwe mkono iweze kujadiliwa inaungwa mkono na Wabunge kumi sio Mbunge mmoja, wawili, wala watatu. Kwa hiyo alisimama mwenye hoja na huyo aliyesimama sasa. Kwa hiyo kumi ninyi mmewatoa wapi mnaohesabu? Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Mimi naomba kupata ufafanuzi tu wa Mheshimiwa Waziri kuhusu kuunda mfuko wa bei ya wakulima wa zao la pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu sasa wakulima wa pamba wamekuwa na shida ya bei kila mara. Na tunavyoelewa kampuni nyingi zinazofanya biashara ya pamba katika nchi yetu zinafunga mkataba na kampuni za nje; kwa maana msimu ujao watauza kwa bei fulani. Sasa, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ya kuweka bei elekezi mwaka jana kwa mfano kulikuwa na bei ya kuanzia shilingi 2,000 na kuendelea. Mwaka huu kumekuwa na 1,560. Kwa hiyo wakulima wa pamba kila mara wanapata bei nzuri wanalima sana, wakilima sana bei inakuwa ndogo, wakilima hivi inakuwa hivi, na wanajua gharama za kuendesha shamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilitaka kupata ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri, kwamba ana mpango gani? Anipe mpango mkakati wa Serikali wa kuunda mfuko wa kulinda bei ya wakulima wa zao la pamba ambayo kwa

wazungu tunaita *benefit of price stability,* tunaunda lini? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kwanza kutoa ufafanuzi kwenye hoja aliyoitoa Mheshimiwa Getere. Ni kweli si tu suala la pamba, mazao mengi yanakabiliwa na *fluctuation* ya *prices*. Bunge lako Tukufu mwaka jana wakati tunapitisha bajeti hapa ambayo tunaitekeleza mwaka huu tuliomba hapa kuanzishwa kwa *Agricultural Development Fund,* Bunge likatupitishia kwenye mabadiliko ya Sheria ya Fedha, kanuni zimetoka Waziri wa Fedha kama wiki moja iliyopita ameshasaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mfuko huu utahusika na *fuctions* tatu. Moja, *stabilization;* pili, itatumika kwa ajili ya *Infrastructure Development;* tatu, mfuko huu utahusika kwa ajili ya kutoa *Input Support.* Kwa hiyo hili jambo Serikali imeshaanza kulichukulia hatua na tumeshaanzisha huu mfuko na tumeanza kuutengenezea utaratibu wake.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Getere naona ameketi. Kwa hivyo ameridhika na majibu yaliyotolewa. Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwashauri Waheshimiwa Mawaziri, kwamba wajibu maswali wanapoulizwa wala wasibebeshe lawama wauliza maswali. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina, muda huu si wa kujibu alicho...

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti…

**MWENYEKITI:** Ngoja tusikilizane kwanza. Muda huu tunajadili kifungu hiki chenye mshahara wa Waziri na una hoja mahususi. Sasa hapo ukianza hoja nyingine, maana ya kwanza maana yake umeshaisema, kwa hiyo hoja yako ni hiyo unayomwambia Waziri ama una hoja nyingine kwenye hapo? Ndiyo maana nakukataza hii sehemu ya mwanzo ili uelekee kwenye hoja yako inayohusu kifungu.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumza kwa uchungu mkubwa juu ya mfumo wa mtandao ambao unatumiwa na Wizara ya Kilimo katika utoaji wa mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kufanya *multiple scanning* ni suala ambalo unaweza, kama mfumo unaruhusu kufanya *multiple scanning* maana yake kwamba hauna *security* hauna usalama. watu wa *e-GA* hawawezi kutoa *clearance* ya mfumo ambao hauna *security,* na mfumo ambao hauna *security* unaweza ukatengeneza malipo hewa, mfumo ambao hauna *security* unaweza ukaibia watu. Huu mfumo umeenda kuwanyima watu wengine mbolea. Tumesema hapa 2,200,000. Huu mfumo umekuwa ukichelewa ku-*left* kiasi kwamba mtu mwingine mtafuta mbolea anaweza akachukua mbolea hata kwa zaidi ya mawakala watatu wanne, lakini mfumo huu umewalazimisha wananchi kutoka kijijini kuja wilayani kuchukua mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wameathirika kwa kiwango kikubwa sana na mfumo huu wa mtandao wa mbolea ulioandaliwa. Mimi nikasema kwa uhakika kwamba *e-GA* hawawezi kutoa *clarence* ya mfumo ambao hauna *security*.

**MWENYEKITI:** Sawa, ngoja nielewe hoja yako. Hapo umeshasema hoja mbili. Hoja ya kwanza *e-GA* haijatoa kibali

kwa Wizara ya Kilimo, hiyo ni hoja ya kwanza. Hoja ya pili, mfumo unaotumiwa na Wizara ya Kilimo hauna usalama. Hizo ni hoja mbili tofauti. Hoja yako ni ipi kati ya hizo? ili nimwambie Waziri afafanue. Hoja yako yaani chagua moja wapo, kwa sababu kanuni yetu hapo uliposimamia inataka hoja moja mahususi ya kisera. Chagua moja kati ya hizo mbili.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu hapa mahususi ni kwamba, ni nani aliyetufikisha kwenye hili tatizo kubwa, ni nani aliyetufikisha kwenye hili tatizo kubwa la kuwa na mfumo ambao hauna usalama? (*Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Haya ashante sana.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kidogo tu li ni - *connect* pale ulipo…

**MWENYEKITI:** Wewe si unamtaka utajiwe? Ngoja uatajiwe. Halafu utasema umeridhika na huyo uliyetajiwa au Hapana. Si ndilo swali lako? Wewe umesema ni nani, kwa hiyo hoja yako imekamilika kiabisa. Mheshimiwa Waziri ni nani aliyewaruhusu ninyi kilimo kuwa na huo mfumo mliotumia? Jibu ni nani? (*Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mpina amekuwa ndani ya Serikali na anajua utaratibu. *Approval*…

**MWENYEKITI:** Wewe niambie tu ni nani, ndilo swali lake.

**WAZIRI WA KILIMO:** …*approval* kwa ajili ya kutekeleza mfumo wowote. *Either* mfumo huo unafanyika kwa mfumo wa *PPP* ama mfumo ambao umetengenezwa ndani ya Wizara husika ni *e-GA,* na sisi Wizara.

**MWENYEKITI:** Naomba hiyo barua; yuko wapi yule, mhudumu yuko wapi? Naomba ile barua. Mheshimiwa Mpina jibu lako umetaka ufafanuzi kutoka kwa Serikali, umeuliza ni nani? Haya ni *e-GA*. Barua ya tarahe 16 Julai, 2022, na ameandikiwa Mkurugenzi Mtendaji Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea *TFRA*, Mtaa wa Kilimo S.L.P Dar es Salaam. Haya umeshajibiwa ni *e-GA*. Haya naona umesimama. (*Makofi)*

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, hili tatizo ni kubwa na ninawaomba Wabunge wenzangu waniunge mkono ili nikamate mshahara wa Mheshimiwa Waziri na jambo hili tulijadili kwa kina…

**MWENYEKITI:** Ngoja, unajua tunaenda hatua kwa hatua. Umeomba kuungwa mkono kwenye hoja yako, na mimi nimegeuza kichwa upande huu namuona mmoja na wewe mwenyewe umeshakaa. Kwa hiyo hoja haijaungwa mkono**.** *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge nimetoka kuwakumbusha hapa sasa hivi; kama ambavyo ilivyo kwa Serikali, Waziri akishasema natoa hoja huwa mnawaona wamesimama, huwa hakuna nafasi ya kusubiri kwa sababu unataka hoja iungwe mkono, ndio utaratibu wetu. Huanzi kusubiria, yaani nani anayekushawishi sasa, maana yake hujashawishiwa na kilichosemwa ndio maana hujasimama. Kwa hiyo Mheshimiwa Esther Edwin Malleko.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Wakati ninatoa mchango wangu jana niliomba ufafanuzi juu ya namna gani katika nchi yetu tunaweza kupata masoko, kwa sababu kumekuwa na uhaba mkubwa wa miundombinu ya masoko ambayo inasababisha watu kupata shida katika kuuza mazao yao. Nikatoa mfano katika Mkoa wa Kilimanjaro wakina mama namna wanavyoteseka katika kuuza zao la ndizi. Ninaomba *commitment* ya Serikali kwenye jambo hili, hasa ikizingatiwa

Mheshimiwa Rais ameongeza bajeti katika Wizara hii kwa asilimia 29, kwa hiyo wana fedha za kutosha. Tunaomba kujua tutafanyiwa nini katika eneo hilo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia bajeti ya mwaka jana Serikali imeamua kuanza kujenga masoko. Na yapo masoko yaliyokuwa ya zamani yaliyokuwa yametelekezwa tumeanza kuya-*revive*. Nimuhakikishie tu Mheshimiwa Esther, na hoja hii ameisema Mheshimiwa Kimei. Katika Mkoa wa Kilimanjario Serikali inafanya *mapping* kwenye maeneo mapya, lakini wakati huo huo tumeanza kujenga masoko ambayo yalikuwa yamechwa tangu muda mrefu ambayo yalikuwa hayajakamilka. Kwa hiyo tunaendelea na huo utaratibu.

**MWENYEKITI:** Haya naona Mheshimiwa Esther Malleko ameridhika na majibu, ameketi. Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo wakati anahitimisha hoja alikiri hapa kwamba sekta ya kilimo inachangia kwa zaidi ya asilimia 25 ya Pato la Taifa, na wamefanya hivyo kwa kutenga mazao ya kimkakati ili yaweze kutuongezea Pato la Taifa na fedha za kigeni; na moja kati ya mazao ya kimkakati ni zao la pamba. Lakini kumekuwa na changamoto kubwa sana, pale inapokuwa Serikali inadaiwa na hawa wakulima wa haya mazao wanancheleweshа sana kuwalipa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano Mheshimiwa Waziri unafahamu katika eneo la pamba peke yake tangu mwaka 2019 hao wadau wa pamba wanadai zaidi ya bilioni 102. Suala hili linasababisha wakulima hao washindwe kuzalisha. Uzalishaji unashuka na wanapata hasara kubwa, na wale

wasambazaji wa pembejeo wanashindwa kusambaza kwa wakati. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha inalipa madeni ya wakulima kwa wakati ili waweze kushiriki katika kuchangia kwenye Pato la Taifa? Nisiporidhika nitashika shilingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salome, Mbunge wa Viti Maalum CHADEMA kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba sekta ya pamba mwaka 2019 ilipopata mtikisiko wa bei na hata tukaamua kwamba bei iwe 1,200 matokeo yake wanunuzi walienda na Serikali ikatoa *guarantee* ya kufidia hasara itakayotokana na sekta. Nataka nimuhakikishie yeye na Bunge lako Tukufu, shilingi bilioni 100 zimeshathibitiswa jati ya bilioni 102; na juzi Wizara ya Fedha imeanza kutoia fedha, tumeanza kulipa. Lakini si hao tu, hata mawakala wa mbolea za ruzuku za mwaka 2015/2016. Kati ya bilioni 70; bilioni 40 zimeshapitiwa na *CAG*. Wizara ya Fedha imeshatukabidhi Wizara ya Kilimo siku mbili zilizopita bilioni 20 za kulipa madeni ya mawakala ya mwaka 2015/2016. Kwa hiyo Serikali imeanza kuchukua hatua kuweza ku-*clean* sekta zetu ili ziweze Kwenda mbele.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome naona umesimama. Mheshimiwa Salome Makamba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeridhika na majibu lakini Serikali izingatie pale kuna riba ambazo zinakuwa *accumulated* na yenyewe wazizingatie pia. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Haya ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge hayo ndiyo majiba yaliyotaka ufafanuzi kwenye eneo hili lenye mshahara wa Waziri. Kifungu kinaafikiwa?

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*......Sh. 2,076,920,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*...........Sh. 4,351,373,000

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nusrat Hanje, anaomba ufafanuzi.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, niliomba kupata ufafanuzi kwenye kifungu hiki cha 20 ambacho kimebeba fedha za kuratibu utekelezaji wa program ya *ASDP* tu. Programu ya kuendeleza…

**MWENYEKITI:** Ishirini ngapi?

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Shilingi 141,200,000.

**MWENYEKITI:** Ishirini ngapi?

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, 20 kwenye kifungu, vile vifungu, kwenye upande wa mshahara hapa hivi vifungu namba 20.

**MWENYEKITI:** Kwenye fungu la mshahara? Namba 20? Ngoja wewe umeomba kwenye *sub vote* 1003. Sasa tusomee huku pembeni ni namba ngapi? Maana hamna hapa kifungu 20. Umebakiwa na sekunde 20.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nime–*withdraw*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1004 – *Agriculture Training Institute*....Sh. 32,185,947,000

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge muda wetu uliobaki unatupeleka kwenye kupitisha mafungu. Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**Fungu 43 – Wizara ya Kilimo**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management*……………………..Sh. 6,594,823,000
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*......Sh. 2,076,920,000
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*............Sh. 4,351,373,000
Kifungu 1004 - *Agriculture Training Institute*….Sh. 32,185,947,000
Kifungu 1005 - *Internal Audit Unit*……..................Sh. 631,170,000
Kifungu 1006 *Procurement Management Unit*....Sh. 851,793,000
Kifungu 1007 - *Government Communication Unit*…….........………………………Sh. 521,747,000
Kifungu 1008 *Legal Service Unit*...........................Sh. 643,768,000
Kifungu 1009 - *Management Information System Unit*……..……………………Sh. 717,261,000
Kifungu 1010 *Environment Management Unit*....Sh. 451,447,000
Kifungu 2001 *Crop Development*……………..…Sh. 47,007,786,000
Kifungu 2002 - *Agricultural Mechanization*.......Sh. 8,389,022,000
Kifungu 2003 - *Agriculture Land Use Planning and Management*…………….………..Sh. 874,277,000
Kifungu 2004 – *Plant Breeders' Unit*.......................Sh. 308,197,000
Kifungu 5001 – *National Food Security*..............Sh. 6,414,100,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 05 – Tume ya Taifa ya Umwagiliaji**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*............................Sh. 2,814,116,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*.........Sh. 502,113,819
Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation*…………...……………...Sh.1,305,840,132
Kifungu 1004 – *Government Communication Unit*……….........………………….Sh. 276,323,000
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*.................................................Sh. 889,116,550
Kifungu 1006 – *Internal Audit Unit*........................Sh. 216,932,500
Kifungu 1007 – *Information Communication Technology Unit*……...………………Sh. 135,729,999
Kifungu 1008 – *Legal Service Unit*…………………Sh. 193,445,000
Kifungu 1009 – *Environment and Social Management Unit*.................................................Sh. 153,360,000
Kifungu 2001 – *Design and Research Division*……...…………………….Sh. 51,503,338,000
Kifungu 2002 – *Irrigation Infrastructure Development*...........................Sh. 13,463,836,000
Kifungu 2004 – *Operations Division*....................Sh. 1,759,244,000
Kifungu 2005 – *Compliance and Quality Assurance Section*........................................Sh. 1334,380,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 24 – Tume ya Maendeleo ya Ushirika**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Division*…………..Sh. 2,047,757,680
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*.........Sh. 279,704,970
Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation Unit*……………………Sh. 383,775,130
Kifungu 1004 – *Government Communication Unit*……………………………..……..Sh. 197,560,710

Kifungu 1005 – *Legal Service Unit*…………...........Sh. 154,661,745
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*……………….............………Sh. 142,289,754
Kifungu 1007 – *Information Communication Technology*……………..........………Sh. 784,669,745
Kifungu 1008 – *Internal Audit Unit*........................Sh. 201,355,745
Kifungu 1009 – *Research and Training Unit*..........Sh. 275,912,310
Kifungu 4001- *Cooperative Promotion and Coordination Section*.....................Sh. 342,891,900
Kifungu 4002 – *Cooperative Microfinance Section*……….......………………Sh. 283,083,900
Kifungu 4003 – *Regional Cooperative Offices*……………………………………..Sh. 5,453,310,080
Kifungu 4004 - *Cooperative Marketing and Investment Section*……...……....Sh. 223,680,720
Kifungu 4005 – *Registration Service Section*........Sh. 252,318,720
Kifungu 4006 - *Inspection and Supervision Services Section*…..…………....…………….Sh. 6,405,100,900

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**NDG. LAWRANCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajielekeza kwenye Kitabu cha Maendeleo. Fungu 43 – Wizara ya Kilimo. Kwenye vishkwambi inaoneshwa kwenye Ukurasa wa 145.

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 43 - Wizara ya Kilimo**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*……………………Sh. 4,100,000,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*.......Sh. 214,962,334,000
Kifungu 1004 – *Agriculture Training Institute*....Sh. 32,989,720,000
Kifungu 1007 – *Government Communication Unit*...............................................Sh. 400,000,000

Kifungu 1009 – *Management Information Systems Unit*…………….................…....Sh. 1,200,000,000
Kifungu 1010 – *Environmental Management Unit*……….............……………….Sh. 203,135,000
Kifungu 2001 – *Crop Development*................Sh.125,744,000,000
Kifungu 2002 – *Agricultural Mechanization*.....Sh.13,129,798,260
Kifungu 2003 – *Agriculture Land Use Planning and Management*……..................…Sh.10,565,878,740
Kifungu 5001 – *National Food Security*...........Sh. 62,403,500,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**NDG. LAWRANCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu linalofuata ni Fungu 05 – Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, kwenye vishkwambi inapatikana ukurasa wa 32.

**Fungu 05 - Tume ya Taifa ya Umwagiliaji**

Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation*....................................Sh. 400,840,000
Kifungu 1006 – *Internal Audit Unit*..........................Sh. 71,304,000
Kifungu 1007 – *Information Communication Technology Unit*…..........................................……..Sh. 671,520,000
Kifungu 1009 – *Environmental and Social Management Unit*……........................................…...Sh. 894,264,000
Kifungu 2001 – *Design and Research Division*…….............................Sh. 42*,085,017,285*
Kifungu 2002 – *Irrigation Infrastructure Development*…………………Sh. 254,468,057,715
Kifungu 2004 – *Operations Division*.......................Sh. 886,320,000
Kifungu 2005 – *Compliance and Quality Assurance Section*…....................................……..Sh. 486,900,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**NDG. LAWRANCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu linalofuata ni Fungu 24 – Tume ya Maendeleo ya Ushirika, kwenye vishkwambi inapatikana ukurasa wa 32.

**Fungu 24 - Tume ya Maendeleo ya Ushirika**

Kifungu 4001 – *Cooperative Promotion and Coordination Section*……..……...Sh. 500,000,000
Kifungu 4004 – *Cooperate Marketing and Investment Section*…………….Sh. 1,172,550,000
Kifungu 4006 – *Inspection and Supervision Services Section*……………..............……...Sh. 500,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**NDG. LAWRANCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Mtoa Hoja, Taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa Taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi imeyapitia makadirio ya matumizi ya fedha ya Wizara ya Kilimo, Fungu 43, Fungu 24 na Fungu 05 kwa mwaka wa fedha 2023/20244 Kifungu kwa Kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo, basi naomba sasa Bunge lako tukufu liyakubali makadirio hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono na sasa nitawahoji kuhusiana na hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Nadhani walioafiki wameshinda. *(Makofi)*

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii kutangaza rasmi kwamba, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 yamepitishwa rasmi na Bunge. *(Makofi)*

Kwa kusema hayo nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wot echini ya Wizara hii kwa kazi nzuri mliyoifanya, lakini pia tuwatakie kila la heri katika utekelezaji wa yale yote ambayo mmewaahidi Wabunge katika hotuba yenu, lakini pia yale ambayo Wabunge wameyachangia hapa na mmesema mnayachukua mnaenda kuyafanyia kazi, tunawatakia utekelezaji mwema. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia niishukuru sana Kamati yetu ambayo kwa kweli ina mambo mengi, lakini yote yana muunganiko mzuri, Kamati yetu ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa kazi nzuri waliyoifanya. Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati hii tunawapongeza sana

kwa kuendelea kuishauri na kuisimamia Serikali vizuri na Wabunge wengine ambao ni wadau katika sekta hii ya kilimo na wale ambao si wadau, lakini wanayafahamu mambo haya, wamepata nafasi ya kuchangia, nao tunawapongeza sana kwa kazi nzuri mliyoifanya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, kuna mambo mawili hapa, halafu Mheshimiwa Mnzava nilimwona anataka kuomba Mwongozo:-

Kwanza ni Mwongozo uliokuwa umeombwa na Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, kuhusu kujibiwa kikamilifu kwa maswali yake ambayo leo aliyauliza.

Waheshimiwa Wabunge, leo katika kikao chetu cha 21 cha Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge, Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu aliomba Mwongozo wa Spika na kwamba, maswali yake mawili ya nyongeza hayakujibiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana. Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Msambatavangu aliuliza swali la msingi namba 264 kwa Ofisi ya Waziri Mkuu.

Aidha, Mheshimiwa Mbunge aliruhusiwa kuuliza maswali mawili ya nyongeza ambapo aliuliza, nanukuu, swali la kwanza: "Tuna malalamiko kutoka kundi muhimu la wafanyakazi ambao wote tunajua historia ya wafanyakazi ndio hasa kundi kubwa lililokuwa likifanya mapinduzi mbalimbali sehemu mbalimbali duniani. Sasa ni lini Serikali pamoja na majibu waliyoyatoa itafanya ile jumuishi kwa sababu, wafanyakazi waliostaafu pia wanasumbuka sana. Wapo ambao walikuwa *NSSF* wakahamishiwa *PSSSF,* wanakwenda kudai mafao yao wanalipwa kidogo na *PSSSF* na wanatakiwa tena kuanza kufuatilia *NSSF,* imeleta usumbufu mkubwa. Ninyi kama Serikali mmejipangaje kuwasaidia ili walipwe mafao yao kwa pamoja?".

Swali la pili, "Askari wetu au Jeshi la Polisi wao ni kama majeshi, lakini kikokotoo hiki kinaonekana kwamba, hakiwahusu majeshi mengine ispokuwa askari wameingizwa kwenye kikokotoo hiki nao hawakubaliani na hiyo. Wanasema kwa nini wao wasiwe *regarded* kama majeshi mengine yalivyokuwa *regarded.* Ahsante." mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Patrobas Katambi, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana alitoa majibu kwa kueleza kuwa kuna ongezeko la fedha zinazolipwa kwa mstaafu kila mwezi na vilevile anazolipwa kwa mkupuo hivyo, kuwepo kwa ongezeko kutoka asilimia 25 mpaka 33. Aidha, alieleza zaidi kwamba, mifuko imeunganishwa na sasa kuna skimu mbili ambazo ni *PSSSF* kwa wafanyakazi wa Serikali na *NSSF* kwa kada nyingine za kawaida.

Waheshimiwa Wabunge, kutokana na majibu hayo Mheshimiwa Msambatavangu aliomba Mwongozo wa Spika, akieleza kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri hakujibu Maswali yake mawili ya nyongeza. Baada ya maombi hayo ya Mwongozo Kiti kilielekeza kuwa kitapitia Taarifa Rasmi za Bunge, ili kujiridhisha iwapo maswali hayo hayakujibiwa.

Baada ya kupitia Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* na maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Msambatavangu pamoja na majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri, nimebaini kwamba maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Msambatavangu yalitaka kujua mambo mawili, kama ifuatavyo; kwanza ni lini Serikali itajumuisha makundi yote ya wafanyakazi kwenye kikokotoo ili kuepusha malalamiko na usumbufu kwa wastaafu ambao walikuwa *NSSF* na kuhamishiwa *PSSSF* na Serikali imejipanga vipi kuwasaidia wafanyakazi walipwe kwa pamoja?

La pili, lilikuwa, Jeshi la Polisi ni sawa na majeshi mengine, lakini kikokotoo kinaonekana hakiyahusu majeshi

mengine. hivyo, ni kwa nini Jeshi la Polisi hawafanani na majeshi mengine katika suala la kikokotoo?

Waheshimiwa Wabunge katika kujibu maswali haya, Mheshimiwa Naibu Waziri alieleza kuwa kuna ongezeko la kiwango cha fedha anazolipwa mstaafu kwa mwezi na kwa mkupuo kutoka asilimia 25 mpaka 33. Vilevile alieleza Bunge kwamba, mifuko imeunganishwa na sasa kuna skimu mbili ambazo ni *PSSSF* kwa wafanyakazi wa Serikali na *NSSF* kwa kada nyingine za kawaida.

Waheshimiwa Wabunge, kwa majibu hayo yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri nimeridhika kuwa maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Msambatavangu hayakujibiwa ipasavyo na majibu hayaendani na maswali yaliyoulizwa. Basi, naagiza maswali hayo yajibiwe upya kwa mujibu wa Kanuni ya 53(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Huo ndio Mwongozo wangu kwa maswali ya Mheshimiwa Msambatavangu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ulikuwepo Mwongozo mwingine ambao uliombwa na Mheshimiwa Jafari Chege, kufuatia lile ambalo lilitokea ama hali iliyojitokeza wakati wa kipindi cha maswali, iliyokuwa inamhusu Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara.

Waheshimiwa Wabunge katika Kikao chetu cha 21 cha Mkutano wa Kumi na Moja wa Bajeti, wakati wa Kipindi cha Maswali na Majibu, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara aliuliza swali la msingi namba 275 kwamba; "Je, ni lini wananchi wa Komarera, Nyamichele na Murwande katika maeneo ya Mgodi wa *Barrick North Mara* watalipwa fidia?"

Swali hilo lilijibiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati kwa niaba ya Waziri wa Madini, ambapo pamoja na mambo mengine alieleza kuwa, nanukuu; "Mheshimiwa Mwenyekiti, Mgodi wa Barrick North Mara ulionesha nia ya

kutaka kuchukua maeneo ya vijiji vya Komarera, Nyamichele na Murwande ambavyo ni sehemu ya vijiji vinavyozunguka mgodi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya wananchi wa vijiji hivyo kupata taarifa ya maeneo yao kuhitajiwa na Mgodi wa Barrick North Mara walianza kuongeza majengo haraka haraka, maarufu kama tegesha. Hali hiyo ilipelekea mgodi huo kuachana na maeneo hayo kwani hayaathiri uendeshaji wa shughuli zao za kila siku." Mwisho wa kunukuu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya majibu hayo kutolewa Kiti kilimpa nafasi Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara kuuliza maswali ya nyongeza. Mheshimiwa Waitara alisimama na badala ya kuuliza maswali ya nyongeza alitoa kauli zilizoonesha wazi kutokuridhishwa na majibu ya Serikali. Hata hivyo, Kiti kilisisitiza Mheshimiwa Waitara kuuliza maswali ya nyongeza, lakini hakufanya hivyo bali aliendelea kutoa malalamiko yake kwa Serikali akisema, nanukuu; "Mheshimiwa Mwenyekiti, sina swali. Hakuna majibu hapa. Swali gani? Majibu ya uongo kabisa haya." Mwisho wa kunukuu.

Baada ya kutoa malalamiko yake dhidi ya majibu ya Serikali, Mheshimiwa Waitara alitoka nje ya Ukumbi wa Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya Kipindi cha Maswali na Majibu, Mheshimiwa Jafari Chege aliomba Mwongozo wa Spika chini ya Kanuni ya 76 ya Kanuni za Kudumu za Bunge kuhusu sintofahamu iliyotokea Bungeni baada ya Mheshimiwa Waitara kutoridhishwa na majibu ya Serikali. Pamoja na mambo mengine Mheshimiwa Chege alisema, nanukuu; "Mwongozo wangu ningetamani Kiti chako kitueleze kwa yale yaliyotokea kwa Mheshimiwa Mbunge kutoridhishwa na yaliyotokea ambayo kimsingi sisi kama Wabunge tunadhani imeleta taharuki ndani ya Bunge." Mwisho wa kunukuu.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni za Kudumu za Bunge zimeweka utaratibu wa namna ya kuuliza maswali na utaratibu ambao Mbunge anatakiwa kuchukua pale ambapo hakuridhika na majibu ya swali lake. Kanuni ya 53 inataka maswali yajibiwe kikamilifu na fasili ya (4) ya Kanuni hiyo inaeleza bayana kuwa, nanukuu; "Iwapo Spika ataridhika kuwa swali la msingi au la nyongeza halijapata majibu ya kuridhisha ataagiza lijibiwe kwa ufasaha zaidi katika kikao kingine cha Bunge." Mwisho wa kunukuu.

Waheshimiwa Wabunge, ili Spika aweze kuagiza swali lijibiwe kwa ufasaha, Mbunge ambaye hakuridhika na majibu anatakiwa kuomba Mwongozo wa Spika, chini ya Kanuni ya 76.

Katika jambo hili Mheshimiwa Waitara, pamoja na kuonesha kwamba hakuridhishwa na majibu ya Serikali, hakutumia nafasi aliyopewa ya kuuliza maswali ya nyongeza ili apewe majibu ya kuridhisha. Halikadhalika alikuwa na nafasi ya kuomba Mwongozo wa Spika, lakini hakuitumia nafasi hiyo badala yake alitoka nje ya Ukumbi wa Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, Mwongozo wangu ni kuwa Mheshimiwa Waitara alikuwa na hiyari ya kutumia nafasi yake ya kuuliza maswali ya nyongeza na kuomba Mwongozo wa Spika, pale ambapo hakuridhika na majibu ya Serikali, lakini alichagua kutokuitumia nafasi hiyo, kwa hiyo, huo ndio Mwongozo wangu.

Pamoja na hayo jambo lingine ambalo limejitokeza leo linalomhusu Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara ni kuwa, akiwa hapa Bungeni kabla hajatoka nje alitoa tai yake na pia, alivua koti alilokuwa amelivaa.

Waheshimiwa Wabunge, hairuhusiwi kufanya hivyo ndani ya Bunge kwa sababu huo ni utovu wa nidhamu na kuzikosea kanuni zetu, kwa sababu kanuni zetu zimeeleza

namna mtu anavyotakiwa kuvaa akiwa Bungeni. Ukivua humu Bungeni maana yake unazikosea kanuni zetu, kwa hivyo, hairuhusiwi.

Sasa nasema hivyo kwa sababu huko nyuma kulishatokea uchangiaji mtu anaamua kupiga magoti, mwingine anaamua kupiga sarakasi, hayo yote nilishayapiga marufuku.

Sasa haya ya mavazi ninyi wengine mnafuatilia vyombo vya habari, kuna nchi moja huko Amerika ya Kusini mtu ametoa nguo zake zote, halafu akaamua kufanya mambo humo Bungeni. Kwa hiyo, hapa hairuhusiwi na isijirudie tena, kama una hasira kaanzie nje ya Bunge, sio hapa ndani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa ninalo tangazo hapa, halafu nitampa dakika mbili Mheshimiwa Mnzava aliyeomba Mwongozo.

Ninalo tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge; Katibu wa Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF)* watatoa huduma ya upimaji wa afya kwa Waheshimiwa Wabunge pamoja na watumishi katika kituo chetu cha afya kilichoko hapa Bungeni, kwenye Jengo la Utawala *Annex*. Zoezi hili limeanza tarehe 7 Mei, 2023 na litaendelea hadi tarehe 19 Mei, 2023. Upimaji huo utahusu magonjwa yafuatayo, ugonjwa wa moyo, uchunguzi wa magonjwa ya macho na uono, uzazi na magonjwa ya kike na kutakuwa na mtaalam wa lishe.

Zoezi hili linashirikisha Madaktari Bingwa kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na Taasisi ya Magonjwa ya Moyo *(JKCI)* na Mloganzila. Waheshimiwa Wabunge mnaombwa mtumie fursa hii kwa ajili ya kufahamu afya zenu.

Baada ya kusema hayo, Mheshimiwa Mnzava, dakika mbili.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 76.

Mheshimiwa Spika, jambo ninalokwenda kuliombea Mwongozo wako naona kama ni jambo muhimu linalogusa heshima ya Bunge lako, lakini pia ni jambo ambalo limeingia kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge ambalo linaweza kutumiwa na kizazi cha sasa na kijacho kama tafsiri ya aina ya Bunge lako, lakini pia, linaweza kutumika kufanyiwa rejea na watu wengine.

Mheshimiwa Spika, siku ya Ijumaa wakati Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara akihitimisha hoja yake, yako maneno ambayo yalitumika ambayo ningependa kupata Mwongozo wako kama ni maneno sahihi ndani ya Bunge letu. Pamoja na maelezo marefu ambayo Mheshimiwa Waziri aliyatoa, lakini yako maneno, naomba niyanukuu, anasema: "Nawashukuru Wabunge ambao wengine wameniambia na wengine wamenionesha picha za watu waliokuwa wakizunguka kuwaomba Wabunge wawaunge mkono kulipinga jambo hili ndani ya Bunge hili," lakini baada ya maelezo kidogo mbele akasema tena maneno mengine: "Waheshimiwa Wabunge nawaomba tusitumike."

Mheshimiwa Spika, kwangu naona maneno haya yanagusa moja kwa moja heshima ya Bunge lako, lakini uhuru wa majadiliano na mijadala ndani ya Bunge hili. Ningeomba kupata Mwongozo wako kama maneno haya ni maneno sahihi kutumika ndani ya Bunge lako? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimempa nafasi Mheshimiwa Mnzava ambaye amesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 76 ili kuweza kuuliza kama jambo lililotokea hapa Bungeni linaruhusiwa ama haliruhusiwi.

Sasa kwa mujibu wa Kanuni hiyo ya 76 inataka jambo liwe limetokea mapema siku hiyo. Sasa changamoto ya matumizi ya hiyo kanuni ni hayo, lakini kwa sababu ya hoja ambayo ameileta na kwamba inahusu majadiliano yetu humu ndani na haki za Wabunge kwa sababu Katiba yetu inatoa hiyo fursa, nitalitazama hilo jambo kwa sababu yeye amesema ananukuu, sasa ile nukuu mimi sikonayo hapa, kwa hiyo, sifahamu maneno halisi ambayo Mheshimiwa Waziri aliyatumia.

Kwa hiyo, nitaenda nifuatilie Taarifa Rasmi za Bunge na yeye hiki alichokisema leo, halafu nitatoa pengine si Mwongozo, lakini maelezo kwa sababu kanuni yetu haitaweza kutumika katika mazingira kama hayo, lakini maelezo ya jumla kwa ajili ya kulinda hadhi ya Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.57 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 10 Mei, 2023, Saa Tatu Asubuhi)*